JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAPENDEKEZO YA MPANGO WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO 2021/22 – 2025/26

"Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu"

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Februari 2021

Orodha ya Vifupisho vya Maneno

ADP	Annual Development Plan (Mpango wa Maendeleo wa Mwaka)
AfCFA	African Continental Free Trade Area (Eneo la Biashara Huru la Bara la Afrika)
AIDS	Acquired Immunodeficiency Syndrome
ASDP II	Agricultural Sector Development Programme II (Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo)
ATCL	Air Tanzania Company Limited (Kampuni ya Ndege ya Tanzania/Shirika la Ndege la Tanzania)
BEST	Business Environment Strengthening for Tanzania (Uimarishaji wa Mazingira ya Kibiashara ya Tanzania)
BITs	Bilateral Investment Treaties (Mikataba ya Uwekezaji Baina/Kati ya Nchi Mbili)
BoT	Bank of Tanzania (Benki Kuu ya Tanzania)
BTAs	Bilateral Trade Agreements (Mikataba ya Kibiashara Baina/Kati ya Nchi Mbili)
CBOs	Community-Based Organisations (Taasisi za Kijamii)
CBWSOs	Community-Based Water Supply Organisations (Taasisi za Huduma za Maji za Kijamii)
CHF	Community Health Fund (Mfuko wa Afya ya Jamii)
COMESA	Common Market for Eastern and Southern Africa (Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika)
COSTECH	Tanzania Commission for Science and Technology (Tume ya Sayansi na Teknolojia)
CSOs	Civil Society Organisations (Asasi za Kiraia)
DANIDA	Danish International Development Agency (Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Denmark)
DART	Dar es Salaam Rapid Transit
DDI	Domestic Direct Investment (Uwekezaji wa Moja kwa Moja wa Ndani)
DFID	Department for International Development (Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Serikali ya Uingereza)
DIB	Development Impact Bond (Hati fungani za Maendeleo ya Matokeo ya Muda Mrefu)
DPs	Development Partners (Washirika wa Maendeleo)
DRC	Democratic Republic of the Congo (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo)

DSA	Debt Sustainability Analysis (Tathmini ya Uhimilivu wa Deni la Taifa)
DSE	Dar es Salaam Stock Exchange (Soko la Hisa Dar es Salaam)
EAC	East African Community (Jumuiya ya Afrika Mashariki)
EACOP	East African Crude Oil Pipeline (Mradi wa Bomba la Mafuta)
EIA	Environmental Impact Assessment (Tathmini ya Athari ya Mazingira)
EPZs	Export Processing Zones (Kanda za Uzalishaji Bidhaa za Kuuza Nje)
ESDP	Education Sector Development Plan (Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu kwa Tanzania Bara)
ESAF	Enhanced Structural Adjustment Facility (Programu ya Maboresho ya Mfumo wa Uchumi)
EWURA	Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji)
FBOs	Faith-Based Organisations (Asasi za Dini)
FCC	Fair Competition Commission (Tume ya Ushindani)
FDCs	Folk Development Colleges (Vyuo vya Maendeleo ya Jamii)
FDI	Foreign Direct Investment (Uwekezaji wa Moja kwa Moja Kutoka Nje)
FYDP	Five Year Development Plan (Mpango wa Maendeleo waTaifa wa Miaka Mitano)
GER	Gross Enrollment Ratio (Uandikishaji wa Jumla wa Wanafunzi)
GDP	Gross Domestic Product (Pato Gafi la Taifa)
HBS	Household Budget Survey (Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya)
HDI	Human Development Index (Fahirisi ya Maendeleo ya Watu)
HIPC	Highly Indebted Poor Countries initiatives (Mpango wa Kusamehe Madeni ya Nchi Maskini Sana)
HIV	Human Immunodeficiency Virus (Virusi vya UKIMWI)
ICT	Information and Communications Technology (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano)
IMF	International Monetary Fund (Shirika la Fedha la Kimataifa)
IMTC	Inter-Ministerial Technical Committee (Kamati

	Maalumu ya Makatibu Wakuu)
JNHPP	Julius Nyerere Hydro Power Project (Mradi wa Kufua Umeme wa Maji Julius Nyerere)
LATRA	Land Transport Regulatory Authorities (Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri na Usafirishaji Nchi Kavu)
LGAs	Local Government Authorities (Mamlaka za Serikali za Mitaa)
LGRP	Local Government Reform Programme (Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa)
LSRP	Legal Sector Reform Programme (Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria)
LTPP	Long Term Perspective Plan (Mpango wa Maendeleo wa Muda Mrefu)
MDAs	Ministries, Departments and Agencies (Wizara, Idara na Wakala za Serikali)
MDRI	Multilateral Debt Relief Initiative (Mpango wa Unafuu wa Madeni wa Taasisi za Kifedha za Kimataifa)
MIGA	Multilateral Investment Guarantees Agency (Taasisi ya Kusimamia Uwekezaji Duniani)
MKUKUTA	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania
MRDTS	Malaria Rapid Diagnostic Tests (Kifaa cha Kupima na Kugundua Malaria kwa Haraka)
MSME	Micro, Small and Medium Enterprise (Wajasiriamali Wadogo na wa Kati)
MW	Megawatt
NACTE	National Council for Technical Education (Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi)
NDC	National Development Corporation (Shirika la Maendeleo la Taifa)
NER	Net Enrollment Ratio (Uandikishaji wa Rika Lengwa)
NGOs	Non-Government Organisations (Taasisi Zisizo za Serikali)
NHIF	National Health Insurance Fund (Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya)
NRW	Non-Revenue Water (Kiwango cha Upotevu wa Maji)
NSSF	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (National Social Security Fund)
OSHA	Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi
PFRP	Public Finance Reform Programme (Programu ya Maboresho katika sekta ya Fedha za Umma)

PPP	Public Private Partnership (Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi)
PPPFF	Public Private Partnerships Facilitation Fund (Mfuko wa Uwezeshaji wa Uwekezaji wa Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi)
PSRP	Public Service Reform Programme (Programu ya Maboresho ya Sekta ya Umma)
PTR	Pupil Teacher Ratio (Uwiano kati ya Wanafunzi na Walimu)
RWSSP	Rural Water Supply and Sanitation Programme (Programu ya Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira)
SADC	Southern African Development Community (Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika)
SATUH	Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati
SDGs	Sustainable Development Goals (Malengo ya Maendeleo Endelevu)
SEZs	Special Economic Zones (Maeneo Maalumu ya Uwekezaji)
SGR	Standard Gauge Railway (Reli ya Kiwango cha Kimataifa)
SIDO	Small Industries Development Organisation (Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo
SME	Small and Medium Enterprise (Wjasiriamali Wadogo na Kati)
SUMATRA	Surface and Marine Transport Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini na Majini)
SWOT	Strength, Weakness, Opportunity and Threats (Uwezo, Udhaifu, Furs ana Viatarishi)
TADB	Tanzania Agricultural Development Bank (Benki ya Maendeleo ya Kilimo)
TAKUKURU	Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa
TANESCO	Tanzania Electric Supply Company Limited (Shirika la Umeme Tanzania)
TANROADS	Tanzania National Roads Agency (Wakala wa Barabara Tanzania)
TAZARA	Tanzania Zambia Railway Authority (Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia)
TBS	Tanzania Bureau of Standard (Shirika la Viwango Tanzania)
TCCIA	Tanzania Chamber of Commerce, Industry and

	Agriculture (Shirikisho la Biashara, Viwanda na Kilimo)
TDV	Tanzania Development Vision (Dira ya Maendeleo ya Taifa – 2025)
TEMDO	Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organisation (Shirika la Uhandisi na Uzalishaji wa Viwanda)
TFDA	Tanzania Food and Drugs Authority (Mamlaka ya Udhibiti wa Chakula na Dawa)
TIC	Tanzania Investment Centre (Kituo cha Uwekezaji Tanzania)
TIN	Taxpayer Identifcation Number (Utambuzi wa Mlipa Kodi)
TIRP	Tanzania Intermodal and Rail Development Project (Mradi wa Ukarabati wa reli ya Kiwango cha Meter Gauge)
TMC	Tanzania Mineral Commission (Tume ya Madini Tanzania)
TMDA	Tanzania Medicines and Medical Devices Authority (Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba)
TNBC	Tanzania National Business Council (Baraza la Taifa la Biashara)
TPA	Tanzania Ports Authority (Mamlaka ya Bandari Tanzania)
TPSF	Tanzania Private Sector Foundation (Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania)
TRA	Tanzania Revenue Authority (Mamlaka ya Mapato Tanzania)
TRC	Tanzania Railways Corporation (Shirika la Reli Tanzania)
TVET	Technical, Vocational and Tertiary Education (Elimu ya Ufundi na Ufundi Stadi)
USD	United States Dollar (Dola za Marekani)
VAT	Value Added Tax (Kodi ya Ongezeko la Thamani)
VETA	Vocational Education and Training Authority (Mamlaka ya Elimu ya Mafunzo na Ufundi Stadi)
VET	Vocational Education and Training (Elimu ya Mafunzo na Ufundi Stadi)
WEO	Taarifa ya Uchumi wa Dunia (World Economic Outlook)
WHO	World Health Organisation (Shirika la Afya Duniani)

RASIMU

YALIYOMO

Orodha ya Majedwali.....xi
Orodha ya Vielelezo.....xii
SURA YA KWANZA 1
1.1 Usuli 1
1.2 Malengo ya Awamu ya Tatu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 4
1.3 Maeneo Muhimu..... 5
1.4 Mchakato wa Maandalizi ya Mpango 6
1.5 Mpangilio wa Kitabu cha Mpango..... 8
SURA YA PILI 9
2.1 Maelezo ya Jumla 9
2.2 Mwenendo wa Uchumi Jumla 9
2.3 Utekelezaji wa Kisekta 16
2.4.1 Elimu 21
2.4.2. Sekta ya Afya 27
2.4.3 Mpango wa Bima za Afya..... 30
2.4.4 Upatikanaji wa Maji Safi na Salama na Uboreshaji wa Usafi wa Mazingira 30
2.5. Kupunguza Umaskini na Uwezeshaji Kiuchumi 30
2.5.2. Ukuzaji wa Ajira..... 32
2.6. Hatua za Kukuza Uwekezaji..... 34
2.6.1 Maboresho ya Miundombinu 34
2.6.2. Maendeleo ya Miundombinu laini 37
2.6.3. Mazingira ya Biashara..... 37
2.6.3.1. Uwezeshaji Sekta Binafsi 39
2.6.3.2 Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi..... 40
2.6.3.3. Utawala Bora , Uwajibikaji na Utoaji haki 40
2.6.5 Amani, Usalama na Utulivu wa Kisiasa 42
2.7. Tathmini ya Ugharamiaji wa Mpango wa Pili 42
2.8. Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Pili 43
2.9. Uwezo, Udhaifu, Fursa na Viatarishi (SWOT) vya Mpango wa Pili 43
2.10 Utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo 45
2.11. Hali ya utekelezaji wa Mpango wa Pili kwa ujumla na Masuala Yaliyojitokeza ... 47
2.11.1 Hali ya utekelezaji wa Mpango wa Pili kwa Ujumla 47
2.11.2 Changamoto za Utekelezaji 48
2.12. Mwelekeo 50

SURA YA TATU 51
3.1 Utangulizi 51
3.2 Sekta Binafsi Nchini 51
Majukumu ya Asasi za Kiraia na Taasisi za Dini 54
Sera na Nafasi ya Taasisi kwenye Maendeleo ya Sekta Binafsi 56
3.4 Matumizi ya Rasilimali za ndani katika uzalishaji na Maendeleo ya Ndani ya Kiuchumi 57
3.5 Kujenga Imani Katika Mijadala kati ya Sekta ya Umma na Binafsi 59
SURA YA NNE 62
4.1 Utangulizi 62
4.2 Kuimarisha Nafasi ya Nchi katika Uchumi wa Kipato cha Kati 62
4.3 Misingi na Kanuni za Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa 64
4.4 Uzoefu wa Nchi nyiingine katika Kujenga Uchumi Shindani 66
4.5 Mfumo wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa 69
4.5.1 Upeo wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa 69
4.5.2 Utawala Bora 71
4.5.3 Ukuaji wa Uchumi 71
4.5.3.1 Uchumi Shindani 72
4.5.3.2 Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda na Huduma 76
4.5.3.3 Biashara na Uwekezaji 82
4.5.4 Maendeleo ya Jamii 83
SURA YA TANO 87
5.1 Utangulizi 87
5.2 Nguzo Kuu za Mpango 87
5.3 Vipaumbele vya Mpango 87
5.4 Hatua za Kisekta za Utekelezaji wa Vipaumbele vya Mpango 88
5.4.1 Kilimo 88
5.4.2 Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika Kuimarisha Tija na Mavuno katika Sekta ya Kilimo 89
5.4.3 Uzalishaji Bidhaa Viwandani 94
5.4.4 Sekta ya Madini 96
5.4.5 Ujenzi 97
5.4.6 Usimamizi wa Mazingira na Maliasili Asilia 97
5.4.7 Uchumi Shindani 98
5.4.8 Kuimarisha Utengemavu wa Uchumi-jumla 99
5.4.9 Huduma za Fedha 100

Sekta ndogo ya Soko la Mitaji 101
5.4.10 Kuimarisha Miundombinu ya Usafiri na Usafirishaji 101
5.4.11 Sekta ya Nishati 102
5.4.12 Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Biashara 104
5.4.13 Kujenga Taasisi Imara 105
5.4.14 Sayansi, Teknolojia na Ubunifu 105
5.4.15 Biashara 107
5.4.16 Sekta ya Utalii 108
5.4.17 Tasnia ya Ubunifu 109
5.4.18 Maendeleo ya Watu 111
5.4.19 Ubora wa Elimu na Maendeleo ya Ujuzi 112
Maendeleo ya Ujuzi 114
5.4.20 Afya 116
5.4.21 Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira 116
5.4.22 Mipango Miji, Maendeleo ya Nyumba na Maendeleo ya Makazi 118
5.4.23 Chakula na Lishe 119
5.4.24 Hifadhi ya Jamii 120
5.4.25 Mahusiano na Nchi za Nje 121
5.4.26 Uongozi Bora na Utawala wa Sheria 122
5.7.1 Ujenzi wa Mji Mkuu Mpya wa Serikali – Dodoma 123
5.7.2 Mifumo ya Utoaji Haki 123
5.7.3 Amani, Utulivu na Usalama 125
5.8 Uchumi wa Rasilimali za Majini 126
5.9 Miradi ya Kielelezo Katika Mpango 127
5.11 Matokeo Tarajiwa 129
SURA YA SITA 131
6.1 Maelezo ya Jumla 131
6.2 Rasilimali Fedha za Kugharamia Mpango 131
6.3 Vyanzo vya Ugharamiaji vya Mpango 133
6.3.1 Vyanzo vya Mapato ya Sekta ya Umma 133
6.3.1.1 Vyanzo vya Ndani 133
6.3.1.2 Mikopo ya Ndani 134
6.3.1.3 Vyanzo vya Nje 134
6.3.2 Vyanzo vya Mapato ya Sekta Binafsi 136
6.3.2.1 Vyanzo vya Ndani vya Sekta Binafsi 136
6.3.2.2 Vyanzo vya Nje vya Sekta Binafsi 137

6.4 Mageuzi ya Mifumo, Taasisi, Sera na Sheria 138
6.4.1 Mapato ya Ndani 138
6.4.2 Ufadhili wa Ndani wa Sekta Binafsi 139
6.4.3 Ugharamiaji Kutoka Nje 140
6.4.4 Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi 141
6.5 Vihatarishi vya Ugharamiaji wa Mpango na Njia za Kukabiliana Navyo 141
6.6 Mchango wa Wadau Katika Kugharamia Mpango 143
6.6.1 Serikali 143
6.6.2 Sekta Binafsi 144
6.6.3 Wadau wa Maendeleo 144
6.6.4 Asasi Zisizo za Kiserikali 144
6.6.5 Watoa Huduma za Kifedha 145
6.6.6 Taasisi za Elimu na Utafiti 145
SURA YA SABA 146
7.1 Utangulizi 146
7.2 Mfumo wa Utekelezaji wa Mpango 146
7.3 Mikakati ya Utekelezaji wa Mpango 146
7.4 Muundo wa Utekelezaji wa Mpango 147
7.5 Muundo wa Uratibu wa Utekelezaji wa Mpango na Mgawanyo wa Majukumu .. 148
7.6 Viatarishi vya Utekelezaji wa Mpango 148
SURA YA NANE 150
8.1 Utangulizi 150
8.2 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango 150
8.3 Malengo ya Ufuatiliaji na Tathmini 151
8.5 Matarajio ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango 151

RASIMU

Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Maboresho ya Sera ya Kodi katika Utekelezaji wa Mpango wa Pili.....11
Jedwali Na. 2: Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje (FDI) 16
Jedwali Na. 3: Mwenendo wa Tofauti za Kipato Tanzania.....32
Jedwali Na.4: Idadi ya Ajira Zilizozalishwa na Sekta Muhimu Kati ya 2016/2017 na 2018/2019 33
Jedwali Na. 5: Mwenendo wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wanawake 34
Jedwali Na. 6: Nafasi ya Tanzania katika Taarifa za Urahisi wa Kufanya Biashara (2015-2020) 38
Jedwali Na. 7 Takwimu za TAKUKURU dhidi ya vitendo vya Rushwa, 2015/16–2019/20 41
Jedwali Na. 8 Uchambuzi (SWOT) wa Utekelezaji wa Mpango wa Pili 44
Jedwali Na. 9 Miradi ya Kielelezo.....46
Jedwali Na. 10 Ongezeko la Mchango wa Ujuzi na Teknolojia (mifano iliyochaguliwa).....77
Jedwali Na. 11 Viashiria na Malengo ya Utekelezaji Katika Kilimo.....92
Jedwali Na. 12 Shabaha na Viashiria vya Mwenendo wa Uzalishaji Viwandani 95
Jedwali Na. 13 Viashiria na shabaha za Utekelezaji Katika Sekta ya Madini.....97
Jedwali Na. 14 Viashiria na Shabaha za Utekelezaji Katika Sekta ya Ujenzi.....97
Jedwali Na. 15 Viashiria na Shabaha za Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira.....98
Jedwali Na. 16 Viashiria vya Jumla vya Uchumi Shindani.....99
Jedwali Na. 17 Viashiria vya Utulivu wa Uchumi-jumla Katika Uchumi Shindani 100
Jedwali Na. 18 Viashiria na Shabaha za Sekta Ndogo ya Bima.....101
Jedwali Na. 19 Viashiria na Shabaha kwa Sekta Ndogo ya Soko la Mitaji.....101
Jedwali Na. 20 Viashiria na Shabaha katika Ujenzi wa Miundombinu.....103
Jedwali Na 21 Shabaha za Jumla za Ufanyaji Biashara 105
Jedwali Na. 22 Shabaha na Viashiria katika Sayansi, Ubunifu na Teknolojia.....106
Jedwali Na. 23 Viashiria na Shabaha katika Ukuzaji Biashara 108
Jedwali Na.24 Viashiria na Shabaha Katika Sekta Ndogo ya Utalii 109
Jedwali Na. 25 Shabaha na Viashiria Katika Tasnia ya Ubunifu 110
Jedwali Na. 26 Viashiria na Shabaha za Maendeleo ya Watu.....111
Jedwali Na. 27 Viashiria na Malengo Katika Elimu na Maendeleo ya Ujuzi 112
Jedwali Na 28 Viashiria na Malengo ya Maendeleo ya Ujuzi.....114
Jedwali Na. 29Viashiria na Shabaha Katika Sekta ya Afya 116
Jedwali Na. 30 Viashiria vya Usambazaji wa Maji na Huduma za Usafi wa Mazingira 117
Jedwali Na. 31 Viashiria na Shabaha ya Uendelezaji Miji, Nyumba na Makazi Endelevu ya Watu.....118
Jedwali Na. 32 Viashiria na Shabaha ya Usalama wa Chakula na Lishe 119
Jedwali Na. 33 Viashiria na Shabaha kwa Hifadhi ya Jamii 120
Jedwali Na. 34 Viashiria na Shabaha Katika Mahusiano na Nchi za Nje na Uchumi wa Kidiplomasia.....122
Jedwali Na. 35 Viashiria na Shabaha za Mfumo Fanisi wa Utoaji Haki.....124
Jedwali Na. 36 Viashiria na Shabaha Katika Uimarishaji wa Usalama wa Umma, Sheria na Taratibu.....125
Jedwali Na 37: Matokeo Yanayotarajiwa.....129
Jedwali Na. 38 Rasilimali Fedha za Kugharamia Mpango (Shilingi Milioni) 132
Jedwali Na. 39 Uwiano kwa Pato la Taifa.....133

Orodha ya Vielelezo

Kielelezo Na. 1 Uandikishaji wa Wanafunzi kwa Elimu ya Awali katika Shule za Serikali na Binafsi kwa Kuzingatia Jinsia, 2014-2018 23
Kielelezo Na. 2 Muundo wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa 70
Kielelezo Na. 3 Mauzo Nje Yanayotumia Teknolojia ya Juu Katika Mauzo ya Jumla (Kwa Asilimia) 78
Kielelezo Na. 4 Utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano .148
Kielelezo Na. 5 Dhana ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango.....150

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo ni nyenzo ya kuunganisha juhudi za Taifa katika kufikia malengo ya maendeleo yanayotarajiwa ya kijamii na kiuchumi ilizinduliwa mwaka 1999. Uzinduzi huo ulifuatiwa na hatua za maboresho i mbalimbali ya kisera, kitaasisi na kimfumo katika miaka ya 2000. Maboresho haya yalikuwa muhimu kutokana na hali ya kiuchumi ambayo Tanzania ilipitia katika miaka ya 1980 na 1990. Katika kipindi hicho, nchi ilikabiliwa na kiwango kidogo cha ukuaji wa uchumi, uhaba mkubwa wa bidhaa na huduma muhimu, mfumuko mkubwa wa bei, madeni makubwa na yasiyohimilika, na makusanyo madogo ya mapato ya Serikali. Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali ilichukua hatua kadhaa za maboresho ya kiuchumi kabla ya kuzindua Dira ya Maendeleo ya Taifa na mpango uliungwa mkono na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) uliojulikana kama programu ya maboresho ya mfumo wa uchumi (*the Enhanced Structural Adjustment Facility - ESAF).*

Katika kipindi cha miaka ya 1990, Serikali ilianzisha programu za maboresho ambazo zililenga kuboresha utendaji na utoaji huduma katika sekta ya umma. Maboresho hayo ni pamoja na Programu ya Maboresho katika Sekta ya Umma (Public Service Reform Programme - PSRP), Programu ya Maboresho katika Serikali za Mitaa (Local Government Reform Programme - LGRP), Programu ya Maboresho katika sekta ya Fedha za Umma (Public Finance Reform Programme - PFRP) na Programu ya Maboresho katika Sekta ya Sheria (Legal Sector Reform Programme - LSRP). Maboresho ya sera na mikakati yalihusisha sekta za huduma za jamii kama vile Elimu, Afya na Maji. Aidha, Serikali ilianzisha taasisi za udhibiti katika sekta za uchumi na miundombinu ikiwa ni pamoja na, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini na Majini (Surface and Marine Transport Regulatory Authority - SUMATRA), ambayo sasa inajulikana kama Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri na Usafirishaji Nchi Kavu (Land and Transport Regulatory Authorities - LATRA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Energy and Water Utilities Regulatory Authority - EWURA) na taasisi nyingine mahsusi kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (Tanzania Revenue Authority - TRA), Mamlaka ya Bandari Tanzania (Tanzania Ports Authority - TPA), na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

Kwa kuzingatia maoni ya wadau katika kipindi hicho, Serikali iliona kuna haja ya kupitia upya majukumu yake ya msingi na ya wadau wengine hususan ya Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia. Kwa msingi huo, Serikali ilianzisha Programu za:

Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (Business Environment Strengthening for Tanzania – BEST); Maboresho ya Sekta ya Fedha; na Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma kwa lengo la kuwezesha sekta binafsi kushiriki katika shughuli za kiuchumi. Aidha, katika kipindi cha 2000 hadi 2010 Serikali iliandaa mipango ya maendeleo ya kisekta ya muda mrefu kama vile Mpango Kabambe Maendeleo wa Sekta ya Usafirishaji, Mpango Kabambe Jumuishi wa Utalii (2002), Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Usafirishaji, Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Bandari (2009), Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Nishati na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme (2008).`

Uzinduzi wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ulifanyika wakati nchi ikikabiliwa na mgogoro wa deni kubwa la nje. Kutokana na hali hiyo, nchi iliingia katika Mpango wa Unafuu wa Madeni wa taasisi za kifedha za kimataifa (Multilateral Debt Relief Initiative -MDRI) na Mpango wa Kusamehe Madeni ya Nchi Maskini Sana (Highly Indebted Poor Countries initiatives - HIPC). Hali hii iliilazimu Serikali kuandaa mipango ya muda wa kati katika waraka wa mkakati wa kupunguza umaskini ulioungwa mkono na taasisi za kifedha za kimatiafa na nchi wahisani. Mikakati iliyoandaliwa ni pamoja na: Mkakati wa Miaka Mitatu wa Kupunguza Umaskini (2000/01 - 2002/03); uliofuatiwa na mkakati wa pili wa miaka mitano uliojulikana kama Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Awamu ya Kwanza (MKUKUTA I) 2005/06 - 2009/10. mkakati huu ulifuatiwa na Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini - MKUKUTA II (2010/11 - 2014/15+1).

Kufuatia tathmini ya kufikiwa kwa malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 iliyofanyika mwaka 2009/10, Serikali iliandaa Mpango Elekezi wa Muda Mrefu (Long-Term Perspective Plan - LTPP) 2011/12 – 2025/26 na kuanzisha mfumo wa uandaaji wa mipango ya maendeleo ya miaka mitano ya utekelezaji wa mpango huo. Uamuzi wa kurejea katika utaratibu wa kuandaa mipango ya muda wa kati ulilenga kuelekeza upya juhudi za kufikia malengo ya Dira kwa kuweka mkazo katika ukuaji wa uchumi sanjari na kupunguza umaskini na kuchochea maendeleo ya watu.

Mipango ya maendeleo ya miaka mitano inahusiana na imeandaliwa kwa kuzingatia dhima mahsusi. Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2011/12 - 2015/16 wenye dhima ya *Kufungulia Fursa Fiche za Ukuaji wa Uchumi*, uliainisha maeneo ambayo hatua zikichukuliwa zitafungua fursa za kiuchumi. Mpango huo ambao ulitekelezwa sanjari na MKUKUTA II ulijielekeza katika kutatua changamoto za miundombinu hususan upatikanaji wa uhakika wa nishati ya umeme (mkazo ukiwekwa katika upatikanaji, ufikiwaji na uhakika), bandari (mkazo ukiwa Bandari ya Dar es Salaam), barabara, reli na upanuzi wa

miundombinu ya huduma za jamii. Jitihada ya kupunguza umaskini, kuboresha maisha ya watu, utawala bora na uwajibikaji zilijumuishwa katika mipango ya maendeleo ya miaka mitano.

Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Miaka Mitano ilibainisha matokeo mchanganyiko; katika baadhi ya maeneo utendaji ulikuwa wa kuridhisha wakati katika maeneo mengine, utekelezaji ulikuwa chini ya malengo yaliyowekwa. Changamoto kubwa iliyobainishwa kwenye tathmini ya Mpango wa Kwanza ni pamoja na: ugharamiaji (mwenendo wa mgao wa fedha za maendeleo ukilinganishwa na utoaji halisi wa fedha, upatikanaji, na utolewaji wa fedha kwa wakati), utendaji hafifu katika usimamizi na kasoro katika mazingira ya biashara na nidhamu katika utekelezaji. Hata hivyo, tathmini hii ilikabiliwa na changamoto upatikanaji wa takwimu.

Dhima ya awali ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21 ilikuwa ni “Kujenga Uchumi wa Viwanda”. Katika kuhimiza umuhimu wa maendeleo ya watu kama ilivyotarajiwa katika Dira, dhima hiyo ilibadilika na kuwa ”Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu”. Mpango wa Pili ambao upo katika mwaka wa mwisho wa utekelezaji, utafuatiwa na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 wenye dhima ya “Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu". Dhima hizi ziliandaliwa ili kuakisi malengo ya Dira ya kujenga uchumi shindani na imara wa kipato cha kati na wa viwanda, unaoweza kushindana kimataifa bila kupoteza lengo la kuleta maendeleo ya watu. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano utawezesha nchi kutumia fursa ya kijiografia na rasilimali zilizopo nchini kwa ajili ya uzalishaji na ukuaji wa uchumi utakaonufaisha wananchi wengi kwa kuzingatia malengo ya Dira ya kuwa na maisha yenye ubora wa juu.

Mpango wa Tatu ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira, hivyo unatarajiwa kuweka mazingira mahsusi na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana tangu Dira ilipozinduliwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Kwa msingi huo, Mpango wa wa Tatu utaendelea kutekeleza miradi na programu za kufungua fursa za kiuchumi, ujenzi wa uchumi wa viwanda, kujielekeza kwenye ushindani wa masoko ya kikanda na dunia na maendeleo ya watu. Mpango huu unatambua kuwa kasi kubwa ya maendeleo na ushindani wa nchi zilizoendelea, na nchi za Asia zenye vipato vya kati na juu imechochewa na matumizi ya sayansi na teknolojia na uwezo katika ubunifu, na kuchagizwa na kuibuka kwa masuala ya digitali. Hivyo, mpango wa Tatu umezingatia umuhimu wa matumizi ya sayansi na teknolojia, uwezo wa ubunifu, na matumizi ya masuala ya digitali ili kuhakikisha kuwa Tanzania haibaki nyuma.

1.2 Malengo ya Awamu ya Tatu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano

Lengo kuu la Mpango wa Tatu ni kufikia malengo ya Dira ya 2025. Malengo hato ni pamoja na Tanzaniakuwa nchi yenye hadhi ya uchumi wa kipato cha kati, na kuendeleza mageuzi ya kuwa nchi ya viwanda yenye kiwango cha juu cha maendeleo ya watu au kiwango cha juu cha maisha. Uchumi huo utakuwa na sifa zifuatazo: hali bora zaidi ya maisha; amani, umoja na mshikamano; utawala bora; jamii iliyoelimika na inayojifunza; na uchumi imara wenye kuhimili ushindani na kunufaisha wananchi wengi.

Hivyo Mpango wa Tatu umeendeleza misingi ya mipango iliyopita kwa kutilia mkazo mageuzi ya kiuchumi, uendelezaji wa viwanda, na maarifa na uwezo wa kushiriki kikamilifu katika biashara za kimataifa. Tanzania inaweza kunufaika zaidi na nafasi yake ya kijografia, wingi wa rasilimali na maliasili zilizopo kuliko ilivyo sasa. Amani na utulivu wa kisiasa wa nchi ni vitu vya thamani pamoja na sababu zingine ndivyo vitakavyovutia wawekezaji wa ndani na nje katika maeneo yenye fursa za kukuza uchumi, hususan katika maeneo ya nchi ambayo kipato kinakua. Aidha, Mpango unahimiza kuongeza uwekezaji katika sayansi, teknolojia na uwezo wa ubunifu kama namna bora ya nchi kutoka kwenye hali ya *fursa linganifu kuingia kwenye fursa shindani* zinazochochea uendelezaji wa viwanda na kuwa shindani katika masoko ya ndani, kikanda na kidunia.

Mpango wa Tatu unalenga kutumia kimkakati rasilimali ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 sanjari na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu - SDGs ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii.

Malengo mahsusi ya Mpango wa Tatau wa Maendeleo wa Taifa ni:

(i) Kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika kufikia Dira 2025 ya kuifanya Tanzania kuwa Taifa la viwanda la uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025;

(ii) Kujenga uwezo katika masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuimarisha ushindani na tija katika sekta zote hususan sekta za uzalishaji, viwanda na huduma ili kuwawezesha watanzania kunufaika na fursa zilizopo ndani ya nchi;

(iii) Kuimarisha uchumi wa viwanda kama msingi wa kuzalisha bidhaa za kuuza nje ikijumuisha kuwekeza kwenye bidhaa na masoko mapya na kuiwezesha Tanzania kuwa kitovu cha uzalishaji katika nchi za ukanda wa Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika na hivyo kuongeza mchango wa nchi katika biashara ya kimataifa;

(iv) Kuongeza wigo wa manufaa ya Tanzania kutokana na fursa ya kimkakati kijiografia kupitia mazingira wezeshi ya biashara yaliyoboreshwa na kuimarisha nafasi ya nchi na kuwa kitovu cha uzalishaji kikanda, biashara na ugavi na usafirishaji;

(v) Kuwezesha kuongezeka kwa uanzishaji wa biashara na ushirikishwaji wa sekta binafsi ili kupata namna bora ya kukuza ukuaji wa sekta hiyo sanjari na ukuzaji wa ajira na kuifanya sekta hiyo kuwa mshirika imara na wa uhakika katika maendeleo;

(vi) Kuongeza mauzo ya huduma nje ikiwa pamoja na: utalii, huduma za kibenki, bima na burudani;

(vii) Kuimarisha utekelezaji wa mpango ikijumuisha uwekaji wa vipaumbele, mpangilio, kufungamanisha na kuoanisha hatua za utekelezaji;

(viii) Kuongeza kasi ya ukuaji uchumi jumuishi na shirikishi kupitia mikakati ya kupunguza umaskini na kuleta maendeleo ya jamii pamoja na kulenga uwezo wa uzalishaji kwa vijana, wanawake na makundi maalumu;

(ix) Kuhakikisha kuwa makubaliano na miadi ya kikanda na dunia inajumuishwa kikamilifu katika maendeleo ya taifa kwa manufaa ya nchi;

(x) Kuimarisha mahusiano kati ya sekta zilizojaaliwa utajiriasilia na maliasilia na sekta nyingine za kiuchumi na kijamii;

(xi) Kuimarisha jukumu la Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuleta maendeleo na kuongeza kipato katika ngazi ya jamii; na

(xii) Kuimarisha uwezo wa nchi katika kugharamia maendeleo kwa kuhakikisha upatikanaji wa mapato ya ndani na usimamizi bora wa matumizi ya umma.

1.3 Maeneo Muhimu

Katika kutekeleza malengo ya Mpango wa Tatu, mkazo utakuwa katika meneo yafuatavyo:

(i) Kuainisha hatua za utekelezaji zinazolenga kuimarisha ushindani wa nchi kiuchumi katika nyanja za uzalishaji na ubora wa bidhaa na huduma na kufanya nchi kuwa kivutio cha uwekezaji kutoka nje. Miongoni mwa vigezo vya kuboresha uzalishaji na ushindani wa kiuchumi ni kuimarisha viwango na ubora wa rasilimali watu, hususan uwezo katika sayansi, teknolojia na ubunifu;

(ii) Hatua za kuimarisha uchumi wa viwanda, unaoongozwa na uwekezaji katika sayansi, teknolojia na uwezo wa ubunifu kwa ajili ya uongezaji thamani wa bidhaa za viwandani na katika sekta za uzalishaji kama vile kilimo, uvuvi, ufugaji, madini, maliasili na nyinginezo;

(iii) Biashara na Uwekezaji: Hatua za kuongeza ushiriki wa Tanzania katika biashara kikanda na dunia, ambapo mauzo nje yatahusisha bidhaa za ndani zilizoongezwa thamani (kutoka kiwango cha kati hadi cha juu cha teknolojia). Aidha, kujenga uelewa wa vigezo vya kisera vya biashara ya kimataifa na diplomasia ya kiuchumi, vitavutia uwekezaji na biashara kutoka nje. Vile vile, kwa kuzingatia nafasi ya sekta binafsi katika uwekezaji, biashara, kuzalisha ajira na kupanua mikakati fungamanishi ya mapato na kupanua uwezo wa

kikodi. Mpango wa Tatu umeweka mkazo katika kuijengea sekta binafsi uwezo na kuongeza ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utekelezaji wa sera ambazo zitawezesha uwekezaji wa ndani na nje na biashara;

(iv) Kuimarisha ubora wa matokeo ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu yanayoendana na lengo la Dira 2025 la kuwa na kiwango cha juu cha maendeleo ya watu, hatua za utekelezaji kwa ajili maendeleo ya jamii zimeainishwa. Msisitizo umewekwa katika upatikanaji na ubora wa huduma ili kufikia maendeleo ya uchumi jumuishi;

(v) Mpango wa Tatu umejikita katika kukuza ujuzi kupitia hatua za kutatua changamoto ya upungufu wa ujuzi katika stadi za kazi (hususan maarifa, ubunifu, uhimilivu, kujituma na mtazamo chanya) na kutowiana kwa ujuzi unaohitajika katika soko la ajira na ule unaotolewa katika taasisi za elimu na mafunzo kwa wanaotafuta kazi. Tabia asilia ya stadi za kazi inahitaji ukuzaji endelevu wa ujuzi kuanzia ngazi ya awali ya elimu ili kuandaa vijana kwa ajili ya ngazi ya juu ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi sanjari na mahitaji ya soko la ajira na kujiajiri. Ni dhahiri kwamba kwa miongo ijayo, nchi zitakazonufaika ni zile zenye ujuzi na uwezo wa ushindani wa kimataifa. Kwa msingi huo, Tanzania haina budi kuendeleza rasilimaliwatu iliyonayo na kuongeza hazina ya ujuzi maalum na adimu katika kutumia utajiri mkubwa wa rasilimali za nchi. Utekelezaji wa maeneo haya utahitaji uratibu na ushirikiano wa sekta zote.

1.4 Mchakato wa Maandalizi ya Mpango

Maandalizi ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo yalitumia mbinu mchanganyiko zilizoandaliwa kwa kuzingatia mifumo ya kitaasisi iliyopo kwenye muundo wa Serikali. Mchakato ulipitia hatua zifuatazo:

(a) Tathmini ya Kina ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili

Serikali kupitia Mtathmini Huru ilifanya mapitio ya kina ya utekelezaji wa Mpango wa Pili. Tathmini hiyo ilipitia malengo na shabaha zaliyowekwa ili kubaini mafanikio, fursa, changamoto na kasoro zilizojitokeza katika kutekeleza Mpango wa Pili kwa lengo la kujifunza na kuboresha uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa Tatu. Aidha, Tathmini ilipima hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa makubaliano ya kikanda na kimataifa.

(b) Mapitio ya Taarifa mbalimbali

Maandalizi ya Mpango huu yalihusisha mapitio ya taarifa mbalimbali zikijumuisha tafiti, vitabu na majarida ya Tanzania na nje ya nchi ili kubaini hali ya Tanzania kiuchumi na kijamii na fursa ya ushindani. Baadhi ya taarifa zilizopitiwa zilihusu tafiti za masuala ya idadi ya watu, ugharimiaji wa maendeleo, uchumi wa rasilimali za maji (blue economy) na uchumi wa kidigitali. Kati ya tafiti na nyaraka rasmi zilizotumika ni pamoja na: Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya, tafiti za

uzalishaji viwandani, Utafiti wa Afya na Idadi ya Watu, tafiti kuhusu sekta isiyo rasmi, hotuba za kisera na miongozo ya viongozi wa kitaifa na nyaraka za Tanzania katika makubaliano ya kikanda na kimataifa. Aidha, nyaraka nyingine zilizotumika ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango Elekezi wa Muda Mrefu 2011/12 – 2025/26, Ajenda ya 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu, Ajenda ya Addis Ababa ya Ugharimiaji wa Maendeleo, Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya TabiaNchi, Dira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050, Dira ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika 2050 na Mpango Mkakati Elekezi wa Jumuiya hiyo (2030), na Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika. Vile vile, Ilani za vyama mbalimbali vya siasa ikiwemo Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025 zilipitiwa ili kuchukuwa mapendekezo muhimu yaliyotolewa. Mapitio ya tafiti na nyaraka hizi yameainisha mifano bora kutoka nchi mbalimbali ambayo inaweza kutumika kwa mazingira ya Tanzania katika kujenga ushindani, uendelezaji wa viwanda na biashara na uwekezaji na maendeleo ya watu.

(c) Ushirikishwaji wa Wadau

Wadau mbali mbali walishirikishwa katika ngazi zote za uandaaji wa mpango ikiwemo:

(i) **Ushirikishwaji wa Wadau wa Ndani:** wadau mbalimbali wa ndani ya taasisi za Serikali ambao ni pamoja na wataalamu, viongozi wa ngazi mbali mbali serikalini walishirikishwa kuanzia hatua za awali ili kupata uelewa wa pamoja wa masuala muhimu ya Mpango;

(ii) **Ushirikishwaji Mpana wa Wadau:** Hatua hii ilihusisha wataalamu wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Taasisi za Mafunzo na Utafiti, Bunge na Washirika wa Maendeleo. Lengo la ushirikishwaji wa wadau lilikuwa ni kukusanya maoni na ushauri, kujenga uelewa wa pamoja na kuboresha maudhui ya mpango.

Mpango wa Tatu umeandaliwa sanjari na mikakati yake ya utekelezaji ikiwemo:

i). Mkakati wa Utekelezaji unaoainisha shughuli na shabaha zitakazotekelezwa;

ii). Mkakati wa ugharamiaji unaoainisha vyanzo vya ugharamiaji wa miradi nya maendeleo na maeneo mengine ya Mpango; na

iii). Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango.

Aidha, Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara ya Fedha na Mipango utahuishwa ili kuwa nyenzo ya kuhakikisha kuwa wadau wote wanahabarishwa kuhusu Mpango wa Tatu.

Uandaaji wa Mpango: Hatua hii ilihusisha vikao kadhaa vya uandishi vilivyoshirikisha wataalamu mbalimbali ili kukamilisha Mpango.

Uidhinishaji wa Mpango: Hatua hii ilihusisha Sekretariati ya Baraza la Mawaziri, Kamati ya Makatibu Wakuu ya Baraza la Mawaziri, Baraza la Mawaziri na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.

Usambazaji wa Mpango: Mpango wa Tatu utasambazwa kwa wadau wa ndani na nje kupitia nakala za vitabu vya Mpango, mifumo ya kidigitali na majukwaa mbalimbali ikiwemo mahojiano na semina.

1.5 Mpangilio wa Kitabu cha Mpango

Kitabu cha Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kimepangwa katika sura nane (8). Sura ya Kwanza ni Utangulizi, Sura ya Pili inahusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa. Sura ya Tatu imejikita katika masuala ya maendeleo ya sekta binafsi. Sura ya Nne inatoa dhana ya kujenga uchumi shindani, maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu na maeneo matano muhimu ya Mpango. Sura ya Tano inaainisha hatua mahususi za kuchukuliwa katika maeneo ya kipaumbele. Sura ya Sita inahusu ugharamiaji wa utekelezaji wa Mpango. Sura ya Saba inaanisha mpangilio wa utekelezaji wa Mpango na Sura ya Nane inaainisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango.

SURA YA PILI

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO 2016/17 – 2020/21

2.1 Maelezo ya Jumla

Sura hii inaeleza kwa muhtasari matokeo ya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21. Inaonesha matokeo ya utekelezaji wa Mpango wa Pili ikilinganishwa na malengo, shabaha, viashiria na vigezo vya utendaji na kuainisha mafanikio, changamoto na masuala muhimu ya kuzingatiwa katika Mpango wa Tatu.

Sehemu ya 2.2 inatoa muhtasari wa mwenendo wa uchumi jumla ikijumuisha ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei, ustahimilivu wa urari wa sekta ya nje, utekelezaji wa Bajeti ya Serikali na uchambuzi wa deni la nje. Sehemu ya 2.3 inaelezea utendaji kisekta ikijumuisha sekta za kilimo, ujenzi, nishati, uchimbaji wa madini, biashara, utalii na maendeleo ya viwanda hususan uzalishaji viwandani. Sehemu ya 2.4 inachambua maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii hususan elimu, afya, maji safi na salama pamoja na usafi wa mazingira. Aidha, Sura hii inatoa maelezo zaidi kuhusu mwenendo wa umaskini na tofauti ya kipato, jinsia na uwezeshaji wa wanawake.

Sehemu ya 2.6 inahusu uwezeshaji katika nyanja mbili za uwekezaji na mazingira ya biashara ambazo ni: mazingira wezeshi kwa kuboresha miundombinu ya barabara, reli, usafiri majini na TEHAMA; na mazingira ya biashara yakijikita katika uwezeshaji wa sekta binafsi, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na utawala na uwajibikaji. Sehemu ya 2.7 inachambua ugharamiaji wa Mpango wa pili, na sehemu ya 2.8 inahusu ufuatiliaji na tathmini ya Mpango wa Pili. Sehemu 2.9 inatoa maelezo kwa kifupu kuhusu utekelezaji wa miradi ya kielelezo. Maelezo kwa kuhusu uwezo (strength), udhaifu (weakness), fursa (opportunities) na viatarishi (threat) ambavyo vilivyoiburiwa kutokana na uchambuzi wa utekelezaji wa Mpango wa Pili Miaka Mitano vimeoneshwa kutokana na majedwali mawili, ikifuatiwa na muhtasari wa utekelezaji wa Mpango kwa ujumla, vikwazo na mwelekeo wa baadaye (sehemu ya 2.11).

2.2 Mwenendo wa Uchumi Jumla

Ukuaji wa Pato la Taifa: Uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa imara na tulivu. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili (2016 – 2019), Pato Taifa liliendelea kukua kwa wastani wa asilimia 6.9 kwa mwaka. Kutokana na ukuaji huo, Tanzania ilifanikiwa kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati wa chini mwezi Julai, 2020. Kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia, wastani wa Pato la Wastani la kila Mtu (Gross National Income per capita) liliongezeka kutoka shilingi 2,225,099 sawa na dola za Marekani 1,022 mwaka 2016 hadi shilingi 2,577,967 sawa na dola za

Marekani 1,080 mwaka 2019, ambalo ni zaidi ya kigezo cha dola za Marekani 1,036 cha kuingia katika kundi hilo.

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili, ukuaji wa uchumi ulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa uwekezaji hususan katika ujenzi wa barabara, reli na viwanja vya ndege; kutengamaa kwa upatikanaji wa nishati ya umeme; kuimarika kwa huduma za usafirishaji; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini hususan dhahabu na makaa ya mawe; na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo. Hii ilitokana na utekelezaji wa miradi mikubwa ya miondombinu hususan katika sekta za usafirishaji na nishati; kuboresha usimamizi wa shughuli za uchimbaji madini zilizolenga katika kuongeza ufanisi wa utendaji na kuzuia magendo na udanganyifu wa bei za madini; kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na kusimamia matumizi; pamoja na hali nzuri ya hewa kwa ajili ya shughuli za kilimo.

Katika kipindi cha mwaka 2016 na 2019, sekta zilizokuwa na ukuaji mkubwa ni pamoja na ujenzi (asilimia 14.4), uzalishaji viwandani (asilimia 8.3), usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (asilimia 8.2), shughuli za uchimbaji madini na mawe (asilimia 8.0); na habari na mawasiliano (asilimia 6.2). Ukuaji wa sekta hizo ulisababisha kupungua kwa mchango wa kilimo katika Pato la Taifa kutoka asilimia 29.0 mwaka 2015 hadi asilimia 26.6 mwaka 2019. Kushuka kwa mchango wa sekta ya kilimo katika Pato la Taifa na ongezeko la mchango wa sekta mpya kunadhihirisha uwepo wa mageuzi ya muundo wa uchumi wa Tanzania uliochangiwa na sera ya kuwa na uchumi wa viwanda, maboresho ya miundombinu na sera za madini, na kuongezeka kwa matuizi ya TEHAMA.

Mfumuko wa Bei: Kasi ya mfumuko bei ilibakia kuwa katika tarakimu moja, ambapo kiwango cha wastani cha mfumuko wa bei kwa mwaka kilikuwa asilimia 4.4 kwa kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Mpango wa Pili. Kiwango hiki ni ni ndani ya lengo la kuwa na mfumuko wa bei usiozidi asilimia 5 kwa mwaka katika kipindi cha Mpango II. Mfumuko wa bei wa jumla (headline inflation) ulipungua kutoka wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2016 hadi wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2020. Kwa ujumla hali hii ilichangiwa na ongezeko la upatikanaji wa chakula katika soko la ndani na nchi jirani, kuimarika kwa bei ya mafuta duniani, na sera madhubuti za bajeti na fedha.

Akiba ya Fedha za Kigeni na Kiwango cha Ubadilishaji wa Fedha za Nje: Katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Mpango wa Pili, kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kilitosheleza mahitaji muhimu kama vile uagizaji wa bidhaa nje, kulipa madeni, na mahitaji mengine ya fedha za kigeni. Mathalani kufikia Desemba 2020, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa Dola za Marekani milioni 4,767.7 kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi 5.6. Kiwango hiki ni zaidi ya kiwango cha lazima kinachohitajika cha miezi 4 na lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki la miezi 4.5. Hali hii nzuri ya akiba ya fedha

za kigeni ilichangiwa na ongezeko la thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma zilizouzwa nje. Akiba ya fedha za kigeni yakutosha imesaidia nchi kukabiliana na mitikisiko ya kiuchumi kutoka nje, kuongeza imani ya wawekezaji na wakopeshaji pamoja na kuiwezesha Benku Kuu ya Tanzania kudhibiti soko la ndani la fedha za kigeni ili kuweka utulivu katika viwango vya ubadilishaji fedha.

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili, thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya fedha za kigeni imeendelea kuwa tulivu. Kwa mujibu wa Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2019/20, kiwango cha ubadilishaji wa Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola moja ya Marekani kilikuwa shilingi 2,230.1 mwishoni mwa mwaka 2016/17 na shilingi 2,295.5 mwishoni mwa mwaka 2019/20. Hali ya utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania inatokana na usimamizi mzuri wa sera na sheria za fedha usimamizi madhubuti wa Benki Kuu katika kuleta uwazi wa biashara katika soko la fedha za kigeni. Sababu nyingine zilizochangia kuwepo kwa utulivu wa kiwango cha ubadilishaji fedha ni kupungua kwa nakisi ya mauzo nje na mfumuko mdogo wa bei kwa washirika wakubwa wa kibiashara na Tanzania.

Utekelezaji wa Bajeti: Mapato ya ndani yamekuwa yakiongezeka kila mwaka katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Pili, licha ya kuwa chini ya lengo la mwaka liliyowekwa. Aidha, uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 13.4 mwaka 2015/16 hadi asilimia 14.7 mwaka 2019/20. Ongezeko hili la mapato lilitokana na utekelezaji wa sera mbalimbali za ukusanyaji wa mapato zilizolenga kupanua wigo wa kodi, kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya mapato vilivyopo hususan kuongeza matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya kukusanya mapaoto, na hatua nyingine za kiutawala. Jedwali Na. 1 linatoa muhtasari wa maboresho ya sera ya kodi katika kipindi cha Mpango wa Pili.

Jedwali Na. 1: Maboresho ya Sera ya Kodi katika Utekelezaji wa Mpango wa Pili

Maboresho ya Kodi	Malengo
Mwaka 2015/16	
Maboresho ya Kodi ya Mapato - Kupunguza kodi ya mapato kwenye mshahara (PAYE) kutoka asilimia 12 hadi asilimia 11 na viwango vya kodi za biashara (presumptive tax regimes) kwa asilimia 25.	• Kupunguza mzigo wa kodi kwa watu wenye kipato cha chini; na • Kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari na kupunguza gharama wa biashara.
Mwaka 2016/17	
Maboresho ya Kodi ya mapato-Kupunguza kodi ya mapato kwenye mshahara (PAYE) kutoka asilimia 11 hadi asilimia 9	• Kupunguza mzigo wa kodi kwa watumishi na wafanyakazi.
Ushuru wa Bidhaa - Kuweka ushuru wa bidhaa katika huduma za kifedha kupitia simu za mikononi ikijumuisha gharama za utoaji fedha	Kudhibiti ukwepaji wa kodi na kuongeza mapato ya Serikali.

Maboresho ya Kodi	Malengo
Maboresho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani - VAT kuanzisha VAT katika ada za huduma za kifedha; kufuta msamaha katika huduma za kitalii na huduma kwa wanajeshi na badala yake kutoa ruzuku kama njia mbadala ya kuwapa mahitaji yao.	• Kuondoa mkanganyiko na kupunguza misamaha ya kodi; • Kupanua wigo wa kodi na kuongeza mapato ya serikali; na • Kuweka usawa kwa wanajeshi wote, na kuepuka mwanya wa kupoteza mapato ya Serikali.
Maboresho ya Ushuru wa Forodha - kuongeza kiwango cha ushuru wa uagizaji saruji kutoka nje kutoka asilimia 25 hadi 35; kuongeza ushuru wa uagizaji samani kutoka asilimia 15 hadi 20; na kufuta misamaha kwa majeshi na badala yake kulipa posho kama njia mbadala ya kuwapatia bidhaa.	Kulinda na kukuza uzalishaji wa samani ndani ya nchi, kukuza ajira, kuleta usawa kwa wanajeshi wote na kuziba mwanya wa kupoteza mapato ya Serikali.
Mwaka 2017/18	
Maboresho ya Ushuru wa Forodha - Kuunganisha ada ya mwaka ya magari na kodi ya mafuta kwa kuongeza viwango vya Ushuru wa Bidhaa kwa petroli na diseli kwa Sh. 40 kwa lita, kutoka Sh 339/= hadi Sh. 379/= kwa lita.	Kurahisisha makusanyo, kupunguza gharama za kukusanya kodi, na hivyo kupunguza adha kwa walipa kodi na kuongeza uhiari wa kulipa; kufidia mapato yaliyofutwa ya ada za mwaka kwa magari.
Maboresho ya Kodi ya Mapato – asilimia 5 ya kodi ya zuio (Withholding Tax) kwa wachimbaji wadogo wa madini na kuongeza kiwango cha kufuzu kupata uchakavu wa magari yasiyo ya kibiashara na kukusanya mapato yote ya kodi za michezo ya kubahatisha.	Kuongeza mapato, kuleta usawa na kuimarisha makusanyo ya Serikali katika michezo ya kubahatisha.
Mwaka 2018/19	
Maboresho ya Kodi ya mapato – kupunguza kiwango cha kodi ya kampuni kutoka asilimia 30 hadi 20 kwa kampuni mpya ya viwanda vya dawa na wazalishaji wa bidhaa za ngozi kwa kipindi cha miaka mitano (5).	• Kutoa motisha kwa uwekazaji katika uzalishaji wa dawa na bidhaa za ngozi ili kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali; na • Kuokoa fedha za kigeni zinazotumika kuagiza bidhaa hizi.
Maboresho ya Ushuru wa Forodha - kuongeza kiwango cha kodi kwa sukari ya nje kutoka asilimia 25 hadi 35.	Kulinda viwanda vya ndani.

Maboresho ya Kodi	Malengo
Maboresho ya Kodi za michezo ya Kubahatisha – kuongeza kiwango cha kodi kutoka asilimia 15 hadi asilimia 18 kwa mapato yote ya shughuli za kasino, na mashine za michezo ya kubahatisha kutoka shilingi 32,000 hadi shilingi 100,000 kwa machine, kwa mwezi. Kuongeza kiwango cha kodi kwa michezo ya kubashiri matokeo ya michezo (sport betting) kutoka asilimia 6 hadi 10 kwa mapato ghafi. Kuongeza kiwango cha kodi kwa ushindi (Gaming Tax on Winnings) kutoka asilimia 18 hadi 20 kwa bahati nasibu za ujumbe mfupi wa simu, kubashiri matokeo ya ushindi wa michezo, mashine za kuechezea (*Slot)*, bahati Nasibu ya Taifa, mashine za *Forty* (Forty machines site) na kasino za mtandaoni (online casino (Internet /online casino).	• Kuongeza mapato ya kodi ya michezo ya kasino; • Kuongeza mapato ya Serikali kutokana na makusanyo ya kodi ya michezo ya kubahatisha; na • Kuongeza mapato ya Serikali.
Mwaka 2019/20	
Maboresho ya mfumo wa kodi (presumptive tax regimes)' kwa walipa kodi wenye mauzo ya mwaka kuanzia shilingi 4,000,000.00 hadi 100,000,000. ambao hawalazimiki kuwasilisha mahesabu yao ya fedha kwa mamlaka ya mapato kwa makadirio ya kodi. (a) Pendekezo la kuanzisha kodi ya mauzo kwa wafanyabiashara wa PIT.	Kupunguza adha ya kukadiria kodi kwa wafanyabiashara wadogo pamoja na kiwianisha viwango vya kodi na mauzo ya chini, yanayohitajika ili biashara zilazimike kutumia mashine za kielektroniki.
Pamoja na hatua hizo, serikali pia ilichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na misamaha (Tax amnesty) na kuanzisha vitambulisho vya wamachinga, ETS,	Kuwapa wadaiwa waliolimbikiza kodi na adhabu unafuu, kuongeza mapato ya serikali, na kuwatambua wafanyabiashara wadogo kwa lengo la kuwarasimisha.

Kwa upande wa matumizi, lengo lililoainishwa kwenye Mpango wa Pili ni kuongeza bajeti ya maendeleo kufikia asilimia 30 hadi 40 ya bajeti yote. Matumizi ya maendeleo yaliongezeka kutoka asilimia 22.5 ya bajeti ya mwaka 2015/16 hadi asilimia 31.4 ya bajeti ya mwaka 2019/20. Utegemezi wa bajeti uliendelea kuwa katika kiwango cha tarakimu moja katika kipindi cha miaka 5 iliyopita, ambapo uwiano kati ya mikopo ya masharti nafuu na misaada ulifikia wastani wa asilimia 9.3 ya Bajeti yote ya mwaka 2019/20. Uwiano wa matumizi ya maendeleo kwa Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 4.3 mwaka 2015/16 hadi asilimia 6.3 mwaka 2019/20. Matumizi ya maendeleo yalielekezwa katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya jamii na utawala bora ikiwemo afya na elimu, majengo ya Serikali

Dodoma na majengo ya mahakama. Aidha, kiasi kikubwa cha fedha za maendeleo kwenye miradi ya sekta ya usafirishaji kama vile ujenzi wa reli kwa kiwango cha kimataifa (SGR), ukarabati wa reli ya kati na kufufua reli ya Tanga – Arusha, ujenzi wa barabara na madaraja makubwa, kufufua Shirika la Ndege Tanzania, kununua meli na vivuko, ujenzi na ukarabati wa bandari, miradi ya umeme ya Kinyerezi I na II, ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), usambazaji wa umeme vijijini,, uboreshaji na ukarabati wa viwanja vya ndege katika mikoa mbalimbali nchini pamoja na ujenzi miundombinu ya umwagiliaji.

Nakisi ya Bajeti ilipungua kutoka asilimia 3.4 mwaka 2015/16 hadi kufikia asimilia 1.4 mwaka 2019/20; na imebakia chini ya asilimia 3, ambalo ni lengo lililowekwa kama kigezo cha mtangamano kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC). Nakisi hii ya bajeti ya iligharamiwa kupitia mikopo ya ndani na nje.

Mwenendo wa Sekta ya Fedha: sBenki Kuu ya Tanzania iliendelea kusimamia sera za fedha ili kuongeza mikopo kwa sekta binafsi. Mwaka 2017, Benki Kuu ya Tanzania ilipunguza riba kutoka asilimia 12.0 hadi asimia 9.0 na kuendelea kupunguza hadi asilimia 5 mwezi Mei, 2020. Vile vile, Benki Kuu iliendelea kuongeza ukwasi katika uchumi kupitia hatua mbalimbali za kisera ili kukidhi matakwa ya soko. Hatua hizi ziliimarisha ukwasi katika masoko ya fedha. Kwa upande wa hati fungani za Serikali, viwango vya riba vilipungua kutoka wastani wa asilimia 17.49 mwezi Desemba 2015 hadi wastani wa asilimia 11.06 mwezi Desemba 2020. Riba za jumla za amana zilipungua kutoka asilimia 9.3 mwezi Desemba 2015 hadi asilimia 7.09 mwezi Desemba 2020.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita sekta ya benki ilibakia kuwa imara ikiwa na viwango vya ukwasi vya juu ya kiwango kinachohitajika na mamlaka za usimamizi. Kufikia tarehe 31 Desemba 2019, kampuni mbili za kuwezesha upatikanaji wa taarifa za wakopaji 'Credit info Tanzania Limited' na 'Dun & Bradstreet Credit Bureau Tanzania Limited'zilikuwa zimeanzishwa. Katika kipindi hiki, taasisi 55 za kibenki kati ya 56 sawa na asilimia 98 ya taasisi za kibenki, zilikuwa zikiwasilisha taarifa katika Kanzidata ya taarifa za Wakopaji. Kufikia mwisho wa mwaka 2019, idadi ya wakopaji na mikopo ya benki iliyowasilishwa na taasisi za kibenki ilifikia shilingi milioni 5.22 na shilingi milioni 3.9 mtawalia. Vile vile, idadi ya mawakala wa benki iliongezeka kutoka 3,299 Desemba 2015, hadi 28,358 Desemba 2019. Ongezeko la mawakala wa benki linaashiria kuongezeka kwa idadi na thamani ya miamala. Kiasi cha fedha zilizowekezwa kwa mawakala kilikuwa shilingi bilioni 5,464.9 mwaka 2019 ikilinganisha na shilingi bilioni 28.37 mwaka 2013. Kwa upande wa fedha zilizotolewa, ilikuwa kiasi cha shilingi bilioni 1,833.1 na bilioni 4.14 mtawalia. Jumla ya mitaji ya kampuni 28 ziliorodheshwa katika Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE) iliongezeka kufikia shilingi bilioni 19,676.92

mwaka 2018, ukilinganisha na jumla ya shilingi bilioni 16,464.3 zilizorekodiwa Desemba 2013. Idadi ya makampuni yaliyoorodheshwa DSE iliongezeka kufikia makampuni 28 mwaka 2018 ikilinganisha na makampuni 18 mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 55.6.

1. **Uhimilivu wa Deni la Taifa:** Deni la Taifa liliendelea kuwa himilivu katika kipindi chote cha utelezaji wa Mpango wa Pili. Viashiria vyote vya uhimilivu wa deni vimekuwa chini ya viwango vya ukomo vilivyokubalika kimataifa vikimaanisha kuwa Deni la Tanzania ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu kwa kwa viashiria vyote muhimu.Uwiano wa Deni la taifa kwa pato la taifa lilikuwa asilimia 39.0 mwaka 2019/20. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Novemba, 2020 imeonesha thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 27.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 70; thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 17.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; na thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 113.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 240. Aidha, ulipaji wa deni la nje kwa mauzo ya bidhaa nje ni asilimia 13.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 23. Matokeo haya ya muda mrefu yanawiana na matarajio ya kiwango kikubwa cha ukuaji wa uchumi na kupungua kwa madeni mapya baada ya kukamilisha utelekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati iliyo katika Mpango wa Pili. Aidha, taarifa ya uchumi wa dunia (World Economic Outlook Report – WEO) ya mwezi Oktoba 2020 inayotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) ilionesha kuwa Tanzania ina uwezo mkubwa wa kuhimili madeni la taifa kutokana na kiwango cha juu (Country Policy and Institutional Assessment = 3.07) cha utekelezaji wa sera

2. **Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje (FDIs*):*** katika kipindi cha utelezaji wa Mpango wa Pili, Tanzania iliendelea kuvutia wawekezaji wa nje. Mitaji ya Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 2.** Sekta zilizovutia zaidi Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje ni shughuli za uchimbaji wa madini na mawe, fedha na bima, chakula na malazi, viwanda na kilimo. Nchi zilizowekeza zilikuwa Uingereza, Afrika ya kusini, Kenya, Ujerumani, Uholanzi, China, India, Mauritius, Oman, Umoja wa Falme za Kiarabu, Canada, na Marekani.
Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili, serikali ilifanya maboresho mbali mbali ya kisera, kisheria na kiutendaji kwa lengo la kuunguza urasimu wa kushughulikia wawekezaji hususan katika utoaji wa vibali vya kazi, majengo, leseni, na kuridhia miradi. Aidha, Serikali ilianzisha Kituo cha pamoja (One Stop Centre-OSC) cha kushughulikia masuala ya wawekezaji katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ili huduma zote muhimu ziweze kupatikana sehemu moja na kuokoa muda wa wawekezaji na kupunguza gharama ya kufuatilia vibali kutoka ofisi moja hadi nyingine.

Jedwali Na. 2: Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje (FDI)

Mwaka	2016	2017	2018	2019
Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje (FDI)	755.4	937.7	971.6	990.6

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

2.3 Utekelezaji wa Kisekta

Sekta ya Kilimo: Malengo makuu yalikuwa:- kufikia kiwango cha ukuaji halisi wa asilimia 7.6; kuchangia asilimia 29.4 ya Pato la Taifa; kuchangia asilimia 24.9 ya mauzo yote nje; na kutoa ajira ya asilimia 56.5 ya ajira zote. Katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Mpango wa Pili, Sekta ya kilimo ilikua kwa wastani wa asilimia 5.1 kwa mwaka na kuchangia kwa wastani wa asilimia 27.7 katika Pato la Taifa, asilimia 24.1 ya mapato yatokanayo na mauzo nje na asilimia 65 ya ajira zote. Uzalishaji wa mazao ya biashara uliongezeka kufikia tani 1,156,389 mwaka 2018/19 kutoka tani 796,502 mwaka 2015/16. Uzalishaji wa mazao ya chakula uliendelea kushamiri kuwezesha nchi kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 118. Mauzo ya maua na mbogamboga nje yaliongezeka kufikia Dola za Marekani 779 mwaka 2018/19 kutoka Dola milioni 412 mwaka 2015. Eneo la umwagiliaji liliongezeka kufikia hekta 694,715 mwaka 2019 kutoka hekta 461,376 mwaka 2015. Uwezo wa kuhifadhi mazao ya chakula uliongezeka kufikia tani 621,000 mwaka 2020 kutoka tani 371,000 mwaka 2015.

Tathmini ilibaini changamoto kwenye kilimo inatokana na tija ndogo ambayo inasababishwa na matumizi ya teknolojia duni za uzalishaji. Kwa mujibu wa matokeo ya awali ya sensa ya kilimo ya mwaka 2019/20, ni asilimia karibia 20 tu ya hekta milioni 13.5 zilizolimwa, ndiyo walitumia mbegu bora; na hekta milioni 2.8 au asilimia 20 tu, walitumia mbolea ya viwandani. Aidha, katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Mpango, miundombinu ya umwagiliaji imejengwa na kuboreshwa ambayo imeongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 461,376 mwaka 2015 hadi hekta 694,715 mwaka 2020. Hadi Desemba 2020, serikali imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za Kigugu – Mvomero yenye hekta 200 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98, Mvumi – Kilosa yenye hekta 249 (asilimia 100), Msolwa Ujamaa – Morogoro yenye hekta 675 (asilimia 98), Njage – Kilombero yenye hekta 325 (asilimia 100), Shamba la Mbegu Kilangali – Kilosa yenye hekta 400 (asilimia 80); kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 36,614 mwaka 2015 hadi tani 71,000 mwaka 2020; kukamilika kwa ujenzi wa maabara ya mbegu katika Makao Makuu ya Wakala wa Mbegu za Kilimo – Morogoro; kuzalishwa kwa kilo 14,700 za mbegu za mpunga za daraja la awali (pre-basic) aina ya TXD 306, TXD 88, Komboka, Tai, Supa na NERICA 1; kuongezeka kwa upatikanaji wa mbolea kutoka tani 302,450 mwaka 2015 hadi tani 727,719 mwaka 2020; kukamilika kwa ujenzi wa maghala matano (5) ya kuhifadhi mpunga kupitia mradi wa kuongeza uzalishaji wa mpunga – *Expanded Rice Production Project*; kusambazwa kwa tani 40,592.6 za salfa na lita 1,314,465 za viuatilifu maji kwa wakulima wa korosho; kuendeshwa kwa minada nane (8) ya kahawa katika mikoa ya Kilimanjaro (2), Songwe (4)

na Ruvuma (2); na kukaguliwa kwa viwanda 24 na maghala 30 na kutolewa leseni za kuendesha biashara ya kahawa.

Sekta ya Ujenzi: Mchango wa sekta ya ujenzi kwa Pato la Taifa uliendelea kuongezeka kila mwaka. Tathmini ya sekta inaonesha kwamba kufikia mwaka 2019 mchango kwa pato la taifa ulikuwa asilimia 14.8, ambao ni juu kwa asilimia 3.7 ikilinganishwa na kiwango cha msingi (baseline) cha asilimia 11.1 na asilimia 3 zaidi ya lengo la Mpango wa Pili la asilimia 11.8. Katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Mpango wa Pili, Sekta ya ujenzi ilikua kwa wastani wa asilimia 14.4 kwa mwaka. Ukuaji huu ulitokana na kazi za ujenzi wa mtandao wa barabara, majengo na uchimbaji madini. Kwa upande wa barabara, Serikali imejenga mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami wenye urefu wa kilomita 3,537 za barabara kati ya mwaka 2015/16 na 2019/20 (barabara kuu na za mikoa kilomita 2,209 na barabara za halmashauri kilomita 1,328) na hivyo kufanya mtandao wa barabara uliojengwa kwa kiwango cha lami hadi mwaka 2019/20 kufikia kilomita 13,044 ambapo kilomita 10,939 ni barabara kuu na kilomita 2,105 ni barabara za mikoa. Aidha, Serikali imekarabati kilomita 300.9 za barabara kuu, na kujenga madaraja makubwa 12, viwanja vya ndege na miundombinu mingine kama vile, miundombinu ya afya na elimu, na majengo ya Serikali.

Katika kipindi hicho, Sekta rasmi ya ujenzi imekua kwa kasi lakini pia ujenzi katika sekta isiyo rasmi nao unakua hususan ujenzi wa majengo, (nyumba za kuishi ambazo zinajengwa bila mikataba ya ujenzi) katika makazi mengi ya mijini na vijijini. Kutokana na changamoto za uwezo wa kitaalamu na kimenejimenti, teknolojia duni na mitaji modogo zinazowakabili makandarasi wa ndani, Serikali imechukua hatua za makusudi za kuhamasisha kampuni za ndani kushiriki katika sekta ya ujenzi ili kukuza utaalamu na kuweza kushindana na kampuni za nje. Uwepo wa kampuni kubwa za kimataifa kwenye sekta ya ujenzi kunatoa fursa ya uhawilishaji wa teknolojia kuwezesha kampuni za ndani kukua na kupata fursa ya kunufaika na uhawilishaji wa teknolojia. Wakati huo huo, Serikali imeendelea kuchukuwa hatua madhubuti kudhiti vitendo vya rushwa katika sekta hii ili kuleta mazingira ya uwazi ambapo kampuni binafsi za ndani zitakuwa na uwezo wa kukua.

Sekta ya Nishati ya Umeme: Katika kipinndi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili, uzalishaji wa nishati ya umeme umeongezeka na kufikia MW 1,602.3 mwaka 2019/20 kutoka MW 1,308 mwaka 2015/16; kiwango cha upotevu wa umeme kimepungua kutoka asilimia 19.0 mwaka 2015/16 hadi asilimia 16.4 mwaka 2019/20; na jumla ya vijiji 10,018 kati ya vijiji 12,317 vimeunganishwa umeme hadi Desemba 2020, sawa na asilimia 81.3, idadi ya wateja waliounganishwa katika gridi ya taifa ilifikia 2,766,745 mwaka 2020 kutoka 1,473,217 mwaka 2016. Kwa ujumla

kiwango cha upatikanaji wa umeme kiliongezeka kutoka asilimia 67.8 hadi asilimia 78.4 katika kipindi hicho. Takriban asilimia 99.6 ya wakazi wa maeneo ya mijini wanaweza kupata umemena upatikanaji wa umeme katika maeneo ya vijijini umeongezeka kutoka asilimia 49.3 mwaka 2016 kufikia asilimia 69.6 mwaka 2019/20. Moja ya sababu za ongezeko la upatikanaji wa umeme vijijini na idadi ya kaya zilizounganishwa katika mtandao wa umeme ni utekelezaji mzuri wa programu ya Wakala wa Umeme Vijijini (REA).

Kwa mujibu wa utafiti kuhusu upatikanaji na hali ya nishati uliofanyika Tanzania Bara mwaka 2019/20, chanzo kikuu cha nishati ya kupikia ni kuni (asilimia 63.5), kikifuatiwa na mkaa (asilimia 26.2), gesi (asilimia 5.1), umeme (asilimia 3), na vyanzo vingine (asilimia 2.2). Vile vile, utafiti unaonesha kwamba kuna ongezeko la matumizi ya nishati ya kisasa kwa taa ambapo mwaka 2020, takriban asilimia 36.3 ya kaya zote ilitumia umeme kama chanzo kikuu cha nishati kwa taa, ikilinganishwa na asilimia 25.1 mwaka 2016, ikifuatiwa na umeme wa jua unaotumiwa na asilimia 30.4 ya kaya, na betri zinazochaji/tochi (asilimia 23). Matumizi ya vyanzo asilia vya nishati ya taa kama vile mafuta ya taa yamepungua kutoka asilimia 22.3 mwaka 2016/17 hadi asilimia 6.4 mwaka 2019/20. Asilimia 4 ya kaya wanatumia vyanzo vingine vya nishati kwa taa.

Sekta ya Madini: Sekta ya Madini imekua kwa wastani wa asilimia 8.0 kati ya mwaka 2016 na 2019; mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa kufikia asilimia 5.2 mwaka 2019/20 kutoka asilimia 4.6 mwaka 2015/16 na kuimarika kwa huduma kwa jamii zinazozunguka migodi. Aidha, mapato ya fedha za kigeni kutokana na mauzo ya madini yaliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 1,912 (sawa na shilingi bilioni 4,464.71) mwaka 2015/16 hadi dola za Marekani milioni 2,898.8 (sawa na shilingi bilioni 6,769.0) mwaka 2019/20; na maduhuli kutoka shilingi bilioni 196 mwaka 2015/16 hadi kufikia shilingi bilioni 528.3 mwaka 2019/20. Hali hii ya kuongezeka kwa mchango wa sekta ya madini unatokana na uambuzi wa serikali kupitia na kutunga Sheria, Sera na kupitia mikataba ya madini. . Kati ya jitihada zilizofanyika ni pamoja na kuanzishwa kwa Kampuni mpya ya Twiga Minerals Corporation inayomilikiwa kwa ubia kati ya Tanzania (hisa asilimia 16) na Kampuni ya Barrick (hisa asilimia 84) ambapo imetoa gawio la shilingi bilioni 100; kusainiwa kwa mkataba wa ubia wa kampuni ya LZ NICKEL na Serikali ya Tanzania kwa ajili ya kuendeleza na kuchimba madini ya Nickel ambapo chini ya mkataba huo imeundwa kampuni ya ubia inayoitwa Tembo Nickel Corporation Limited (kwa umiliki wa hisa asilimia 84 kwa Kampuni ya LZ Nickel na Serikali ya Tanzania Hisa asilimia 16); kujengwa kwa masoko 39 ya madini na vituo 41 vya kuuzia madini; kukamilika kwa ujenzi wa vituo vinne (4) vya umahiri katika maeneo ya Bariadi, Musoma, Bukoba na Handeni na kuendelea na ujenzi wa vituo vya Songea, Mpanda na Chunya; kuimarishwa kwa ulinzi wa rasilimali za madini

kwa kujenga ukuta wenye mzingo wa kilomita 24 wa Mirerani mkoani Manyara pamoja na kujenga One Stop Centre, kufunga vifaa vya ulinzi ikiwa ni pamoja na taa na CCTV Camera kuzunguka ukuta na barabara ya kuzunguka ukuta wa ndani; kuimarisha taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kuzipatia vitendea kazi; na kukamilisha ujenzi wa vituo vitatu (3) vya mfano vya uchenjuaji wa madini ya dhahabu kwa ajili ya wachimbaji wadogo katika maeneo ya Lwamgasa (Geita), Katente (Bukombe) na Itumbi (Chunya).

Kwa upande wa ajira, kati ya mwaka 2016/17 na 2019/20 sekta ya madini iliajiri watu 1,000,505 ambapo ajira 809,696 sawa na asilimia 80.9 niza moja kwa moja. Sekta ndogo ya wachimbaji wadogo wadogo na uchimbaji mdogo wa madini iliajiri watu milioni 1.5 katika maeneo ya vijijini. .na hivyo kuchangia sio tu kuongeza kipato cha kaya, bali pia kuunga mkono jitihada za Serikali za kupunguza umaskini hususan katika maeneo ya vijijini.

Sekta ya Biashara: Kwa upande wa biashara kuna ongezeko la mchango wa mauzo nje kwa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kutoka kiwango cha kizio (baseline) cha asilimia 12 mwaka 2015 kufikia asilimia 14 mwaka 2019. Mchango wa mauzo nje kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulipungua kutoka asilimia 16.0 mwaka 2015 hadi asilimia 12.3 mwaka 2019. Kwa ujumla, mwenendo wa biashara kati ya Tanzania na nchi za EAC na SADC katika kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka 2015 hadi 2019 yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka hivyo kuifanya Tanzania kuwa na Urari Chanya wa Biashara. Mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda nchi za EAC yaliongezeka kutoka dola za marekani milioni 430.6 mwaka 2016 hadi dola za Marekani na 674.4 mwaka 2019. Kwa upande wa SADC, mauzo ya Tanzania yaliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 1,112.7 mwaka 2016 hadi dola za Marekani 1,350.9 mwaka 2019. Thamani ya mauzo kwenda nchi za SADC yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na mauzo ya madini kwa wingi ambayo yana thamani kubwa ukilinganisha na bidhaa zingine za viwandani. Bidhaa zinazoongozwa kuuzwa katika nchi za SADC ni pamoja na dhahabu, sabuni, sigara, chokaa, vipodozi, chupa za kioo, unga wa ngano, saruji, mafuta ya kupakaa, magunia ya sandarusi (jute bags), vyandarua, fulana, kahawa ghafi, vyombo vya plastiki, vilainishi vya magari, pamba, madaftari, tumbaku, nywele za bandia (wigs), mabomba ya chuma, marumaru, chai ghafi, korosho. Kwa upande wa EAC, bidhaa zinazoongoza kuuzwa kwenda nchi za EAC ni pamoja na mahindi, karatasi, chai ghafi, vipodozi (mafuta ya kujipaka), mabati, magunia ya sandarusi (Jute Bags), vilainishi vya magari, vipodozi, saruji, vitunguu, ng'ombe, chupa za kioo, mashudu, unga wa ngano, marumaru, kamba za mkonge, makaa ya mawe, fulana (T-shirt), chumvi, taulo za watoto (baby diaper), vyandarua, mchele, lebo za karatasi, konyagi na vyombo vya nyumbani (plastics na aluminium).Mafanikio mengine ni pamoja na ongezeko la mauzo ya bidhaa za viwandani kutoka asilimia 6.3 mwaka 2016 kufikia

asilimia 10.8 mwaka 2019 ambalo ni ongezeko la nukta asilimia 3 zaidi ya lengo la Mpango wa Pili la asimilia 7.

Sekta ya Utalii: Idadi ya watalii walioingia nchini kutoka watalii 1,137,182 mwaka 2015 hadi 1,527,230 mwaka 2019. Aidha, wastani wa idadi ya siku zinazotumiwa na watalii kukaa nchini zimeongezeka kufikia siku 13 mwaka 2019 ikilinganishwa na siku 10 mwaka 2015. Mafanikio yalipatikana pia katika kiashiria cha Mpango wa Pili cha "mapato ya utalii" ambapo mapato yatokanayo na utalii yameongezeka kutoka dola za arekani bilioni 1.9 (sawa na shilingi bilioni 4,436.7) mwaka 2015 hadi dola za Marekani bilioni 2.6 (sawa na shilingi bilioni 6,071.3) mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 36.8. Hata hivyo kutokana na janga la UVIKO-19 (COVID-19) mapato ya utalii yanatarajiwa kupungua kwa kiasi kikubwa hivyo kuna uwezekano wa kutofikiwa kwa lengo la Mpango wa Pili la dola za Marekani bilioni 3.6. Pamoja na kupungua kwa mapato ya watalii, watalii waliotembelea mambo ya kale na Halmashauri za wilaya mwaka 2016, uchambuzi wa mwaka 2019, unaonesha kwamba kulikuwepo na ongezeko la mapato kufikia Dola za Marekani Milioni 186, ikiwa ni ongezeko la asimilia 19.2 zaidi ya kiwango cha msingi cha Dola milioni 156 (2015).

Sekta ya Viwanda: Mpango wa Pili uliainisha ujenzi wa viwanda sanjari na maendeleo ya watu na kuimarisha utekelezaji kama malengo makuu ya kisera na pia kama vichocheo vya mageuzi ya kiuchumi. Mwaka 2016 Serikali iliandaa Mpango Kazi wa viwanda kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Pili. Mpango huo uliweka mkazo katika matumizi ya rasilimali na malighafi za ndani na kuweka mazingira wezeshi kwa uwekezaji wa sekta binafsi katika viwanda na pia kuvutia uwekazi kutoka nje. Jumla ya viwanda vipya 8,477 kati ya mwaka 2015 – 2019 vilijengwa ambapo viwanda vikubwa ni 201, vya kati 460, vidogo 3,406 na vidogo sana 4,410. Katika mwaka 2019/20 pekee, viwanda 303 vilianzishwa, kati ya hivyo vikubwa vilikuwa 138 ambapo viwanda 95 vilianzishwa kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania. Ujenzi wa viwanda hivyo umeongeza idadi ya viwanda nchini kutoka 52,633 mwaka 2015 hadi viwanda 61,110 mwaka 2019. Kuongezeka kwa mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa kutoka asilimia 7.9 mwaka 2015 hadi asilimia 8.5 mwaka 2019; kukua kwa sekta ya uzalishaji viwandani kwa wastani wa asilimia 8.3 kwa mwaka kumechangia kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani ikijumuisha saruji, marumaru, nondo na bati; kuzalishwa kwa fursa za ajira kutoka ajira 254,786 mwaka 2015 hadi ajira 482,601 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 47.2; na kuchangia katika mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi kutoka asilimia 13.8 mwaka 2016/17 hadi asilimia 14.2 mwaka 2019/20. Kwa ujumla mpaka Septemba 2020, Serikali ilifanikiwa kufikia asilimia 75 ya malengo iliyojiwekea mwaka 2015/16.

Katika kusukuma ajenda ya viwanda, Serikali ilitoa wito kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kushiriki kwa kugharamia ufufuaji wa viwanda ambavyo vilisimamisha uzalishaji muda mrefu na kuwekeza katika viwanda vipya. Kwa kuitikia wito huu, zaidi ya viwanda 35 viligharamiwa kupitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na hivyo kuzalisha ajira ya watu 250,000. Viwanda vikubwa vilivyoanzishwa ni pamoja na:

(a) Uwekezaji wa shilingi bilioni 54 katika kiwanda cha viatu Moshi kwa kushirikiana na TIRDO na iliyokuwa Mfuko wa Pensheni ya Mashirika ya Umma (PPF);

(b) Mradi wa ubia wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) wa ujenzi wa kiwanda cha sukari Mkulazi Morogoro chenye uwezo wa kuzalisha tani 200,000 za sukari kwa mwaka katika gereza la Mukulazi Morogoro;

(c) Mkopo wa NSSF wa shilingi bilioni 9 kufufua kiwanda cha usagishaji nafaka Mwanza; na shilingi bilioni 4.7 kwa ajili ya kupanua kiwanda cha Shirika la Maendeleo la Taifa -NDC cha Biotech Product Kibaha; na

(d) Zaidi ya shilingi bilioni 339 zimewekezwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika viwanda 12 na katika shughuli nyinginezo.

2.4 Maendeleo ya Rasilimali Watu na Huduma za Jamii

2.4.1 Elimu

Utekelezaji wa Mpango wa Pili kwenye sekta ya elimu ulihusisa, ujenzi wa miundombinu muhimu katika shule 3,904 (Msingi 3,021 na Sekondari 883), mabweni 547, nyumba za walimu 101, majengo ya utawala 25 na maktaba 43; kukamilika kwa ujenzi wa maboma 2,815 katika shule za msingi 2,133; kukarabatiwa shule kongwe 84 kati ya 89; kuboreshwa kwa miundombinu ya vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi (Folk Development Colleges - FDC). Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili Serkali imeweza kuongeza idadi ya madarasa kutoka 115,665 mwaka 2015 hadi kufikia 136,292 mwaka 2020; madawati kutoka 3,024,311 hadi 8,095,207; na shule za msingi kutoka 16,899 mwaka 2015 hadi 18,158 mwaka 2020. Vilevile, idadi ya shule za sekondari imeongezeka kutoka 4,708 mwaka 2015 hadi kufikia shule 5,402 mwaka 2020. Aidha, Serikali iliendelea kutoa mikopo ya elimu ya juu ambapo jumla ya shilingi trilioni 2.26 zilitolewa; kuendelea kugharamia posho ya madaraka kwa walimu wakuu, fidia ya ada kwa wanafunzi na ruzuku ya uendeshaji wa shule ambapo shilingi trilioni 1.22 zilitolewa kwa ajili ya kugharamia elimumsingi bila ada; kuanzishwa kwa vituo vya umahiri vya mafunzo katika taasisi za elimu ya ufundi; na kuimarishwa kwa vyuo vya ufundi na vyuo vikuu. Pia, shule 1,696 zimezipatiwa vifaa vya maabara vya masomo ya sayansi. Kati ya hizo shule 1,625 ni za wananchi (maarufu kama Shule za Kata) na 71 ni shule kongwe.

Kwa ujumla, tathmini inabainisha kuwa utekelezaji wa Mpango wa Pili umechangia: kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na mafunzo ya ufundi stadi kutoka 196,091 mwaka 2015/16 hadi 320,143 mwaka 2019/20 na elimu ya ufundi kutoka 117,067 mwaka 2015/16 hadi 151,379 mwaka 2019/20; kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu nchini kutoka 65,064 mwaka 2015/16 hadi kufikia 87,813 mwaka 2019/20; na kuongezeka kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kutoka wanafunzi 125,126 mwaka 2015 hadi kufikia 132,392 mwaka 2020. Aidha, kiwango cha ufaulu wa mitihani ya Darasa la Saba kimeongezeka kutoka asilimia 67 mwaka 2015 hadi asilimia 81.5 mwaka 2019 na Sekondari (Kidato cha nne) kutoka asilimia 68 mwaka 2015 hadi asilimia 80.7 mwaka 2019. Vile vile, wanafunzi waliohitimu elimu ya juu walifikia 60,940 mwaka 2019/20, elimu ya mafunzo stadi 90,849 mwaka 2018/19 na elimu ya ufundi 86,547 mwaka 2019/20. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, kiasi cha shilingi trilioni 3.15 zimetumika kwa ajili ya kuboresha sekta ya elimu. Viashiria vya sekta ya elimu ni kama ifuatavyo:

Uandikishaji wa Jumla wa Wanafunzi: Uandikishaji wa Jumla wa Wanafunzi (Gross Enrolment Ratio - GER) kwa elimu ya awali ulishuka kutoka asilimia 112 mwaka 2016 kufikia asilimia 76.2 mwaka 2020. Ushukaji huu ulitokana na kupungua kwa idadi ya watoto waliokuwa na sifa za kujiandikisha. Uandikishaji wa Jumla wa Wanafunzi (GER) kwa elimu ya msingi imekuwa ikiongezeka mfululizo kila mwaka kuanzia mwaka 2016 na kufikia asilimia 107.4 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 93 mwaka 2016. Vilevile, mwaka 2020, uwiano wa wanafunzi wa kike na kiume (GPI) ulikuwa 1.01 ikimaanisha kwamba idadi ya wanafunzi wa kike na kiume ni karibu sawa elimu ya msingi. Kuhusu elimu ya sekondari ngazi ya chini Uandikishaji wa Jumla wa Wanafunzi (GER) ulionesha ongezeko kutoka asilimia 36 mwaka 2016 hadi asilimia 43.9 mwaka 2020. Ongezeko hili linamaanisha kwamba wanafunzi wengi zaidi wanafuzu elimu ya msingi na kuingia sekondari. Kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi kwa elimu ya msingi na sekondari kulitokana na utekelezaji wa sera ya elimumsingi bila ada.

***Uandikishaji wa Rika Lengwa*:** Uandikishaji wa Rika Lengwa (NER) katika elimu ya awali ulipungua kutoka asilimia 44.6 mwaka 2016 hadi asilimia 38.7 mwaka 2019. Uandikishaji wa Rika Lengwa (NER) kwa wasichana ulikuwa asilimia 40.3 ikiwa ni juu ya wavulana ambao ulikuwa asilimia 39.6 kama inavyonekana katika Kielelezo Na. 1. Hii inamaanisha uwepo wa usawa wa kijinsia katika uandikishaji wa wanafunzi katika elimu ya awali. Uandikishaji mkubwa wa wanafunzi mwaka 2016 ulitokana hasa na sera ya Serikali ya elimumsingi bila ada kwa elimu ya msingi na sekondari.

Vilevile, Uandikishaji wa Rika Lengwa (NER) katika elimu ya msingi Uliongezeka kutoka asilimia 84 mwaka 2016 hadi asilimia 95.4 mwaka 2019 ukimaanisha kuwa ushiriki mkubwa wa rika lengwa kwenye elimu ya msingi. Huu ni uandikishaji mkubwa unaoonesha kwamba jitihada za Serikali na wadau wengine wa elimu za kuboresha upatikanaji wa elimu ya msingi na usawa wa kijinsia zilizaa matunda. Hata hivyo, idadi kubwa ya Wanafunzi walisajiliwa katika shule za Serikali, ingawa kuna ongezeko la usajili katika shule Serikali na binafsi. Kuhusiana na elimu ya sekondari ngazi ya chini, Uandikishaji wa Rika Lengwa (NER) uliongezeka kutoka asilimia 33.3 mwaka 2016 hadi asilimia 34.8 mwaka 2019.

Kielelezo Na. 1 Uandikishaji wa Wanafunzi kwa Elimu ya Awali katika Shule za Serikali na Binafsi kwa Kuzingatia Jinsia, 2014-2018



Chanzo: ESPR 2017/18

Uwiano Kati ya Wanafunzi na Walimu (PTR): Uwiano sahihi wa wanafunzi na walimu kwa elimu ya awali ni 1:25. Aidha, kutokana na uandikishaji mkubwa wa wanafunzi uwiano huu ulikuwa 1:114 mwaka 2016 na kupungua kidogo hadi uwiano wa 1:104 mwaka 2020. Mafanikio haya yanatokana na jitihada ya kuongeza walimu wa elimu ya awali kutoka waalimu 10,991 mwaka 2018 hadi walimu 13,227 mwaka 2020. Uwiano katika elimu ya msingi uliongeza kutoka 1:42 mwaka 2016 na kufikia 1:56 mwaka 2020. Hali hii ilisababishwa na kupungua kwa idadi ya walimu kwa asilimia 5.8 kutoka waalimu 206,806 mwaka 2016 hadi walimu 194,736 mwaka 2020. Hata hivyo, hali hii inatarajiwa kuimarika kutokana na kuajiriwa kwa walimu wapya 13,000 Oktoba 2020.

Elimu ya Sekondari kwa Wote: Serikali iliamua elimu ya sekondari ngazi ya chini kuwa ni elimu kwa wote. Uamuzi huu unaendana na Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu kwa Tanzania Bara (ESDP) 2016/17-2020/21. Mpango huu ulilenga kuboresha sekta ya elimu ili iwe na ufanisi zaidi na kulenga matokeo chanya ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora kwa wote na kwa usawa, wakiwepo wanafunzi wenye changamoto maalumu, ili kuendana na lengo Na. 10 la Malengo ya Maendeleo Endelevu. Vipaumbele vya Mpango huu ni pamoja na

ushiriki sawa bila ada, mkazo ukiwekwa kwa makundi yenye changamoto zaidi katika jamii, watoto wenye ulemavu na watoto walioshindwa kujiunga katika mfumo rasmi wa elimu ya msingi. Lengo ni kuhakikisha watoto wote wanapata elimu ya miaka 12 kupitia mpango huu wa elimu kwa wote kwa elimu ya sekondari ngazi ya chini.

Matokeo ya jitihada hizi ni kuwa Uandikishaji wa Jumla wa Wanafunzi iliongezeka kutoka asilimia 30.1 mwaka 2016 hadi asilimia 31.0 mwaka 2018; na Uandikishaji wa Rika Lengwa kutoka asilimia 27.0 mwaka 2016 hadi asilimia 31.0 mwaka 2018. Hii inamaanisha uwepo wa mafanikio katika kupunguza utoro shuleni na idadi ya wanafunzi wanaoacha shule. Aidha, utekelezaji wa sera ya elimu kwa wote imeimarisha utoaji elimu kwa watoto wa kike na kiume katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili.

Elimu ya Ufundi, Ufundi Stadi na Elimu ya Kati: Mpango huu unatoa nafasi ya mafunzo ya ziada baada ya kumaliza elimu ya msingi na ya sekondari ngazi ya chini na ngazi ya juu. Lengo lake ni kuandaa mafundi mchundo, mafundi stadi na wataalamu katika nyanja za ujenzi, uzalishaji viwandani, kilimo, madini, usafirishaji, nishati na teknolojia ya habari na mawasialiano. Kuna mamlaka mbili za usimamizi wa taasisi za elimu ya kati na ufundi. Mamlaka hizi ni Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ambalo linasimamia ubora wa elimu katika vyuo vya ufundi (ukiondoa Vyuo Vikuu) na Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ambayo inasimamia ubora wa elimu ya ufundi stadi.

Kufikia Januari 2019, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi lilikuwa limesajili vyuo vya ufundi 540 ambavyo, kwa mwaka 2018/19, vilikuwa na uwezo wa kudahili jumla ya wanafunzi 254,172. Hadi sasa, idadi ya vyuo vya ufundi stadi nchini ni 603 ambapo vyuo 28 viko chini ya Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi na vina wanafunzi 34,326 na Vyuo 575 viko chini ya taasisi nyingine zinazotoa mafunzo ya ufundi stadi. Vyuo vilivyosajiliwa na VETA vina uwezo wa kupokea jumla ya wanafunzi 222,680. Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi - FDCs, kwa sasa vinafikia 55, vikifundisha programu mbalimbali za elimu ya ufundi. Vyuo hivi vinawapa wanafunzi elimu na stadi muhimu ili waweze kujiajiri na kujitegemea na kutatua matatizo yanayojitokeza katika jamii. Vyuo vinatoa elimu ya ufundi na stadi muhimu katika maeneo ya kilimo, ufundi useremala, uashi, utengenezaji magari, ushonaji wa nguo, mapishi, ufugaji na umeme. Kwa sasa kuna mafundi mchundo 5,783 waliopitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa kushirikiana na wadau wengine.

Serikali imechukua hatua kadhaa ikiwemo kukarabati, kuimarisha na kupanua miundombinu ya vyuo vya ufundi viliyopo. Lengo likiwa ni kuboresha elimu, kuongeza wigo na kuleta usawa katika upatikanaji wa elimu ya ufundi. Katika bajeti ya mwaka 2019/20 Serikali ilitenga fedha za ujenzi wa vituo 25 vya ufundi stadi katika wilaya mbalimbali. Vile vile, Serikali inatekeleza mradi wa vituo vya umahiri katika ngazi za ufundi na ujenzi na ukarabati wa vyuo 54 vya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Kukuza Ujuzi: Utafiti kuhusu hali ya soko la ajira uliofanywa na iliyokuwa Tume ya Mipango mwaka 2014 kuhusu *Maendeleo ya Ujuzi Utakaoiwezesha Tanzania Kuwa na Uchumi Imara na Shindani Ifikapo mwaka 2025* inabainisha umuhimu wa kutatua changamoto ya tofauti kati ya ujuzi unaohitajika katika soko la ajira na ujuzi unaotolewa na taasisi za elimu na mafunzo. Utafiti ulibanisha kuwa viwango vya ujuzi vya watafuta ajira viko chini ya kiwango kinachohitajika na waajiri. Vile vile, utafiti umebaini kuwa watafuta ajira wengi wanaupungufu wa ujuzi katika stadi za kazi ikijumuisha uwezo mdogo katika mawasiliano, kutokujiamini, kukosa ubunifu, kutokujituma katika kutatua changamoto, udhaifu katika uongozi na uwezo mdogo wa kutumia nadharia katika vitendo, matumizi mabaya ya muda, kutokumjali mteja na kukosa mtazamo chanya wa kufanya kazi kwa kushirikiana na wengine.

Utafiti huo ulianisha ujuzi unaohitajika kufikia malengo ya mipango ya maendeleo kwa muktadha wa Mpango Elekezi wa Muda Mrefu – LTPP wa kujenga uchumi wa viwanda na shindani. Aidha, utafiti ulianisha uzoefu kutoka nchi zilizofanikiwa ikiwemo India, Afrika Kusini, Malaysia na Singapore kuhusu kazi zitakazoiwezesha Tanzania kufikia lengo la uchumi wa kipato cha kati kabla ya mwaka 2025. Yafuatayo ni mambo muhimu yaliyojitokeza katika na utafiti huu:

(i) Ukuzaji ujuzi unapaswa kuwa endelevu kutoka ngazi ya awali ya elimu ili kuandaa vijana kwa ajili ya elimu ya juu na ufundi stadi ili waweze kuajiriwa na kujiajiri pamoja na kuzalisha ajira;

(ii) Katika kuziba pengo la upungufu wa ujuzi katika stadi za kazi, nchi inatakiwa iwekeze mara tano zaidi katika kuongeza ujuzi katika ngazi za juu za ajira ikiwemo (meneja, wataalamu na mafundi sanifu) zaidi ya kada ya kati ambayo ni karani, wahudumu, mafundi mchundo, wafanyabiashara na maafisa ugani mara wanaotakiwa kuongezwa mara tatu zaidi, kwa wastani;

(iii) Takribani asilimia 80 ya kazi nchini zinahitaji ujuzi katika Hisabati na Sayansi wakati mwenendo wa udahili katika masomo hayo ni wa kiwango cha chini ikilinganishwa na udahili katika masomo ya Sayansi ya Jamii. Hivyo, kuna umuhimu wa Serikali kuongeza ugharamiaji katika masomo hayo na kuhamisisha udahili katika masomo ya hisabati, sayansi asilia, udaktari na uhandisi;

(iv) Licha ya umuhimu wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi katika kujiajiri, katika miaka ya hivi karibuni, udahili katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ni wa kiwango cha chini ikilinganishwa na udahili unaoongezeka kwa kasi katika ngazi ya elimu ya juu. Hata hivyo, kati ya elimu ya vyuo vikuu na vyuo vya ufundi stadi, changamoto ya upungufu wa ujuzi katika stadi za kazi imeendelea kuwepo ambayo inahitaji kutatuliwa kwa kutumia tafiti za waajiri;

(v) Uchambuzi wa mwenendo wa ajira kupitia tafiti rasmi za kazi na ajira, tafiti za waajiri na tafiti za ufuatiliaji wa ujuzi unaotolewa katika taasisi za mafunzo zinabainisha kuwa sekta binafsi inazalisha fursa nyingi za ajira zaidi ya sekta ya umma. Hatua mahsusi zinapaswa kuchukuliwa kwa lengo la kuziba pengo la kujiajiri kupitia vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kufikia lengo la Mpango la kuzalisha fursa za ajira milioni nane (8);

(vi) Kuna umuhimu wa kuanzisha vyuo vingi vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, na kuimarisha ufundishaji katika vyuo hivyo ikijumuisha kuboresha mitaala, mazingira ya kujifunzia na kufundishia pamoja na vifaa;

(vii) Hatua za kuboresha mazingira ya kufanya biashara sanjari na kuboresha mfumo wa upatikanaji wa mitaji pamoja na msaada wa kitaalamu katika ujuzi wa usimamizi wa biashara utawezesha wahitimu wa mafunzo ya ufundi stadi kuanzisha biashara zitakazozalisha ajira. Hatua hizo zitakuwa na matokeo chanya katika kuwavutia wafanyabiashara katika sekta isiyo rasmi kurasimisha biashara zao na hivyo kuongeza ukubwa wa sekta rasmi yenye matokeo kuzalisha fursa za ajira; na

(viii) Ni muhimu kuhamasisha vyuo vya elimu ya ufundi, mafunzo ya ufundi stadi na taasisi za elimu ya juu kufanya tafiti za kufuatilia utendaji wa wahitimu wa vyuo hivyo katika maeneo ya kazi, kuboresha mahusiano ya karibu na waajiri hususan sekta binafsi, kwa kuwa sehemu kubwa ya fursa za ajira zinapatikana. Tafiti hizo zitasaidia taasisi hizo kuboresha mitaala kulingana na mahitaji ya soko la ajira.

Uwiano wa watu wanaoingia katika soko la ajira wakiwa na ujuzi kutoka vyuo vya elimu ya ufundi, umeendelea kuongezeka kutoka asilimia 1 mwaka 2007 hadi asilimia 3 mwaka 2016. Hata hivyo, idadi ya watu waliokuwa wanataaluma wenye ujuzi mkubwa iliendelea kuwa ndogo (asilimia 3.3) ukilinganisha na lengo la taifa la asilimia 12. Mahitaji ya soko la ajira na kiwango cha ujuzi kinachopatikana katika vyuo vya elimu ya juu haviwiani. Mitaala ya vyuo vya elimu ya juu mingine imepitwa na wakati, mingine haina ulinganifu wa moja kwa moja na soko la ajira na na haitoshelezi mahitaji ya soko. Sekta binafsi imeonesha dhamira ya kushirikiana na Serikali katika kuziba pengo la ujuzi kwa kutumia majukwaa ya kijamii ya uwekezaji.

Uhamaji wa nguvukazi (kutoka kazi moja kwenda kazi nyingine na mwajiri mmoja kwenda kwa mwingine) ya nchi unakabiliwa na changamoto ya kiwango kidogo cha ujuzi. Nguvu kazi kubwa ya nchi ina kiwango kidogo cha ujuzi ikilinganishwa na kiwango kinachohitajika kufikia maendeleo endelevu ya viwanda. Uhitaji wa kiwango cha juu cha ujuzi unaongezeka katika sekta zote za uchumi. Ili kuziba pengo la ujuzi na uwiano kati ya wahitimu wa vyuo na mahitaji ya soko, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine iliandaa Programu ya Kitaifa ya Kukuza Ujuzi ili na mfumo kuinua viwango cha ujuzi na kuwezesha wahitimu wa vyuo kuajirika.

Kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi, wastani wa vijana 42,407 walio katika soko la ajira, wanapata mafunzo ya ujuzi mbalimbali (Apprentieship, Internship and Recognition of Prior Learning) kila mwaka. Programu hii imejikita katika sekta za kipaumbele za uzalishaji viwandani, huduma, nguo, ngozi, kilimo, ujenzi na TEHAMA. Vile vile, Serikali imeendelea kutoa ruzuku kupitia utaratibu wa '*Trainee Voucher Scheme*' ambapo vijana 7,000 walisaidiwa kupata mafunzo ya ufundi stadi na pia kuhakikisha kuwa miongozo ya mafunzo kazini na ufundi mchundo imeandaliwa kwa ajili ya Serikali na sekta binafsi.

Kuwezesha Vijana: Hatua kadhaa zilichukuliwa kuhakikisha vijana wanawezeshwa kiuchumi. Hii ni pamoja na kutoa mafunzo ya ujasiriamali, uendeshaji wa biashara na urasimishaji wa kampuni za biashara, kwa vijana 28,390. Vile vile, mikopo ya masharti nafuu yenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 32.6 ilitolewa kwa vikundi 2,560 vya vijana. Aidha jumla ya wakufunzi 78 walipata mafunzo ya stadi za maisha kwa ajili ya makuzi mazuri ya vijana. Kupitia wakufunzi hawa vijana 12,500 walipata mafunzo ya stadi za maisha katika ngazi za wilaya. Mafunzo haya ni muhimu ili kuwaandaa vijana kujitambua, kuweka malengo ya maisha na kufanya maamuzi sahihi.

2.4.2. Sekta ya Afya

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, Serikali iliweza kuongeza idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya kutoka vituo 7,014 mwaka 2015 hadi kufikia vituo 8,783 Desemba 2020 ambapo Serikali imejenga Zahanati 1,198; Vituo vya Afya 487; Hospitali mpya 99 za Halmashauri; Hospitali 10 za Rufaa za mikoa ya Geita, Katavi, Simiyu, Njombe, Songwe, Mwanza, Shinyanga, Singida, Manyara, Arusha na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara - Kwangwa iliyosimama kwa kipindi cha kirefu. Serikali pia imeendelea na ujenzi wa Hospitali 3 za Rufaa za Kanda (Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – Mbeya, Kanda ya Kusini Mtwara na Hospitali ya Chato). Aidha, katika kipindi hiki, Serikali imekamilisha ujenzi wa wa jengo la wodi namba 18 ya Sewa Haji pamoja na ujenzi wa wodi za kulaza wagonjwa binafsi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, ujenzi

wa jengo la huduma za dharura na ukarabati wa jengo la X-ray katika Hospitali ya Rufaa Dodoma, kukamilika kwa asilimia 98.2 ya ujenzi wa Hospitali ya Uhuru – Dodoma; na kununua na kufunga vifaa vya kisasa katika vituo vya kutolea huduma. Viashiria vya sekta ya afya ni kama ifuatavyo:

Vifo vya Uzazi, Vifo vya Watoto Wachanga na Vifo vya Watoto Chini ya Umri wa Miaka 5: Kiwango cha vifo vya watoto chini na umri wa miaka mitano kimepungua kwa kiwango cha kuridhisha kikifuatiwa na kiwango cha vifo vya watoto wachanga. Kiwango cha idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano kilipungua kutoka wastani wa vifo 67 kwa vizazi hai 1000 mwaka 2014/15 hadi vifo 50.3 mwaka 2019/20; kupungua kwa vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua kutoka vifo 432 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2015/16 hadi vifo 321 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2019/20; na kuongezeka kwa watoto wanaozaliwa kwa kuhudumiwa na wahudumu wa afya wenye ujuzi kutoka asilimia 51 mwaka 2015/16 hadi asilimia 80 mwaka 2019/20. Aidha, wastani wa umri wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 62 mwaka 2015/16 hadi miaka 66 mwaka 2019/20. Tanzania imeendelea kuwa moja ya nchi za afrika zinazoongoza kwa kutoa chanjo kwa watoto chini ya umri wa mwaka mmoja. Mwaka 2019/20, asilimia 98 ya Watoto wote chini ya umri wa mwaka mmoja walipata chanjo ukilinganisha na asilimia 82 mwaka 2015/16 na hivyo kuvuka lengo asilimia 90 kilichowekwa na shirika la afya duniani (WHO).

Mwenendo wa Idadi ya Watu: Kiwango cha uzazi kilirekodiwa kuwa niwastani wa watoto 4.9 kwa mwanamke mmoja, mwaka 2019, kikipungua kutoka wastani wa watoto 5.2 mwaka 2016. Kiwango hiki kikubwa cha uzazi, kikiendana na kupungua kwa vifo, kinamaanisha kwamba Tanzania ina vijana wengi. Watoto wa umri wa miaka kati ya 0 -14 ni asilimia 44 ya idadi ya watu Tanzania. Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 ilibainisha kuwa uwiano wa utegemezi kuendana na umri ulikuwa 92, ikimaanisha kulikuwa na watu 100 wenye umri kati ya miaka 15 - 64 ambao walitegemeza watu 92 wenye umri wa miaka kati ya 0 – 14 na wa umri wa miaka 65 na zaidi. Utegemezi mkubwa wa watoto unaongeza mzigo kwenye uchumi na kuathiri tija katika uzalishaji. Wazazi wenye Watoto wengi wanahangaika katika utoaji wa mahitaji ya afya, elimu na mahitaji mengine ya watoto wao, hali hii inathiri ubora katika kizazi kijacho cha nguvukazi. Kiwango kikubwa cha uzazi vile vile kinahusishwa na viwango vidigo vya elimu kwa kina mama na ushiriki mdogo wa wanawake katika soko rasmi la ajira.

Nchi zenye kiwango kikubwa cha uzazi zina hangaika katika kutoa huduma bora za afya na elimu kwa watoto na hivyo rasilimali chache kwenye uendelezaji wa miundombinu na vichocheo vingine vya ukuaji wa kiuchumi. Kama ilivyoainishwa katika sera ya maendeleo ya watu ya mwaka 2006 na Mpango wa Pili, ongezeko kubwa la idadi ya watu na kiwango kikubwa cha utegemezi, ni sababu muhimu

zinazoathiri maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini Tanzania. Sera na Mpango zinainisha kwamba ongezeko kubwa la watu linadumaza ukuaji wa pato la taifa kwa kupunguza kasi ya mchakato wa kukuza mitaji na akiba ya rasimali kwa ajili ya uwekezaji katika uzalishaji. Msukumo ambao unasababishwa na kasi ya ongezeko la watu unaonekana bayana katika bajeti ya Serikali kwenye sekta za: afya, elimu na sekta nyingine za maendeleo ya rasilimali watu.

Kuenea kwa Udumavu na Ukondefu: Mkakati wa Taifa wa Lishe bora umeendelea kuongoza masuala ya lishe yanayolenga kupunguza aina zote za utapiamlo. Hali ya lishe kwa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano imeendelea kuboreshwa. Watoto wenye umri wa chini ya miaka 5 wenye uzito mdogo walipungua kutoka asilimia 13 mwaka 2014/15 hadi asilimia 10 mwaka 2019/20; wakati watoto waliozaliwa wakiwa na uzito chini ya kilo 2.5 ilipungua kutoka asilimia 6.5 mwaka 2014/15 hadi asilimia 5.6 mwaka 2019/20.

Maambukizi ya UKIMWI: Mwenendo wa maambukizi ya UKIMWI (HIV/AIDS) nchini unaonekana kupungua kufuatia mikakati bora ya kuzuia maambukizi, uhamasishaji wa programu za upimaji na ushauri nasaha pamoja na programu za kijamii zilizohimiza mabadiliko ya tabia

Matukio ya Kifua Kikuu: Ugonjwa wa Kifua Kikuu umeendelea kuwa moja ya sababu kubwa za vifo hapa nchini. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili, Serikali mashine za digital X-ray na ultrasound, vifaa vya maabara na mashine za uchunguzi wa kifua kikuu kwa kuotesha vimelea BACTEC 960 (Mycobacteria Growth Indicator Tube - MGIT) na Blood culture machine katika Hospitali ya Rufaa ya Magonjwa ya Kifua Kikuu – Kibong'oto. Huduma shirikishi za kifua kikuu na UKIMWI zimeboreshwa na upimaji wa virusi vya UKIMWI kwa wagonjwa wa kifua kikuu ulifikia asilimia 99 mwaka 2019/20 kutoka asilimia 93 mwaka 2014/15. Katika mwaka 2019/20 asilimia 92 ya wagonjwa wa kifua kikuu walipata matibabu na kupona ikilinganishwa na asilimia 90 ya waliotibiwa na kupona mwaka 2014/15.

Matukio ya Malaria: Vifo vya malaria kwa rika zote vimepungua kwa asilimia 67 kutoka vifo 6,311 mwaka 2015 hadi 2,079 mwaka 2019. Kati ya vifo 2,079 vya malaria vilivyotokea mwaka 2019, vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano, vilikuwa 957, sawa na asilimia 46 ya vifo vyote vilivyosababishwa na ugongwa wa malaria. Watu waliopimwa na kuonekana kuwa na malaria waliongezeka katika kipindi cha miaka ya 2015 na 2019 kutokana na kuwepo kwa vifaa vya utambuzi hususan kifaa cha kupima na kugundua malaria kwa haraka (MRDTs). Kuanzishwa kwa mpango wa huduma za malaria na uboreshaji wa takwimu (MSDQI) umeongeza utendaji wa vituo vya kutolea huduma za afya kwenye viashiria vya malaria.

2.4.3 Mpango wa Bima za Afya

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, kwa mwaka 2019/20, Tanzania ilikadiriwa kuwa na idadi ya watu milioni 55.9. kwa mujibu wa makadirio hayo, Asilimia 33 ya Watanzania, wanatumia Mfumo wa Bima ya Afya ambapo, asilimia 25 ni wanufaika wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), asilimia 7 ni wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na asilimia 1 ni wa Bima Binafsi. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili, jumla ya wanufaika wa mifuko hii miwili kwa pamoja waliongezeka kutoka asilimia 20 mwaka 2015 hadi asilimia 33 mwaka 2019. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umeendelea kuwa nyenzo muhimu ya kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wote. Idadi ya wanachama wa mfuko iliongezeka kutoka 753,892 mwaka 2016/17 kufikia wanachama 858,446 mwaka 2017/18 na kuendelea kuongezeka hadi wanachama 966,792 mwaka 2018/19.. Kufikia mwaka 2019 mfuko wa Afya ya Jamii ulihusisha wanufaika 13,029,636 sawa na asilimia 25 ya watanzania wote. Tanzania inafanya mapitio ya Sheria ya Bima ya Mwaka 2019 kwa lengo la kuanzisha mfuko mmoja wa bima ya afya na hivyo kuondokana na mfumo wa mifuko hii miwili ya bima ya afya.

2.4.4 Upatikanaji wa Maji Safi na Salama na Uboreshaji wa Usafi wa Mazingira

Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi Desemba, 2020, Serikali imekamilisha jumla ya miradi 1,845 ambapo miradi 1,623 ipo katika maeneo ya vijijini na miradi 222 ni ya mijini. Aidha, Serikali inaendelea kutekeleza jumla ya miradi 991 ambapo miradi 881 ni ya vijijini na miradi 110 ni ya mijini. Hadi kufikia Desemba 2020, jumla ya miradi ya maji 1,423 ilijengwa na ilikuwa na jumla ya vituo vya kuchotea maji 131,370 vinavyonufaisha watu 25,359,290 sawa na asilimia 70.1 ya idadi ya watu vijijini. Hata hivyo, katika kipindi cha mwezi Disemba, 2019 hadi Januari, 2020, jumla ya vituo vya maji 3,493 vilikuwa havitoi maji kutokana changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na kukauka kwa vyanzo, kuharibika kwa miundombinu ya kuzalisha nishati na hujuma katika miundombinu. Baada ya marekebisho ya miradi ya maji, jumla ya vituo vya maji 2,348 vilifufuliwa na kuanza kutoa huduma ya maji kwa watu waliokusudiwa. Aidha, jumla ya vituo 1,145 vinaendelea kukarabatiwa na matarajiwa ni kukamilisha hadi kufikia mwezi Machi, 2021 kabla kukamilika kwa muda wa utekelezaji wa Mpango wa Pili. Kwa upande wa maeneo ya mijini, idadi ya watu wanaopata maji ya bomba au wanaopata maji kutoka katika vyanzo salama ilifikia asilimia 80. Tathmini imebainisha kuwa, uwekezaji katika sekta ya maji ukijumuisha Programu ya Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (RWSSP) unaonesha mabadiliko chanya.

2.5. Kupunguza Umaskini na Uwezeshaji Kiuchumi

2.5.1 Fahirisi ya Maendeleo ya Watu, Hali ya Umaskini na Tofauti za Kipato: Fahirisi ya maendeleo ya watu (HDI) imeboreshwa kutoka 0.52 mwaka 2015 hadi 0.528 mwaka 2018, juu ya wastani wa 0.507 kwa kundi la nchi za kiwango kidogo

cha maendeleo ya watu. Uchambuzi wa fahirisi hii kwa kuangalia vipengele vyake, ni wazi kwamba nchi imepiga hatua kubwa katika kuinua umri wa wastani wa kuishi kutoka miaka 63.1 mwaka 2015 kufikia miaka 66.0 mwaka 2019 na kuongeza kiwango cha kujua kusoma na kuandika ambapo miaka ya shule iliongezeka kutoka 5.3 mwaka 2010 kufikia 8.0 mwaka 2019; na wastani na miaka ya shule umeongezeka kutoka miaka 5.1 kufikia miaka 6.0 katika kipindi hicho. Fahirisi nyingine za maendeleo ya watu zinazoonesha mafanikio makubwa ni fahirisi ya usawa wa kijinsia ambapo kiashiria cha tofauti ya kijinsia kilipungua kutoka 0.556 mwaka 2013 kufikia 0.539 mwaka 2019; na fahirisi ya maendeleo ya jinsia inayoonesha tofauti iliyopo kati ya wanawake na wanaume ambayo imebakia katika kiwango cha takribani 0.936 katika kipindi cha miaka ya 2015 – 2019.

Hali ya Umaskini: Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS) unaonesha kuwa uwepo wa mahitaji muhimu umepungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 kufikia asilimia 26.4 mwaka 2017/18 wakati umaskini wa chakula ulipungua kutoka asilimia 9.7 mwaka 2011/12 kufikia asilimia 8.0 mwaka 2017/18. Haya ni matokeo ya juhudi endelevu za Serikali za kuboresha hali ya maisha, ustawi wa jamii, kupunguza umaskini na kuboresha maendeleo ya watu. Matokeo ya upatikanaji wa huduma za msingi na mali zinazotumika katika uzalishaji kama vile upatikanaji wa nishati, barabara unganishi, masoko na maji, na huduma za afya na elimu. Kama ilivyokuwa kwa tafiti zilizotangulia, uchambuzi wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya mwaka 2017/18 unaonesha kwamba hali ya umaskini wa mtu mmoja mmoja kwa mahitaji muhimu kwa maeneo ya vijijini Tanzania bara ipo juu sawa na asilimia 31.3 ukilinganisha na mijini sawa na asilimia 15.8.

Umaskini Upimwao kwa Vigezo Visivyo vya Kipato: Tanzania kama zilivyo nchi nyingine imejipanga kuandaa fahirisi ya umaskini wa kipato na usio wa kipato kwa ajili ya kutathmini viwango vya umaskini wa kipato na usio wa kipato kwa muktadha wa nchi ili kuwa na sera za kuondoa umaskini. Mbinu za kukokotoa fahirishi hiyo zimeandaliwa. Inatarajiwa kuwa taarifa ya Umaskini Upimwao kwa Vigezo Visivyo vya Kipato itakokotolewa na kuzinduliwa kwa kutumia takwimu za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya za mwaka 2017/18. Vile vile, lengo ni kuandaa maswali yatakayojumuishwa kwenye tafiti za taifa kwa ajili ya kuwezesha upimaji wa fahirisi hiyo kwa kipindi husika. Hatua hii itawezesha ufuatiliaji wa viashiria vitakavyochaguliwa na nchi kwa kipindi husika. Kwa msingi huo, kuwa na Umaskini Upimwao kwa Vigezo Visivyo vya Kipato katika vipindi tofauti katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu utawezesha kupima na kufuatilia viashiria vinavyohusu umasikini vitakavyojumuishwa katika mkakati wa ufuatiliaji na tahmini ya Mpango wa Tatu.

Tofauti za Kipato: Utafiti wa Matumizi na Mapato ya Kaya (2017/18) inaonesha kwamba kuna ongezeko la tofauti ya kipato. Kuongezeka kwa tofauti ya matumizi ya kipato kutokana na kipimo cha *Gini (*Gini Coefficient*)* kutoka 0.34 mwaka 2011/12 hadi 0.38 mwaka 2017/18. Ongezeko hili la tofauti ya kipato lilijitokeza vile vile katika maeneo mengine ya mijini kutoka 0.37 kufikia 0.38. Tofauti ya kipato kwa Dar es Salaam iliongezeka kutoka kipimo cha Gini cha 0.35 na kufikia 0.42 na katika maeneo ya vijijni iliongezeka kutoka kipimo cha Gini cha 0.29 na kufikia 0.32. Hii inaonesha kuwa, tofauti ya kipato ni kubwa zaidi kwa Dar es Salaam kwa kipimo cha Gini cha 0.42 ikilinganishwa na maeneo mingine mijini kipimo cha Gini cha 0.38 na maeneo ya vijijni yenye kipimo cha Gini cha 0.32. Hali hii ilisababishwa na watu wengi wa vijijini kuhamia Dar es Salaam kutafuta ajira za viwandani na maisha bora zaidi. Tofauti hii ya kipato imesababishwa na ukweli kwamba watu kutoka vijijini wanahamia Dar es Salaam kutumia fursa za maendeleo ya viwanda na kuongezeka kwa kipato. Jedwali Na. 3 linaonesha mwenendo wa tofauti za kipato Tanzania bara.

Jedwali Na. 3: Mwenendo wa Tofauti za Kipato Tanzania

Mwaka	Dar es Salaam	Miji Mingine	Vijijini	Tanzania Bara
1991/92	0.30	0.35	0.33	0.34
2000/01	0.36	0.36	0.33	0.35
2007	0.34	0.35	0.33	0.35
2011/12	0.35	0.37	0.29	0.34
2017/18	0.42	0.38	0.32	0.38

Chanzo: Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya 2017/18

Kuongezeka kwa tofauti za kipato kama ilivyoainishwa katika Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya unahitaji hatua za kina za kisera ambazo zinalenga kushinda nguvu za kimuundo ambazo zinaleta na kuendeleza tofauti ya kipato na juhudi za kuharakisha upunguzaji wa umaskini zinazotakiwa kuwa sehemu ya mchakato wa maendeleo.

2.5.2. Ukuzaji wa Ajira

Kutokana na mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2016/17 hadi mwaka 2020/21 jumla ya ajira 12,773,126 zimezalishwa. Kati ya ajira hizo, ajira za moja kwa moja ni 11,891,772 na ajira zisizo za moja kwa moja ni 881,354. Aidha, jumla ya vijana 65,008 katika kipindi cha mwaka 2017 hadi 2020 wamepatiwa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi ikiwemo mafunzo ya uanagenzi katika fani za ujenzi, useremala, umeme wa majumbani na viwandani, umeme wa jua, ufundi magari, ufundi bomba, utengenezaji wa vifaa vya aluminium, uchomeleaji na uungaji vyuma, kilimo na ufugaji, ushonaji, uchorongaji vipuli, uchapaji nyaraka na TEHAMA.

Aidha, kwa kutambua ukubwa wa tatizo la ajira na madhara yake, katika kipindi cha 2016/17 – 2018/19, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine ilitekeleza sera za kukuza ajira na programu na miradi ya kuwezesha vijana kuajiriwa na kujiajiri. Vile vile, Serikali iliongeza mgao wa fedha za mikopo kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa reli kwa kiwango cha kimataifa (SGR), ujenzi wa barabara, vituo vya afya 487 na hospitali 101, viwanja vya ndege; ujenzi wa miradi ya maji 1,423; na kuanzishwa kwa viwanda katika kila mkoa vimeongeza takribani 1,167,988 ajira mpya kwa kipindi kati ya mwaka 2016 na 2019 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4.

Jedwali Na.4: Idadi ya Ajira Zilizozalishwa na Sekta Muhimu Kati ya 2016/2017 na 2018/2019

Sekta Muhimu	Idadi ya Ajira Zilizozalishwa
Sekta ya Umma	112,645
Miradi ya Maendeleo	663,227
Sekta Binafsi	451,464
Jumla	**1,167,988**

Chanzo: Takwimu za kiutawala, Ofisi ya Waziri Mkuu, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu.

Jedwali Na.4 linaonesha ajira zaidi zilizalishwa katika sekta binafsi ikilinganishwa na sekta ya umma. Hii inamaanisha kuwa sekta binafsi ina mchango mkubwa katika kupambana na umaskini kwa kuongeza ajira. Ongezeko la ajira linaongeza kipato kwa waajiriwa, linaboresha hifadhi ya jamii na kupunguza idadi ya watu waliokatika hali duni.

2.5.3. Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi

Ushiriki wa wanawake katika nyanja mbalimbali ni muhimu katika kuwa na maendeleo endelevu ili kuleta usawa na kuondoa ukatili wa kijinsia. Serikali iliendelea kutekeleza programu mbalimbali na kuwawezesha wanawake kwa lengo la kuongeza fursa za kiuchumi, kuwajengea uwezo wa kufanya biashara, upatikanaji wa mitaji, masoko na mikopo. Kati ya mwaka 2015/16 na 2019/20, jumla ya shilingi bilioni 63.49 zilitolewa kwa wajasiriamali wanawake 938,802, katika Mamlaka mbalimbalui za Serikali za Mitaa nchini, kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 5.

Jedwali Na. 5: Mwenendo wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wanawake

Mwaka	Mikopo iliyotolewa	Idadi ya vikundi vilivyokopeshwa	Wajasiriali Wanawake Waliokopeshwa
2015/16	3,388,747,160	2,225	21,167
2016/17	8,816,700,165	5,899	772,245
2017/18	16,319,517,502	6,852	39,449
2018/19	11,128,114,993	4,898	44,210
2019/20	23,836,238,260	6,859	61,731
Jumla	**63,489,318,080**	**26,733**	**938,802**

Chanzo: Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Serikali iliendelea kutoa mikopo nafuu kwa wanawake wajasiriamali kupitia dirisha la wanawake lililofunguliwa katika Benki ya Posta. Mwaka 2019/20, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 3.586 ilitolewa kwa wanawake 14,271 ukilinganisha na shilingi bilioni 2.05, zilizotolewa kwa wanawake wajasiriamali 3,035, mwaka 2018/19. Vile vile, mafunzo ya ujasiriamali yalitolewa kwa wajasiriamali 718 wakiwemo wanawake 334 na wanaume 384 katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Geita na Mbeya. Mafunzo haya yaliwaongezea wanawake ujuzi kuhusu namna ya kuongeza thamani ya bidhaa, kupata mitaji, utafiti wa masoko, kuweka akiba na usimamizi mzuri wa fedha na hivyo kuboresha maisha yao na kupunguza umaskini.

2.6. Hatua za Kukuza Uwekezaji

Katika sehemu hii, mazingira wezeshi yanajumuisha hatua zilizochukuliwa na Serikali kuboresha miundombinu migumu na laini kama hatua muhimu ya kuvutia wawekezaji binafsi. Miundombinu hiyo kwa kiasi kikubwa hugharamiwa na Serikali kwa sababu ni miradi mikubwa na inahitaji uwekezaji mkubwa ambao sekta binafsi haziko tayari kuingia katika miradi hiyo. Kama ilivyo katika sehemu ndogo 2.6.1; wakati sehemu ndogo 2.6.1 inayohusu mazingira ya biashara inagusia uwezeshaji wa kiutawala, mfumo wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, na sera ambazo serikali imetekeleza ili kuhakikisha kuwa mazingira ya uwezeshaji na biashara ni rahisi, wazi na hayana viashiria vya rushwa.

2.6.1 Maboresho ya Miundombinu

Barabara:

Kati ya mwaka 2015 na 2020, Serikali ilijenga barabara za lami zenye urefu wa km 3,537.0 na barabara za mzunguko za kuepusha na kupunguza msongamano wa magari mijini, zenye urefu wa km 82.6. Kufikia Juni 2020, km 1,298.44 za barabara

za lami zilikuwa katika matengenezo. Barabara kuu zenye urefu wa km 300.9 zilikarabatiwa. Ujenzi wa madaraja makubwa 12 ulikamilika, nayo ni: Daraja la Magufuli, Magara, Kavuu, Ruvu Chini, Lukuledi, Mlalakuwa, Momba, Lukuledi II, Mara, Sibiti, Mtibwa na Daraja la Nyerere (Kigamboni). Ujenzi wa madaraja 5 unaendelea; madaraja hayo ni:- Tanzanite, Mitomoni, Wami, Kitengule na Ruhuhu. Madaraja mengine yaliyokuwa katika hatua za awali za ujenzi yalikuwa ni:- Kigongo – Busisi ambalo ujenzi wake umeanza, Sukuma, Simiyu, Mkenda, Mtera, Godegode, Malagarasi Chini na Ugalla. Miradi iliyokamilika kwa asilimia 100 ni:- barabara ya Manyoni - Itigi (km 245), kipande cha Masasi-Songea-Mbinga katika barabara Mtwara - Mbamba Bay (hadi Oktoba 2020 km 20 zilikuwa zimebakia), barabara ya juu Mfugale (Flyover) na Ubungo Interchange ambayo sasa inatumika. Miradi iliyo katika hatua za mwisho za ujenzi ambayo inatarajiwa kukamilika kabla ya Juni 2021 ni Daraja la Tanzanite, barabara ya Itoni-Ludewa, na barabara ya Tabora-Mpanda.

Reli:

Reli ya Kiwango cha Kimataifa – SGR: Serikali inajenga reli ya kati kwa kwaingo cha kimatifa (SGR) ya gharama ya Dola za Marekani bilioni 7.6. Utekelezaji ulianza mwaka 2017 kwa vipande viwili kati ya Dar es Salaam na Makutupora mkoani Singida. Kipande cha kwanza kati ya Dar es Salaam na Morogoro kina urefu wa jumla ya km 300. Kipande cha pili kati ya Morogoro na Makutupora mkoani Singida kina jumla ya km 422 . Ujenzi wa Kipande cha Dar es Salaam - Morogoro umefikia asilimia 90 na kati ya Morogoro na Makutupora umefikia asilimia 49.2.

Ukarabati wa Reli ya Kati: Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania – TRC inatekeleza mradi wa ukarabati wa reli iliyopo kwa kiwango cha *Meter Gauge* (TIRP) kwa lengo la kuwa na miundombinu ya usafirishaji ya uhakika katika kipande kati ya Dar es Salaam na Isaka chenye km 970 katika reli ya kati. Mkazo umewekwa katika ukarabati ili wenye kuwezesha kiwango cha chini cha mzigo kuwa tani 18.5 kwa ekseli (*axle),* kutandika upya reli kwa km 970 kutoka Dar es Salaam Isaka kwa mataruma yenye uzani wa ratili 80 kwa kila yadi kwa taruma na ununuzi wa mabehewa na injini za treni. Kazi kubwa za ukarabati zilizopangwa kufanyika katika reli ya kati, kipande cha kutoka Dar es Salaam mpaka Isaka (km 970) zinaendelea ambapo kipande cha Dar es Salaam - Kilosa (km 283) umefikia asilimia 94 na Kilosa – Isaka (km 687) umefikia asilimia 99.8 mwaka 2020. Serikali imejenga vituo vya kuhifadhia makasha ya mizigo (makontena) katika mikoa ya Mwanza na Shinyanga ili kurahisisha upakiaji na upakuzi wa mizigo. Vile vile, Serikali imefufua reli ya Dar es Salaam – Tanga mpaka Moshi na Arusha ambayo imekuwa haifanyi kazi kwa zaidi ya miaka 30 iliyopita.

Vifaa na Nyenzo za Reli: Serikali imejitahidi kuhakikisha kuwa reli iliyopo ya kiwango cha meter gauge inafanya kazi vizuri na kwa ufanisi. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kukarabati na kuunda upya vichwa 14 vya treni vya kukusanya na kupanga mabehewa, kukarabati mabehewa 347 ya mizigo, mabehewa 20 ya abiria wa mjini (commuter couches) na mabehewa 13 ya abiria wa safari ndefu; na ununuzi wa mabehewa 44 ya kubeba makasha ya mizigo na mabehewa ya abiria mapya 22 na vichwa 3 vipya vya treni.

Bandari:

Tanzania ina bandari kuu tatu ambazo ni Dar es Salaam, Tanga na Mtwara; bandari ndogo tatu ambazo ni Kilwa, Mafia na Lindi; na bandari kubwa katika maziwa nazo ni: Mwanza, Kigoma na Itungi-Kyela. Bandari ya Dar es Salaam ndiyo kubwa kuliko zote nchini. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili, shughuli zilizofanyika katika Bandari ya Dar es Salaam ni: Kuboreshwa kwa gati namba 1 – 4 (gati namba 1-3 kwa ajili ya mizigo mchanganyiko na gati namba 4 kwa ajili ya mizigo ya kichele mfano ngano na mbolea); kukamilika kwa ujenzi wa gati la kupakia na kushushia magari (RoRo); na kuendelea na uboreshaji wa gati Na. 5 hadi 7 (gati namba 5 kwa ajili ya mizigo ya kichele na gati namba 6-7 ni kwa ajili ya makontena). Hatua hizi zimechangia kupungua kwa idadi ya siku za meli kukaa bandarini kutoka siku saba (7) hadi siku tano (5) na kuongezeka kwa shehena ya mizigo iliyohudumiwa kutoka tani milioni 15.4 hadi tani milioni 19.52. Serikali pia ilijenga bandari kavu ya Kwala katika mkoa wa Pwani, kwa gharama ya shilingi bilioni 35, ili kupunguza msongamano wa mizigo katika bandari ya Dar es Salaam. Uwekezaji umefanywa katika vifaa vya kupakia, kupakua na ukaguzi wa mizigo. Upanuzi wa Bandari ya Tanga unaendelea ambapo uongezaji wa kina cha bandari ulifanyika ili kuwezesha meli kubwa kutia nanga katika bandari pamoja na ukarabati wa maghala katika gati namba 1 na 2. Uwezo wa kuhudumia mizigo uliongezeka kutoka tani 700,000 hadi tani 1,200,000 kwa mwaka. Kazi ya ukarabati wa gati na. 2 ilifanyika kati ya Septemba 2016 na Juni 2017.

Kazi zilizofanyika katika Bandari ya Mtwara ni pamoja na: kupanua eneo la zege kwa mita za mraba 600, pamoja na ujenzi wa gati lenye urefu wa mita 300 ambalo limekamilika.

Katika Ziwa Victoria magati yaliyojengwa ni Lushamba, Ntama, Magarini, Mwigobero, na Nyamirembe. Kwa upande wa Ziwa Tanganyika, gati limejengwa Kagunga; na katika Ziwa Nyasa magati yamejengwa Kiwira na Itungi.

Kuhusiana na Vifaa Majini, Serikali imejenga meli mbili za mizigo ambazo ni MV Ruvuma na MV Njombe zenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja, na nyingine ambayo ni MV Mbeya II yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo

katika ziwa Nyasa. Katika Ziwa Victoria meli za zamani ambazo ni MV Victoria na MV Butiama zilifanyiwa matengenezo makubwa na sasa hivi zinafanya kazi. Vile vile meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo inaendelea kujengwa.

Usafiri wa Anga:

Utekelezaji wa Mpango wa pili umehusisha kununuliwa kwa ndege mpya 11 kutoka ndege moja (1) iliyokuwepo mwaka 2015 na kuifanya ATCL kuwa na jumla ya ndege 12; na kupatiwa mafunzo kwa marubani 110, wahandisi 127 na wahudumu wa ndani ya ndege 131. Manunuzi ya ndege mpya yanaenda pamoja na ujenzi na ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya mikoa na vya kimataifa. Hatua hizi zimechangia kuimarika kwa huduma za usafiri wa anga kutoka vituo vinne (4) mwaka 2015 hadi vituo 13 vya ndani ya nchi na vituo saba (7) vya nje ya nchi mwaka 2020 na kuongezeka kwa idadi ya miruko ya ndege ndani na nje kutoka 225,103 mwaka 2015 hadi miruko 292,105 mwaka 2019. Abiria waliosafiri kwa ndege nao waliongezeka kutoa abiria 4,207,286 mwaka 2016 na kufikia abiria 4,268,896 mwaka 2018.

Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, kiasi cha shilingi trilioni 1.24 kimetumika kuboresha Shirika la Ndege Tanzania

2.6.2. Maendeleo ya Miundombinu laini

Jumla ya km 27,912 za mkongo wa taifa wa TEHAMA zimejengwa ambapo km 7,910 zilijengwa na Serikali. Vile vile, hatua nyingine zilichukuliwa kuhakikisha wadau wote ikiwa ni pamoja na sekta binafsi na wananchi kwaujumla wananufaika na rasilimali za umma ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili, huduma za TEHAMA ziliimarishwa kwa kutandika nyaya za mawasiliano. Hadi kufikia Aprili 2019 matumizi ya mawasiliano kwa simu za mikononi (mobile communication coverage) yalifikia asilimia 94 ya idadi ya watu na asilimia 66 ya mtandao kuenea kwenye maeneo mbalimbali nchini. Maendeleo haya yamebadili kwa kiasi kikubwa hali ya maisha ya wananchi hasa upande wa mawasiliano na huduma za kifedha kupitia simu za mikononi. Hata hivyo, bado kuna haja ya kuhamasisha wadau wote waweze kutumia TEHAMA wakiwa nyumbani, mashuleni na katika biashara. Maboresho ya TEHAMA yanatarajiwa kuleta matokeo mazuri katika kujifunza pamoja na kuongeza shughuli katika mnyororo wa thamani wa kilimobiashara.

2.6.3. Mazingira ya Biashara

Kwa mujibu wa Taarifa ya Mazingira ya Biashara (*Ease of Doing Business)* Tanzania nafasi ya Tanzania katika mazingira ya kufanya biashara kwa vigezo vya Benki ya Dunia ilishuka lakini imefanya vizuri kutoka nafasi ya 144 mwaka 2019 hadi nafasi

ya 141 mwaka 2020 kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 6. Lengo la Serikali ni kuimarisha nafasi ya Tanzania na kuweza kufikia lengo la nafasi ya tarakimu mbili.

Jedwali Na. 6: Nafasi ya Tanzania katika Taarifa za Urahisi wa Kufanya Biashara (2015-2020)

Mwaka	2015	2016	2017	2018	2019	2020
Nafasi	131	139	132	137	144	141

Chanzo: Benki ya Dunia (2020)

Serikali imechukua hatua kadhaa ili kuboresha mazingira ya kufanya biashara ikiwemo:-

(i) Kupunguza urasimu katika taratibu za kupata vibali mbalimbali vya biashara na huduma nyingine kwa lengo la kupunguza gharama za kufanya biashara. Kati ya mwaka 2017/18 na 2020/21 ada na tozo mbalimbali katika sekta ya kilimo na mifugo zilifutwa kupitia sheria ya fedha. Aidha, sehemu ya majukumu ya iliyokuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Chakula na Dawa - TFDA yalihamishiwa Shirika la Viwango Tanzania - TBS ili kuondoa mwingiliano wa majukumu. Mwaka 2019/20 jumla ya ada na tozo 60 zinazohusiana na leseni za biashara, vibali na vyeti vya usajili, ikiwa ni pamoja na ukaguzi uliokuwa ukifanywa na Tume ya Ushindani - FCC, Wakala wa Usajili wa Kampuni - BRELA, Shirika la Viwango Tanzania -TBS, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi - OSHA, na ada za zima moto na uokozi zilifutwa.

(ii) Taasisi mbalimbali zimeanzisha mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma. Hii ni pamoja na mifumo ya kujiandikisha kupitia mtandao kwa usajili wa kampuni, majina ya biashara, alama za biashara na huduma, hati miliki na leseni za viwanda; kupata leseni za biashara kupitia Mtandao wa Biashara wa Taifa; kurahisisha utoaji wa mizigo bandarini kupitia mfumo wa dirisha moja -TeSWS; kutoa leseni na vibali kwa njia ya mtandao vya OSHA, TMDA, TBS, NEMC na Wizara ya Kilimo na ya Mali Asili na Utalii; na kuanzishwa kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo ya Serikali – GePG kwa ada, tozo na adhabu; na kutoa hati za kusafiria za kielektroniki pamoja na VISA na vibali vya kazi na makazi.

(iii) Serikali imeanzisha vituo vya utoaji huduma za pamoja mipakani - OSBP katika vituo vya mipakani vya Rusumo, Mutukula, Holili, Kabanga, Horohoro, Sirari, Namanga na Tunduma ili kurahisisha huduma za upitishaji wa mizigo.

(iv) Idadi ya vizuizi katika barabara kati (central cooridor) imepungua kutoka vizuizi 15 hadi 3. Hii imepunguza muda na gharama ya usafirishaji wa mizigo njiani.

(v) Kuboresha kituo cha pamoja cha utoaji huduma kilichopo TIC kwa kuongeza

idadi ya taasisi zinazofanya kazi kwa pamoja kupitia kituo hicho kufikia taasisi 11.

Pamoja na maboresho haya yaliyolenga kufanya uchumi ushamiri, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi iliandaa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara (*Blueprint)* na mpango kazi wa utekelezaji wake. Mpango kazi huo utaenda pamoja na mwongozo madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini pamoja na mkakati wa mawasiliano unaolenga kuhusisha wadau kutoka sekta ya umma na binafsi.

2.6.3.1. Uwezeshaji Sekta Binafsi

Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango wa Pili. Jukumu kubwa la sekta binafsi ni kuwekeza katika miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na viwanda vya kuongeza thamani bidhaa.

Serikali imetekeleza jukumu la uwezeshi kwa kuendeleza sekta binafsi kupitia njia zifuatazo:-

(i) Kuanzisha kituo cha Pamoja chini ya TIC ambacho kinashirikisha taasisi 11 za Serikali na wakala mbalimbali na hivyo kuwezesha huduma mbalimbali kutolewa sehemu moja kama vile vibali, leseni na kupata idhini za mamlaka husika kwa wafanya biashara wa ndani na nje pamoja na wawekezaji na hivyo punguza muda wa kupita katika ofisi mbalimbali. Kufikia Februari 2020, jumla ya miradi 146 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1,514.57, ambayo ilitarajiwa kutoa ajira mpya 26,384, ilisajiliwa.

(ii) Kutambua mali binafsi na kuzilinda na vihatarishi visivyo vya kibiashara. Tanzania ni mwanachama hai wa bima kwa ajili ya uwekezaji nje chini ya Benki ya Dunia, na Wakala wa Kimataifa ya Dhamana za Uwekezaji - MIGA. Vile vile, Tanzania ni mwanachama wa Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji – ICSID, taasisi hii pia iko chini ya Benki ya Dunia.

(iii) Sheria ya kodi ya mapato inaruhusu msamaha wa asilimia 50 ya kodi katika mwaka wa kwanza wa matumizi ya mitambo na mashine zinazotumika viwandani ambazo zimefungwa katika kiwanda, mashamba ya ufugaji samaki; au utoaji huduma kwa watalii na katika mahoteli.

(iv) Asilimia sifuri (0) ya kodi ya: ushuru wa forodha kwenyue bidhaa za mitaji kwenye miradi; kompyuta na vifaa vya kompyuta; malighafi na vipuri kwa ajili ya zana za kilimo, ufugaji na uvuvi; dawa za binadamu na mifugo na dawa zingine; vifaa vinavyotumika kuunganisha magari ambavyo viko katika mfumo wa vipande (CKD); na malighafi kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa za dawa.

(v) Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwa vifaa vinavyoingizwa nchini

na watafutaji wa madini waliosajiriwa na wenye leseni nchini kwa ajili ya kazi mahsusi za utafutaji wa mafuta, gesi na madini au shughuli nyingine za utafutaji;

(vi) Kupunguza kiwango cha kodi ya mapato kwa kampuni kwa kampuni mpya zinazoanzishwa kwa ajili ya kuzalisha bidhaa za dawa, ngozi na taulo za kike; na

(vii) Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) ilianzisha jukwaa mtandao la malalamiko na mrejesho ili kuboresha mazingira ya biashara nchini. Jukwa hili lilianza shughuli zake mwaka wa fedha 2020/21.

2.6.3.2 Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Katika kuwezesha ushiriki mzuri wa sekta binafsi katika miradi ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (Public Private Partnership - PPP), Serikali iliimarisha mifumo ya sheria na ya kitaasisi husika hususan sheria ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi Sura ya 103 kwa lengo la kuboresha usimamizi na uratibu. Vile vile, mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu wa programu ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi uliboreshwa. Hii ni Pamoja na kuweka Programu na Kituo cha ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi chini ya Wizara ya Fedha na Mipango. Lengo ni kurahisisha na kuharakisha upatikanaji wa vibali kwa miradi ya ubia. Wizara ya Fedha na Mipango imeweka mazingira wezeshi ya kusaidia taasisi za Serikali kuandaa miradi ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Hatua nyingine zilijumuisha kuiongezea mtaji Benki ya Uwekezaji na kuanzisha dirisha la mikopo ya muda mrefu katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo.

Kutokana na uwepo wa mazingira wezeshi kwa uwekezaji kupitia utaratibu wa PPP, taasisi za Umma zinapaswa kuchangamkia matumizi ya mfumo huo katika kugharamia miradi ya maendeleo inayokidhi vigezo vya njia ya PPP na kuendana na ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Utayari wa kutumia utaratibu huu unaongezeka kutokana na kutungwa kwa Sheria ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi Sura ya 103. Miradi inayotekelezwa kwa utaratibu huo imeongezeka kutoka miradi 5 mwaka 2018 kufikia zaidi ya miradi 49 Desemba 2020. Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kwa kuzingatia sheria ya PPP.

2.6.3.3. Utawala Bora , Uwajibikaji na Utoaji haki

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili, Serikali iliendelea kupambana na rushwa, kuongeza uwajibikaji kwa watumishi wa umma, na kujenga miundo ya utoaji haki na kudumisha utawala bora. Shughuli zilizotekelezwa katika kipindi hiki ni pamoja na: kuanzishwa kwa mahakama ya makosa ya rushwa na uhujumu uchumi; ujenzi wa ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi; kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama Kuu mbili (2) na ukarabati wa Mahakama Kuu tatu (3); kukamilika kwa

ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi tano (5); kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama za Wilaya 15; kukamilika kwa Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo 18; ujenzi wa majengo ya Serikali Dodoma, na kuanzishwa kwa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Thamini imebainisha kuwa idadi ya kesi za rushwa zilizotolewa maamuzi iliongezeka kutoka asilimia 10.4 mwaka 2015/16 hadi asilimia 82.0 mwaka 2019/20; mlundikano wa mashauri katika mahakama ya Tanzania umepungua kutoka asilimia 13 ya mashauri yaliyokuwepo mahakamani mwaka 2015 hadi asilimia tano (5) mwaka 2019; na kuongezeka kwa upatikanaji wa haki karibu na wananchi.

Hatua nyingine zilizochukuliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ni pamoja na kufuatilia matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo kupitia ofisi za Wilaya na Mikoa na kuanzisha vitengo vya kufuatilia na kuokoa mali ambavyo vinawajibika kufuatilia na kukamata mali na fedha zilizopatikana kwa njia ya rushwa. Jedwali Na. 7 linaainisha juhudi zilizochukuliwa na TAKUKURU katika kupambana na rushwa.

Jedwali Na. 7 Takwimu za TAKUKURU dhidi ya vitendo vya Rushwa, 2015/16–2019/20

Mwaka/Aina	Tuhuma zilizopokelewa	Mafaili ya yaliyochunguzwa	Uchunguzi unaoendelea	Mafaili yaliyofungwa lekwa kwa Mkurugenzi wa Mashitaka	Kesi mpya zilizofunguliwa	Zinazoendelea	Hukumu zilizotolewa	Watuhumiwa Walioachiliwa	Jumla ya Hukumu	Mali/fedha zilizookolewa (bil)
2015/2016	7,303	788	3,525	34	336	443	578	249	275	524	53.9
2016/2017	7,452	956	2,818	103	575	435	602	159	234	393	14.68
2017/2018	8,724	906	723	78	467	495	624	178	118	296	70.3
2018/2019	8,234	894	1,160	15	388	497	672	206	135	341	82.8
2019/2020	13,313	1,079	1,380	72	443	586	633	267	114	381	96.02

Chanzo: Taarifa za Mwaka za TAKUKURU

Mwenendo wa mashauri mapya yaliyofunguliwa mahakamani kuanzia mwaka 2016 mpaka 2020 na idadi ya kesi zilizoamuliwa unadhihirisha juhudi na mkazo mkubwa uliowekwa na TAKUKURU katika kupambana na rushwa. Jitihada hizi zimewezesha Serikali kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 215.45 katika kipindi hicho. Kwa mujibu wa *Transparency International Corruption Perception Index* Tanzania imepata mafanikio ya kupata alama 37 mwaka 2019 ikilinganishwa na alama 32 mwaka 2016. Alama zinazotelwa kwa nchi zinakuwa kati ya sifuri na mia moja, ambapo alama sifuri inaonesha kiwango kikubwa cha rushwa na alama mia moja kiwango kidogo cha rushwa.

2.6.5 Amani, Usalama na Utulivu wa Kisiasa

Maendeleo na ustawi wa Taifa yanategemea uwepo wa amani, usalama na utulivu wa kisiasa. Katika kuhakikisha nchi inaendelea kuwa na amani, usalama na utulivu wa kisiasa, maboresho ya kimkakati yanatakiwa kuchukuliwa yakijumuisha maboresho ya sera ya sekta ya sheria na mfumo wa makosa ya jinai nchini.

Maadili ya Viongozi wa Umma: Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili, kama njia ya kuhamasisha utawala bora na kujenga utamaduni wa uwajibikaji kwa viongozi wa umma, Serikali ilielekeza nguvu zake katika kuhakikisha viongozi wanakidhi kanuni za maadili kulingana na marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma 2016; kufanya marekebisho ya taratibu kuu za utendaji wa Baraza la Maadili; na kutungwa kwa kanuni mpya mbili ambazo ni Usimamizi wa Mgongano wa Maslahi ya Machi, 2020 na Matamko ya Ahadi za Uadilifu kwa Viongozi wa Umma ya Novemba, 2020. Vile vile, katika kipindi cha mapitio ya Mpango wa Pili kumekuwepo na ongezeko la viongozi wa umma kutangaza mali na madeni kutoka asilimia 86 ya viongozi wote mwaka 2015 kufikia asilimia 98 mwaka 2019. Aidha, malalamiko yaliyowasilishwa katika Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma 2016, yamepungua.

2.7. Tathmini ya Ugharamiaji wa Mpango wa Pili

Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Pili ulilenga kukusanya kiasi cha shilingi trilioni 136. Kati ya hizo shilingi trilioni 82.4 zilitarajiwa kutoka katika vyanzo vya kawaida kama vile mapato ya Serikali, misaada, na mikopo yenye masharti nafuu na shilingi trilioni 53.3 kutoka vyanzo vingine kama vile hatifungani za Serikali. Tathmini imeonesha kwamba Serikali iliweza kukusanya mapato ya kodi kwa asilimia 98 ya lengo. Uwiano wa mapato ya ndani na Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 13 hadi 15. Kwa upande mwingine mikopo ya kibiashara ilikuwa zaidi ya mara mbili ya lengo kwa kufikia shilingi trilioni 12.2 ikilinganishwa na lengo la shilingi trilioni 5.7. Mikopo yenye masharti nafuu ilikuwa zaidi ya lengo kwa kufikia shilingi trilioni 10.2 ikilinganishwa na lengo la shilingi trilioni 6.2 sawa na asilimia 64 zaidi ya lengo.

Aida, utekelezaji wa Mpango wa Pili ulikadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi trilioni 107 sawa na wastani wa shilingi trilioni 21.4 kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano. Sekta ya umma ilitarajiwa kuchangia kiasi cha shilingi trilioni 59, na sekta binafsi kiasi cha shilingi trilioni 48. Utekelezaji wa Mpango wa Pili katika miaka minne ya mwanzo umebainisha kuwa sekta ya umma ilichangia kiasi cha shilingi trilioni 34.9 sawa na asilimia 76.5 ya lengo la miaka minne la shilingi trilioni 45.6. Kwa upande mwingine, uchambuzi wa tathmini ya Mpango wa Pili imebaini kuwa uwekezaji wa sekta binafsi katika uchumi ulifikia shilingi trilioni 152. Vile vile,

tathmini imebainisha kuwa uwekezaji wa sekta binafsi kwenye maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Pili, kwa kipindi cha miaka minne iliyopita ilifikia shilingi trilioni 32.6 sawa na asilimia 85 ya makadirio ya shilingi trilioni 38.4. Maeneo makuu ambayo sekta binafsi iliwekeza ni pamoja na maendeleo ya viwanda, shule binafsi, hospitali, hoteli, uchimbaji madini usafirishaji na huduma za usafirishaji.

2.8. Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Pili

Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Pili ni moja ya nyenzo ya utekelezaji wa malengo na viashiria vya Mpango wa Pili vilivyowekwa mwaka 2016/17. Tathmini inaonesha kwamba pamoja na kuwa na mkakati fasaha wa ufuatiliaji na tathmini wenye malengo ya kimkakati, hatua stahiki za utekelezaji na viashiria vya kupima utekelezaji, Mkakati haukutekelezwa ipasavyo. Hata hivyo, Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetumia njia za ufuatiliaji na tathmini ambazo hazikuainishwa katika Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini uliopendekezwa katika Mpango wa Pili katika utekelezaji wa miradi. Aidha, mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini imeendelea kuboreshwa ambapo Wizara ya Fedha na Mipango imeanzisha kitengo maalumu cha Ufuatiliaji na Tathmini, kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa miradi ya maendeleo na kuanza maandalizi ya mwongozo wa Tathmini.

2.9. Uwezo, Udhaifu, Fursa na Viatarishi (SWOT) vya Mpango wa Pili

Jedwali Na.8 linachambua uwezo, udhaifu, fursa na viatarishi vilivyojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Pili, kwa lengo la kupata mafunzo katuika kutekeleza Mpango wa Tatu.

Jedwali Na. 8 Uchambuzi (SWOT) wa Utekelezaji wa Mpango wa Pili

Uwezo (Strengths)	**Udhaifu (Weaknesses)**
i. Utashi wa kisiasa, amani na utulivu wa hali ya kisiasa; ii. Utajiri wa maliasili – Ardhi, Wanyama pori, madini, misitu -fursa ya kufanya shughuli mbalimbali; iii. Uwepo wa mfumo wa kisheria na kitaasisi kwa ajili ya ya msuala katika uwekezaji; iv. Ukuaji mkubwa wa uchumi kwa wastani wa asilimia 6.9 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita; v. Fursa nyingi za uwekazaji wenye faida - mafuta na gesi, kufua umeme na miradi ya usafirishaji; vi. Fursa nyingi za kilimobiashara katika sekta ya kilimo; vii. Fursa nyingi za upanuzi wa miundombinu katika sekta ya: usafiri wa anga, na ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, bandari, nyumba na mkongo wa TEHAMA; viii. Kuwepo kwenye sehemu ya kimkakati kijiografia iliyozungukwa na nchi zisizo na bahari katika soko la EAC, SADC na nchi nyingine duniani; ix. Uwepo wa mwambao wa mrefu wa bahari ambao una mfumo wa kiikolojia unaowezesha shughuli rasimali bahari; na x. Idadi ya watu inayoongezeka kwa haraka na hivyo kuwezesha ongezeko la nguvukazi na kukua kwa tabaka la kati huku kukiwa na uhakika wa soko la ndani.	i. Kiwango kidogo cha maendeleo ya watu, uwezo mdogo wa Sayansi, teknolojia na ubunifu; kiwango cha chini cha ujuzi adimu kwenye sekta ya uchimbaji madini; ii. Tatizo la upatikanaji wa takwimu kwa ajili ya mipango na ufuatiliaji; iii. Ufuatiliaji na tathmini usioridhisha; iv. Ushiriki mdogo wa Sekta binafsi; na v. Kipato kidogo cha pato la mtu.
Fursa (Opportunities)	**Tishio (Threats)**

i. Uwezekano wa kuboresha mazingira ya biashara kwa ukuaji wa biashara ndogo; mageuzi zaidi katika sekta ya kilimo na kupunguza uwezo wa kuathari na mitikisiko hasi ya kiuchumi ya ndani, kimataifa na ya hali mbaya ya hewa; ii. Kuibuka kwa viashiria vya kuongezeka ushiriki wa watu maskini katika mchakato wa ukuaji wa uchumi kama vile vitambulisho vya wajasiriamali wadogo (Machinga) na fursa endapo urasimishaji utafanikiwa; iii. Kuendelea kuimarika kwa utulivu wa uchumi jumla na diplomasia ya uchumi kwa lengo la kupata masoko ya nje na kuvutia uwekezaji kutoka nje; iv. Uwepo wa miongozo ya uwekezaji katika mikoa na Mamlaka ya Serikali za mitaa yenye taarifa za fursa za viwanda na maendeleo ya watu; v. Ardhi yenye rutuba na inayofaa kwa umwagiliaji; vi. Miundombinu bora ya masoko kwa ajili ya kufanikisha uzalishaji katika kilimo; vii. Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara (Blueprint) ambao unaonesha orodha ya maeneo ya maboresho katika maeneo mtambuka; viii. Uendelezaji wa miundombinu muhimu katika maeneo maalum ya uwekezaji (SEZ)/EPZ) hususan katika mikoa ya mipakani; na ix. Masoko ya dunia na kikanda ikiwemo SADC, EAC na AfCFA.	i. Mitikisiko ya nje – kutotengamaa ndani ya kanda; ii. Mabadiliko ya tabianchi; iii. Majanga asilia; iv. Milipuko ya magonjwa; na v. Kutotengemaa kwa siasa za dunia na kikanda kama vile mzozo wa kibiashara kati ya China na Marekani na migogoro ya siasa kikanda.

2.10 Utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo

Jedwali Na. 9 linaainisha kwa muhtasari hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya kielelezo iliyoainishwa katika Mpango wa Pili. Hii inasaidia kuweka usimamizi wa karibu ili kufikia matarajio ya kukamilisha utekelezaji kwa wakati hususan kudhihirisha uwezo wa kugharamia miradi hiyo kikamilifu ikijumuisha uendeshaji na matengenezo.

Jedwali Na. 9 Miradi ya Kielelezo

Na.	Miradi ya kielelezo	Hali ya utekelezaji
1.	Ujenzi wa reli kwa kiwango cha kimataifa (SGR)	Utekelezaji wa mradi wa SGR ulianza mwaka 2017 ukiwa na vipande viwili vya Dar es Salaam mpaka Morogoro (km 300) na Morogoro mpaka Makutupora, Singida (km 422). Kazi za ujenzi kati ya Dar es Salam na Morogoro ilifikia asilimia 90 na ulitarajiwa kukamilika mwaka mwanzoni 2021; na kipande cha Morogoro hadi Makutopora, Singida kimefikia asilimia 49.2.
2.	Ujenzi wa mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115	Ujenzi wa mtambo wa umeme unaendelea na hatua ya utekelezaji ni kama ifuatavyo: Bwawa kuu (asilimia 6.72); handaki la kuchepusha maji lipo katika hatua ya mwisho ya utekelezaji; ujenzi wa maporomoko ya maji (asilimia 8.54); na uwekaji wa zege kweny kuta za handaki na asilimia 90. Kwa ujumla kazi za ujenzi zimefikia asilimia 25.8.
3.	Miradi ya Mchuchuma na Liganga	Serikali imechukua hatua za kuanza utekelezaji wa Miradi ya Mchuchuma na Liganga ambayo ina akiba kubwa ya Makaa ya mawe, chuma na madini ya *vanadium,* na *titanium*. Mpaka sasa uthaminishaji wa mali za watu walio katika maeneo ya miradi umekamilika na jumla ya shilingi bilioni 11.037 zinatarajiwa kulipwa kama fidia kwa wananchi 1,145 watakaopisha mradi. Kwa upande mwingine, Serikali pamoja na mwekezaji wanapitia mkataba na masuala ya kisheria kuhusu miradi hii.
4.	Bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima (Uganda) mpaka bandari ya Tanga eneo la Chongoleani.	Kazi zote za maandalizi ya mradi zimekamilika na utekelezaji wa mradi unatarajiwa kuanza baada ya kampuni zinazohuisika katika utekelezaji kukamilisha taratibu zote za kimkataba.
5.	Ufufuaji wa shirika la ndege Tanzania	Katika kipindi cha kati ya 2016 na Desemba 2020, Serikali ilinunua na kupokea ndege nane (8). Vile vile, ndege nyingine tatu (3) zaidi zimeagizwa na zinatarajiwa kupokelewa hivi karibuni.

2.11. Hali ya utekelezaji wa Mpango wa Pili kwa ujumla na Masuala Yaliyojitokeza

2.11.1 Hali ya utekelezaji wa Mpango wa Pili kwa Ujumla

Tathmini ya jumla ya utekelezaji wa Mpango wa Pili inaonesha ufanisi mkubwa katika kudumisha uhimilivu wa uchumi jumla. Takriban asilimia 93.8 ya malengo ya uchumi jumla yalifikiwa. Utekelezaji katika sekta ya viwanda ulifikia asilimia 75 ya lengo lililowekwa. Mchango wa sekta ya viwanda kwa Pato la Taifa uliongezeka kufikia asilimia 8.5 mwaka 2019/20 kutoka asilimia 7.9 mwaka 2015/16. Sekta hii imekuwa ikikua kwa wastani wa asilimia 8.3 kila mwaka kwa kipindi hicho. Kufikia Juni 2020 viwanda 8,477 vilikuwa tayari vimeanzishwa na hivyo kutoa ajira mpya 482,601. Malengo yaliyowekwa kwa sekta ya viwanda katika Mpango wa Pili yalifikiwa kwa asilimia 66.6. Hatua zilizochuliwa katika sekta ya kilimo na sekta ndogo katika utekelezaji wa Mpango wa Pili zilikuwa na matokeo mazuri kwani ziliwezesha kufikia asilimia 77 ya malengo yaliyowekwa. Kiwango cha ukuaji halisi wa sekta kiliongezeka kwa wastani wa asilimia 5.1 katika miaka 4 iliyopita ya utekelezaji wa Mpango wa Pili. Katika sekta ya madini malengo yote yaliyowekwa yalifikiwa kwa asilimia 100 katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili. Ukuaji wa kila mwaka wa sekta ya madini uliongezeka kufikia asilimia 17.7 mwaka 2019 kutoka asilimia 6.9 mwaka 2015/16 na mchango wa sekta kwa Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 4.9 mwaka 2016 hadi asilimia 5.2 mwaka 2019.

Kiwango cha mauzo ya Tanzania kwa nchi za SADC kiliongezeka kutoka asilimia 19.0 mwaka 2015 kufikia asilimia 24.5 mwaka 2019. Katika sekta ya utalii kulikuwa na mafanikio makubwa yalipatikana ambapo idadi ya watalii walioingia nchini ilifikia 1,510,151 mwaka 2019 kutoka watalii 1,137,182 mwaka 2015, sambamba na kuongezeka kwa siku za kukaa hotelini kwa kila mtalii kutoka siku 10 mwaka 2015 kufikia 13 mwaka 2019. Mapato kutokana na utalii yaliongeka kutoka Dola za Marekani bilioni 1.9 mwaka 2015 kufikia Dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2019. Utekelezaji wa jumla wa malengo ya maendeleo ya miundombinu na huduma ulikuwa asilimia 91.0. Hii ilichangia kufikiwa kwa malengo katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili. Aidha, tathmini inaonesha kwamba kuna hatua nyingine zilizokamilika kwa takriban asilimia 100 au zaidi ikiwa ni pamoja na kuunganisha taasisi za umma kwenye Serikali Mtandao ambayo ni asilimia 247, ongezeko la watu wanaotumia mtandao asilimia 177, nafasi ya bandari katika viwango vya kimataifa asilimia 105; na mikoa iliyounganishwa kwenye umeme asilimia 95.7.

Utekelezaji wa jumla katika sekta za huduma za jamii ulikuwa wa kiwango cha juu ambapo takribani asilimia 70 ya malengo zilifikiwa kama inavyoshuhudiwa na kushuka kwa kupungua kwa vifo vya watoto wachanga na walio chini ya umri wa miaka mitano kufikia asilimia 38.4 na asilimia 53 kwa vizazi hai 1,000 waliozaliwa

hai mtawalia; kupungua kwa vifo vya kina mama wajawazito wakati wa kujifungua kwa asilimia 25.7; kuongezeka kwa wazazi waliohudumiwa na wakunga wenye ujuzi wakati wa kujifungua; na kwa ujumla wastani wa umri wa watu wa kuishi uliongezeka kutoka miaka 62 hadi 66. Upatikanaji wa maji uliongezeka kufikia asilimia 85 katika Jiji la Dar es Salaam, asilimia 80 katika makao makuu ya mikoa na asilimia 64 katika makao makuu ya wilaya. Uwiano wa kaya zinazopata maji kutoka katika vyanzo vilivyohifadhiwa, wakati wa mvua na wakati wa kiangazi ilifikia asilimia 88 na 77 mtawalia. Uwiano wa kaya zenye huduma za choo ilifikia asilimia 93. Malengo yaliyowekwa katika sekta ya maji na usafi wa mazingira yalifikiwa kwa asilimia 80 Desemba 2018. Mafanikio katika sekta ya elimu ni pamoja na kuanza kutekeleza sera ya elimumsingi bila ada, ujenzi wa madarasa, ongezeko la udahili katika vyuo vya ualimu, usambazaji wa vifaa vya kufundishia, maabara na TEHAMA.

2.11.2 Changamoto za Utekelezaji

Wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Pili changamoto kadhaa zilijitokeza. Changamoto hizi kwa kiasi fulani zilipunguza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Changamoto zilizojitokeza ni za kitaalamu na kiuendeshaji na za kifedha. Changamoto nyingine zilikuwa za kisekta na nyingine zilikuwa mtambuka kwa sekta zote, hususan uwezo wa kitaasisi na mifumo ya kisheria na udhibiti. Aidha, changamoto nyingine zilitokana na masuala yaliyo nje ya Tanzania ikiwemo mlipuko wa magonjwa, mgogoro wa kiuchumi kati ya Marekani na China, na Uingereza kujitoa kwenye jumuiya ya Ulaya.. Kundi la pili la changamoto ni zile ambazo ni mahsusi katika utekelezaji wa Mpango kwa namna iliyobora.

Changamoto za Sekta

Changamoto zakawaida za kisekta zimeorodheshwa katika makundi ya kisekta huku tukichukua tahadhari ya kwamba changamoto hizi zinaathiri makundi kwa namna tofauti. Zifuatazo ni changamoto ambazo ni muhimu zikabainishwa:

(i) Sekta za uzalishaji yaani kilimo, ujenzi, na uzalishaji viwandani: matumizi madogo ya teknolojia; uwezo mdogo wa kuhifadhi bidhaa na mazao na nyenzo za kuongeza thamani; gharama kubwa za uzalishaji; na uhaba wa malighafi; na mitaji kwa ajili ya uwekezaji;

(ii) Maendeleo ya viwanda: kiwango kidogo cha ujuzi, maarifa na kujenga uwezo utaboreshwa kupitia mafunzo ya ufundi stadi/ufundi, uanagenzi n.k; uhaba wa mitaji; mikopo midogo kutoka benki za kibiashara. Mikopo kwa viwanda ni asilimia 10.5 wakati kiwango kikubwa cha mikopo kilitolewa kwenye mikopo binafsi ambayo ni asilimia 27.4 ikifuatiwa na ya biashara asilimia 20.5; na uwekezaji mdogo kutoka nje uliotokana na ongezeko la uwekezaji

wa ndani katika maeneo ambayo awali yalivutia zaidi uwekezaji kutoka nje pamoja na mitikisiko duniani;

(iii) Sekta za ujenzi: uwezo mdogo wa kampuni za ndani za ujenzi; mabadiliko ya haraka ya teknolojia ikiwa ni pamoja na matishio ya usalama; kupanuka kwa miji kiholela; na kukosekana kwa utaratibu wa kufanya matenegenzo muhimu kwa wakati muafaka na kwa ufanisi; na

(iv) Huduma za jamii: ufinyu wa upatikanaji wa huduma hasa katika maeneo ya vijijini.

Changamoto Zilizoathiri Utekelezaji

(i). *Kuchelewa kutekelezwa kwa mkakati wa Utekelezaji*: Mkakati wa utelezaji wa Mpango wa Pili ulianza kutekelezwa mwaka 2017, miaka miwili baada ya mpango kuidhinishwa. Mkakati wa utekelezaji ulikuwa katika nyaraka nne ambazo ni Mpango Kazi, Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini, Mkakati wa Ugharamiaji na Mkakati wa Mawasiliano. Kuchelewa kuanza kwa utekelezaji wa mikakati hii kuliathiri utekelezaji wa baadhi ya shughuli za miradi na hata upatikanaji wa fedha za kugharamia mpango;

(ii). Ugumu wa kupata taarifa za uwekezaji wa sekta binafsi**:** Imekuwa vigumu kutoa taarifa kuhusu mchango wa sekta binafsi katika utekelezaji wa mpango, kwani hakukuwa na utaratibu madhubuti wa kupata taarifa za sekta binafsi. Uwekezeaji wa sekta binafsi kwa miradi iliyoanishwa katika Mpango ulikuwa wa kusuasua na taarifa za shughuli zilizofanywa na sekta binafsi zilikuwa chache na hivyo kusababisha ugumu katika kufanya maamuzi sahihi ya kiwango cha uwekezaji kilichofanywa na sekta binafsi;

(iii). *Maandalizi ya Miradi***:** Changamoto kubwa ilikuwa ni uhaba wa watumishi wenye ujuzi wa kutosha wa kuandaa miradi katika baadhi ya sekta. Matokeo yake miradi mingi haikuandaliwa vizuri na kusababisha kukosa fedha za ndani na nje ya nchi;

(iv). *Ufuatiliaji na tathmini*: Kukosekana kwa mpango madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini ilikuwa kikwazo katika upimaji wa matokeo halisi ya Mpango katika ngazi zote. Hali hii ilileta ugumu katika kuanisha mambo muhimu yaliyohitaji uchambuzi wa kina na hatua stahiki za kisera kwa wakati.

(v). *Fedha za Miradi ya Maendeleo kutopatikana kwa wakati*: Upatikanaji wa fedha za miradi kwa wakati umekuwa mgumu kutokana na mlolongo mrefu wa majadiliano na wakopeshaji, ukusanyaji mapato wa msimu, na kuchelewa kupatikana kwa fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

(vi). *Ushiriki wa Sekta Binafsi katika ugharamiaji na utekelezaji w miradi ya kipaumbele***:** Pamoja na mchango mkubwa wa sekta binafsi kwenye uchumi katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili, kumekuwepo na changamoto sekta binafsi kutokushiriki moja kwa moja kugharamia na kutekeleza miradi ya kimkakati na kipaumbele iliyokuwa imeainishwa kwenye Mpango.

(vii). *Upatikanaji na ubora wa takwimu:* Mojawapo ya vikwazo vilivyojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Pili ilikuwa ni upatikani na ubora wa takwimu. Kwa mfano, takwimu nyingi hazijitoshelezi na kusababisha ugumu wa kufanya uchambuzi wa mwelekeo na maoteo. Katika Mpango wa Tatu, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaweka mkazo katika usahihi na ukusanyaji wa takwimu kwa wakati.

2.12. Mwelekeo

Kuendeleza Utulivu wa Uchumi Jumla: Utulivu wa uchumi jumla unahitaji hatua za kushughulikia uwiano wa viashiria vya uchumi kama vile mfumuko wa bei, kiwango cha ubadilishaji wa fedha za kigeni, kiwango cha riba, mizania ya malipo na nchi za nje, nakisi ya bajeti, deni la nje, kukuza biashara ya nje pamoja na usimamizi madhubuti wa uwiano kati ya mahitaji ya vitu na upatikanaji wake katika soko, ili kuwezesha utulivu wa uchumi. Mojawapo ya masuala ya msingi katika kuimarisha uchumi jumla ni kupanua wigo wa vyanzo vya ndani ya kodi na visivyo ya kodi. Ili kuhakikisha usimamizi mzuri wa uchumi jumla, Serikali itaendelea kufuatilia kwa ukaribu vihatarishi vya nje na vitendo vya kibiashara vinavyoweza kuathiri utulivu wa uchumi wa Tanzania na nchi nyingine.

Kuongeza Ubora wa Huduma: pamoja na kuendelea na uwekezaji kwenye miundombinu ya huduma za jamii ikiwemo miundombinu ya afya na elimu, serikali itaweka nguvu zaidi katika kuimarisha ubora wa huduma za jamii zinazotolewa.

Hatua za Kuendeleza Ujuzi: Uwezo wa rasilimali watu ni changamoto mtambuka kwa maana ya idadi na ubora katika sekta zote. Sekta zinatakiwa kuandaa programu za mafunzo za muda mfupi na wa kati ili kujaza nafasi kwa kuzingatia ujuzi unaohitajika. Hata hivyo, kama ilivyoainishwa katika sura ya utangulizi suala hili litachukuliwa hatua kupitia mikakati madhubuti za kukuza ujuzi itakazohusisha ushirikiano kati ya: (i) programu zinazotolewa na taasisi za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na elimu ya juu, kwa kuweka kipaumbele katika elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi; (ii) Serikali na (iii) Sekta Binafsi na Asasi zisizo za Kiserikali hususan taasisi za dini na asasi za kijamii na kiraia.

Kuimarisha Mfumo wa Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi: Katika kipindi cha Mpango wa Pili, Utashi wa kisiasa na msimamo wa kukuza uwekezaji wa sekta binafsi ulikuwa mkubwa na bayana. Kikwazo kikubwa kilikuwa ni namna ya kutafsiri maelekezo ya kisiasa na kisera kwa ajili ya hatua au utekelezaji makini katika ngazi zote za Serikali yaani Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Mpango wa tatu umetoa uzito wa kipekee kwa sekta binafsi ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati ya kurasimisha sekta isiyorasimi, kujengea uwezo sekta binafsi ya ndani na kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango.

SURA YA TATU

KUKUZA USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI KWENYE MAENDELEO YA KIUCHUMI

3.1 Utangulizi

Sura hii inajenga hoja ya ushiriki wa sekta binafsi kama chachu ya uchumi shindani kwa ajili ya kuibakisha Tanzania katika hadhi ya udhumi wa kati na kuboresha maendeleo ya watu. Sura hii inachukua mtazamo wa kuangalia historia na mwelekeo katika kuchambua ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi shindani. Hii ni pamoja na tathmini ya hali sekta binafsi na ushiriki wa sekta hiyo kwenye utekelezaji wa Mpango na maendeleo ya nchi.. Uchambuzi unatoa msingi wa kutengeneza utaratibu mzuri na usimamizi wa mageuzi ya maendeleo ya sekta binafsi na ushiriki wake katika uchumi wa taifa. Sura hii, inatoa mwongozo kwa wadau juu ya maendeleo na kuishirikisha sekta binafsi ili iweze kujiimarisha na kuendana na hali ya uchumi wa kati. Sura hii, inataka kuwepo kwa juhudi za pamoja za kuongeza ukuaji na ari ya sekta binafsi, kuongeza urasimishaji, kuongeza utawala bora, kuimarisha uwezo wa sekta binafsi ili iweze kutumia fursa za biashara na uwekezaji na kuongeza uendelevu wa shughuli za sekta binafsi. Hii itawezesha ukuaji wa uchumi, ajira, ushindani na maendeleo ya watu.

3.2 Sekta Binafsi Nchini

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikitekeleza maboresho ya sektya binafsi tangu kati kati ya miaka ya 1980. Maboresho haya yalilenga kuondoa ushiriki wa moja kwa moja wa Serikali kwenye uzalishaji wa kiuchumi na kuekekeza nguzu na rasimali katika kusimamia sheria na taratibu, kuboresha miundombinu, utoaji wa huduma za kijamii, na kuweka mazingira bora ya biashara na uwekezaji kwa lengo la kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi. Katika kipindi cha miaka ya 1990, sekta binafsi ilikuwa kwa kasi kutoka kwenye hatua ya uchanga ikiwa ni matokeo ya sera za uchumi huru na mageuzi ya kiuchumi ambayo ilikuwa ni pamoja na ubinafsishaji wa mashirika ya umma na maboresho ya sekta ya fedha. Katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, ukuaji wa sekta binafsi ulitawaliwa na ongezoeko kubwa la mitaji kutoka nje hususan katika sekta ya uchumbaji madini na utafutaji wa gesi na mafuta. Aidha, kulikuwa na kiwango kidogo cha mitaji ya nje kwenye sekta pana na jumuishi hususan kilimo na kilimobiashara.

Mazingira ya sekta binafsi nchini Tanzania yanahusisha washiriki wengi wakiwemo wakulima wadogo, wafugaji, wajasiriamali wadogo sana, wadogo wadogo, wadogo, na wa kati, wajasiriamali jamii, madalali wa bidhaa na huduma na vyama vya makundi mbalimbali ya wajasiriamali. Kwa kiasi kikubwa sekta binafsi nchini imetawaliwa na biashara zisizo rasmi. Utafiti wa Kitaifa wa msingi wa wajasiriamali

wadogo na wa kati wa mwaka 2012 umekadiria kuwa wafanyakazi wanne kati ya watano kwenye sekta binafsi wanafanya shughuli zisiszo rasmi. Wajasiriamali wadogo sana wanashughuli zinazohusisha kuanzia mtu mmoja mpaka watatu, wajasiriaali wadogo ni wenye shughuli zinazohusisa hadi watu wanne na mara nyingi nishughuli za kifamilia zenye mtaji unaofikia shilingi milioni 5 na zenye mauzo ya shilingi milioni 12. Mara nyingi biashara ndogo sana na ndogo ndogo zinaangukia katika sekta isio rasmi vile vile zinajumuisha shughuli za kujikimu ambazo zinazalisha kipato chini ya kiwango cha chini cha mapato au chini ya mstari wa umasikini. Shughuli hizo hazina wafanyakazi wanaolipwa mshahara na thamani ya mali ni ndogo, mfano wa shughuli hizo pamoja na wachuuzi, madalali na wamachinga. Changamoto kubwa ya biashara ndogo sani ni uendelevu wa biashara na hivyo ni vigumu kuwafuatilia wafanyabiashara na kuwahudumia.

Uchambuzi unaonesha kuwa sekta binafsi inakabiliwa na matatizo makubwa manne:

(i) **Uwiano wa sekta isiyorasimi,** takribani kaya milioni 4.3 zimeajiriwa katika sekta isiyo rasmi, na mara nyingi hazina uwezo wa kufikia huduma saidizi na fursa za kazi zenye staha.

(ii) **Biashara ndogo kutokuwa endelevu** wastani wa maisha ya biashara ndogo Tanzania ni miaka 4.1. Sehemu kubwa ya shughuli za sekta binafsi ambayo imetawaliwa na biashara ndogo zina kawaida ya kuwa na maisha mafupi na hivyo kuchagiza udhaifu wa kiuchumi.

(iii) **Mazingira na mifumo isiyo rafiki;** suala kubwa linalokwaza shughuli za sekta binafsi katika kuongeza usajiri wa mali, urahisi wa kupata mikopo, kulinda wawekezaji wadogo, ulipaji wa kodi, biashara mipakani na usimamizi wa mikataba ni mifumo ya kitaasisi, kisheria na mazingira ya biashara.

(iv) **Uwezo mdogo wa sekta binafsi;** kwa ujumla sekta binafsi inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa wataalamu na menejimenti, tekinolojia duni, na mitaji midogo hivyo kupelekea sekta binafsi kushindwa kuwa shindani kikanda na kimataifa.

Licha ya changamoto za ujumla zilizobainishwa hapo juu, sekta binafsi imesajili asilimia 68 ya ongezeko la mtaji kati yam waka 2016 hadi 2019, ajira 716,624 zilizalishwa na sekta binafsi kufuatia juhudi ya Serikali katika kuendeleza sekta binafsi. Utekelezaji wa sera rafiki kwa sekta binafsi kulisababisha kupanuka kwa sekta hiyo, kuongeza mchango wake kwenye uchumi, kuongeza uwekezaji binafsi, kuzalisha ajira, uhawilishaji wa teknolojia na ujuzi na kuingia kwa washiriki kutoka nje katika shughuli za kiuchumi. Mafaniko yaliyopatikana yanajumuisha kuongezaka kwa mitaji ya binafsi kufikia shilingi kufikia trilioni 41.8 mwaka 2019 kutoka shilingi trilioni 24.9 2016. Aidha, Sekta binafsi nchini Tanzania imekuwa

msitari wa mbele katika mageuzi ya kiuchumi ambapo mchango wake kwenye ajira zisizo za kilimo umeongezeka kufikia asilimia 30.2 kutoka asilimia 29.1 kati ya mwaka 2006 na 2016. Ongezeko hili limesababisha kushuka kwa mchango wa sekta ya kilimo kwenye Pato la Taifa kutoka asilimia 28.4 mwaka 2016 hadi asilimia 26.6 Mwaka 2019.

Licha ya sekta binafsi kuongeza mchango wake kwenye ukuaji wa uchumi na uzalishaji ajira, sekta hii imeendelea kutokuwa rasmi na hivyo kupunguza manufaa ya ukuaji wa uchumi kwa watu wa chini. Mbali na sekta ya kilimo ambayo inatawaliwa zaidi na sekta isiyo rasmi, Utafiti wa Taifa wa Nguvukazi na Ajira wa Mwaka 2014 unakadiria kuwa sekta isiyo rasmi inaajiri takribani asilimia 21.7 ya nguvu kazi yote nchini. Kutokuwa rasimi inaaminisha kutotambuliwa uwepo wake kisheria. Hii imekuwa na madhara makubwa kwa sekta hii kwa kuifanya ishindwe kutumia fursa mbalimbali ikiwepo upatikanaji wa: mikopo, ulinzi wa kisheria wa ajira na vipato, malipo yasiyotabirika, na mazingira duni ya kazi. Utafiti wa Mwaka 2012 unakadiria kwamba asimilia 3.9 tu ya shughuli za ujasiriamali ndogo sana, ndogo na kati zisizo za kilimo nchini Tanzania ndio zenye usajili rasimi. Aidha, utafiti wa Taifa wa Nguvukazi na Ajira wa Mwaka 2014 umebaini kuwa ajira kwenye sekta isiyo rasimi imeongeza kwa karibu mara 3 kutoka ajira 1,682,383 mwaka 2006 hadi ajira 4,344,580 mwaka 2016. Kwa ulinganisho mchango wa ajira kwa sekta isiyo rasimi isiyo ya kilimo imeongezeka kutoka asilimia 46.1 hadi asilimia 71.8. Kwa uhakika, Utafiti wa Taifa wa Nguvukazi na Ajira wa Mwaka 2014 imebeinisha kuwa wastani wa kati wa kipato cha mwezi kwa sekta binafsi isiyo rasimi ulikuwa shilingi l20,000 ikilinganishwa na shilingi 220,000 kwenye sekta binafsi rasimi isiyo ya kilimo, na shilingi 500,000 katika sekta ya umma.

3.2.1 Ushiriki katika kilimo

Uchumi wa Tanzania umeendelea kutegemea zaidi kilimo, licha ya mchango wake kwenye Pato la Taifa kuendelea kushuka. Kilimo kinaajiri takribani asilimia 66.3 ya nguvukazi ya Tanzania. Uzalishaji mkubwa wa kilimo unafanywa na sekta binafsi. Utafiti unaonesha kwamba katika kipindi cha kati ya mwaka 1960 hadi 1970, sekta binafsi kupitia wakulima wadogo na kilimo kidogo cha kibiashara iliwezakuchangia kati ya asilimia 90 hadi 96 ya usalama wa chakula nchini. Kutokana na maboresho ya uchumi wa masoko yaliyofanyika miaka ya 1990, uzalishaji wa chakula ulifikia asilimia 100 kwa mujibu wa mahataji ya usalama wa chakula yaliyowekwa na Shirika la Chakula Dunian (FAO). Hata hivyo, wakati sekta binfsi imeendelea kuwezesha usalama wa chakula kwa kipindi kirefu, bado uzalishaji ni wa kujikimu.

Licha ya kusaidia usalama wa chakula sekta binafsi imekuwa na mchango mkubwa kwenye ongezeko la uzalishaji wa mazao ya biashara. Mazao makuu biashara ya Tanzania yanayouzwa nje ya nchi ni: tumbaku, korosho, kahawa, chai, karafuu,

pamba na katani. Zao la korosho linahusika kwa asilimia 75 na maisha ya kaya zaidi ya 700,000, na ni zao muhimu sana la biashara linalouzwa nje na mchango wake umekuwa kufikia dola milioni 353.1 mwaka 2019 kutoka dola milioni 201 mwaka 2016 ikifuatiwa na zao la kahawa ambalo uuzwaji wake nje umekuwa kutoka dola za Marekani milioni 153.4 kutoka dola milioni 109 kwa kipindi hicho. Pamoja na mafanikio hayo, sekta hii inahitaji kuwezeshwa na kujengewa uwezo wa uzalishaji, uchakati, ufungashaji, usafirishaji, uhifadhi na masoko ili kuweza kutoa mchango mkubwa zaidi kwa kuzalisha na kuuza mazao ya kilimo kwenye masoko ya ndani na ya nje.

Ushiriki kwenye sekta nyingine za uzalishaji

Sensa ya Uzalishaji Viwandani ya Mwaka 2013 iliyochapishwa mwaka 2016 inaonesha kuwa sekta binafsi inachangia kwa asilimia 99.6 ya uzalishaji wote viwandani nchini Tanzania kupitia umiliki binafsi(sole ownership) ambao ni asilimia 99.5 au ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ambayo ni asilimia 0.1. Ushiriki wa sekta binafsi kwenye uzalishaji wa viwandani umejikita zaidi kwenye uzalishaji wa: bidhaa za chakula asilimia 39.9; mavazi asilimia 27.0; na samani asilimia 13.8. Sambamba na msukumo wa maendeleo ya viwanda uliopo kwenye Mpango Elekezi wa Muda Mrefu wa Tanzania, bado kuna fursa ya kuongeza ukuaji wa sekta binafsi na uzalishaji viwandani kwa kuongeza thamani bidhaa kama vile bidhaa za chuma, mavazi, bidhaa za ngozi na mazao yake, bidhaa za mpira na plastiki na dawa. Seikali inaamini kuwa sekta binafsi hususani wajasiriamali wadogo na wakati wakijengewa uwezo wana fursa kubwa ya kuwa kitovu cha msukumo mpya wa maendeleo ya viwanda.

Mpango wa Tatu unatoa uzito wa kipekee kwa sekta binafsi ambapo uchambuzi wa kina wa changamoto na vikwazo vinanavyoikabili sekta binafsi umefanyika. Aidha Mpango umeeleza hatua muhimu za kuboresha sekta binafsi na kuoanisha ushiriki wa wake katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu.

Majukumu ya Asasi za Kiraia na Taasisi za Dini

Sekta binafsi yasiyo ya kibiashara ambayo yanajumuisha asasi za kiraia na kidini imekuwa na mchango mkubwa kwenye huduma za kijamii hususan afya, elimu na ujuzi. Katika kufikia mwaka 2020, sekta binafsi isiyokuwa ya kibiashara inamiliki takribani ya asilimia 50 ya taasisi za elimu ya juu, asilimia 40 vituo vya afya msingi na asilimia25 ya uwekezaji katikaelimu. Sekta ndogo hii imekuwa muasisi wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi huku shughuli zake nyingi zikinufaika na mchango Serikali kwa namna moja au nyingine.

Mpango huu, unalenga kuunganisha mchango wa sekta hii katika maendeleo ya uchumi kupitia mifumo ya kitaasisi inayofaa katika kuendeleza mshikamano mzuri wa sekta hii na sekta binafsi pamoja na sekta ya umma. Aidha, Mpango utajikiata katika kukuza uwekezaji mbalimbali katika maeneo mengine muhimu ya kimkakati ya uzalishaji wenye kuongeza thamani na shughuli zinazozalisha ajira. Hii inahusisha kukuza mashirika ya kijamii yasiyokuwa ya kibiashara ambayo yanahudumia wanawake na makundi ya vijana katika uchakataji wa mazao ya chakula, utengenezaji wa vinyago, kilimobiashara, katika sekta za jamii na mazingira kama vile elimu, afya, mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa mazingira.

3.3 Changamoto za Kisera na Kiudhibiti zinavyoathiri Maendeleo ya Sekta Binafsi

Sekta binafsi nchini Tanzania inasimamiwa na sheria na taasisi mbalimbali. Serikali imechukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na: Mpango wa Maboresha ya Mazingira ya Biashara na Uwekezaji wa Mwaka 2010, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) wa mwaka 2004, kuta vitambulisho vya taifa, kuandaa mpango wa kuboresha mifumo ya udhibiti wa biashara ili kuimarisha mazingira ya uwekezaji (Blueprint for Regulatory reforms to Improve the Business Environment) kwa kushirikiana na sekta binafsi, na kufanya marekebisho ya Kanuni za Sheria ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa kupunguza viwango vya ada na tozo; Kuhuisha majukumu ya Shirika la Viwango (TBS) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ili kuondoa muingiliano wa majukumu; kutoa Mwongozo unaoelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa vibali vya ujenzi ndani ya siku saba za kazi; Kuanzishwa kwa mfumo wa malipo ya kodi na tozo za Serikali kwa njia ya kieletroniki; kuanzishwa kwa Kituo kimoja cha utoaji huduma bandarini kinachofanya kazi masaa 24 na kuanzishwa kwa vituo vya utoaji wa huduma kwa pamoja mipakani (One Stop Border Posts). Hatua hizi zmesababisha kuongezeka kwa ushiriki na washiriki mbalimbali wa sekta binafsi kwenye uchumi wa taifa.

Pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali, bado kuna na ugumu au gharama za biashara za mipakani, kuanzisha biashara, udhaifu wa kulinda uwekezaji wa sekta binafsi, kodi na tozo mbalimbali, na udhaifu wa usimamizi wa mikataba. Serikali itaendelea kuchukua hatua katika maeneo haya muhimu kwa kuendelea na maboresho ya kisera, kisheria, kiutendaji na kitaasisi ikiwa ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa mikopo, urahisishaji wa kupata vibali vya ujenzi na usajili wa mali, na uamuzi wa ufilisi. Lengo hasa ni kurahisisha na kupunguzia sekta binafsi gharama ya rasilimali fedha na muda pamoja na kujenga misingi ya kuaminiana kati ya Sekta binafsi na Sekta ya Ummma.

Utekelezaji wa Mpango wa Tatu umelenga kufanyia kazi changamoto za miundombinu, ujuzi na tafiti, vikwazo vya kisera na kiudhibiti katika maeneo muhimu yafuatayo ya uendeshaji wa sekta binafsi:

(i) **Miundombinu:** Serikali itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya usafir na usafirishaji, nishati, maji na uhifadhi ili kuweza kupungu gharama za uzalishaji na usafirishaji na kuifanya Sekta binafsi kuwa shindani.

(ii) **Ujuzi na tafiti:** Serikali itaendelea kuwekeza kwa wingi kwenye miundombinu ya elimu na maendeleo ya taifi kwa lengo hasa la kuzalisha wataalamu wengi wenye ujuzi wa hali ya juu katika ngazi zote unaoendana na mahitaji ya sekta binafsi. Aidha, serikali iwawekeza kwenye tafiti za mbegu bora na teknolojia mbali mbali ili kuwezesha sekta binafsi kunufaika na matokeo ya tafiti hizo na kuongeza tija na ushindani. Katika hili, serikali itaandaa mfumo ambao uahakikisha kuwa seri ya umma, sekta binafi na taasisi za tafiti na uvumbuzi zinashirikiana kwa kazibu

(iii) **Tozo na Ada:** serikali itaendelea kuboresha mfumo wa tozo na ada ili kupunguza wingi wa tozo na ada ambazo husababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na hivyo kuifanye sekta ishindwe kushindana na hivyo inathiri utendaji na ukuaji.;

(iv) **Mitaji na mikopo:** Kampuni ndogo ndogo, ndogo na za kati (MSMEs) zinashindwa kupata rasilimali fedha kutoka benki na taasisi za fedha kutokana na taasisi hizo kuhitaji dhamana, taarifa sahihi za kihasibu na maandiko ya miradi inayokopesheka. Kukabiliana na changamoto hizi Mpango wa tatu utaweka mikaka yah atua za kuchukua kuhakikisha kuwa mikopo kwa sekta hii inapatikana;

(v) **Ardhi ya uwekezaji:** Kupitia Mpango wa Tatu, serikali imeweka hatua mbali mbali za kuchukua kwa lengo la kurahisiha upatikanani wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya uwekezaji kama vile mashamba, viwanda, huduma za afya, shule, hoteli na mali nyinginezo za kibiashara.

Ushirikiano kati ya sekta binafsi na serikali: changamoto za sekta binafsi haziwezi kutatuliwa na serikali peke yake bila ushiriki wa dhati wa sekta binafsi. Mpango wa Tatu unaweka mfumo wa ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi kwa lengo la kujadili na kutafuta ufumbuzi wa pamoja na kujenga kuaminiana kwa pande zote.

Sera na Nafasi ya Taasisi kwenye Maendeleo ya Sekta Binafsi

Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mazingira ya biashara kwa maendeleo ya sekta binafsi. Katika kujenga mazingira haya kuna maboresho kadhaa yamechukuliwa na Serikali. Hii ni pamoja na: uanzishwaji wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) kama jukwaa la masahuriano ya mara kwa mara kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kutatua changamoto zinazoikabili sekta binafsi; Mpango wa Maboresho ya Mazingira ya Biashara na Uwekezaji ya mwaka 2010; Mpango wa Maboresho ya Mfumo wa Sheria na Udhibiti; kuanzishwa kwa vitambulisho kwa

wajasiriamali wadogo; Kuanzisha Vitengo vinachosimamia Matumizi ya Rasilimali za Ndani; na kuyapandisha hadhi masuala ya uwekezaji kuwa chini ya Ofisi ya Rais. Maboresho haya ya sera na kitaasisi yamesaidia kubadili mitazamo na muitikio wa sekta binafsi. Ili kufanikiwa zaidi, masuala yote haya yatakuwa na matokeo makubwa endapo kutakuwa na uratibu wa hatua muhimu za kimkakati katika kuhudumia sekta binafsi.

Majukwaa ya majadiliano kupitia Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) katika ngazi ya Taifa, wizara, mikoa na wilaya yametoa wigo kwa kushughulikia masuala ya sekta binafsi na kuhamasisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kujenga maafikiano na uelewa wa pamoja. Hata hivyo, imebainika uwezo wa asasi mwamvuli za kusimamia maendeleo ya sekta binafsi katika kuwakilisha wanachama wake kwenye majadiliano ya Sekta ya Umma na Binafsi ni dhaifu, zinakosa takwimu na msimamo wa pamoja na kukosa agenda zilizofanyiwa utafiti wa kutosha. Asasi mwamvuli hizo za uwakilishi ni pamoja na Jukwa la Sekta Binafsi - TPSF, Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania - CTI au Shirikisho la Biashara, Viwanda na Kilimo-TCCIA hazijaweza kuwavutia wadau wote katika sekta binafsi katika majukumu yao. Hii ni kwasababu hazijaweza kuanzisha hatua za kushughulikia changamoto mtambuka katika sekta zote. Aidha, Mpango wa Tatu unalenga kuwa na mfumo mpana wa taasisi mpya kama vile waendeshaji wapya wa sekta binafsi, watu wenye ulemavu kujumishwa katika ngazi ya sekta. Kuongezeka huko kwa mawanda ya mfumo kwa kuzihusisha taasisi nyingine kama vile Kitengo cha Taifa cha Tija itakuwa ni muhimu kuboresha mitazamo ya sekta binafsi katika masuala ya ufanisi ushindani na ubora wa utoaji huduma bora. Hivyo, uhusiano unaoendelea kati ya sekta ya umma na sekta binafsi utaimarishwa zaidi kwa kipindi cha miaka mitano ya Mpango wa Tatu.

3.4 Matumizi ya Rasilimali za ndani katika uzalishaji na Maendeleo ya Ndani ya Kiuchumi

Katika kufikia ushindani unaoongozwa na uchumi wa viwanda, Mpango wa Tatu umelenga kuhamasisha uzalisha kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchi. Aidha, mpango unalongo la kuvutia uwekezaji kutoka nje na ushirikiano wa wawekezaji kutoka nje na wawekezaji wa ndani ili ili kuweza kupata mitaji mipya, teknolojia na ujuzi wa kimenejimenti. Hii ni muhimu katika kuimarisha wafanyabiashara wa ndani kushiriki kwenye sekta zenye fursa kubwa kwa ushiriki mpana na jumuishi ukiwemo kilimo, uchimbaji wa madini na utalii. Utumiaji wa rasilimali za ndani katika uzalishaji ni muhimu zaidi katika sekta mpya na zinazoibuka kama vile mafuta na gesi ambazo programu za ubunifu na hatua za kutengeneza fursa kuwezesha ushiriki mkubwa kwenye fursa za uwekezaji zinazoibuka unahitajika. Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuandaa sera ya utumiaji wa rasilimali za ndani katika uzalishaji kwenye sekta ya mafuta na

gesi. Vile vile serikali itaandaa, miongozo madhubuti ya kisheria na kiutawala ikiwa pamoja na masuala ya ubora, bei, muda na chanzo.

Ili kuwa na matokeo mikakati ya utumiaji wa rasilimali za ndani na maendeleo ya kiuchumi ya jamii yatarasimishwa kwa ajili ya kuwa na uhakika na kutabirika, hivyo kuruhusu biashara kujumuishwa kwenye mipango yao na taratibu za usimamizi wa minyororo ya ugavi. Mpango wa Tatu utashuhudia kustawi kwa daraja la wajasiriamali wa ndani katika jamii na kueleza bayana sio tu katika kuzalisha fursa endelevu za ajira na kuharakisha ukuaji wa uchumi.

3.6 Hatua za kimkakati kwa maendeleo ya sekta binafsi

Hatua zinazopendekezwa katika ngazi ya sekta zimezingatia nafasi muhimu ya sekta binafsi, ikijumuisha kuifahamu vizuri na kukidhi mahitaji ya watendaji wa sekta binafsi. Serikali inatambua umuhimu wa kuwezesha sekta binafsi kwa kuchukua hatua za kimkakati zenye kuleta matokeo yaliyokusudiwa. Hatua mahsusi ambazo sekta ya umma itazichukua kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango zinajumuisha maeneo mapana yafuatayo: (A: kuboresha mazingira ya biashara; B: kupanua upatikanaji wa miundombinu ya kiuchumi na kijamii; na C: kusaidia uendelezaji wa shughuli za kibiashara).

(a) Kuboresha mazingira ya biashara

Mazingira mazuri kwa ajili ya mipango ya kibiashara na uendeshaji ni muhimu kwa sekta binafsi iliyothabiti yenye ushindani na endelevu. Hatua zitakazopewa kipaumbele katika kuboresha mazingira ya biashara ni:

i. Utulivu wa uchumi jumla. Serikali itaendeleza utulivu wa uchumi jumla ambao utawezesha ukuaji wa uchumi kwa kiwango cha watsani wa asilimia 8 kwa mwaka ifikapo 2025, mfumuko mdogo wa bei kwa mwaka usiozidi asilimia 5, utulivu wa sarafu, na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni.

ii. Kuendelea na utekelezaji shirikishi wa Mpango wa Maboresho ya Mfumo wa Sheria na Udhibiti.

iii. Kuimarisha majadiliano ya kisera kati ya sekta ya umma na binafsi kupitia kwa mfumo gatuzi na ulioimarishwa wa Baraza la Taifa la Biashara na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEMC).

iv. Kuboresha mfumo wa usimamizi wa masoko ili kuwezesha ushindani uwe haki na kwa gharama nafuu.

(b) kupanua upatikanaji wa miundombinu ya kiuchumi na kijamii

Miundombinu toshelezi ikijumuisha taratibu na umiliki wa ardhi, usafiri, umeme, maji, na miundombinu ya TEHAMA ni suala muhimu la uendeshaji wa biashara vizuri na wenye nafuu katika uendeshaji wa biashara. Vile vile, upatikanaji wa

huduma bora za jamii kama vile elimu, afya, huduma za mahakama unapunguza athari ya gharama kubwa ya uendeshaji wa shughuli za kibiashara, hivyo kuchangia maendeleo ya haraka ya sekta binafsi. Kwa msingi huo, hatua zifuatazo zitachangia juhudi za kuendeleza ushiriki wa sekta binafsi katika maendeleo ya kiuchumi nchini Tanzania.

i. Kuendelea kuwekeza katika rasilimali watu katika sekta za afya, elimu na nyinginezo na mifumo ya kiutawala kama ilivyooneshwa kwenye programu za kisekta

ii. Uwekezaji katika miundimbinu ya kiuchumi kama ilivyooneshwa kwenye programu za kisekta

iii. Uwekezaji ambao utaiweka Tanzania kuwa kitovu cha biashara kikanda kwa kuwa na usafiri wa anga, ardhini, baharini na usafiri wa maziwa na wenye ufanisi namuunganiko kwenye mfumo TEHAMA.

(c) Kusaidia uendelezaji wa shughuli za kibiashara

Mabadiliko halisi yanahitaji taarifa, takwimu na uchambuzi wa fursa na vikwazo vinavyokabili shughuli za kibiashara wakati wanaendelea na juhudi za kubaini hali halisi, na kuwezesha maamuzi yanayozingatia ushahidi na kutathmini ubora wa maamuzi yao. Mpango wa Tatu unaweka hatua na mazingira ya kuzilea biashara changa ili ziweze kukuwa Hatua hizo ni pamoja na:

i. Kutoa huduma wezeshi za kibiashara ikiwemo utoaji na ugharamiaji wa mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali wenye sifa, kuwezesha usajili/urasimishaji, kuboresha mipango ya biashara, na kutoa msaada wa kitaalamu wakati wa majadiliano na taasisi za kifedha;

ii. Kusaidia kutoa taarifa zinazohusu fursa, utetezi na ukuzaji wa vitega uchumi kwa ujumla;

iii. Kukuza madirisha mahsusi ya ugharamiaji kwa shughuli za biashara zenye sifa;

iv. Kuandaa au kusaidia maabara za uatamizi wa biashara, ikijumuisha wabunifu;

v. Kuwezesha uendelezaji na ufahamu wa huduma za maendeleo ya biashara ili kusaidia uwezo/ujuzi wa sekta binafsi kuendana na mnyororo wa thamani kwenye sekta za kipaumbele na kutumia fursa za upatikanaji wa masoko; na

vi. Kuimarisha kuendeleza utumiaji wa rasilimali za ndani na mikakati ya maendeleo ya uchumi wa jamii.

3.5 Kujenga Imani Katika Mijadala kati ya Sekta ya Umma na Binafsi

Mapitio ya uzoefu wa nchi unaonesha kwamba mara nyingi hayafanikiwi kutokana na kutoaminiana kati ya Serikali na sekta Binafsi. Ili sekta binafsi iweze kuimarika na kuwa na mchango mkubwa kwenye uchumi ni lazima pandezote mbili

ziaminiane. Hii itawezekana kwa kila upande kutimiza wajibu wake. Serikali inawajibu wa kuweka mazingira wezeshi na salama kwa sekta binafsi lakini pia sekta binafsi inawajibu ya kufanya shughuli zake kwa uwazi na kutoa taarifa sahihi kwa serikali. Mpango wa tatu unaweka msingi wa majadiliano kama nguzo kuu ya kujenga kuaminiana kwa kuhakikisha kuwa kuna mifumo ya kusikilizana na kufanyia kazi malalamiko, hoja na maoni ya sekta binafsi. Kwa upande wa sekta binafsi, mikakati ya Mpango wa Tatu inaitaka kuwa wawazi na kutoa taarifa sahihi za biashara, kuwa na ushindani wa haki, na matumizi sahihi ya vivutio vya uwekezaji vinavyotolewana Serikali. Mpango umeweka mazingira ya kuwa na uongozi wa juu wa nchi wenye dhamira ya dhati ya kushirikisha sekta binafsi. Inaaminika kuwa tofauii kati kati ya maofisa wa ngazi za juu wa Serikali na kundi la wafanyabiashara utapungua. Mfano unaotolewa wa Malaysia katika kipindi cha nyuma cha mwaka 1983, Rais wa Nchi alianzisha *Dhana ya Malaysia ya Pamoja* (Malaysia Incorporated Concept) ambapo viongozi wa juu waliishawishi sekta binafsi kuona kuwa maendeleo ya taifa ni kama shirika (corporate entity) ambapo sekta ya umma na sekta binafsi ni washirika. Dhana ya Malaysia ya Pamoja ilipatanisha mitazamo tofauti ya pande zote ambayo ilidumu kwa muda mrefu. Aidha, Malaysia ilitekeleza Mkataba wa Uadilifu (intergrity pact) ambao uliisaidia Serikali, wafanyabiashara na asasi za kiraia kupambana na rushwa kwenye manunuzi ya umma.

Tathmini ya kina itafanywa na mamlaka za nchi kama inavyohitajika na sheria ambapo itawataka sekta binafsi kutoa taarifa sahihi na hivyo imani ya sekta binasi itapimwa.

Boksi 1: Uanzishaji Biashara
Tanzania ni nchi yenye idadi ya watu ambayo ni vijana: asilimia 75 ya idadi kubwa ya watu iko chini ya umri wa miaka 35. Inakadiriwa kuwa kati ya vijana milioni moja (1) wanaoingia kwenye soko la ajira kila mwaka, ni vijana 200,000 ndiyo wanaofanikiwa kupata ajira wakati huo huo, na waliobaki 800,000 hawana uhakika wa kupata ajira rasmi na hivyo kujihusisha katika baadhi ya shughuli za ujasiriamali kwenye sekta rasmi na isiyo rasmi. Hivyo, ujasiriamali umekuwa njia pekee kwa vijana kujikimu wenyewe, hususan kwa kuanzisha shughuli za biashara ndogo na za kati kama wanaoanza biashara, shughuli za kibiashara ndogo na za kati, shughuli za biashara za kijamii. Baadhi ya vijana wajasirisamali wa leo wana ujuzi zaidi wa kuitumia ubunifu na teknolojia katika kupanua haraka shughuli zao katika kutatua changamoto za kijamii za nchi. Kuwepo kwa mazingira ya kidhibiti na kibiashara kwa biashara kama hizo ni muhimu katika kutatua changamoto kwa vijana Pamoja na changamoto kubwa kwa vijana katika kubadilisha mawazo yao na dira na kuwa mapato binafsi na kusaidia jamii na pia kuzifanya biashara zao. Ubunifu na fursa ya kukua haraka ni tofauti kubwa ikilinganishwa na biashara asilia ndogo na za kati. Ili kupata manufaa yanayotokana na biashara zinzaoanzishwa, na kutatua changamoto zilizotajwa hapo juu Serikali katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu utajikita katika kuweka mikakati inayolenga kuweka mfumo sahihi wa kisheria na uendeshaji biashara utakaotambua mahitaji mahsusi uanzishaji wa biashara, ikiwemo na upatikanaji wa mikopo na

msoko. Vile vile, hatua zilizopangwa chini ya Mpango Kambambe wa Maendeleo ya Fedha wa mwaka 2020/21 hadi 2029/30 Serikali itahamasisha manunuzi ya ndani kama eneo muhimu la mkakati wa kuongeza matumizi ya rasilimali za ndani kwa sekta zote za umma, matumizi ya mashirika ya umma kwa kuandaa mkakati wa manunuzi ya ndani na kuhamasisha matumizi ya Tathmini ya Fursa za Manunuzi ya Ndani kama sehemu ya Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii kwa miradi yote mikubwa. Kampuni zitahamasishwa kushiriki kwenye mpango maalumu wa manunuzi ya ndani kama sehemu ya taarifa za uwajibu wa mashirika kwa jamii. Serikali, itafanya uchambuzi wa uwezekano wa kuwa na vivutio maalumu kwa ajili ya utekelezaji wenye matokeo ya mikakati hiyo.

SURA YA NNE

MSINGI WA UTEKELEZAJI WA MIKAKATI YA MPANGO

4.1 Utangulizi

Kama inavyoelezwa katika Sura ya Kwanza, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa unaelekeza juhudi za Taifa katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na kuimarisha nafasi ya Tanzania katika uchumi wa kipato cha kati yenye uchumi shindani, shirikishi, unaochagizwa na viwanda na unaozingatia maendeleo ya watu. Sura hii inatoa msingi, msukumo na dhana ya Mpango kwa kuainisha maeneo muhimu ya utekelezaji ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa. Pamoja na mambo mengine, Mpango unasisitiza umuhimu wa sayansi, teknolojia na ubunifu katika kuimarisha uchumi shindani ili Taifa liweze kuwa na ushiriki wenye manufaa katika biashara ya kimataifa.

Sehemu ya 4.2 inajikita kuimarisha nafasi ya Tanzania katika uchumi wa kipato cha kati. Sehemu ya 4.3 inaweka misingi inayoongoza hatua mahsusi za utekelezaji ili kufikia malengo ya Dira 2025. Sehemu ya 4.4 ni mapitio ya uzoefu wa kujenga uchumi shindani katika soko la kimataifa na kwa nia ya kujifunza. Sehemu ya 4.5 inafungamanisha dhana ya Mpango na ushindani, uchumi wa viwanda na biashara, ambapo utawala bora na maendeleo ya jamii zinategemewa kuoanisha Mpango na malengo ya Dira 2025. Sehemu ya 4.6 inaelezea dhana fungamanishi kama mwongozo kwa Serikali na sekta binafsi katika kubuni na kutekeleza mikakati mahsusi ya kuongeza kasi ya kufikia malengo ya Dira 2025.

4.2 Kuimarisha Nafasi ya Nchi katika Uchumi wa Kipato cha Kati

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa unakusudia kuendeleza mafanikio ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo iliyotangulia ikiwemo Mikakati ya Kupunguza Umaskini na Mpango Elekezi wa Muda Mrefu (LTPP). Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Kwanzaulilenga kuibua fursa fiche kwa kuwekeza kwenye miundombinu msingi na Mpango wa Pili ulijikita kujenga uchumi wa viwanda. Kama ilivyokuwa kwa mikakati iliyotangulia ya kupunguza umaskini, Mpango wa kwanza na wa pili iliendelea kusisitiza umuhimu wa maendeleo ya watu kama lengo kuu.

Ujenzi wa miundombinu kwa nchi kama Tanzania, ni mchakato endelevu ujenzi wa uchumi wa viwanda. Mikakati inayopendekezwa katika Mpango wa Tatu ni mwendelezo wa kujenga mifumo ya miundombinu ya uchukuzi, usambazaji maji, gridi ya Taifa ya umeme, na mtandao wa mawasiliano vijijini na mijini. Mifumo hiyo ya miundombinu itarahisisha upatikanaji wa masoko na urahisi wa utoaji kutoa huduma za kijamii. Sera za kiuchumi zitahimiza utulivu wa uchumi na

mazingira rafiki ya uwekezaji na biashara, matumizi endelevu ya rasimali za nchi na kunufaika na nafasi ya nchi kijiografia. Yote haya yanalenga kuimarisha uwezo wa uzalishaji na hivyo kujenga msingi wa kukuza uchumi.

Kwa kufikia uchumi wa kati kabla ya muda uliokusudiwa, Tanzania inaongeza matumaini ya kufikia malengo mengine ya Dira ifikapo mwaka 2025. Hata hivyo, msukumo mkubwa zaidi unahitajika, kwani kama ilivyoainishwa katika Sura ya Pili, Tanzania haijawahi kufikia lengo la ukuaji la asilimia 8. Jitihada za kuimarisha uchumi wa viwanda, ushindani na biashara ya kimataifa zinatarajiwa kuwa msingi wa kuongeza tija na mauzo nje. Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa inaleta pamoja malengo yanayoshabihiana katika kujenga uchumi imara na shindani. Chini ya Mpango huu, mkazo utawekwa katika ujenzi wa uchumi wa viwanda na kuuza nje bidhaa na huduma zilizoongezwa thamani pamoja na kutosheleza soko la ndani. Ili kuongeza ushiriki katika biashara ya kimataifa, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:

(a) Uelewa wa mwenendo, fursa, na changamoto zinazotokana na mpangilio wa sasa wa uchumi wa dunia. Suala hili linahitaji uelewa zaidi wa dhana ya ushindani wa biashara kimataifa; na
(b) Msingi imara wa uzalishaji unaojipambanua kwa mageuzi ya kisekta, hususani mchango wa sekta ya kilimo katika pato ghafi la taifa (GDP) ukilinganishwa na viwanda na huduma.

Kwa msingi huo, Mpango unajumuisha vichocheo vya ushindani katika masoko ya ndani na ya kimataifa na sekta zote kwa kutumia Sayansi-Teknolojia-Ubunifu (SATU) ili kuongeza wigo wa uzalishajina mauzo ya nje. Mbali ya ukuaji wa uchumi, malengo mengine yanayohusiana na maendeleo ya watu ni muhimu yafikiwe. Kwa mantiki hiyo, uchumi unahitajika kukua zaidi ili kuongeza rasilimali fedha za kugharamia shughuli za maendeleo ya kijamii. Uchumi unaokua kwa kasi utaepusha nchi kurudi kwenye kundi la nchi zenye uchumi wa kipato cha chini. Hivyo, Mpango unategemewa kulielekeza Taifa kufikia uchumi wa kipato cha kati cha juu (upper-middle income status).

Pamoja na jitihada za kuongeza mauzo nje, Tanzania ina kila sababu za kuimarisha soko la ndani kwa kuongeza bidhaa za viwandani ili kukidhi mahitaji yanayoshabihiana na kipato na ubora wa maisha yanayoendana na uchumi wa kipato cha kati. Kadiri kipato cha wastani cha kila Mtanzania kinavyoongezeka, soko imara la ndani linahitajika ili kupunguza athari ya kudorora kwa mauzo nje ya nchi kutokana na mtikisiko unaoweza kutokea katika masoko ya Kimataifa. Kimsingi, ukuaji madhubuti wa uchumi utasaidia kujenga ustahimilivu na utayari wa kukabiliana na athari hasi za mitikisiko ya kiuchumi na kijamii ikiwemo

magonjwa ya mlipuko, mabadiliko ya tabia ya nchi, kuporomoka kwa bei kwenye soko la dunia, ushindani wa kibiashara na mahusiano mabaya ya kidiplomasia.

Katika jitihada za Kujenga Uchumi Shindani wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu, Mpango unaasili mazingira ya Tanzania na kutumia uzoefu wa nchi zilizoendelea na zinazoendelea kiviwanda katika kuandaa mikakati na vipaumbele. Aidha, Mpango huu umezingatia makubaliano na mikataba ya kikanda na kimataifa ikiwemo ya mazingira na mabadiliko ya tabia-nchi inayotoa mwanga na miongozo ya kimkakati katika nyanja za maendeleo ya jamii.

4.3 Misingi na Kanuni za Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa

Mpango unatambua kuwa umoja wa kitaifa na kijamii, utawala wa sheria, haki za binadamu, usawa, na amani na usalama, ni misingi muhimu inayowezesha kufanyika kwa shughuli zote za kiuchumi na maendeleo ya jamii. Mambo mengine yanayoendana na misingi hii ni utawala bora, kuendeleza vita dhidi ya rushwa na matumizi sahihi ya rasilimali fedha na maliasili.

Katika kutekeleza Mpango huu na hata baada ya hapo, sera za kiuchumi zitajikita katika kujenga uchumi jumuishi, shindani, na wenye mtangamano (integrated) kisekta. Uchumi huu utategemea ujenzi wa viwanda na utoaji wa huduma kwa kutumia mifumo iliyojikita kwenye matumizi ya Sayansi,Technolojia na Ubinifu (SATU). Ili Mpango huu uweze kuleta matarijio ya kiuchumi na kijamii yaliyokusudiwa, utekelezaji wake utapaswa kuongozwa na misingi ifuatayo:

(i) Kuwa na kiwango cha ukuaji wa uchumi (GDP) usiopungua asilimia nane (8%) kwa mwaka. Mwenendo huu utaifanya Tanzania kuimarika kama nchi ya uchumi wa kati, hususani kwa upande wa kipato na maendeleo ya jamii na hivyo kukwepa hatari ya kurudi nyuma na kuwa nchi ya kipato cha chini;

(ii) Watanzania watatakiwa kuimarika na kusimamia haki zao za maamuzi ya kiuchumi kikamilifu kwa ajili ya manufaa ya raia wote, hususani maamuzi ya umiliki na uvunaji wa maliasili za Taifa, ikiwa ni pamoja na ardhi, anga, maji, madini, mafuta, gesi asilia na misitu;

(iii) Taifa kuendelea kusimamia kwa karibu uvunaji wa maliasili. Hili linajumuisha kujenga uwezo kwa wataalamu wa ndani katika teknolojia ya uziduaji, uchenjuaji, na michakato mingine ya kuongeza thamani; kujenga uwezo wa ndani katika kusimamia mikataba, majadiliano juu ya uzalishaji, na mgawanyo wa faida; kuimarisha ushiriki wa wazawa; na kuhakikisha kwamba uziduaji unafuata kanuni za mazingara endelevu kwa ajili ya manufaa ya kizazi cha sasa na cha baadaye;

(iv) Nchi itaendelea kuwekeza kwenye miundombinu msingi ya kiuchumi (kama vile miundombinu ya usafiri wa nchi kavu, majini, na anga; nishati na huduma ya maji). Aidha, miradi yote ya maendeleo itatakiwa kutenga

gharama za uendeshaji na matengenezo na kuhakikisha upo ulinzi dhidi ya wanaohujumu miundombinu ili kuhakikisha kuwa ubora wa huduma zitolewazo na miundombinu hiyo unakuwa endelevu;

(v) Nchi itaendelea kuimarisha miundombinu ya mifumo ya kidigitali – mfano, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa ajili ya mtandao wa mawasiliano ya simu nchi nzima ili kuwezesha wananchi kupata manufaa ya mapinduzi ya kidigitali/TEHAMA na maendeleo ya huduma za kimtandao kwenye sekta ya fedha, afya, elimu, utawala wa umma, mahakama na taarifa za masoko;

(vi) Kilimo kitafanyiwa mageuzi na kuwa cha kibishara, badala yakuwa tu kwa ajili ya usalama wa chakula, na kwamba wakulima watapewa motisha kuwekeza katika kilimo hicho;

(vii) Kwa kutumia ushirikiano wa kimataifa, Tanzania ishiriki kikamilifu kudumisha amani kimataifa na kikanda na kutumia diplomasia ya uchumi katika kuimarisha biashara ya nje na uwekezaji wakati huo huo ikisimamia ushindani halali katika soko la ndani na masoko ya nje;

(viii) Tanzania itaweka mazingira wezeshi ya biashara yaliyoboreshwa na yenye uwazi kuruhusu sekta binafsi kushamiri na kurasimisha sekta isiyo rasmi. Katika hili, mambo yafuatayo yatahitajika:

a) Kuunganisha kanuni na matakwa ya usajili, malipo ya tozo na kodi na masharti mengine ili iwe rahisi kwa wafanyabiashara kutii bila shuruti.

b) Kupitia upya majukumu ya mamlaka za udhibiti ili kubainisha na kutenganisha jukumu la kukusanya mapato ya Serikali na lile la kuwezesha biashara.

c) Kujenga uwezo na kuimarisha matumizi ya kidigitali/TEHAMA ili kupunguza mianya ya rushwa, ikiwa ni pamoja na mamlaka za udhibiti kupunguza kutoa huduma za ana kwa ana kwa wateja wao.

(ix) Ili kukuza ajira, mikakati zaidi inahitajika mbali ya mikakati ya kuimarisha sekta binafsi. Mikakati hiyo ni pamoja na:

a) Kupitia kwa makini adhima ya kuuimarisha mipango iliyopo ya kuwawezesha vijana na wanawake, hususani kwa kuwapatia maarifa maalumu na mikopo ya riba nafuu; na

b) Kusaidia wahitimu wa ufundi na uhandisi ambao wameonesha uwezo wa kuanzisha biashara na uzalishaji kwenye sekta ya teknolojia. Katika haya mawili – (a) na (b) hapo juu, unahitajika ufuatiliaji na tathimini (M&E) ili kubaini mafanikio ya wanufaika na mwenendo wa marejesho ya mkopo kwa lengo la kuwanufaisha wengine;

(x) Serikali itashiriki kwenye uwekezaji na biashara za kimkakati, zenye maslahi ya kitaifa, na ambazo ama hazivutii uwekezaji wa sekta binafsi au sekta binafsi haina uwezo wa kugharamia; na kwamba mashirika ya umma na ya sekta binafsi yatajitahidi kuongeza ushindani katika soko la ndani na la kimataifa;

(xi) Kuongeza mawanda ya mazungumzo kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kutanzua masuala yenye maslahi kwa pande zote;

(xii) Serikali itasimamia mazingira ya uwekezaji na biashara ambayo ni imara na ya kutabirika ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. Pamoja na mambo mengine, juhudi zitaelekezwa kwenye:

a) Kusimamia uchumi imara na unaokua kwa kasi, kusimamia makusanyo ya mapato ya ndani na sera za kudhibiti mfumuko wa bei kwa kutumia sera wezeshi za kifedha na kodi;
b) Kupunguza utegemezi wa misaada toka nje;
c) Kujenga na kuimarisha rasilimali watu, kwa kuwa na watu walioelimika, wanaopenda kujifunza na wenye ujuzi hususani kwenye sayansi na teknolojia;
d) Kuhakikisha kwamba nguvu kazi inapewa motisha stahiki;
e) Kuimarisha na kulinda ustawi na mazingira ya kazi katika sekta zote; na
f) Kuimarisha uhifadhi na ulinzi wa mazingira ili kupunguza athari za mabadiliko ya tabia-nchi.

4.4 Uzoefu wa Nchi nyiingine katika Kujenga Uchumi Shindani

Dhana ya uchumi shindani ni pale ambapo kampuni zinapoweza kuuza bidhaa katika mazingira huru na ya haki katika soko la dunia kwa kuzingatia ushindani wa bei na ubora wa bidhaa na huduma. Dhana hii inachukulia soko la dunia kuwa ni soko lisilo na ukinzani wa aina yoyote. Lengo la kila taifa ni kuongeza ushiriki katika biashara ya kimataifa na kuvuta mitaji , huku ikiimarisha uwezo wake wa uzalishaji na kuongeza wigo wa bidhaa kulingana na mahitaji ya soko.

Kutokana na sababu mbalimbali, ushindani katika soko la dunia siyo kila wakati unakuwa huru na haki. Kwa sababu za kiuchumi na kisiasa, nchi mbalimbali huweka vizuizi vya kibiashara kwa kutumia ushuru wa forodha au vikwazo vya biashara visivyo vya ushuru. Kutokana na vizuizi hivi, mifumo ya kimataifa ya biashara imetumika kutoa fursa kwa nchi mbalimbali kukubaliana namna ya kufungua masokoIkiwemo kwa mfano, makubaliano ya kibiashara ya kupendeleana (preferential trade arrangements). Hata hivyo, makubaliano kama hayo aghalabu huficha ukweli uliopo wa ushindani baina ya nchi na nchi. Ukweli ni kwamba kila taifa linajitahidi kuweka mazingira ya biashara ya nje yanayowezesha kampuni zake kuuza zaidi na kuongeza ushiriki wake kwenye soko la kimataifa, kuvutia mitaji ya nje na kuimarisha ajira kwa watu wake. Mataifa hufanya hivyo kwa kusimamia, pamoja na mambo mengine, mazingira bora ya uwekezaji na biashara, miundombinu imara, ubora wa nguvukazi, ufanisi wa forodha na sera rafiki za kikodi na zinazotabirika.

RASIMU

Machapisho mbalimbali ya kupima uchumi shindani yameainisha vigezo mbalimbali vinavyozingatiwa na waandaji wa sera katika jitihada za kuyawezesha makampuni ya nchi zao kukua na kushindana kimataifa na kuvutia uwekezaji kutoka nje. Vigezo hivyo kwa pamoja vinaonesha maeneo ya kuwekewa mkazo na Serikali na kampuni za ndani. Maeneo ya kuzingatia ni: uimara wa uchumi, ubora wa miundombinu (uchukuzi, nishati, mawasiliano); rasilimali watu (vipaji, ujuzi, afya, ubunifu, na uadilifu); ufanisi wa taasisi;kiwango cha mtaji/ugharamiaji; uwazi na kutabirika kwa mfumo wa udhibiti wa biashara;; gharama za kufanya biashara; uimara wa thamani ya sarafu; na mchango wa Serikali katika Tafiti & Maendeleo (T&M).

Uchambuzi unaonesha kuwa, vigezo vinavyochochea uchumi shindani vile vile huvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ya nchi. Nchi mbalimbali hujitahidi kupunguza gharama za uzalishaji (kwa kuboresha miundombinu) na kuongeza tija ya nguvukazi kama vichocheo vikuu katika kujenga uchumi shindani wenye manufaa kwa nchi. Ushindani huu unatokana shughuli za kuongeza thamani zinazoongozwa na matumizi ya Sayansi-Teknolojia-na- Ubunifu. Ubunifu huwezesha uzalishaji wa bidhaa mpya, hupunguza gharama za uzalishaji na huongeza ubora wa bidhaa zinazozalishwa. Vile vile, ubunifu unaleta mbinu mpya za uzalishaji, bidhaa mpya, mbinu mpya za kusimamia uzalishaji, kubadilishana uzoefu na kujenga mahusiano ya kibiashara na jumuiya ya kimataifa. Uzoefu wa nchi zilizoendelea kiviwanda na nchi za Asia zinaendelea unaonesha kwamba ugharamiaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (SATU) na Tafiti na Maendeleo (T&M) umesaidia sana kuendeleza ubunifu. Pale inapobidi, Serikali hulazimika kutumia nguvu ya ziada ili kuhakikisha kuwa matokeo ya tafiti, maendeleo na ubunifu yanafanyiwa kazi ili kuimarisha ushindani wa nchi kibiashara.

Uzoefu unaonesha kwamba rasilimali watu, hususani, ujuzi wa hali ya juu, na maendeleo ya teknolojia ni msingi wa mageuzi katika mauzo nje ambayo sehemu kubwa ya thamani inatokana na mchango wa ujuzi. Uzoefu huu ni muhimu kwa Tanzania ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikiuza nje bidhaa ghafi. Rasilmali watu iliyobobea kwenye masuala ya SATU itawezesha kuzalisha bidhaa mbalimbali na kuiwezesha Tanzania kushiriki kwenye Mnyororo wa Thamani wa Dunia. Kwa ujumla, faida za ushindani katika soko la kimataifa huishia kwa nchi ambazo zinafanya vizuri kwenye Sayansi na Teknolojia katika kujenga uchumi shindani. Nchi hizo zimefanikiwa kuwa vinara katika mauzo kwenye soko la kimataifa kwa kuuza bidhaa ambazo zina ongezeko kubwa la thamani inayotokana na teknolojia ya kiwango cha kati na juu.

Kwa upande wa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ya nchi, katika miongo sita iliyopita, serikali za nchi zilizoendelea na zinazoendelea zimeanzisha taasisi za

ummaza kusaidia wawekezaji. Kwa nchi kupata wawekezaji wa nje kunamaanisha mtaji mpya unaoambatana na teknoljia mpya na ya hali ya juu, ujuzi wa usimamizi na masoko, mafungamano ya kibiashara na fursa za kuongeza mauzo nje. Kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania ni muhimu kuweka mkazo pia katika kuiwezesha sekta binafsi ya ndani ambayo bado ni changa.

Mtizamo mwingine wa Tanzania kwa sasa na siku zijazo ni kutofanya maamuzi ya shinikizo/haraka kuhusiana na rasilimali zilizopo kama vile madini, mafuta na gesi ambazo zinakimbiliwa na nchi zilizoendelea kiviwanda (Global rush) kutoka nchi zinazoendelea, ikiwemo Afrika. Nchi zinazoendelea zinaweza kuchagua: *ama* (i) kuendelea kuuza nje maliasili kabla ya kuzichakata kikamilifu *au* (ii) kuhakikisha maliasili zinaongezewa thamani kikamilifu kabla ya kuuza nje ya nchi. Chaguo la pili ndilo sahihi kwa maslahi mapana ya nchi. Hata hivyo, chaguo hili linahitaji mambo makuu mawili ambayo ni: (a) rasilimali watu yenye uwezo imara katika elimu, sayansi, na teknolojia; na (b) utashi wa kisiasa kusimamia makubaliano yenye manufaa kwa nchi. Mtazamo huu unapaswa pia kujumuisha maliasili zote, ikiwemo mazao ya uvuvi na misitu.

Tafiti katika nchi za Asia, ambazo zilitoka kwenye kundi la nchi za kipato cha kati cha chini na kuwa nchi za kipato cha kati cha juu tangu miaka ya 1960 hadi 2014, na kufanikiwa kuwa mahiri kwenye biashara ya nje, zinaonesha kuwa, mbali na vigezo vya nchi husika, kama vile idadi ya watu, maendeleo ya sekta ya fedha na kufanya kazi kwa bidii, bado mchango wa Serikali ni muhimu katika:

(i) Kuweka kipaumbele katika kugharamia maendeleo ya rasilimali watu kama msingi wa kuongeza thamani, kuendesha Tafiti na Maendeleo (TM), na ubunifu;
(ii) Kujenga miundombinu muhimu;
(iii) kujenga misingi ya utawala bora kwenye Sekta ya umma na taasisi; na
(iv) Kusaidia kukua na kuendeleza tabaka imara la wawekezaji wazawa.
(v) Ubunifu na utekelezaji wa mikakati na sera ya kuongeza mauzo nje uliwasaidia kuhama haraka kutoka kwenye uzalishaji wa bidhaa zilizokuwa zikiagizwa kutoka nje hadi uzalishaji wa bidhaa unaokidhi mahitaji ya ndani na ziada kwa ajili ya mauzo nje. Nchi hizo ziliweka jitihada za makusudi kwa kujenga uwezo wa ndani wa kiteknolojia uliowawezesha kukua, kuunda mitambo na taratibu kuanza kupunguza utegemezi wa kuagiza mitambo na teknolojia kutoka nje.

Katika nchi kama vile Korea ya Kusini, Brazil, Chile, Indonesia, Malaysia, Singapore, Thailand, na Vietnam, Serikali zilitengeneza dira zenye mvuto na kuwahamasisha wananchi kuitikia na kufuata kwa vitendo dira hizo. Maono hayo ya Serikali yalipokelewa vyema na wananchi wenye nidhamu na mitazamo chanya ya

uwekezaji. Hali hii iliwezesha tabaka la wawekezaji wazawa kuimarika na kushiriki kikamilifu katika mnyororo wa uongezaji thamani Kimataifa sawa na Makampuni mengine ya kimataifa yaliyokuwepo muda mrefu.

4.5 Mfumo wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa

4.5.1 Mawanda ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa

Mfumo wa Mpango unajikita katika kuimarisha nafasi ya Tanzania katika kundi la kipato cha kati yenye matokeo bora yanayotarajiwa. Mawanda ya utekelezaji wa Mpango yanafungamanishwa na dhana ndogo tano (5), ambazo utekelezaji wake unahitaji kuratibiwa na Sekta zote:

(a) *Uchumi Shindani*: Kukuza uchumi shindani unaotegemea maarifa mapya, SATU, na mapinduzi ya kidigitali katika sekta zote. Hii itaongeza fursa na shughuli za kuongeza thamani, ikiwa ni pamoja na kuzalisha bidhaa na huduma bora na za kisasa, na kuongeza tija katika uzalishaji;

(b) *Uchumi wa Viwanda na Huduma*: Mpango unaendeleza azma ya kujenga uchumi wa viwanda na utoaji wa huduma kwa kutumia maarifa mapya, SATU na mapinduzi ya kidigitali. Katika hili, Nchi itaongeza idadi ya viwanda vinavyotumia SATU katika kuongeza thamani kwenye sekta zote za uzalishaji na huduma. Hii itapelekea upatikanaji endelevu wa bidhaa na huduma kwenye soko la ndani na kwa ajili ya soko la nje. Aidha, msisitizo utawekwa kuhakikisha kwamba bidhaa za viwandani zinazouzwa nje zinakuwa na ubora na thamani ya hali ya juu.

(c) *Biashara na Uwekezaji:* Ukuaji wa mauzo nje utaongezeka kutokana na (i) kuimarika kwa ushindani; (ii) kuimarika kwa ujenzi wa viwanda na utoaji wa huduma. Njia bora ni pale bidhaa zinazouzwa nje zinapoongezewa thamani kwa kuzingatia matumizi sahihi ya SATUili kupata bei nzuri sokoni. Kwa kutambua mchango wa sekta binafsi katika uzalishaji na biashara, Mpango unalenga kutambua wajibu wa Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na ushiriki wa sekta binafsi katika biashara ya kimataifa. Malengo ya muda mrefu ni kuanza kuzalisha mitambo na malighafi za uzalishaji viwandani zinazoagizwa kutoka nje ya nchi kwa sasa;

(d) *Ubora wa Matokeo Tarajiwa ya Mpango:* Ubora wa matokeo tarajiwa ya Mpango ni ustawi na maendeleo ya watu - kama ilivyoelezwa kwenye Dira 2025. Malengo haya yatafikiwa kwa kugharamia shughuli za maendeleo ya jamii, hususani, upatikanaji elimu, afya, maji, na huduma za sheria na mahakama katika jitihada za kuleta maendeleo jumuishi; na

(e) *Maendeleo ya Watu*: Maendeleo ya watu yatajikita katika kuendeleza ujuzi wa rasilimali watu katika kutatua changamoto ya ujuzi mdogo (kama ilivyoainishwa katika Sura ya Pili). Uendelezaji wa rasilimali watu utaanzia katika ngazi ya elimu ya wali hadi elimu ya juu ikiwemo kuwawezesha vijana kujiajiri. Vile vile, msisistizo utawekwa katika kuboresha viwango vya utoaji

wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na ujuzi adimu kwa lengo la kuongeza tija na ushindani wa wananchi katika kutumia rasimali zilizopo nchini pamoja na kushiriki kikamilifu katika usanifu na ujenzi wa miradi mikubwa ya maendeleo. Hatua zilizoainishwa katika kuendeleza rasimali watu zinalenga kuendeleza maendeleo ya watu.

Wakati ukuaji wa uchumi utatokana na kuimarika kwa uchumi shindani, kasi ya ujenzi wa viwanda na utoaji wa huduma, na kuvutia biashara na uwekezaji maendeleo ya jamii yanatarajiwakuongeza ubora wa ukuaji huo. Muundo, unaooneshwa (Kielelezo Na. 2)umeanisha umuhimu wa utawala bora ambao ukikosekana mikakati ya kukuza uchumi na maendeleo ya jamii haiwezi kutekelezwa kwa misingi endelevu.

Kielelezo Na. 2 Muundo wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa



4.5.2 Utawala Bora

Dhana ya utawala bora inajumuisha tunu za Taifa kama vile umoja wa kitaifa; umoja wa kitaifa na utengamano wa watu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; amani na usalama; jamii inayoheshimu haki, usawana utu; utawala wa sheria; na utulivu wa kisiasa. Dhana hii pia inahitaji uwepo wa uwajibikaji kwa upande wa viongozi na raia. Mpango utaendelea kuenzi dhana hii kwa kuhakikisha kwamba wananchi wanashiriki katika maamuzi ya uzalishaji na ugawanaji wa pato litakalotokana na kukua kwa uchumi.

Katika utawala bora, Serikali ina wajibu wa kuimarisha mahusiano ya kimkakati na sekta binafsi nakutoa mwongozo wa masuala ya kiuchumi kwenye mahusiano ya kimataifa. Katika mahusiano ya kimataifa, Tanzania itafuata sera ya diplomasia ya uchumi yenye lengo la kuimarisha amani na usalama; usawa; na kuheshimu uhuru wa nchi nyingine kitaifa na kimataifa. Hivyo ni vigezo vya msingi ambavyo vikikosekana, shughuli za uzalishaji na biashara hazitaweza kufanyika kwa ufanisi ndani na nje ya nchi.. Diplomasia ya uchumi inahamasisha uwekezaji kutoka nje, biashara, na mawazo mapya ya maendeleo (elimu, uzoefu, mazungumzo, na maridhiano) kwa manufaa ya pande zote na kuimarisha uhuru wa kiuchumi. Aidha, taasisi za biashara na uwekezajina balozi za Tanzania nchi za nje kwa pamoja wataandaa na kusambaza taarifa juu ya fursa za uwekezaji na vivutio vya utalii.

Utekelezaji wa Mpango unategemea uaminifu na imani yawananchi iliyojengeka kutokana na mafanikio ya huduma za umma yaliyotokana na usimamizi mahiri na utawala bora wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo. Hatua madhubuti zilizochukuliwa katika kipindi hicho ni pamoja na mapambano dhidi ya rushwa, kuondoa wafanyakazi hewa, kudhibiti wizi kwenye sekta ya madini na maliasili nyingine, na vita dhidi ya biashara na matumizi ya madawa ya kulevya. Kuongezeka kwa nidhamu kazini, ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi ya fedha za miradi ya umma, kumeongeza hamasa na utashi wa wananchi katika kuunga mkono agenda ya kulinda rasilimali asili, tamaduni na maadili ya Taifa.

4.5.3 Ukuaji wa Uchumi

Eneo la kukuza uchumi katika Mpango huu linahimiza na kuleta matamanio ya kuongeza tija na ubunifu kwenye sekta zote za uchumi. Tija na ubunifu vinaleta ushindani katika ngazi ya mtu mmoja mmoja, kampuni, na hatimaye Taifa; na ushindani huo unatarajiwa kuongeza mauzo nje ya nchi. Katika eneo hili la kukuza uchumi, yapo maeneo matatu ambayo yana uhusiano wa karibu. Kwanza ni uchumi shindani kama inavyoainishwa katika Dira 2025. Vigezo vyake vikuu ni kama vilivyoainishwa katika Kielelezo na. 4.1. Hii inafuatiwa na ukuaji wa viwanda na huduma pamoja na biashara na uwekezaji. Ukuaji wa viwanda na huduma

unalenga mabadiliko ya kiuchumi yanayozingatia umuhimu wa ukuaji wa pato la Taifa ikizingatia (a) uzalishaji viwandani (b) kilimo (mazao,mifugo,misitu na uvuvi) na madini; na (c) huduma na biashara ambayo inaongozwa na mauzo nje pamoja na ongezeko la ukuaji wa uwekezaji kutoka nje.

4.5.3.1 Uchumi Shindani

Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha vigezo vinavyochangia kiwango cha ushindani wa kiuchumi ambavyo ni (a) maendeleo ya watu; (b) mazingira wezeshi ya uwekezaji na biashara; (c) mfumo wa masoko; na (d) mageuzi ya kidigitali katika kile kinachojulikana kama mapinduzi ya nne ya viwanda (4th Industrial Revolution). Katika maandiko mengi, vigezo hivyo vinatumika katika modeli mbalimbali na kulinganishwa katika nyanja tofauti za ushindani wa kimataifa. Vigezo hivi pia vinahusiana kwa namna moja au nyingine hususani katika namna vinavyopima maendeleo ya sekta binafsi.

(a) Maendeleo ya Rasilimali Watu

Uchumi shindani, kimsingi, unaimarishwa na rasilmali watu. Maendeleo ya rasilimali watu yanapatikana kwa kujenga na kutumia maarifa na maendeleo ya SATU katika kuongeza tija na ushindani katika sekta zote. Maendeleo ya rasilimali watu huwezesha kutumia maarifa na teknolojia kuongeza tija, thamani na ubora wa bidhaa zinazozalishwa katika sekta mbalimbali za kiuchumi zikiwemo bidhaa viwandani, kilimo, madini, ujenzi, na huduma. Katika hili, maeneo ya msingi ya kuzingatia ni kutumia bunifu mbalimbali za nchi zilizotangulia kwa kuimarisha mafunzo kwenye mapinduzi ya kidigitali yanayolenga kuongeza tija na uwezo wa ubunifu katika uzalishaji na huduma.

Rasilimali watu inachochea ujuzi, sayansi, teknolojia na uwezo wa ubunifu ikijumuisha uwezo wa usimamizi na kujenga mtandao wa mahusiano. Aidha, maendeleo ya rasilimali watu hutoa mwanya wa kufanya maboresho kuendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya soko. Dira ya Maendeleo 2025 sio tu kwamba inakusudia kujenga uchumi shindani bali pia uchumi wenye uwezo wa kufafanua na kulinda maslahi ya taifa na kuweza kubadilika kuendana na mahitaji ya masoko ya kikanda na kimataifa. Uwezo wa kubadilika kuendana na masoko unategemea uwezo uliojengwa kuendana na SATU. Teknolojia hii inawezesha kampuni kubuni, bidhaa mpya na za aina tofauti, mifumo mipya ya ubunifu, kubadili viwango vya uzalishaji, kuongeza ufanisi wa mitambo, kutumia malighafi chache,kupunguza gharama za uzalishaji na kuongezeka kwa tija. Yote haya yanawezesha kampuni hizi bunifu kuwa shindani na kukua kwa kasi.

RASIMU

Rasilimali watu huanza kujengwa tangu utotoni (early child development -ECD) na kwa kuimarisha lishe na afya katika miaka yote ya kwenda shuleni na mafunzoni na mkazo ukiwekwa katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, na Hisabati (SATUH). Kwa muda mrefu sasa, mataifa yaliyoendelea yamekuwa yakiwekeza kwenye Sayansi, teknolojia, uhandisi, na hisabati (SATUH) kwa kutambua kwamba ni njia madhubuti ya kukuza ubunifu, hususani katika viwanda. Mathalan, SATUH inahusishwa na mafanikio makubwa ya kiteknolojia yaliyofikiwa na nchi za Asia. Aidha, jitihada za ziada zinahitajika ili kuongeza hamasa ya wanafunzi wa kike katika masomo hayo.

Mpango utaelekeza rasilimali zilizopo ili kuhakikisha kuwa elimu ya msingi hadi ya juu na elimu ya ufundi zinazingatia mafunzo ya SATU na kidigitali. Hii ni pamoja na kuendelea kupanua miundombinu na vifaa vya kufundishia kulingana na mabadiliko ya idadi ya watu, ili kutoa huduma bora za elimu na afya zinazokidhi viwango vinavyopendekezwa kitaalamu (idadi ya wanafunzi kwa darasa; uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu; vifaa ya kufundishia; uwiano wa madaktari kwa idadi ya watu). Elimu inayokidhi viwango itahakikisha kuwa Taifa linapata rasilimali watu yenye ubora.

Kwa kifupi, yafuatayo yanapaswa kufanyika ili kuongeza rasilmali watu yenye ubora unaotakiwa:

(i) Elimu ya msingi na sekondari: kuboresha elimu kuanzia ngazi ya msingi hadi sekondari na kuifanya iweze kuendana na mahitaji ya SATU na maendeleo ya kidigitali;

(ii) Vyuo vikuu, vyuo vya ufundi, na taasisi za T&M: kupanga upya mtaala kwa kukazia masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (SATUH) na kusisitiza elimu kwa vitendo. Ili kufanikisha hilo, utawekwa utaratibu rasmi kuunganisha taasisi za elimu ya juu na vyuo vya ufundi na soko la ajira ili kuhakikisha taasisi hizo zinafundisha ujuzi unaohitajika sokoni;

(iii) Mafunzo na elimu ya ufundi: Eneo hili litaimarishwa kwa kufanya yafuatayo: (a) kuimarisha na kupanua elimu na mafunzo ya ufundi; na (b) kubuni programu ya kiwango cha juu ya mafunzo (miaka 3 hadi 4) kwa ajili ya kupata mafundi wa hali ya juu; na

(iv) Kuanzisha mfuko maalum (mbali na mifuko iliyopo) wa kuwawezesha na kuwachochea wahitimu wa vyuo kubuni miradi ya pamoja ya uzalishaji na biashara. Mfuko huu pia utawezesha kubuni na kutekeleza programu za miradi anzilishi ya teknolojia kama sehemu ya mkakati wa kitaifa wa mapinduzi ya kidigitali.

Jukumu la Taasisi za Ubunifu

Serikali kupitia 'taasisi za ubunifu' itaweka njia bora ya kuharakisha utekelezaji na uimarishaji wa taasisi hizi. Hata hivyo, kuna haja ya kupitia tena majukumu ya taasisi hizo kwa madhumuni ya kuzifanya ziweze kutoa suluhisho kwa changamoto za wakulima, wenye viwanda, na watumiaji wengine wa teknolojia. Taasisi hizo ni pamoja Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Shirika la Uhandisi na Uzalishaji wa Viwanda (TEMDO), Kituo cha Zana za Kisasa cha Kilimo na Teknolojia ya Vijijini (CAMARTEC), Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO). Na kwa afya ya umma, ni Taasisi ya Kitaifa ya Utafiti wa Tiba, (NIMR). Aidha, taasisi nyingine ni vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu ambazo zinatoa taaluma kadhaa, kufundisha na kufanya utafiti. Matokeo ya tafiti mbalimbali zitafuatiwa na maelezo ya kiufundi, majaribio ya matumizi, modeli-elekezi (prototypes), majaribio ya ustahimilivu, usalama wa watumiaji na kisaliji hataza na hati miliki. Kubadilisha matokeo ya utafiti kwenda kwenye matumizi makubwa ya uzalishaji kutafanywa baada ya itifaki ya uchambuzi wa mradi kukamilika.

(b) Mazingira Wezeshi ya Biashara na Uwekezaji

Mazingira ya biashara na uwekezaji yanajumuisha masuala kadhaa, yakiwemo kuunda taasisi sahihi na zenye uwazi, sera, sheria, na kanuni ambazo zinawezesha biashara na uwekezaji kuwa wa faida na endelevu . Aidha, ni lazima kuwe na uchumi imara na miundombinu wezeshi ili kupunguza gharama za kufanya biashara na mifumo inayotabirika na ya uwazi ya kisheria na usimamizi.

Mpango utaendelea kupanua mtandao na ubora wa miundombinu ili kuwawezesha wawekezaji na wazalishaji kupata ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji. Pamoja na hayo miundombinu iliyoboreshwa inaongeza ujumuishi kwa kurahisisha upatikanaji wa huduma za jamii zikiwemo maji safi na salama, huduma za afya na elimu, masoko, na huduma za fedha.

Ingawa mengi yamefanywa kurahisisha mazingira ya biashara na uwekezaji kupitia utekelezaji wa "Mkakati wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji" (*Blueprint*) bado yapo mambo kadhaa yanayopaswa kutekelezwa. Masuala hayo ni pamoja na: ushindani usio wa haki; mawanda ya mazungumzo ya sekta ya umma na ya sekta binafsi; na kutokuaminiana kati ya sekta binafsi na sekta ya umma.

Suala la ushindani wa haki ni lazima lipewe kipaumbele kwa kusimamia sheria zilizopo. Vitendo visivyo vya kishindani vya kampuni zenye nguvu zaidi dhidi ya wazalishaji na wafanyabiashara wadogo lazima vichunguzwe na kudhibitiwa.

Wigo na mawanda ya mazungumzo ya sekta ya umma na sekta binafsi yataimarishwa na kufanywa shirikishi kiasi kwamba wafanyabiashara wadogo na wa kati wanawakilishwa vema kutoka ngazi za chini hadi kitaifa. Kipaumbele kitawekwa kulingana na mazingira na changamoto za sekta husika .

Kadiri wafanyabiashara wanavyofuata kanuni zinazosimamia urahisi wa kuanza, kusajili, kuendesha biashara, kulipa ushuru, kupata vibali, mtaji, na ushirikiano, Serikali itahakikisha kuwa itaondoa migongano ya kutoaminiana kati ya sekta binafsi na sekta ya umma . Kutanzua hili, maelewano kati ya pande zote mbili (wafanyabiashara na taasisi za umma) ni muhimu na pia Serikali itaweka mifumo ya uwazi inayohamasisha kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa.

Taasisi za kuwezesha wawekezaji, wawe wa nje au wa ndani, zitapitia na kurekebisha taratibu zao za utendaji na kuangalia uwezekano wa kufanya kazi kwa pamoja kwenye mfumo wenye uwazi, unaookoa muda, na ambao hauna urasimu usio na tija (mfano: kuhusu vibali, leseni nk.).

(c) Masoko

'Masoko' ni kigezo kingine katika kulinganisha uchumi shindani kimataifa katika nyanja mbalimbali. Aina kuu za masoko ni pamoja na masoko ya bidhaa, huduma na vizalishaji (ardhi, nguvukazi na mtaji). Wawekezaji wa ndani na nje wanavutiwa na ubora na tija ya vizalishaji; na ushindani, ufanisi na usimamizi wa masoko. Kwa upande wa nguvu kazi, wawekezaji hutafuta vipaji, ujuzi na uadilifu. Upatikanaji wa ardhi ni kigezo kingine muhimu cha kuvutia uwekezaji na Tanzania ina eneo kubwa la ardhi kwa matumizi mbalimbali. Aidha, maendeleo ya sekta ya fedha ni muhimu ili kuwezesha upatikanaji wa fedha za mtaji wa kuwekeza katika maeneo mbalimbali. Dhana ya masoko pia inahusisha biashara ya kuuza na kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi. Kuwepo kwa 'makubaliano' kikanda na kimataifa juu ya biashara ya bidhaa na huduma, na 'vita vya kibiashara' baina ya mataifa wanachama, ni ishara kuwa biashara ya kimataifa 'sio huru'.

Ni muhimu kwa nchi kama Tanzania kuongeza juhudi na kuwekeza rasilimali za kuiwezesha sekta binafsi kupata maarifa ya kiufundi yanayohitajika kufikia viwango vya ubora, afya, mazingira na viwango vingine vya kimataifa. Sekta ndogo ya kilimo cha bustani na mbogamboga ni moja ya sekta zilizofanikiwa kufikia viwango vya kimataifa na kupenya kwenye masoko ya nje. Hivyo,

Mpango utasimamia Mkakati wa Maendeleo ya Biashara ya Nje kwa kukuza uwezo wa kiufundi kufikia viwango vya kimataifa katika sekta zote.

(d) Mapindizi ya Kidijitali

Mageuzi ya kidijitali yanajumuisha teknolojia inayokua haraka ya matumizi ya TEHAMA ambayo ni nyenzo muhimu katika kuongeza ufanisi kwenye mifumo ya uzalishaji, huduma, na utawala. Ingawa si rahisi kuingia na kufika teknolojia za kidijitali za hali ya juu, nchi kadhaa za Afrika tayari zimeshuhudia ongezeko la idadi ya wabunifu katika maeneo mbali mbali.

Mpango unasisitiza kuweka uhusiano mzuri wa kazi za SATU na mazingira wezeshi ya uwekezaji wa sekta binafsi kwenye tafiti za teknolojia za kidigitali, ikiwa ni pamoja na kwenye awamu ya nne ya mageuzi ya viwanda (4iR). Aidha, mageuzi haya yanatarajiwa kukuza ajira, hususani kwa vijana ambao wanazidi kuwa wa-kidigitali kutokana na kusambaa kwa simu za mkononi na mitandao. Ili kuwa tayari kwa matumizi ya teknolojia ya kidigitali, Mpango unaweka mkazo kwenye kuwekeza katika miundombinu ya SATU na TEHAMA na ujuzi na maarifa kwenye teknolojia ya digitali. Sekta ya huduma, ambayo mchango wake kwenye Pato la Taifa umekuwa ukiongezeka, ni moja ya sekta zitakazonufaika na mageuzi ya kidigitali.

Mkakati wa Kitaifa wa digitali, utasaidia kutoa mwongozo katika juhudi za kuimarisha matumizi ya digitali. Ili kufanikiwa, mkakati huu utazingatia yafuatayo:

(a) Kuwepo kwa mfumo rahisi wa kisheria na udhibiti wa shughuli za uvumbuzi wa kidigitali, kama vile utafiti na uanzishaji kampuni mpya za teknolojia na uanzishwaji vituo atamizi vya teknolojia ya digitali. Mfumo huo utazingatia ushindani wa haki, ulinzi wa hati-miliki, usajili, usalama mtandaoni, na masuala ya maadili;

(b) Mkakati unaoshirikisha sekta ya umma na binafsi katika kugharamia uanzishaji kampuni mpya za teknolojia; na

(c) Uanzishwaji wa T&M ya viwanda na kongani za ubunifu ili kuunganisha vyuo na sekta binafsi katika kutoa teknolojia za kidigitali kutoka kwenye hatua za majaribio na kuzifikisha kutumika kibiashara sokoni.

4.5.3.2 Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda na Huduma

Ujenzi wa uchumi wa viwanda una maeneo matatu (i) uzalishaji wa bidhaa za viwandani (ii) kilimo, uchimbaji madini and viwanda vingine vya uchimbaji, na (iii) huduma. Dhana kuu ya ujenzi wa uchumi wa viwanda ni kuongeza thamani

kutokana na maarifa na ujuzi unaopatikana kutokana na uzoefu na mafunzo. Dhana hiyo inatumika kwa sekta zote za uzalishaji na huduma, hivyo kuongeza tija na ubunifu kuwezesha ushindani. Katika **Mchoro Na 4.1** maeneo yote matatu ya sehemu hii ya ujenzi wa uchumi wa viwanda na huduma yanahusisha kampuni shindani za kibinafsi na za Serikali. Wakati utafika ambapo itaamuliwa: ni kampuni zipi ziendeshwe na Serikali na zipi ziendeshwe na sekta binafsi. Serikali itasimamia udhibiti (kuweka mazingira wezeshi ya biashara) na sera zitakazoongoza maeneo shindani.

(a) Uzalishaji Viwandani

Kulingana na mfumo wa takwimu za Pato la Taifa, uzalishaji viwandani unahusisha; uzalishaji wa bidhaa za chakula, vinywaji, bidhaa zitokanazo na tumbaku, mavazi, ngozi na bidhaa zake, bidhaa zitokanazo na mbao, kemikali na bidhaa zake, dawa na kemikali za dawa, mpira na bidhaa za plastiki, vipuri muhimu, kompyuta na vifaa vya umeme, mashine, magari, makontena,vifaa ya usafirishaji, samani na vinginevyo. Sehemu kubwa ya uzalishaji viwandani hapa nchini inatawaliwa na wazalishaji wadogo ambao wanahitaji kukua. Aidha, wazalishaji wakubwa nao wanahitaji kuwa wakubwa ziadi. Shughuli nyingi za uzalishaji zimejikita katika bidhaa za chakula, mavazi na samani. Kuna wazalishaji wachache wa bidhaa wanaotumia teknolojia ya hali ya juu.

Kwa kuangalia viwango vya ujuzi na teknolojia katika shughuli za viwandani (Jedwali 4.1),Taarifa ya SMT /UNIDO (2012) mauzo ya nje toka nchi nyingi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara yanatokana zaidi na maliasili na hutumia teknolojia ya chini. Ili kwenda kwa kasi na kutengeneza bidhaa zinazotumia teknolojia ya kati na ya juu, uwekezaji mkubwa katika rasilimali watu unahitajika.

Jedwali Na. 10 Ongezeko la Mchango wa Ujuzi na Teknolojia (mifano iliyochaguliwa)

Maliasili na Teknolojia ya Chini	Viwanda vya Teknolojia ya Kati	Viwanda vya Teknolojia ya Juu
Chakula na vinywaji, saruji, vito viliyokata, glasi, vitambaa vya nguo, bidhaa za ngozi, vipuri rahisi, ,samani, vito na bidhaa za plastiki.	Magari ya abiria na ya kibiashara na vipuri yake, pikipiki na vipuri vyake, nyuzi za bandia, kemikali na rangi, mbolea, injini, mota, mitambo ya viwandani, ujenzi wa meli.	Vifaa vya TEHAMA na data, seti za Televisheni, transista; mitambo na mashine za kuzalishia umeme, dawa za binadamu,; na vifaa vya safari na uvumbuzi wa anga.

Chanzo: Taarifa ya SMT/UNIDO 2012

Ili kuonesha kiwango cha juhudi ambazo Tanzania inabidi kufanya, takwimu za COMTRADE (**Kielelezo Na. 3**) zinaonesha uwiano wa bidhaa za mauzo nje za teknolojia ya juu katika mauzo ya jumla (kwa asilimia). Hii inaonesha wastani wa kipato kikubwa na cha kati na nchi za uchumi wa kati kama ilivyo kwa Tanzania. Kati ya mwaka 2008 na 2018, Tanzania ilikuwa chini ya wastani wa nchi za kipato cha kati.

Kielelezo Na. 3 Mauzo Nje Yanayotumia Teknolojia ya Juu Katika Mauzo ya Jumla (Kwa Asilimia)



Chanzo: Taarifa za COMTRADE

Kimsingi hata hivyo, sekta ya uzalishaji viwandani itaendelea kuwa njia ya kuleta maendeleo katika sekta zingine zote na huduma. Lengo la muda mrefu la sekta ya uzalishaji viwandani iwe ni kujiimarisha na kuwa na uwezo wa kubuni na kuzalisha mitambo na vipuli kwa ajili ya kuvitumia katika uzalishaji na kutumika katika sekta zingine ikiwa ni pamoja na sekta za uzalishaji kwa kutumia maliasili. Aidha, kuna umuhimu wa kuziwezesha karakana za sekta binafsi zinazochipukia ambazo zitajielekeza katika kutengeneza vipuri, zana, na mitambo kwa ujumla.

Ili kufanikisha hili, kunahitajika kuwa na mkakati wa kuunganisha hatua zinazochukuliwa kwenye kuimarisha rasilimali watu (SATU / SATUH), T&M, mafunzo ya ufundi, kwa upande mmoja; na kwa upande mwingine, mikakati ya sekta ya viwanda na sekta ya uziduaji maliasili. Mahusiano haya yatasaidia kuainisha mbinu muhimu za kitaalamu na kubaini suluhisho na majawabu ya kiufundi yanayofaa na sahihi kwa changamoto zitakazo wakabili.

Mchango wa Kanda Maalumu za Uwekezaji

Kutokana na matokeo yasiyoridhisha ya sera ya udhibiti wa bidhaa kutoka nje ili kuongeza uzalishaji kwenye viwanda vya ndani, sera ya Kanda Maalum za Uwekezaji ziliibuliwa kama nyenzo ya kukuza mauzo nje katika nchi zinazoendelea, japokuwa sio zote zinakubalika na kuleta matokeo yaliyotarajiwa.

Tanzania ni moja ya nchi ambazo zinatekeleza dhana ya Kanda Maalumu za Uwekezaji. Ufanisi wa moduli hii unapaswa kutathminiwa kulingana na hali ya kila mradi au hatua zilizochukuliwa, kwa kuzingatia faida na gharama; aina na uhawilishaji wa teknolojia na mikakati ya kuzipata, kutumia maarifa na ujuzi katika teknolojia mpya; vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi vilivyotolewa; mchango halisi kwenye mauzo ya nje; mchango katika kutengeneza ajira; na mahusiano kazini, ikiwa ni pamoja na masuala ya ajira zenye staha na haki za wafanyakazi.

(b) Fursa ya Kuongeza Thamani kwenye Kilimo, Uchimbaji Madini, na Sekta Nyingine

Sekta kuu katika kundi hili ni kilimo cha mazao, ufugaji, uvuvi, misitu; na madini na uchimbaji mawe. Sekta hizi zinawakilisha maeneo yenye fursa na manufaa makubwa kwa taifa. Ni sekta ambazo kihistoria zimetoa mchango mkubwa katika kutengeneza ajira na mauzo ghafi nje ya nchi; japo zimeendelea kuwa na uwezo mdogo wa kuchakata na kuongeza thamani.

Dhana fungamanishi kwenye dhima ya kujenga uchumi wa viwanda ni katika matumizi ya maarifa na teknolojia kugeuza fursa hizo kuwa bidhaa zenye kuleta ushindani sokoni na wakati huo huo kupanua wigo wa bidhaa. Mpango unahimiza wadau wa sekta hizo kutoka Serikalini na sekta binafsi kwa pamoja kufanyia kazi masuala yaliyopo kwenye maeneo yao kwa kuzingatia angalau mifano ya kinadharia katika ngazi tatu (3) zifuatazo:

***Ngazi ya Kwanza*:** *Kutumia sayansi teknolojia na ubunifu / utafiti na maendeleo (SATU / T & M) pamoja na matokeo mengine ya utafiti ili kuongeza tija na ubora:*

Hii inahusisha matumizi ya mbinu za kisayansi kwenye kilimo cha mazao, uvuvi, misitu na shughuli za uchimbaji madini ili kuchakata na kusindika kwa kiwango cha awali na kuongeza thamani au kuchakata kwa kiwango kidogo. Hatua hii itawezesha kuwa na bidhaa zenye ubora wa hali ya juu ikiwa ni pamoja na ngozi, bidhaa za samaki, mbao, na bidhaa zitokanazo na asali. Ngazi hii pia itakuwa na malengo maalum ya kupunguza upotezaji wa mazao baada ya mavuno (post-harvest loss), kubuni matumizi mengine au bidhaa zingine, na kupunguza mabaki kutoka kwenye madini.

Ngazi ya Pili: *Matumizi ya sayansi teknolojia na ubunifu / utafiti na maendeleo (SATU / T& M) na vifaa na mbinu za teknolojia ya hali ya juu zaidi, 'kugundua' aina mpya za bidhaa, n.k. kutoka kwenye malighafi na matumizi ya mabaki ya michakato ya awali*. Ngazi hii inaweza kuitwa "maendeleo ya bidhaa" ('product development'), amabyo itaongeza wigo wa anuwai ya bidhaa mpya na zenye thamani kubwa zaidi. Ni vema kama haya yatafanyika hapa nchini ili nguvukazi ya Tanzania ipate ujuzi zaidi, kama mifano ifuatayo inavyofafanua :

(i) Kwa upande wa korosho, upo uwezekano wa kuongeza thamani hadi mara kumi (10) ya thamani ya soko kama korosho mbichi itachakatwa kuwa bidhaa mbalimbali.

Boksi Na. 2: Bidhaa Zinazotokana na Korosho

- *Kiini cha Korosho:* Kutumika kwenye viwanda vya chakula na pipi (confectionaries);
- *Mafuta ya kokwa la korosho:* Kama malighafi katika dawa, wino, vitambaa, vipodozi, rangi, tiba ya ngozi.
- *Kokwa la korosho:* chanzo cha nishati (e.g., briquettes);
- *Maganda (Testa/peal):* Kutengeneza vinyonya sumu vinavyotumika kwa viwanda vya ngozi;
- *Bibo (Cashew apple):* Dawa na chakula (sharubati, vinywaji, jamu, chutney)

(ii) Metali ghafi inaweza kuchakatwa kuwa bidhaa tofauti kwa matumizi ya nyumbani kwa kuongeza thamani kwenye viwanda vya uchenjuaji (kwa mfano, aloi za dhahabu zinazotumiwa kutengeneza vito, sarafu, au aloi za shaba, fedha na platinamu).

(iii) Inawezekana kuzalisha bidhaa mbalimbali kutoka kwa mazao ya misitu, kama mbao, karatasi, vifungashio vya bidhaa; *selulosi* na *lignin* inayotumika katika kutengeneza bidhaa mbalimbali za nyumbani kama rangi, meza za mpira wa mezani (*ping-pong)*, na taulo za *rayon* iliyotengenezwa kwa selulosi.

Hii ni kuonyesha kuwa, badala ya kuendelea kuuza malighafi, Tanzania yenye utajiri mwingi wa maliasili inapaswa kuwekeza kwa bidii kwenye rasilimali watu (ufundi, ujuzi, na ubunifu) ili kuzalisha bidhaa mpya, (zilizoongezwa thamani) na zenye uwezo wa kushindana katika masoko ya ndani na nje.

Utafiti na uchimbaji wa madini na gesi asilia unahitaji utaalam mwingi na uwekezaji mkubwa wa kifedha. Gesi asilia inaweza kutumika kuzalisha nishati na malighafi kwenye viwanda vya kemikali kama vile uzalishaji wa methanoli, plastiki na malighafi zake, dawa za binadamu, na mafuta ya nishati. Kwa kuzingatia kuongezeka mashindano ya kimataifa kuelekeza mitaji yao kwenye madini na maliasili za nishati barani Afrika, juhudi zinahitajika katika kuharakisha kujifunza na kujenga uwezo wa taifa katika uwezo wa teknolojia kwenye chuma, teknolojia mpya za uchakataji, na masuala ya kisheria na majadiliano yanayohusiana na sekta za uchimbaji.

Kwa upande wa madini, zinahitajika taratibu sahihi za kibiashara (taasisi na mifumo) kuhakikisha wachimbaji wanapata thamani stahiki. Uwezeshaji unaoendelea utaongezwa kwa kuwajengea uwezo wa kiufundi wachimbaji wadogo. Aidha, sera ya kuwawezesha wazawa, sheria na taratibu zake ni muhimu katika kuongeza mchango wa sekta ya madini kwa maendeleo ya kitaifa.

Ngazi ya Tatu: Katika ngazi ya kwanza na ya pili, sehemu kubwa ya mitambo na mashine inaagizwa toka nje. *Katika ngazi ya tatu, nchi inakuwa na uwezo wa kiufundi na kiuhandisi kuzalisha mitambo na mashine kwa kushirikiana na wataalam wa sekta.* Wahandisi na mafundi na wataalamu wa kisekta (kilimo, tiba, ujenzi, uvuvi nk) hutengeneza mashine na vifaa maalum kwa kisekta (mashine ya kuchana karatasi, mashine ya kupandia mbegu, nk.) na kutengeneza vipuri hapa hapa nchini (vifaa hivyo pia vinaweza kuagizwa kutoka nje). Madhumuni ni kupunguza utegemezi kwenye mitaji ya kigeni na malighafi za kati (intermediate inputs) upo uwezekano wa kusafirisha teknolojia kama hizo nje ya nchi.

Ni muhimu kufanya mapitio (kwa nia ya kufufua) dhana iliyopelekea kuanzisha kwa vituo vya maendeleo ya mitambo na teknolojia na miradi ya kutengeneza magari. Dhana hii sio tu ina manufaa kibiashara; bali ni ya kimkakati kwa kuwa itasaidia wakati wa dharura au wakati Taifa haliwezi kupata bidhaa hizo kutoka mahali pengine. Kwa sababu ya kiasi kikubwa cha mtaji wa uwekezaji unaohitajika, na kwa sababu ya mnaufaa ya kimkakati ya fursa shindani, ni muhimu kuunda shirika la umma au kuanzisha kitengo mahsusi cha Serikali kusimamia utekelezaji wa "miradi" hii muhimu.

(c) Huduma

Katika mfumo wa takwimu za Pato la Taifa, sekta ya huduma inajumuisha biashara ya jumla na rejareja; uchukuzi na uhifadhi; malazi na huduma za chakula; habari na mawasiliano; shughuli za kifedha na bima; upangishaji majengo; shughuli za kitaaluma, kisayansi na kiufundi; shughuli na huduma za kiutawala; utawala wa

umma na ulinzi; elimu; shughuli za afya ya binadamu na ustawi wa kijamii; sanaa, burudani na starehe.

Sekta-ndogo zote zinachangia kwenye ukuaji wa uchumi na ajira. Mpango unatarajia kuongezeka kwa tija kutokana na matumizi ya mbinu za kisasa. Huduma nyingi hutolewa na sekta binafsi; zingine hutolewa na sekta ya umma (kwa mfano, katika utawala wa umma na ulinzi). Aidha, kuna viwango tofauti vya ushiriki wa sekta ya umma katika baadhi ya sekta ndogo; zipo biashara zinazomilikiwa na Serikali sambamba na zile za sekta binafsi. Pamoja na tofauti hizo, matarajio ya Mpango III kwa sekta zote za huduma ni kuongezeka kwa tija na ushindani kwa kunufaika na vifaa vya kisasa vya uzalishaji au vya kidigitali vitakavyowezesha kutoa huduma bora (kwa mfano: kupunguza muda wa kufikisha huduma, kumjali mteja, na ustahifu) sambamba na kuzingatia weledi wa kitaalamu katika kutoa huduma.

Utalii, kama sekta ndogo ya huduma, inajumuisha huduma zaidi ya moja ikiwemo usafirishaji, malazi na chakula, habari na mawasiliano. Utalii ni moja ya sekta inayoingiza fedha nyingi za kigeni. Aidha, sekta ya utalii ina uhusiano mkubwa wa moja kwa moja na usiyo wa moja kwa moja na sekta nyingine za uchumi kama vile kutoa ajira na soko la bidhaa na huduma zinazohitajika katika maeneo yanayozunguka vivutio vya utalii. Hata hivyo, athari hasi kwenye sekta ya utalii zilizotokana na janga la ugonjwa wa homa kali ya mapafu imetuachia funzo muhimu la uchumi kutotegemea sekta moja; bidhaa moja, na soko moja na badala yake kupanua wigo wa bidhaa na masoko.

4.5.3.3 Biashara na Uwekezaji

Biashara inahusu ushiriki wa nchi katika biashara ya kimataifa, kikanda na ndani ya nchi kwa kuzingatia ushindani wa makampuni kwenye sekta za uzalishaji viwandani, kilimo na shughuli za huduma. Biashara inahusisha kuagiza na kuuza bidhaa na huduma ndani na nje ya nchi.

Kutokana na malengo ya kuongeza mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani, na mahitaji ya uwekezaji katika maeneo ambayo Tanzania ina fursa nyingi, lazima hatua za kuimarisha mazingira ya uwekezaji ziwe ni sehemu ya mkakati. Hata hivyo, sehemu kubwa ya uwekazaji unalenga uwezekano wa kuuza nje kutokana na kiwango kidogo cha uhitaji katika soko la ndani .

Ushiriki katika biashara ya kimataifa na ya kikanda, ikijumuisha uagizaji wa bidhaa, huvutia uwekezaji wa ndani na nje na upatikanaji wa teknolojia mpya na ujuzi wa kiutawala. Mauzo nje hupunguza uhaba wa fedha za kigeni, hutengeneza ajira na

matumizi ya rasilimali za ndani, na hivyo kuchangia ukuaji jumla wa uchumi. Masuala yafuatayo yanayohusiana na biashara yanapaswa kuzingatiwa:

Kwanza, sehemu kubwa ya mauzo ya Tanzania nje ya nchi ni bidhaa ghafi, ikiwa ni pamoja na madini na mauzo ya kilimo yaliyosindikwa kwa kiwango kidogo. Mauzo haya yana matokeo madogo ya maendeleo ya teknolojia kwa wazalishaji wa ndani na ajira kidogo katika soko la ndani. Katika kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo, mageuzi ya mauzo ya nje yanahitaji kuongezeka kwa idadi ya bidhaa zinazozalishwa ndani zinazotumia kiwango cha kati hadi cha juu cha teknolojia.

Pili, baadhi ya bidhaa za kilimo zinazouzwa nje , bidhaa za walaji na bidhaa nyingine za viwandani zinakabiliwa na vikwazo vya kikodi na visivyo vya kikodi ambapo hutozwa ushuru mkubwa zinapoingia nchi zilizoendelea. Hali hii imekuwa ni kikwazo kwa muda mrefu. Hata hivyo, ingawa ni sahihi kuhitaji usawa katika matumizi ya vikwazo vya kiufundi kwa biashara na usafi na usafi wa mazingira na viwango vingine vya afya na mazingira, ni muhimu kwa Tanzania kujenga uwezo wake wa kiutaalamu na kiufundi ili kufikia viwango hivyo vya ubora - ambavyo pia vinaweza kuwa muhimu kwa walaji wa Tanzania.

Tatu, kadiri wafanyabiashara wa Tanzania wanavyoendelea kupata uzoefu wa ushindani wa kimataifa, ikiwa ni pamoja na biashara ya kuagiza bidhaa, itaendelea kujifunza mbinu za ushindani, lakini ushindani lazima uwe wa haki kwa kusimamia sheria zilizopo. Mienendo inayofifisha ushindani ni lazima idhibitiwe. Aidha, sera ya kulinda viwanda vya ndani itatumiwa pale ushindani wa haki unapokuwa hatarini.

Nne, katika ngazi pana ambapo nchi ni mwanachama wa jumuiya shindani za kikanda, na kanda hizo ziko katika hatua tofauti za utekelezaji wa mtengamano wa kibiashara (kwa mfano, EAC, SADC, na mapendekezo ya mkataba wa pande tatu (COMESA, EAC na SADC)), tahadhari hazina budi kuchukuliwa hasa namna Serikali inahusisha wadau wa sekta binafsi (wauazaji na waagizaji) kukajadiliana juu ya ratiba za utekelezaji wa makubaliano tofauti tofauti. Kwa wadau wengi wa sekta binafsi, taratibu nyingi zianaweza kuwa za kitaalam zaidi hususan kwenye masuala ya kisheria na viwango. Hivyo, Serikali, kwa kadiri itakavyowezekana, itawapa wafanyabiashara taarifa za makubaliano ya kimataifa na maazimio ambayo yana madhara ya moja kwa moja na shughuli za sekta binafsi.

4.5.4 Maendeleo ya Jamii

Jumuishi inahusisha usawa na ni kigezo cha utulivu wa kijamii wa mfumo wowote wa kiuchumi. Ukuaji wa uchumi unaotarajiwa hautakiwi tu wa juu au haraka; bali uhusishe utulivu wa jamii na kuwa jumuishi.Aidha, maendeleo shirikishi

yatafikiwa kwa sera zinazojielekeza kwenye (i) matumizi kwenye maendeleo ya jamii (afya na elimu, makazi ya watu, maji safi na salama, mazingira, jinsia) na (ii) kupanua mitandao ya miundombinu ya kiuchumi, kama vile barabara, nishati, mawasiliano kwenda maeneo yenye fursa lakini magumu kufikika na maeneo na sehemu ya jamii yenye mahitaji maalum. Upatikanaji wa huduma za fedha kwa kaya nyingi maskini katika maeneo ya mijini na vijijni zimewezeshwa na kwa haraka na mitandao ya simu. Matokeo ya maendeleo ya jamii katka maeneo yafuatayo yanahitaji kuzingatiwa:

(i). *Afya*: kama sehemu ya kuimarisha mtaji watu na ubora wa maisha (ustawi); kuendeleza mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano, ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya, kuboresha upatikanaji wa huduma za afya na matibabu;

(ii). *Elimu*: (kama ilivyo katika kuimarisha mtaji watu); msisitizo mkubwa mbali na ubora, msisitizo uwe kwenye upatikanaji wa elimu kwa wote – ambao utawezesha watoto wote kupata fursa za elimu, huku jamii ikihimizwa kuendelea kutafuta maarifa na taarifa mpya;

(iii). *Maji safi na maji-taka* (kama huduma ya jamii na sehemu ya miundombinu);

(iv). *Ulinzi wa jamii*: Kwa ujumla, hatua za kuimarisha ustahimilivu wa kaya na watu masikini na makundi ya jamii yaliyo katika mazingira magumu zinahitajika ili kuwawezesha kuhimili maisha yao na kuepuka kutumbukia moja kwa moja kwenye dimbwi la umaskini. Uwezakano wa kuongeza ulinzi wa jamii ikihusisha walengwa na faida zake yaendane na ahadi na uwezekano wa wanufaika kushiriki katika shughuli za uzalishaji;

(v). *Maendeleo ya Vijana na Program za Ajira*

- Ifanyike tathmini kwenye ukubwa, upeo na matokeo (hadi sasa) ya mifuko ya kijamii, ikiwa ni pamoja na zile zinazosimamiwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa; aidha, tathmini iangalie ufanisi/faida (kwa wale wanaofaidika) na viwango cha marejesho (wanufaika wa baadaye);
- Ifanyike tathmini ya mchango wa mifuko hii ya kijamii kwenye ukuaji wa sekta binafsi. Je! Shughuli hizo ni endelevu kifedha? Ufanyike ufuatiliaji kujua ikiwa wanufaika 'wanahitimu' na kufanya maamuzi juu ya mpango sahihi wa kuendelea kuwasaidia;
- Uangaliwe uwezekano wa kufanya fedha hizo kuwafikia wahitimu katika elimu ya msingi, sekondari,vyuo vya kati, elimu ya ufundi;
- Kuviwezesha viatamizi vya teknolojia na biashara mpya.

(vi). *Makazi*: Mambo muhimu ya kuzingatia, makazi ya kisasa kwa ajili ya ongezeko la idadi ya kaya za vijijini na mijini; vifaa vya ujenzi wa nyumba na teknolojia za ujenzi ambazo ni nafuu, kuongeza upatikanaji wa maeneo vilivyopangwa na vyenye miundombinu ya huduma.

(vii). *Utawala*: kutoa huduma bora na kwa ufanisi na kupunguza urasimu kwa kuchukua hatua stahiki kwenye sheria na taratibu; hatua mahususi za kiutawala (kupambana na rushwa), amani na usalama.

(viii). *Masuala ya Jinsia*: pamoja na hatua nyingine, hatua za kuleta usawa wa kijinsia kwa wanawake na wasichana; kuongeza fursa za elimu na mafunzo kwa msichana; hatua za haraka dhidi ya ubaguzi katika maswala ya umiliki wa ardhi na urithi, unyanyasaji dhidi ya wanawake, na kuongeza elimu dhidi ya mila na tamaduni zinazomkandamiza mwanamke.

(ix). *Ulinzi wa mazingira na kupunguza athari ya mabadiliko ya tabia-nchi*: Pamoja na mambo mengi, kuhakikisha matumizi sahihi na usimamizi wa ardhi, kulinda vyanzo vya maji, matumizi ya teknolojia za kuvuna maji ya mvua, programu za upandaji miti, programu za jamii kusimamia maliasili, utekelezaji wa sheria dhidi ya aina zote za uchafuzi wa mazingira na dhidi ya mbinu za uchimbaji zinazoharibu mazingira; na hatua za kupunguza madhara ya maafa ya kimazingira (kwa mfano, mafuriko, ukame, na athari za wakimbizi).

Kwa pamoja, hatua za maendeleo ya kijamii zinaongeza ubora wa 'ukuaji wa uchumi', na hivyo kuimarisha ukuaji wa uchumi moja kwa moja.

4.6 Kuelekea Hatua Mahsusi

Sura hii ya muundo inaainisha maeneo makuu ya hatua za utekelezaji na namna yanavyohusiana. Maeneo yaliyoainishwa katika Mpango uliojielekeza katika ushindani umefanunua, kuimarisha ushiriki wa Tanzania kwenye biashara ya kimataifa na uwekezaji unaotegemea kuongeza uwekezaji katika mtaji watu, hususani kuimarisha elimu na mafunzo bora na stahiki kwenye maarifa na ujuzi wa sayansi, teknolojia na ubunifu. Maelezo ya hatua mahsusi na programu yameachwa kwa sekta ambazo zinatoa mwongozo wa sera na Asasi zisizo za kiserikali, hususan sekta binafsi zinazofanya uzalishaji.

Dhana fungamanishi katika hatua zote za utekelezaji ni kuongeza tija na ushindani kwa kukuza na kuajiri rasilimali watu yenye ubora wa hali ya juu, pamoja na matumizi ya sayansi na ubunifu wa kiteknolojia ili kujenga faida za kiushindani katika bidhaa na huduma kwa masoko ya nje na ya ndani.

RASIMU

Mpango wa Tatu ni sehemu ya juhudi zinazoendelea za maendeleo ya kijamii na kiuchumi na zinatambua muendelezo wa hatua za mipango iliyopita. Rasilimali zitatumika kuhakikisha kiwango cha juu cha utawala bora na uadilifu wa amani na umoja, sheria na taratibu na utulivu wa kisiasa wa nchi. Uwekezaji wenye matokeo makubwa, hususani miundombinu, utaendelea kupewa umuhimu katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara kwa ukuaji wa sekta binafsi. Msisitizo wa kipekee utaelekezwa katika kuhakikisha maendeleo endelevu kijamii na kimazingira. Maendeleo endelevu kijamii yatatokana na hatua ambazo zinahakikisha ushiriki wenye usawa katika 'mali za kitaifa' (mitandao ya miundombinu na huduma za kijamii) kwa maendeleo ya watu na ustawi.

SURA YA TANO

NGUZO KUU, VIPAUMBELE NA HATUA ZA KIMKAKATI ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO

5.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea nguzo kuu, vipaumbele na hatua za kisekta za utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 -2025/26. Nguzo kuu za Mpango ni: Utawala Bora: Ukuaji wa Uchumi; na Maendeleo ya Watu. Nguzo hizi ni msingi wa vipaumbele vya Mpango ambavyo ni: Kuchochea Uchumi Shirikishi na Shindani; Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma; Kukuza Uwekezaji na Biashara; Kuchochea Maendeleo ya Watu; na Kuendeleza Rasilimali Watu. Aidha, sura hii itaainisha shabaha zitakazofikiwa ifikapo mwaka 2026 kutokana na utekelezaji wa Mpango.

5.2 Nguzo Kuu za Mpango

Utawala bora, ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu ni nguzo kuu za Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 -2025/26. Utawala bora unajumuisha haki, usawa, uwazi, ushirikishwaji na uwajibikaji katika utekelezaji wa Mpango. Aidha, ukuaji wa uchumi ni msingi muhimu unaotokana na sera madhubuti za fedha na bajeti na uwekezaji katika sekta za kiuchumi na uzalishaji. Vile vile, maendeleo ya watu matokeo yatokanayo na utekelezaji wa Mpango kwa kuzingatia utawala bora na ukuaji wa uchumi.

5.3 Vipaumbele vya Mpango

Vipaumbele vya Mpango ni pamoja na: Kuchochea Uchumi Shirikishi na Shindani Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma; Kukuza Uwekezaji na Biashara; Kuchochea Maendeleo ya Watu; na Kuendeleza Rasilimali Watu.

5.3.1 Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi: Eneo hili linajumuisha miradi ambayo itajikita katika: kujenga jamii yenye uwezo wa kushindana kikanda na kimataifa; kuchochea utulivu wa viashiria vya uchumi jumla; kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuchochea uvumbuzi na uhawilishaji wa teknolojia kutoka nje; na kuendeleza miundombinu na huduma za reli, barabara, madaraja, usafiri wa majini na angani, TEHAMA, nishati, bandari na viwanja vya ndege;

5.3.2 Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma: Eneo hili linajumuisha miradi ya viwanda inayolenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na madini pamoja na kuzalisha bidhaa zitakazotumia malighafi na rasilimali zinazopatikana nchini. Aidha, eneo

hili linajumuisha pia miradi na programu inayolenga kuboresha huduma za utalii, fedha na bima;

5.3.3 Kukuza Uwekezaji na Biashara: Eneo hili linajumuisha programu zitakazoimarisha masoko ya ndani na kutumia fursa za masoko ya kikanda na kimataifa katika kukuza biashara. Aidha, masoko yanayolengwa ni yale yatakayotoa fursa kwa bidhaa zinazozalishwa nchini, ikiwemo bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu;

5.3.4 Kuchochea Maendeleo ya Watu: Eneo hili linajumuisha utekelezaji wa miradi ambayo inajikita katika kuboresha maisha ya watu ikiwemo: elimu na mafunzo kwa ujumla; afya na ustawi wa jamii; kinga ya jamii; huduma za maji na usafi wa mazingira; mipango miji, nyumba na maendeleo ya makazi; na athari dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi; na

5.3.5 Kuendeleza Rasilimali Watu: Eneo hili linajumuisha programu na mikakati inayolenga kuendeleza maarifa na ujuzi wa rasimali watu nchini, kuanzia ngazi za elimu ya awali hadi elimu ya juu ikiwemo kuwawezesha vijana kujiajiri. Vile vile, eneo hili linajumuisha hatua za kuboresha viwango vya utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na ujuzi adimu kwa lengo la kuongeza tija na ushindani wa wananchi katika kutumia rasimali zilizopo nchini ili kuleta maendeleo.

5.4 Hatua za Kisekta za Utekelezaji wa Vipaumbele vya Mpango

5.4.1 Kilimo

Sekta ya Kilimo inaendelea kuwa kitovu cha ukuzaji wa viwanda na maisha ya watu nchini, ambapo inakadiriwa kuwa asilimia 65 ya watu wanapata riziki kutokana na shughuli za kilimo. Kwa kipindi chote cha Mpango, juhudi zitaelekezwa katika kuunganisha na kuimarisha mafanikio yaliyopatikana hadi sasa kwa kufanya yafuatayo:

(i). Kujenga mahusiano imara kati ya sekta ya kilimo na sekta nyingine za kiuchumi;

(ii). Kujenga mazingira mazuri kwa sekta binafsi kuendesha shughuli za uzalishaji na uuzaji nje wa malighafi za kilimo na bidhaa zilizochakatwa;

(iii). Kuandaa programu za mafunzo na tafiti kwa manufaa ya wadau muhimu wa kilimo; na

(iv). Kuendeleza tafiti endelevu za mazo ya kilimo ili kufungamanisha mnyororo wa thamani wa ndani na kimataifa.

Hatua hizi zitaongeza thamani na tija ya uzalishaji wa mazao ya kilimo, kuzalisha ajira, kutanua wigo mseto wa bidhaa na kuimarisha mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo.

5.4.2 Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika Kuimarisha Tija na Mavuno katika Sekta ya Kilimo

Sekta ya kilimo inachangia takribani asilimia 27 ya Pato la Taifa na asilimia 24 ya mauzo nje. Kwa kuzingatia muundo wa uchumi, kuna uhusiano kati ya maendeleo ya sekta ya kilimo na kupungua kwa umaskini. Hata hivyo, kasi ya ukuaji wa sekta ya kilimo imekuwa ndogo na hivyo kuhitaji matumizi ya teknolojia na tafiti ili kuongeza tija na mavuno. Matumizi sahihi ya taarifa za tafiti na teknolojia yataongeza mavuno, kupunguza bei ya chakula, kupunguza vihatarishi na kuongeza faida na hivyo wananchi kunufaika na mfumo funganishi wa sekta ya kilimo.

Ili kuongeza tija na ufanisi katika sekta ya kilimo, Mpango utajielekeza katika maeneo yafuatayo;

Mazao: Mazao ya kipaumbele ni mahindi, mpunga, pamba, korosho, chai, kahawa, tumbaku, mkonge, michikichi, ngano, maharage ya soya, mhogo, miwa, mboga mboga na matunda na alizeti.

Hatua Muhimu;

(i) Kuimarisha tafiti na maendeleo katika mazao ya kimkakati;
(ii) Kuboresha Mpango Jumuishi wa Matumizi endelevu ya maji na ardhi kupitia programu jumuishi ya mipango na matumizi ya ardhi na uboreshaji wa mifumo ya umwagiliaji;
(iii) Kuimarisha ushindani wa mnyororo wa thamani wa mazao na ubiasharishaji;
(iv) Kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika uendeshaji wa vyama vya ushirika; na
(v) Kuanzisha mifumo ya kisasa ya utunzaji wa mazao.

Boksi Na. 3: Kilimo cha Matunda, Mbogamboga na Maua

Kilimo cha matunda, mbogamboga na maua kinajumuisha viungo, mimea ya dawa, na mbegu za mazao. Maeneo ya uzalishaji ni nyanda za juu kusini (Mbeya, Njombe, Iringa na Songwe), ukanda wa kaskazini (Kilimanjaro, Manyara, Arusha na Tanga), kanda ya pwani na kati (Morogoro na Pwani) na kanda ya Ziwa Victoria. Sekta ndogo ya matunda, mbogamboga na maua inaajiri takribani watu milioni 4. Aidha, wawekezaji wa kati na wakubwa wanaendesha shughuli zao katika sekta hii wao wenyewe, au kwa kuwashirikisha wakulima wadogo wadogo (out-growers). Inatarajiwa kuwa, ifikapo mwaka 2026 sekta hii ndogo itaweza kuzalisha kiasi cha Dola za Marekani bilioni 2 kupitia mauzo nje ya nchi.

Kilimo cha matunda, mbogamboga na maua kinachangia zaidi ya asilimia 40 ya mapato ya fedha za kigeni. Matokeo ya mchango wa sekta hii unatokana na ushirikishwaji wa wakulima wadogo wadogo kwenye mnyororo wa thamani wa mauzo nje. Takribani asilimia 90 ya mazao ya matunda, mbogamboga na maua yanayozalishwa yanatumika nchini, na asilimia 10 huuzwa nje.

Pamoja na asilimia ndogo (10) ya mauzo nje , kilimo cha matunda, mbogamboga na maua kinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa miundombinu wezeshi ya uhifadhi wa mazao, maabara za ithibati na wataalamu wenye ujuzi katika teknolojia ya mimea, viungo, matunda na mbegu.

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 unalenga kutatua changamoto za mazao ya matunda, mbogamboga na maua kwa kuwekeza pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya sekta binafsi kuwekeza katika miundombinu ya uhifadhi, usafiri na usafirishaji, maabara ya ithibati na kuandaa na kujenga uwezo wa wataalamu waliopo.

Mifugo: **Hatua Muhimu:**

(i) Kuongeza idadi na uwezo wa viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo (ngozi, maziwa na nyama);
(ii) Kuwezesha utambuzi, usajili na kuhamasisha mauzo ya bidhaa za mifugo nje;
(iii) Kuwezesha na kuhamasisha ujenzi wa masoko ya mifugo, machinjio ya kisasa na ujenzi wa vituo vya kukusanyia maziwa;
(iv) Kuhamasisha na kuwezesha uzalishaji wa mbegu bora za mifugo;
(v) Kuiimarisha ranchi za Taifa, hussan rachi ya Kongwa, Ruvu, Kalambo, Misenyi na Kilimanjaro magharibi ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya mifugo;
(vi) Kuimarisha mifumo ya kufuatilia na kudhibiti magonjwa ya wanyama;
(vii) Kuwezesha upatikanaji wa chanjo bora ya magonjwa ya mifugo;
(viii) Kuhamasisha ujenzi wa majosho ya mifugo ili kudhibiti vimelea;
(ix) Kutenga, kupima na kuendeleza maeneo ya malisho;
(x) Kuboresha usimamizi na matumizi ya majani ya kulishia mifugo;
(xi) Kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya virutubisho na vyakula vya wanyama;
(xii) Kuongeza idadi ya miundombinu ya maji ya kunyweshea mifugo;

(xiii) Kuhamasisha matumizi ya teknolojia za kisasa katika uzalishaji na utafutaji wa masoko ya mazao ya mifugo;
(xiv) Kuwezesha utafiti katika uzalishaji wa mifugo, mazao ya mifugo, uhifadhi wa mbegu na kurutubisha vinasaba;
(xv) Kuboresha taasisi za mafunzo ya mifugo na mitaala; na
(xvi) Kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za ugani katika ngazi za vijiji na kata;

Boksi Na. 4: Viwanda vya Ngozi

Katika mwaka 2020, Tanzania ilikuwa na viwanda vya kusindika ngozi kumi (10). Kati ya viwanda hivyo, viwanda vitano (5) vinafanya kazi. Aidha, kati ya viwanda vitano vinavyofanya kazi, viwanda vitatu (3) vinachakata ngozi hadi hatua ya kati na viwili (2) vinasindika hadi hatua ya mwisho. Uwezo wa usindikaji wa viwanda hivyo (installed capacity) ni vipande 2,459,000 vya ngozi za ng'ombe na vipande 7,628,000 vya ngozi za kondoo/mbuzi, sawa na asilimia 60.6 ya uwezo wa kusindika. Makadirio ya sekta ya viwanda vya kusindika ngozi yanaonesha kuwa, uzalishaji wa viatu vya ngozi ni jozi 1,200,000 kwa mwaka ikilinganishwa mahitaji ya jozi milioni 54.2. Hivyo, kuna fursa ya uwekezaji kwenye biashara ya viatu vya ngozi. Vile vile, sekta ya usindikaji wa ngozi ina fursa ya uzalishaji wa bidhaa nyingine kama mikanda, mikoba, majaketi na pochi.

Pamoja na fursa zilizopo, viwanda vya ngozi vinakabiliwa na changamoto zifuatazo: biashara haramu ya kusafirisha ngozi ghafi nje ya nchi; uhafifu wa ubora wa ngozi zinazozalishwa; ukosefu wa machinjio ya kisasa; ukosefu wa wachunaji wenye ujuzi; na kutozingatia kanuni na taratibu za ufugaji na uzalishaji wa ngozi; matumizi ya visu visivyokidhi; na matumizi ya teknolojia duni.

Ili kukabiliana na changamoto za sekta ndogo ya ngozi, Serikali imeteua na kuwezesha jumla ya wakaguzi wa ngozi 113 na wachunaji 735. Hatua nyingine ni pamoja na: kuwezesha mafunzo kwa wafanyabiashara 10 wa ngozi kuhusu upangaji wa madaraja ngozi; kutoa ruzuku ya majosho ya mifugo; kudhibiti biashara haramu ya ngozi kwa kuweka tozo ya asilimia 80 kwenye mauzo ya ngozi ghafi nje na asilimia 10 kwa mauzo ya ngozi iliyochakatwa kwa kiwango cha kati (wet-blue); na kufanikisha ujenzi wa kiwanda cha Kilimanjaro International Leather Industries Co. Ltd pamoja machinjio ya kisasa 30.

Uvuvi: Mageuzi katika sekta ya uvuvi yanajuimuisha uwezo wa kutumia fursa ya uchumi wa rasilimali za maji, hususan bahari na maji baridi. Maeneo ya kipaumbele ya sekta yatajumuisha uvuvi katika maji baridi na bahari, kilimo cha majini, uhifadhi wa maeneo tengefu na uboreshaji wa uvuvi baharini katika kina kirefu.

Hatua Muhimu:
(i) Kuwezesha upatikanaji wa meli na ujenzi wa bandari ya uvuvi;
(ii) Kuimarisha uwezo wa taasisi za Uvuvi, hususan Shirika la Uvuvi;

(iii) Kuwezesha sekta binafsi kuanzisha na kukarabati viwanda vya mazao ya uvuvi;
(iv) Kuhifadhi na kulinda maeneo tengefu ya bahari na maji baridi;
(v) Kulinda na kuhifadhi makazi ya viumbe muhimu na viumbe wa majini walio katika hatari ya kutoweka;
(vi) Kuwezesha na uhamasisha uwekezaji katika miundombinu ya uvuvi, vifaa na ufugaji wa kibiashara wa samaki;
(vii) Kuwezeshasha upatikanaji wa mitaji, utalaamu, ujuzi, maarifa na zana za kisasa za uvuvi kupitia vikundi vya kijamii;
(viii) Kufungamanisha utafiti, ugani, uvuvi na kilimo cha majini;
(ix) Kudhibiti ubora, usalama na viwango vya mazao ya samaki na uvuvi;
(x) Kuboresha maabara za uhakiki ubora wa rasilimali za majini na maeneo ya gati za uvuvi;
(xi) Kuwezesha mipango ya matumizi endelevu na usimamizi wa rasilimali za bahari; na
(xii) Kuhamasisha utalii katika maeneo tengefu ya bahari.

Jedwali Na. 11 Viashiria na Malengo ya Utekelezaji Katika Kilimo

Na.	Viashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1	**Kilimo**		
1.1	Kiwango cha Wastani wa Ukuaji (%)	4.4	4.5
1.2	Asilimia katika Pato la Taifa (bei za sasa)	25.6	24.4
1.3	Asilimia katika Mapato ya Mauzo Nje	20.0	25.0
1.4	Asilimia ya Jumla ya Ajira	65	60
1.5	Tija (asilimi) ya ukuaji	4.0	4.7
2.	**Mazao**		
2.1	Wastani wa Ukuaji (%)	4.0	4.2
2.2	Asilimia katika Pato la Taifa (bei za sasa)	13.2	12.0
2.3	Asilimia katika Mapato yote ya Mauzo Nje	13.0	19.0
2.5	Hekta za Umwagiliwa	694,715	1,200,000
2.6	Ongezeko la wanafunzi waliodahiliwa	2,600	3,600
2.7	Idadi ya maafisa ugani	6,704	20,538
2.8	Mbegu zilizoidhinishwa na zilizozalishwa	71,000	140,000
2.9	Asilimia ya upotevu wa mavuno (postharvest loss)	35	17.5
2.10	Akiba ya taifa ya chakula	501,000	700,000
2.11	Kiasi cha mazao ya bustani yaliyozalishwa (tani)	6,556,102	14,600,000
2.12	Kiasi cha uzalishaji wa mazao ya biashara ya asili (traditional) (tani).	794,500	1,583,200

2.13	Asilimia ya ardhi ya kilimo inayotumia zana za kisasa (mechanization services) katika mnyororo wa thamani	47	75
2.14	Idadi yaa mashamba makubwa (Block Farms)	110	200
2.15	Idadi ya viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika	113	183
2.16	Idadi ya vyama vya ushirika vinavotumia mfumo wa soko rasmi	3,001	4,039
	Idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika (milioni)	5.9	14.5
2.17	Kiwango cha utoshelevu wa chakula (asilimia)	121	140
3.	**Mifugo**		
3.1	Kiwango cha Wastani wa Ukuaji (asilimia)	4.0	4.5
3.2	Asilimia katika Pato la Taifa (bei za sasa)	7.0	6.6
3.3	Kiwango cha Vifo vya Mifugo	27	12
3.4	Kiwango cha Magonjwa ya Mifugo	6	3
3.5	Kiwango cha Uogeshaji Mifugo	70	85
3.6	Kiwango cha Chanjo ya Mifugo	25	50
3.7	Kiwango cha Uzalishaji Maziwa, Ng'ombe wa Asili (Lita)	2	4
3.8	Uzalishaji wa Nyama, Ng'ombe wa Asili (Uzito wa ng'ombe kwa Kg)	75	130
3.9	Asilimia ya Ngozi Nzuri	10	50
3.10	Uzalishaji wa Nyama (Tani, '000')	702	951.7
3.11	Uzalishaji wa Maziwa (Lita, kwa billion)	3.01	4.3
3.12	Asilimia ya Maziwa Yaliyochakatwa	5	14
3.13	Uchakataji wa Nyama (Tani)	286	500
3.14	Ngozi Zilizochakatwa (Tani)	1,190	9,210.6
3.15	Mauzo ya Nyama Nje (Tani)	692	7,200
3.16	Mauzo Nje ya Ngozi Safi (Tani)	25.5	92
4	**Uvuvi**		
4.1	Kiwango cha Wastani wa Ukuaji (%)	3.7	3.9
4.2	Asilimia katika Pato la Taifa (bei za sasa	1.8	3
4.3	Asilimia katika Mapato yatokanayo na Mauzo Nje	3.0	4.5
4.4	Ulaji kwa kila Mtu	8.5	10.5
4.5	Mchango katika Ulaji wa Protini ya Wanyama Kitaifa	30	35
4.6	Uzalishaji wa samaki (tani)	497,567.28	600,000
4.7	Idadi ya viwanda vya kusindika samaki	12	17
4.8	Idadi ya vituo vya kilimo majini (Aquaculture Development Centres - ADC)	9	12
4.9	Uzalishaji wa chakula cha samaki (tani)	464	2,500
4.10	Idadi ya maafisa ugani wa uvuvi	657	1,850

5.4.3 Uzalishaji Bidhaa Viwandani

Ubunifu ni mojawapo ya kigezo muhimu cha maendeleo ya biashara, hususan uwezo wa kuzalisha, matumizi ya teknolojia na mbinu za kisasa na ufanisi wa soko huria. Kuendeleza ubunifu na ushindani ni mbinu muhimu ya kujenga uwezo wa sekta ya uzalishaji bidhaa viwandani ili kuzalisha ajira, kuwezesha uwekezaji na biashara. Ubunifu unahusisha matumizi ya maarifa yanayochagiza njia mbadala za uzalishaji, uchakataji, upatikanaji wa masoko pamoja na matumizi ya moduli za kitaasisi na kibiashara kwa lengo la kuongeza thamani ya bidhaa.

Sekta ya uzalishaji viwandani inajumuisha: Maeneo Maalum ya Uwekezaji kwa ajili ya bidhaa za kuuza nje, maeneo kwa ajili ya biashara ndogo na za kati; viwanda vya petroli na kemikali; viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo; viwanda vya makaa ya mawe kwa ajili ya matumizi ya viwandani na majumbani; urani kwa ajili ya kuzalisha nishati; chuma cha kawaida na chuma cha pua; na viwanda vya magari.

Hatua Muhimu:

(i) Kuhamasisha uwekezaji na biashara katika maeneo maalumu ya uwekezaji (SEZ/EPZ);
(ii) Kuendeleza biashara na huduma sanjari na maeneo ya viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo;
(iii) Kukuza wajasiriamali wadogo na wa kati;
(iv) Kuboresha vitambulisho vya wajasiriamali ili kupanua wigo wa upatikanaji wa mitaji;
(v) Kutoa mafunzo ya ujasiriamali, kuhamasisha na kulea biashara changa;
(vi) Kuhamasisha uzalishaji wa magadi soda, vioo, aluminiamu, chumvi, gesi ya heliamu, kemikali na bidhaa zinazohusiana;
(vii) kuhamasisha na kuwezesha viwanda vya uchakataji wa mazao ya kilimo, hususan viwanda vya ngozi na mafuta ya kula;
(viii) Kuanzisha mafunzo kwa ajili ya uzalishaji na uchakataji wa chakula kwa wajasiriamali wadogo;
(ix) Kuhamasisha matumizi ya teknolojia endelevu kwa mazingira;
(x) Kuhamasisha matumizi ya nishati ya atomiki na teknolojia ya nyuklia;
(xi) Kuendeleza teknolojia ya chuma cha kawaida na chuma cha pua, na kufufua viwanda vilivyobinafsishwa;
(xii) Kuhamasisha ushindani wa kitaifa na kimataifa, hususan viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, nguo na mavazi, ngozi, kemikali, dawa na vifaa vya ujenzi;
(xiii) Kuimarisha kituo cha kuendeleza teknolojia za magari; na
(xiv) Kuimarisha utafiti na maendeleo katika uzalishaji viwandani.

Jedwali Na. 12 Shabaha na Viashiria vya Mwenendo wa Uzalishaji Viwandani

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1.1	Mchango katika Pato la Taifa, bei za sasa (%)	8.2	8.5
1.2	Ukuaji Halisi wa Pato la Taifa (%)	5.6	7.0
1.3	Mchango wa Ajira zote (%)	6.75	12.8
1.5	Mchango wa Mapato ya Mauzo Nje (%)	17.1	19
1.6	Mchango wa Teknolojia ya Chini (%)	35	42
1.7	Mchango wa Teknolojia ya Kati (%)	28	39
1.8	Mchago wa Teknolojia ya Juu (%)	8	10
1.9	Idadi ya Kampuni zinazouza Nje	1,180	2,114
1.10	Mchango katika Mauzo yote Nje (%)	16.9 (2019)	24

Boksi 6 Ubiasharishaji na Maendeleo ya Teknolojia

Kubuni, kuendeleza na kubiasharisha Vifaa Tiba

Serikali imeimarisha miundombinu ya huduma za afya kwa kujenga vituo zaidi ya 9,104 nchini. Maboresho ya miundombinu ya huduma za afya imeongeza mahitaji ya vifaa na zana za kitabibu. Ongezeko la mahitaji ya vifaa na zana za kitabibu ni fursa ya uwekezaji kwa wajasiriamali wa ndani na nje. Kwa msingi huo, Mpango utajielekeza katika kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia uwekezaji na uhawilishaji wa teknolojia kwenye sekta hii muhimu.

Uzalishaji wa Kibiashara wa zao la Katani na Miwa

Ujenzi wa viwanda umeendelea kupewa kipaumbele ili kuongeza uwezo wa Taifa wa kujitegemea na kukuza soko la ndani la mali ghafi za mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu, madini na vito vya thamani. Sambamba kuongeza uwezo wa kujitegemea na kukuza soko la mali ghafi za ndani, ujenzi wa viwanda ni muhimu katika kuzalisha ajira, uhawilishaji wa teknolojia na kuongeza mauzo ya bidhaa zilizochakatwa nje. Katika kipindi cha mwongo moja uliopita, mnyororo wa thamani umeongezeka kwa baadhi ya mazao na bidhaa, hususan sukari na katani kupitia mradi wa TEMDO. Mradi wa TEMDO unahusisha ubunifu wa teknolojia ya kisasa kwa ajili ya uzalishaji na usindikaji wa mazao ya miwa na katani.

5.4.4 Sekta ya Madini

Ufanisi wa sekta ya madini umeiwezesha Tanzania kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI), ikilinganishwa nchi nyingine za Afrika. Miongoni mwa madini na vito vya thamani vinavyovutia uwekezaji ni pamoja na: dhahabu; almasi; tanzanite; rubi; magadi; makaa ya mawe; madini ya chuma; udongo wa mfinyanzi; na urani. Hivyo, Mpango unalenga kuweka mazingira wezeshi na kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya madini.

Hatua Muhimu:

(i) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa uchimbaji mkubwa na wa kati;
(ii) Kuwezesha wachimbaji wadogo kushiriki katika shughuli za uchimbaji na upatikanaji wa masoko;
(iii) Kuimarisha Tume ya Madini, Taasisi ya Jeolojia na Utafiti wa Madini, na Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC);
(iv) Kuhamasisha uongezaji thamani ya madini;
(v) Kuainisha, kuhamasisha na kuwezesha uchimbaji wa madini adimu; na
(vi) Kuimarisha mashirika na masoko ya madini, vituo vya maonesho na umahiri.

Jedwali Na. 13 Viashiria na shabaha za Utekelezaji Katika Sekta ya Madini

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1.1	Wastani wa Ukuaji (%)	8.6	8.0
1.2	Mchango kwenye Pato la Taifa (%)	5.2	10.0
1.3	Jumla ya Mapato ya Fedha za Nje (Dola za Marekani milioni)	2,997	5,505
1.3.1	% ya mauzo ghafi nje	15	5
1.3.2	% ya zilizoongezwa thamani	85	95
1.4	% Mchango katika mapato yote ya fedha za nje	50.3	50.5

5.4.5 Ujenzi

Ujenzi ni miongoni mwa sekta chake zinazokua kwa kasi na kuchanjia sehemu kubwa katika Pato la Taifa. Sekta ya ujenzi inajumuisha miundombinu ya barabara, madaraja, reli, bandari, viwanja vya ndege na makazi. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango, Serikali itaendelea kuimarisha na kujenga miundombinu msingi ili kuchochea shughuli za kiuchumi.

Hatua Muhimu zinahusiha:

(i) Kutoa kupaumbele kwa kampuni za ndani za ujenzi;
(ii) Kuimarisha maendeleo ya ujuzi;
(iii) Kuimarisha programu za mafunzo na kujenga uwezo wa wataalamu wa ndani (wakandarasi, wahandisi, wasanifu majengo na wakadiria majenzi);
(iv) Kuanzisha dirisha la utoaji wa taarifa za kihandisi;
(v) Kujenga majengo ya Serikali na nyumba za wafanyakazi;
(vi) Kuimarisha miundombinu ya nchi kavu, baharini na anga; na
(vii) Kurasimisha na kuimarisha Mfuko wa Kusaidia Wakandarasi.

Jedwali Na. 14 Viashiria na Shabaha za Utekelezaji Katika Sekta ya Ujenzi

Na.	Kiashiria/ Shabaha	2020/21	2025/26
1.1	Wastani wa Ukuaji (%)	14.8	18
1.2	Mchango katika Pato la Taifa (%)	14.3	17.3
1.3	Mchango wa kampuni za Ndani kwenye Soko la Ujenzi (%)	35	60
1.4	Idadi ya Ajira zilizozalishwa katika Miradi ya Maendeleo	23,585	30,129 (2024/25)
1.5	Mchango katika Jumla ya Ajira Zote (%)	14.7	18.8

5.4.6 Usimamizi wa Mazingira na Maliasili Asilia

Mazingira na maliasili asilia ni tunu ya Taifa na msingi wa maendeleo endelevu. Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya utunzaji wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali asilia kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Matumizi endelevu, ulinzi na ustawi wa wanyamapori, misitu, mito, maziwa,

bahari, mabonde, milima, makazi ya viumbehai, ardhi, madini na vito vya thamini ni miongoni mwa maeneo muhimu yatakayozingatiwa katika Mpango huu.

Hatua Muhimu zinahusisha:

(i) Kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu;
(ii) Kuimarisha usimamizi wa tathmini ya athari ya mazingira na jamii;
(iii) Kuimarisha na kuhamasisha matumizi endelevu ya maliasili asilia kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii;
(iv) Kupunguza uchafuzi wa mazingira pamoja na madhara yake;
(v) Kuimarisha uwezo wa Taifa kukabiliana na matokeo ya mabadiliko ya tabianchi; na
(vi) Kuimarisha usalama katika matumizi ya teknolojia mpya ya kibaiolojia.

Jedwali Na. 15 Viashiria na Shabaha za Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1.1	Wastani wa Ukuaji (%)	4	7
1.2	Mchango katika Pato la Taifa kutokana na matumizi endelevu ya misitu, maji na rasilimali za bahari	4	7
1.3	Mchango wa utalii endelevu katika Pato la Taifa (%)	6	11
1.5	Eneo la msitu chini ya jamii (Area under Community Plantations) (Ha))	120,000	160,000
1.6	Kiwango cha kupungua kwa uharibifu wa misitu (Reduced Deforestation Rate) (Ha.)	469,420	234,710
1.7	Maeneo ya misitu ya kibishara (commercial forest Plantation) yaliyoanzishwa (Ha)	500,000	550,000
1.8	Matumizi ya nishati mbadala ya mkaa (tani)	100	100,000
1.9	Asilimia ya miradi mikubwa inayokidhi uchambuzi wa athari kwa mazingira (EIA) na kanuni za ukaguzi	90	90

5.4.7 Uchumi Shindani

Uchumi shindani unahusisha miundombinu thabiti, taasisi imara, utengemavu wa uchumi-jumla na upatikanaji wa taarifa kuwezesha ustawi wa biashara katika ngazi ya taifa na kimataifa. Uchumi huu huwezesha biashara kukua, kuzalisha ajira na kuvutia uwekezaji wa ndani na nje. Maeneo ya kuzingatia katika Mpango huu ni pamoja na: malighafi, mchakato wa uzalishaji, ubora wa bidhaa na huduma na kiwango cha ushindani. Kwa msingi huo, dhana hii inalenga kuimarisha taasisi, sera, na mazingira wezeshi ili kuongeza tija katika uzalishaji.

Hatua Muhimu zinahusisha:

(i) Kuimarisha utulivu wa uchumi jumla;
(ii) Kujenga, kukarabati na kufungamanisha miundombinu wezeshi;
(iii) Kuimarisha mifumo ya kitaasisi na miongozo ya udhibiti;

(iv) Kuhamasisha ubunifu na matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma;
(v) Kuhamasisha masoko ya bidhaa, fedha na ajira;
(vi) Kuhamasisha ujuzi, maarifa na uhawilishaji wa teknolojia;
(vii) Kuhamasisha mifumo ya biashara na ugharamiaji;

Jedwali Na. 16 Viashiria vya Jumla vya Uchumi Shindani

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2019/20	2025/26
1.1	Utengemavu wa uchumi-jumla	86/141	40/141
1.2	Miundombinu	121/141	60/141
1.3	Taasisi	97/141	50/141
1.3.2	Matumizi ya TEHAMA	133/141	70/141
1.3.4	Afya	114/141	70/141
1.3.5	Ujuzi	126/141	60/141
1.3.6	Soko la Bidhaa	107/141	60/141
1.3.7	Soko la Ajira	86/141	40/141
1.3.8	Sekta ya Fedha	114/141	70/141
1.3.9	Kiwango cha Soko	73/141	45/141
1.3.10	Hamasa ya Kibiashara	107/141	50/141
1.3.11	Uwezo wa Ubunifu	123/141	50/141

5.4.8 Kuimarisha Utengemavu wa Uchumi-jumla

Uchumi shindani unategemea utengamavu viashiria vya uchumi-jumla vinavyotabirika. Tanzania imeendelea kunufaika na ukuaji wa uchumi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, ambapo kiwango cha wastani cha ukuaji pato ghafi ulikuwa asilimia 6.9, mfumuko wa bei asilimia 4.4 na nakisi ya bajeti kufikia asilimia 1.4 mwaka 2019/20 kutoka asilimia 3.4 mwaka 2015/16. Mpango huu unalenga kuimarisha sera na utulivu wa viashiria vya uchumi-jumla, hususan mfumuko wa bei, thamani ya shilingi, riba, urari wa malipo, urari wa biashara, nakisi ya bajeti na deni la Taifa.

Hatua Muhimu zinahusisha:

(i) Kuimarisha sera za fedha;
(ii) Kuimarisha mifumo ya kiutawala na kibajeti katika ukusanyaji wa mapato ya ndani;
(iii) Kuimarisha na kutekeleza hatua madhubuti za udhibiti wa matumizi ya fedha za umma;
(iv) Kuelekeza fedha za mikopo na misaada kwenye miradi yenye matokeo makubwa kijamii na kiuchumi;
(v) Kuhamasisha mauzo ya bidhaa nje;
(vi) Kuimarisha mazingira wezesheji ya uendeshaji wa viwanda;
(vii) Kuhamasisha na kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji wa kimkakati, ikijumuisha miradi ya ubia;

(viii) Kuhimiza utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara; .
(ix) Kuimarisha usimamizi wa benki na masoko ya mitaji na dhamana;
(x) Kuanzisha Kituo cha Ubia na Mfuko wa Kuwezesha miradi ya ubia;
(xi) Kuhamasisha na kuimarisha mifuko ya uwekezaji, uwezeshaji na vituo vya ujasiriamali; na
(xii) Kuimarisha mifumo ya kukusanya, kuchakata na kusambaza takwimu rasimi.

Jedwali Na. 17 Viashiria vya Utulivu wa Uchumi-jumla Katika Uchumi Shindani

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1.1	Ukuaji halisi wa Uchumi	5.6	8.0
1.2	Mfumuko wa Bei	3.4	3.0
1.3	**Uwiano wa Mapato ya Serikali kwa Pato la Taifa (%)**	**15.**6	16.9
1.4	Uwiano wa Mapato ya Kodi kwa Pato la Taifa (%)	13.1	14.4
1.5	Kiwango cha Ubadilishanaji na Fedha za Kigeni (TZ/USD)	2,340	2,497
1.6	Nakisi ya bajeti (%)	-2.6	≤ -3.0
1.7	% ya Deni la Taifa kwa Pato la Taifa	27.9	28.2
1.8	Kiwango cha ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi-M3) (%)	≥ 10.0	≥ 10.0
1.9	Akiba ya fedha za nje	≥ 4 miezi	≥4 miezi
1.11	Muda unaotumika kukamilisha shughuli za forodha tangu kukabidhi nyaraka hadi kutolewa idhini ya kuchukua mizigo – Bandari ya Dar es salaam (siku)	1	0.25
1.12	Kiwango cha uelewa wa walipa-kodi, juu ya programu za elimu kwa walipa-kodi	79	100

5.4.9 Huduma za Fedha

Sekta ndogo ya Bima

Bima ni bidhaa inayotumika kulinda biashara, uwekezaji, mitaji, mali na maisha dhidi ya madhara yatokanayo na majanga. Ili kupunguza vihatarishi vya madhara ya majanga na kuongeza mchango wa sekta katika pato la taifa, Mpango utajielekeza katika maeneo makuu matatu ambayo ni: Kujenga uelewa na hamasa kwa umma kuhusu faida ya bidhaa za bima; kubuni bidhaa za bima kuendana na mahitaji ya soko; na mifumo ya kushughulikia madai, malipo na malalamiko ya wateja.

Hatua Muhimu zinahusisha:

(i). Kuhamasisha na kuendesha programu za elimu ya bima kwa umma;
(ii). Kuanzisha na kuhamasisha bidhaa za bima zinazohitajika katika soko; na
(iii). Kuanzisha mfumo madhubuti wa kushughulikia madai, malipo na malalamiko ya wateja.

Jedwali Na. 18 Viashiria na Shabaha za Sekta Ndogo ya Bima

Na.	Viashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
	Mchango kwenye Pato la Taifa (%)	0.7	2
	Kiwango cha ukuaji halisi (%)	28.5	29.1
	Kiwango cha uelewa wa wananchi juu ya masuala ya bima (%)	36	78
	Kiwango cha kuridhika kwa wateja/ulinzi (%)	70	80
	Idha ya bidhaa za bima zilizoingia sokoni kufuatia mahitaji ya wateja	2	7
	% ya watu wazima wanaotumia huduma za bima	6	18
	Kiwango cha rasilimali za bima kwa Pato la Taifa (%)	0.9	3
	Idadi ya watu wanaotumia huduma za bima	3,582,000	12,278,000

Sekta ndogo ya Soko la Mitaji

Masoko ya Mitaji huwezesha utafutaji na upatikanaji wa mitaji. Mchakato huo unahusisha uuzaji na ununuzi wa hisa na skimu za uwekezaji wa pamoja. Hivyo, masoko ya mitaji ni muhimu katika kuelekeza mitaji kwa wawekezaji wenye nia ya kuwekeza katika sekta za uzalishaji na huduma.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kuhamasisha na kutekeleza programu za kujenga uelewa wa masoko ya mitaji;
(ii) Kuhamasisha uanzishaji wa bidhaa na huduma nafuu za mitaji;
(iii) Kuimarisha mazingira ya kisera, mifumo ya kisheria na miundo ya kitaasisi ya masoko ya mitaji; na
(iv) Kuhamasisha uanzishaji wa masoko ya mitaji.

Jedwali Na. 19 Viashiria na Shabaha kwa Sekta Ndogo ya Soko la Mitaji

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1.1	% ya watu waliowekeza kwenye Soko la Mitaji	1.3	3
1.2	Idadi ya kampuni zilizo orodheshwa Soko la Mitaji	28	35
1.3	Uwiano wa mtaji wa Soko la Mitaji kwa Pato la Taifa (%)	7.4	10

5.4.10 Kuimarisha Miundombinu ya Usafiri na Usafirishaji

Miundombinu ya usafiri na usafirishaji, ikijumuisha barabara, reli na bandari ni muhimu katika kuchochea shughuli za kiuchumi. Aidha, eneo la jiografia linaipa fursa ya kipekee Tanzania katika usafirishaji, biashara na uwekezaji, ikilinganishwa na nchi jirani. Kutokana na faida linganifu, Mpango utajielekeza katika kuboresha miundombinu ya barabara, reli na bandari.

Hatua Muhimu zinahusisha:

Barabara

(i) Kukamilisha ujenzi wa kilometa 2,500 za barabara kwa kiwango cha lami;
(ii) Kupunguza msongamano wa magari katika majiji;
(iii) Kuanza ujenzi wa kilometa 6,006 za barabara kwa kiwango cha lami;
(iv) Kuanza ujenzi wa madaraja 14; na
(v) Kukamilisha ujenzi wa madaraja 7.

Reli

(i) Kuendelea kuimarisha miundombinu ya reli ya TAZARA, kati, kasikazini na kusini na kukarabati mabehewa;
(ii) Kukamilisha ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha SGR na ununuzi wa mabehewa; na
(iii) Kuanzisha vituo vya biashara katika maeneo ya vituo vya treni; na

Bandari

(i) Utanuzi wa bandari za Dar es salaam, Tanga na Mtwara na maziwa makuu (Mwanza, Kigoma na Itungi);
(ii) Ununuzi wa vifaa vya kupakua na kupakia mizigo;
(iii) Ununuzi na ukarabati wa meli; na
(iv) Kuanzisha bandari kavu.

5.4.11 Sekta ya Nishati

Sekta hii ni wezeshi katika uzalishaji viwandani, biashara na shughuli nyingine za kiuchumi na kijamii. Kwa msingi huo, sekta ya nishati iendelezwe kimkakati ili kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii, hususan uzalishaji na usambazaji wa umeme mijini na vijijini, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi na kuboresha mazingira wezeshi ya uwekezaji wa sekta binafsi.

Hatua Muhimu zitahusisha:

(i) Kuimarisha upatikanaji wa nishati ya umeme;
(ii) Kujenga na kuimarisha miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia kwa matumizi ya majumbani, viwandani na usafirishaji;
(iii) Kuhamasisha na kuendeleza teknolojia na miradi ya nishati jadidifu;
(iv) Kuimarisha usimamizi na matumizi endelevu ya nishati ya mafuta na gesi; na
(v) Kuhamasisha utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

Jedwali Na. 20 Viashiria na Shabaha katika Ujenzi wa Miundombinu

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
	Miundombinu (Nafasi katika mpangilio, kati ya nchi 189 kimataifa	102	100
	Barabara		
	Nafasi ya barabara katika mpangilio wa kimataifa	86	55
	Uwiano wa barabara za lami katika mfumo wa barabara zote (%)	8.9	12
	Reli		
	Nafasi ya reli katika mpangilio wa kidunia	83	70
	Urefu wa reli ya kati ya mwendo-kasi (SGR) kwa kilometa	395.2	1,219
	Kiasi cha shehena kinachosafirishwa na reli (tani)	1,569,536	2,162,258
	Idadi ya abiria wanaosafirishwa na reli	972,000	2,272,682
	Bandari		
	Nafasi ya bandari katika mpangilio wa kidunia	72	50
	Muda wa meli kurejea kituoni kwake (siku)	3	2
	Idadi ya meli zinazoingia bandarini kwa mwezi	2,106	3050
	Muda wa makasha kukaa bandarini (siku)	7	5
	Muda wa meli kukaa bandarini (siku)	2	2
	Idadi ya bandari kavu	2	3
	Idadi ya meli zinazohudumiwa	3,704	4,000
	Mizigo inayopita bandarini (tani)		
	Mizigo inayotoka nje kuelekea nchi za jirani (tani milioni)	15.1	18.0
	Mizigo ya kwenda nje toka kwa nchi jirani (tani milioni)	6.3	10.0
	Usafiri wa Anga		
5.1	Idadi ya ndege zilizonunuliwa	10	19
5.2	Idadi ya viwanja vya ndege vyenye vifaa	4	10
5.3	Idadi ya ndege za mizigo zilizonunuliwa	0	1
5.4	Idadi ya ndege za abiria za masafa marefu zilizonunuliwa	2	3
5.5	Idadi ya ndege za abiria za masafa ya kati (kanda) zilizonunuliwa	2	8
5.6	Idadi ya ndege za ATCL zinazofanya kazi	10	19
5.7	Idadi ya wanaanga waliofunzwa	61	1,359
5.8	Idadi ya Viwanja vya ndege vyenye mifumo ya usimamizi wa taarifa za viwanja vya ndege	1	14
5.9	Idadi ya mitambo ya ulinzi kwenye viwanja vya ndege (X-ray machines)	46	71
5.10	Viwanja vya ndege vyenye uzio kuzunguka kiwanja	9	27
5.11	Idadi ya rada za hali ya hewa zilizonunuliwa	5	7
	Mawasiliano		

	% ya watumiaji wa mtandao wa intanet	43	80
	Eneo la masafa ya mawasiliano (Broadband coverage)	45	80
	% ya taasisi za Serikali zilizoungwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano	20	70
	%Kaya zenye angalau mwanakaya mmoja anayemiliki simu ya mkononi	82.6	87.8
	%ya mchango wa sekta ya mawasiliano katika Pato la Taifa	1.5	3
	Idadi ya watu wanaomiliki simu za mkononi (milioni)	25.1	28.6
	Idadi ya Kaya zinazotumia mfumo wa anwani za makazi na misimbo ya posta	450,980	1,975,000
	Idadi za Taasisi za Umma zinazotumia mfumo anwani na misimbo ya posta	48,516	97,000
	% ya idadi ya watu wanaopata mtandao wa simu za mkononi	94	100
	Idadi ya wataalamu wa TEHAMA waliosajiliwa	283	5,000
	Urefu wa Mkongo wa Taifa wa Mawasisiliano (NICTBB) uliojengwa, kwa kilometa	7,910	15,000
	Eneo la huduma ya mawasiliano ya simu (%)	86	95
	Idadi ya tarafa zilizowekewa mfumo wa anwani za makazi na misimbo ya posta (postcode)	118	4,067
	Idadi ya akaunti za fedha za simu za mkononi	30,586,806	40,000,000
	Nishati		
	Nishati ya Umeme (MW)	1,602.3	4,915
	Umeme – Idadi ya mikoa iliyounganishwa kwenye gridi ya taifa	23	26
	Umeme – urefu wa gridi ya taifa (km)	5,896.3	9,351
7.4	Umeme – Matumizi ya mtu mmoja (KWh)	137	220
7.5	Kupungua kwa upotevu wa umeme (%)	16.19	12.3
7.6	Kiasi cha watu waliofikiwa na umeme (%)	78.4	85
7.7	Kiasi cha watu walioungnishiwa umeme (%)	39.9	60

5.4.12 Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Biashara

Mazingira rafiki ya uwekezaji na biashara ni muhimu katika kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi. Mpango utajielekeza katika kutatua changamoto zinazokwamisha uwekezaji na biashara nchini. Hatua hizo zitaongeza kasi ya ushindani, ubora wa bidhaa na huduma na kupunguza urasimu katika utendaji wa taasisi zinazosimamia uwekezaji na biashara.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kurahisisha michakato ya uwekezaji na biashara;

(ii) Kuimarisha mifumo ya kitaasisi, sera na sheria za kodi;

(iii) Kupunguza gharama za uwekezaji na biashara;

(iv) Kuimarisha usimamizi wa kanuni za kitaalamu na viwango vya kimataifa; na
(v) Kuboresha mifumo ya ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za biashara na masoko.

5.4.13 Kujenga Taasisi Imara

Taasisi imara, ikijumuisha sera, sheria, kanuni, mikakati na miongozo huwezesha usimamizi bora wa uwekezaji na biashara. Kwa msingu huo, maboresho ya taasisi huongeza tija katika utendaji, kujenga imani miongoni mwa wadau na kupandisha fursa ya nchi katika kuvutia uwekezaji na biashara. Hivyo, Mpango huu utashughulikia vikwazo vya kitaasisi ili kunufaika na fursa linganifu kikanda na kimataifa.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kuimarisha ufanisi katika usimamizi na umiliki wa ardhi;
(ii) Kuwezesha upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji wa kimkakati;
(iii) Kuharakisha urasimishaji wa makazi na maeneo ya uwekezaji na biashara;
(iv) Kutatua migogoro ya ardhi kati ya wawekezaji na wananchi;
(v) Kuimarisha utawala bora katika taasisi za umma na binafsi;
(vi) Kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha mfumo wa Udhibiti wa Biashara; na
(vii) Kuwianisha vivutio vya uwekezaji na biashara na sheria za kodi na tozo;

Jedwali Na 21 Shabaha za Jumla za Ufanyaji Biashara

Na.	Viashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1.1	Urahisi wa Kufanya Biashara (nafasi kidunia)	141/190	95/190
1.1.1	Uanzishaji wa Biashara	162/190	91/190
1.1.2	Kushughulikia Vibali vya Ujenzi	149/190	87/190
1.1.3	Upatikanaji wa Umeme	85/190	50/190
1.1.4	Kusajili Mali	146/190	55/190
1.1.5	Upatikanaji wa Mikopo	67/190	50/190
1.1.6	Kulinda Wawekezaji	105/190	40/190
1.1.7	Ulipaji Kodi	165/190	92/190
1.1.8	Biashara Nje ya Mipaka	182/190	102/190
1.1.8.1	Muda wa Kuuza Nje (siku)	8	< siku 4
1.1.8.2	Gharama za Kuuza Nje (Dola za Marekani)	1,175	600 – 800
1.1.8.3	Nyaraka za Kuuza Nje (idadi)	8	< 5
1.1.9	Utekelezaji wa Mikataba	71/190	14/190

5.4.14 Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

Matumizi ya sayanzi, teknolojia na ubunifu yameongeza ufanisi katika uzalishaji na usambazi wa bidhaa na huduma. Aidha, maeneo yaliyonufaika zaidi ni pamoja na: mawasiliano, huduma za fedha, utawala, masoko, afya, tafiti na usimamizi wa fedha

za umma. Sekta hii inaendelea kukua na inatarajiwa kuwa na matokeo chanya, hususan kwa kutumia mifumo ya kujitegemea ya kiintelijensia (artificial intelligence). Kwa muktadha huo, Mpango unatarajiwa kuhimiza matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu, hususan matumizi ya data, mitambo inayojiendesha, kompyuta na roboti.

Hatua Muhimu zinahusisha:

(i) Kuhamasisha na kuongeza mawanda ya matumizi ya mtandao;
(ii) Kubaini, kuwekeza na kurasimisha wataalamu wa TEHAMA;
(iii) Kuboresha miundombinu na kutanua wigo wa huduma ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;
(iv) Kuimarisha utendaji wa mamlaka za mawasiliano nchini;
(v) Kusajili misimbo ya posta nchini;
(vi) Kuhamasisha tafiti, uwekezaji na uzalishaji wa vifaa vya TEHAMA;
(vii) Kuimarisha ushirikiano na taasisi za sayansi, teknolojia na ubunifu za kikanda na kimataifa;
(viii) Kuhamasisha ubunifu wa bidhaa mpya za TEHAMA na kuzipa hati miliki; na
(ix) Kuanzisha na kuendeleza vituo vya umahiri vya TEHAMA (ICT - Centres of Excellence).

Jedwali Na. 22 Shabaha na Viashiria katika Sayansi, Ubunifu na Teknolojia

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
	Matumizi katika Utafiti na Maendeleo		
	Uwiano wa Matumizi ya T&M kwa Pato la Taifa (%)	0.8	1
	Jumla ya Matumizi Yote (Shilingi bilioni)	90.2	139.7
	Ambapo matumizi kwa Kilimo ni (%)	38.8	40.0
	Ambapo Matumizi kwa Uzalishaji Viwandani ni (%)	40.0	42.8
	Ambapo Matumizi kwa Uchimbaji Madini, Ujenzi & Huduma ni (%)	13.5	10.6
	Ambapo Huduma ni %	8.5	6.6
	Uwezo wa Kiteknolojia wa Taasisi		
	Matumizi ya T&M katika Sekta ya Umma (%)	68.3	72
	Idadi ya Watafiti Waliohitimu	9,556	12,639
	Taasisi za Utafiti zenye Ushirikiano na Taasisi nyingine za Nje	22	32
	Idadi ya Kampuni Zinazoshiriki katika TIUMP	80	200
	Idadi ya Kampuni Zinazoendesha KAIZEN	132	140
	Uwiano wa Wahandisi na Jumla ya Fedha Zote Zinazotolewa na Serikali kwa Mafunzo yaElimu ya Juu	1,567	2,660

Boksi 7 Uchumi wa Kidigitali

Uchumi wa kidigitali unaotegemea matumizi ya teknolojia ya kompyuta. Matumizi ya kompyuta yameongeza ufanisi na fursa za kiuchumi, hususan upatikanaji wa taarifa za masoko ya bidhaa na huduma, mbinu mbadala za uzalishaji na utoaji wa huduma na kupunguza gharama za miamala. Aidha, matumizi ya mifumo ya kidigitali ni matokeo ya uwekezaji wa Serikali katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Kituo cha Taifa cha Data.

Mpango huu unatarajiwa kujenga uwezo wa taasisi wa kuratibu, kusimamia na kuendeleza uchumi wa kidigitali, hususan ubunifu, uzalishaji viwandani na biashara mtandao. Aidha, Serikali itaweka mazingira wezeshi ili kuhamasisha ubunifu na uhawilishaji wa teknolojia kulingana na mahitaji ya soko.

5.4.15 Biashara

Ufanisi katika biashara unategemea mtandao imara wa miundombinu ya barabara, reli, bandari, maji na umeme. Aidha, mifumo na miundo ya taasisi, sera, sheria, kanuni, mikakati na miongozo ni msingi muhimu katika kuwezesha biashara. Ili kuimarisha ushindani na kuongeza mchango wa sekta ya biashara kwenye Pato la Taifa, Mpango utajielekeza katika kuimarisha na kuboresha mifumo, taasisi, miundombinu na mahusiano ya kibiashara kikanda na kimataifa.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kubainisha na kuingia makubaliano ya kimikataba ya biashara na masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini;
(ii) Kuanzisha vituo vya kuendeleza ujarisiriamali na huduma za kibiashara;
(iii) Kurahisisha na kuwianisha taratibu za kutatua vikwazo vya biashara visivyo vya kikodi;
(iv) Kuimarisha ufanisi, miundombinu ya usafirishaji, mamlaka za udhibiti na watoa huduma;
(v) Kupunguza vihatarishi vya biashara katika mnyororo wa thamani;
(vi) Kuratibu na kuwezesha masoko bidhaa na huduma mipakani;
(vii) Kuhamasisha biashara ya bidhaa na huduma zilizoongezwa thamani; na
(viii) Kuhamasisha ubunifu wa bidhaa na huduma zenye chapa (brand) ya Tanzania.

Jedwali Na. 23 Viashiria na Shabaha katika Ukuzaji Biashara

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
	Mauzo Nje		
	Mchango wa Mauzo Nje katika Pato la Taifa (%)	16.1	28.0
	Mchango wa Bidhaa za Viwanda katika Mauzo Nje (%)	35	40
	Mchango wa Huduma katika Mauzo Nje (%)	45	50
	Mchango wa Mauzo Nje katika Soko la Dunia (%)	0.1	0.15
	Mchango wa Mauzo Nje katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (%)	7	15
	Ambapo sehemu ya bidhaa za viwanda ni (%)	10.8	14
	Mchango wa Mauzo Nje SADC (%)	14	30
	Uagizaji Bidhaa toka Nje		
	Mchango wa Uagizaji Bidhaa toka Nje katika Pato la Taifa (%)	17.9	13
	Mchango wa Bidhaa za Kawaida katika Uagizaji wa Bidhaa toka Nje (%)	15	12
	Mchango wa Bidhaa za Kati katika Uagizaji wa Bidhaa toka Nje (%)	32	23
	Mchango wa Uagizaji Bidhaa toka Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (%)	7.5	11
	Mchango wa Uagizaji Bidhaa toka SADC (%)	10	10

5.4.16 Sekta ya Utalii

Sekta ya utalii inachangia zaidi ya asilimia 17 katika Pato la Taifa na asilimia 25 ya fedha za kigeni. Sekta hii ina fursa ya kuchangia zaidi kwenye Pato la Taifa na kuliingizia Taifa fedha za kigeni kutokana na kuwa na vivutio adimu, ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika. Vivutio vya utalii vinavyopatikana Tanzania ni pamoja na: mbuga za wanyama; maeneo tengefu; mimea; milima; mabonde; maporomoko na ukanda wa bahari. Mpango unatoa kipaumbele katika kukuza na kuendeleza sekta ya utalii, hususan kuboresha miundombinu na mazingira ya utalii, mifumo na miuondo ya kitaasisi na kufungamanisha maeneo adimu ya utalii.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kufungamanisha mikutano na makongamano ya utalii na vivutio vya utalii;
(ii) Kuhamasisha na kuimarisha utalii wa uwindaji, bahari, utamaduni, sanaa na michezo, jiolojia na ikolojia;
(iii) Kubuni na kuendeleza bidhaa za utalii;
(iv) Kuimarisha usimamizi wa maeneo ya kihistoria na malikale; na
(v) Kuimarisha utekelezaji wa sera, sheria, kanuni na miongozo ya utalii nchini; na

Jedwali Na.24 Viashiria na Shabaha Katika Sekta Ndogo ya Utalii

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1.1	Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa, bei za sasa (%)	17.5	11
1.2	Ukuaji Halisi wa Sekta (%)	1.5	2.0
1.3	Idadi ya Watalii	1,527,230	5,000,000
1.4	Wastani wa idadi ya siku walizolala Watalii nchini	13	14
1.5	Wastani wa Matumizi ya Mtalii kwa Siku (yasiyo ya mkataba/ya mkataba) (Dola za Marekani)	216/379	326/455
1.6	Ajira (idadi)	1,500,000	1,750,000
1.7	Mchango katika Mapato yote ya Fedha za Kigeni (%)	25	27
1.8	Mapato toka kwa Watalii (Dola za Marekani bilioni)	2.6	6.0

5.4.17 Tasnia ya Ubunifu

Tasnia ya sanaa na burudani ni moja ya sekta ya huduma inayokua kwa kasi Tanzania, ikivutia nguvukazi ya vijana. Sekta hii inajumuisha muziki, vichekesho, filamu, michezo na michezo ya kubahatisha. Kwa kutambua umuhimu wa sanaa na burudani, Mpango utaweka mazingira rafiki ili kuchochea ubunifu, kuzalisha ajira na kuongeza mchango sekta katika Pato la Taifa.

Hatua muhimu unahusisha:

(i) Kuhamasisha uwekezaji wa kimkakati katika tasnia ya sanaa na burudani;
(ii) Kuimarisha na kulinda kazi za ubunifu wa sanaa na burudani;
(iii) Kuandaa programu za mafunzo kuhusu ubunifu na usimamizi wa sanaa na burudani;
(iv) Kuendeleza tafiti na uhifadhi wa tamaduni, mila na desturi za kitanzania;
(v) Kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Urithi wa Ukombozi Afrika (African Liberations Heritage Programme);
(vi) Kuimarisha Baraza la Kiswahili la Afrika Mashariki na kuhamasisha matumizi ya kiswahili katika kikanda na kimataifa;
(vii) Kujenga uwanja wa mpira wa miguu wa kisasa jijini Dodoma na kuboresha eneo changamani la michezo Dar es Salaam;
(viii) Kulinda kazi za michezo, sanaa na utamaduni;
(ix) Kutenga na kulinda maeneo maalumu kwa ajili ya shughuli za utamaduni, sanaa, michezo na burudani;
(x) Kuimarisha na kuboresha taasisi za tasinia ya habari;
(xi) Kuimarisha na kuboresha huduma za uchapaji; na
(xii) Kuboresha miundombinu ya mafunzo na vifaa.

Jedwali Na. 25 Shabaha na Viashiria Katika Tasnia ya Ubunifu

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1.1	Idadi ya wilaya zinazofikiwa na matangazo ya TBC (TBC_{FM} na TBC_{Taifa}).	102	161
1.2	Idadi miundombinu ya michezo na iliyoboreshwa nchini kote	63	72
1.3	Idadi ya miundombinu iliyojengwa/kukarabatiwa katika Chuo cha Kuendeleza Michezo cha Malya na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni cha Bagamaoyo (TaSUBa).	35	40
1.4	Idadi ya filamu na muziki iliyoidhinishwa kusambazwa/kutumika	15,303	25,735
1.5	Idadi ya wasanii katika tasnia ya ubunifu waliosajiliwa	3,462	8,666
1.6	Idadi ya mikutano ya waandishi wa habari iliyofanyika kuhusu utekelezaji wa sera, mipango na miradi ya serikali	64	144
1.7	Idadi ya kumbi za sinema na burudani zilizosajiliwa	442	709
1.8	Idadi ya wataalamu katika tasnia ya ubunifu waliopata mafunzo	2,852	4,297
1.9	Idadi ya michezo na mashindano ya kimataifa yaliyoandaliwa na kushiriki	178	350
1.10	Idadi ya vibali vilivyotolewa kwa vyama vya michezo na wanamichezo binafsi	178	400
1.11	Idadi ya wanariadha wanaocheza nje ya nchi	54	150
1.12	Idadi ya wageni wanaoendesha shughuli za kuzalisha filamu nchini Tanzania.	359	1,059
1.13	Idadi ya magazeti yanayozalishwa na Shirika la Magazeti la Taifa (TSN)	4,158,642	4,659,975
1.14	Idadi ya wasanii/wataalamu katika tasnia ya ubunifu/makundi yanayofanya maonesho yao nje ya nchi	1,620	1,755
1.15	Idadi ya wasanii wa nje/wataalamu katika tasnia ya ubunifu wanaofanya maonesho yao nchini Tanzania	720	2,312
1.16	Mapambano ya uharamia wa filamu na shughuli za muziki	3,050,638	1,000,000
	Kiasi cha mrahaba kinachotolewa kwa wasanii na idadi ya wasanii walionufaika (shilingi milioni)/wasanii	220.01	1,225.00
		1,934	2,100
1.17	Idadi ya wataalamu wa Kiswahili wanaofanya kazi nje ya Tanzania	56	656
1.18	Idadi ya machapisho ya Kiswahili yaliyouzwa nje ya nchi	200	700
1.19	Idadi ya tuzo za kimataifa zilizotolewa zilizoandaliwa na kutolewa kwenye utamaduni, sanaa na tasnia ya ubunifu	47	130
1.20	Idadi ya wataalamu wa nje katika utamaduni na sanaa walioshiriki katika matamasha ya kimamatifa yanayoandaliwa kila mwaka na TaSUBa	5	20
1.21	Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa Chuo cha Kuendeleza Michezo cha Malya	300	1,300
1.22	Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa TaSUBa	350	950
1.23	Bodi ya Ithbati ya Waandishi wa Habari (Journalists Accreditation Board)	0	1
1.24	Baraza Huru la Wanhabari (Independent Media Council)	0	1

1.25	Mfuko wa Mafunzo ya Wanahabari (Media Training Fund)	0	1

5.4.18 Maendeleo ya Watu

Maendeleo ya watu ni hatima kuu ya mpango wa maendeleo nchini. Katika kufanikisha hilo, ni muhimu Mpango ukajikita katika kuboresha huduma za afya, elimu na ujuzi, maji, lishe, makazi, mipango miji na hifadhi ya jamii na hivyo kuimarisha ustawi wa jamii.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kuimarisha miundombinu ya huduma za jamii na vitendea kazi;
(ii) Kuanzisha programu mahsusi za kuongeza ujuzi na maarifa kwa nguvukazi;
(iii) Kuanzisha na kuwezesha programu za mafunzo kwa kada adimu;
(iv) Kuimarisha vituo vya mafunzo ya ufundi na ufundi stadi;
(v) Kuwezesha sekta binafsi kuwekeza katika ujuzi adimu;
(vi) Kuhamasisha na kuwezesha shughuli za kiuchumi kwa watu wa kipato cha chini;
(vii) Kuhamasisha programu za ustawi wa jamii, upatikanaji wa huduma ya bima ya afya na hifadhi ya jamii; na
(viii) Kuhamasisha programu za mafunzo kwa vitendo.

Jedwali Na. 26 Viashiria na Shabaha za Maendeleo ya Watu

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	**2025/26**
1.1	Fahirisi cha Maendeleo ya Watu (HDI)	0.57	0.60
2.1	Uwiano wa idadi ya watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji muhimu (kitaifa)	26.4 (2018)	22
2.2	Uwiano wa idadi ya watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji muhimu (vijijini)	31.3 (2018)	28.4
2.3	Uwiano wa idadi ya watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji muhimu (mijini)	15.8 (2018)	13.2
2.4	Uwiano wa idadi ya watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya chakula (kitaifa)	8.0 (2018)	5.8
2.5	Uwiano wa idadi ya watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya chakula (vijijini)	9.7	8.0
2.6	Uwiano wa idadi ya watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya chakula (mijini)	4.4	3.1
2.7	*Poverty Head Count*	26.4	20.2
3.1	Utofauti wa kipato (kitaifa)	0.38*	0.36
3.2	Utofauti wa kipato (vijijini)	0.32*	0.30
3.3	Utofauti wa kipato (mijini)	0.38*	0.37
3.4	Kiwango cha ukosefu wa ajira (kitaifa)	9.7**	8.0

*HBS 2017/18

** ILFS 2014/15

5.4.19 Ubora wa Elimu na Maendeleo ya Ujuzi

Ubora wa Elimu

Ubora wa elimu unajumuisha maarifa na ujuzi ambao unaendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi. Maarifa na ujuzi stahiki huongeza tija katika uzalishaji na utoaji huduma. Kwa msingi huo, Mpango utajielekeza kuboresha mifumo ya elimu, kuwianisha elimu na mahitaji ya soko la ajira, ikiwa ni pamoja na kuchochea uvumbuzi na uhawilishaji wa teknolojia.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kuongeza bajeti ya Tafiti na Maendeleo (T&M) katika sekta ya elimu;
(ii) Kuimarisha mashirikiano ya kikanda na kimataifa katika elimu, sayansi, teknolijia, ufundi na ufundi stadi;
(iii) Kuboresha miundombinu ya vyuo vya kada maalumu na adimu;
(iv) Kuwianisha idadi ya walimu, madarasa, vitabu, madawati na wanafunzi katika ngazi zote za elimu;
(v) Kuhuisha na kuboresha umahiri wa walimu katika masomo ya hisabati na sayansi;
(vi) Kuwezesha upatikanaji wa vifaa na zana kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu;
(vii) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wanaochukua masomo ya sayansi, hesabu, kada maalumu na adimu;
(viii) Kuhamasisha na kuwezesha matumizi ya TEHAMA kufundisha na kujifunza katika ngazi zote za elimu; na
(ix) Kuboresha mazingira ya kufanya kazi kwa walimu katika ngazi zote za elimu.

Jedwali Na. 27 Viashiria na Malengo Katika Elimu na Maendeleo ya Ujuzi

Na.	Viashiria/Malengo	2020/21	2025/26
1	**Elimu**		
1.1	**Elimu ya Awali**		
1.1.1	Kiwango cha udahili wa jumla (% ya wanaostahili)	78.5	100
1.1.2	Kiwango cha udahili halisi (% ya wanaostahili)	35.9	80
1.1.3	Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa mmoja (Pupil/Qualified Teacher Ratio - PTR)	130:1	50:1
1.1.4	Idadi ya walimu wenye sifa	8,000	8,727
1.2	**Elimu ya Msingi**		
1.2.1	Kiwango cha udahili wa jumla (% ya wanaostahili)	110.6	100
1.2.2	Kiwango cha udahili halisi (% ya wanaostahili)	95.7	100
1.2.4	Asilimia ya kundi wanaofaulu mtihani (PSLE)	82.24	100
1.2.5	Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu mmoja	56:1	50:1

1.2.6	Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa kitabu kimoja	4:1	1:1
1.2.7	Uwiano wa idadi ya wanafunzi katika darasa moja (Pupil/Classroom Ratio)	75:1	60:1
1.2.8	Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa choo kimoja (wavulana)	54:1	25:1
1.2.9	Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa choo kimoja (wasichana)	51:1	20:1
1.2.10	Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa dawati moja (Pupil/desk Ratio)	4:1	2:1
1.2.11	% ya shule zenye maji	49.3	60.0
1.2.12	% ya shule zenye umeme	43.5	60.0
1.2.13	Kiwango cha ufaulu kutoka darasa la saba kuingia kidato cha kwanza	77.55	95.9
1.2.14.	Kiwango cha elimu a watu wazima	77.6	81.6
1.3	**Elimu ya Sekondari**		
1.3.1	Kiwango cha udahili wa jumla, sekondari za chini (% ya wanaostahili)	46	48
1.3.2	Kiwango cha udahili halisi, sekondari za chini (% ya wanaostahili)	36	42
1.3.3	Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu mmoja, sekondari za chini	23:1	20:1
1.3.4	Uwiano wa idadi ya wanafunzi katika darasa moja, sekondari za chini	41:1	40:1
1.3.5	Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa choo kimoja	27:1	20:1
1.3.6	% ya shule zenye maji safi	68.5	88.5
1.3.7	% ya shule zenye umeme	69.8	85
1.3.8	% ufaulu wa wanafunzi katika mtihani wa kidato cha IV	80.65	90.0
1.3.9	% ufaulu wa wanafunzi kutoka kidato cha IV kuingia kidato cha V	19.2	23
1.3.10	Kuboresha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika somo la hisabati	20	25
1.3.11	Kuboresha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika masomo ya sayansi	56.2	60.2
1.4	**Elimuya Sekondari za Juu**		
1.4.1	Kiwango cha udahili wa jumla, (% ya wanaostahili)	6.9	10
1.4.2	Kiwango cha udahili halisi, (% ya wanaostahili)	3.3	8
1.4.3	ambapo wa kiume ni	3.3	4
1.4.4	ambapo wa kike ni	3.2	4
1.4.5	Kiwango cha ufaulu mtihani wa kidato cha VI	99.51	100
1.5	**Elimu ya Juu**		
1.5.1	Udahili katika elimu ya juu	8.2	10
1.5.2	% wa kiume	4.5	6
1.5.3	% wa kike	3.7	4
1.5.4	% ya wahitimu wa sayansi na hisabati kati ya wahitimu wote wa vyuo vikuu graduates	26	30
1.5.5	Idadi ya wanafunzi waliopata mikopo ya elimu ya juu	132,392	180,000

1.5.6	Uwiano wa mikopo inayotolewa kwa masomo ya sayansi (Loan/Grant to science subjects)	63.9	70
1.5.7	Idadi ya wahitimu wa vyuo vikuu	60,940	70,081
1.5.7.1	wa kiume	34,513	39,690
1.5.7.2	wa kike	26,427	44,700
1.6	**Elimu ya Juu ikijumuisha Vyuo vya Ufundi**		
1.6.1	Udahili katika elimu ya juu (%)	4.5	6.0
1.6.2	Idadi ya wanafunzi wanaohitimu kwa mwaka	55,501	120,000
1.6.3	Wanafunzi wa sayansi na uhandisi (%)	36	40
1.6.4	Wanafunzi wa kike (%)	42	43
1.6.5	% ya wanafunzi wa elimu ya juu wanaopata mikopo	60	90

Maendeleo ya Ujuzi

Maendeleo ya ujuzi ni dhana ya kukuza na kuendeleza ujuzi kwa lengo la kuandaa nguvukazi kutekeleza shughuli za kiuchumi na kutoa huduma kwa ufanisi. Dhana hii inafungamanisha mafunzo ya nadharia na vitendo. Kwa muktadha huo, Mpango utajielekeza katika kuimarisha mifumo ya usimamizi wa taasisi za maendeleo ya ujuzi. Aidha, mambo mengine yatakayozingatiwa ni pamoja na: kuwezesha upatikanaji wa vifaa, karakana, wakufunzi wenye sifa stahiki na kuchochea uwekezaji katika maendeleo ya ujuzi.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kuhuisha na kufungamanisha mitaala ya nadharia na vitendo;
(ii) Kuimarisha, kuanzisha na kuendeleza programu za mafunzo kwa vitendo, mahali pa kazi, kabla ya ithibati na mafunzo ya kujiendeleza;
(iii) Kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika mafunzo kwa njia ya vitendo;
(iv) Kuhamasisha ubunifu na uhawilishaji wa ujuzi na teknolojia;
(v) Kuwezesha na kuendeleza ujuzi kwa makundi yenye mahitaji maalumu; na
(vi) Kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kukuza Ujuzi (2021/22-2025/26).

Jedwali Na 28 Viashiria na Malengo ya Maendeleo ya Ujuzi.

Na.	Viashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1.0	Technical Education		
1.1	Idadi ya wastani ya wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya ufundi	160,000	700,000
1.2	(%) ya wanawake/wasichana	48.8	50
1.3	(%) ya wenye ulemavu	0.09	0.1
1.4	Udahili wa jumla katika elimu ya ufundi (%)	5.8	6.9
1.5	Idadi ya wanafunzi wanaohitimu elimu ya ufundi	135,200	680,000
1.6	% ya wanafunzi wa sayansi na uhandisi	24.2	40
1.7	% ya wanawake/wasichana	44.8	50

1.8	% ya wanafunzi wa elimu ya ufundi wanaopata mikopo ya wanafunzi	20	35
1.9	Idadi ya wakufunzi	10,072	15,000
1.10	% ya wakufunzi wa kike	26.6	50
1.11	Idadi ya taarifa za utafiti katika soko la ajira zilizotolewa	17	25
1.12	Idadi ta taarifa za tafiti za ufuatiliaji wahitimu wa Mpango wa TVET (Training and Vocational Education and Training)	0	4
1.13	Idadi ya Vituo Atamizi vilivyoanzishwa	2	30
1.14	% ya shughuli za TVET zinazojiendesha zenyewe	20	60
1.15	Idadi ya taasisi za TVET zinazofuatiliwa kuhakiki ubora	407	800
1.16	Idadi ya taasisi za TVET mpya zilizosajiriwa	486	545
1.17	Uwiiano wa wahandisi-mafundi-wasaidizi	N/A	1:5:25
1.18	Idadi ya wahitimu	86,547	99,529
1.18.1	wa kiume	43,384	49,892
1.18.2	wa kike	43,163	49,637
	Vocational Training		
	Idadi ya wastani ya udahili katika Vyuo vya Ufundi na Mafunzo	320,143	1,000,000
	% ya wanawake/wasichana	37	45
	% ya wenye ulemavu	0.03	0.05
	Idadi ya wakufunzi	10,112	12,321
	% ya wakufunzi wa kike	36	47
	Idadi ya taarifa za tathmini ya soko la ajira zilizotolewa	9	15
	Idadi ya Vituo Atamizi vilivyoanzishwa	5	30
	Idadi ya wahitimu	118,270	207,518
	Kati yao, wanaume	72,861	128,195
	Kati yao, wanawake	45,409	79,323
	Other Training		
3.1	Watu wenye ujuzi uliopatikana kutoka mfumo usio rasmi, kwa sekta sita za kipaumbele (kwa mwaka)	20,886	100,000
3.2	Mafunzo kazini kabla ya ithbati kwa wahitimu wa vyuo vikuu (kwa mwaka)	745	5,000
	Viwango vya Ujuzi		
	Wafanyakazi wenye viwango vya juu vya ujuzi (%)	3.3	12.1
	Wafanyakazi wenye viwango vya kati vya ujuzi (%)	33.7	54.0
	Ujuzi Unaoajirika		
	Idadi ya walio katika mafunzo ya kazi kabla ya ithbati	30,000	150,000
	Idadi ya walio katika mafunzo mahali pa kazi	46,200	231,000
	Idadi ya watu wenye teknolojia ya kisasa ya kilimo (Modern Agricultural Farming Technology)	40,000	200,000
	Idadi ya watu wenye ujuzi unaotambulika uliopatikana awali (Recognized Prior Learning Skills Development)	20,000	100,000

*Nje ya shule/nguvukazi ya chuo

5.4.20 Afya

Sekta ya afya ni muhimu kwa maendeleo ya watu. Sekta hii inajumuisha miundombinu, wataalamu, vifaa na vifaa tiba, vitendanishi, dawa, tiba, kinga na bima ya afya. Hivyo, Mpango huu unalenga kuimarisha mifumo ya usimamizi, upatikanaji na utoaji wa huduma za afya. Aidha, Mpango utajielekeza pia katika kutatua changamoto ya ubora wa huduma za afya.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kujenga na kukarabati vituo vya huduma za afya;
(ii) Kuimarisha upatikanaji wa wataalamu wa afya, dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo;
(iii) Kutanua wigo wa upatikanaji wa huduma za bima ya afya;
(iv) Kuimarisha huduma za kibingwa katika hospitali za rufaa za kikanda, maalumu na kitaifa;
(v) Kuboresha huduma za tiba asilia/tiba mbadala;
(vi) Kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji katika viwanda vya kuzalisha chanjo, dawa na vifaa tiba;
(vii) Kuhamasisha na kuwezesha sekta binafsi kuwekeza katika mnyororo wa usambazaji wa bidhaa na huduma za afya;
(viii) Kuimarisha mifumo ya kusafirisha na kuhifadhi bidhaa za afya;
(ix) Kuimarisha mifumo ya kukabiliana na magonjwa ya mlipuko; na
(x) Kuimarisha huduma za dharura za afya.

Jedwali Na. 29Viashiria na Shabaha Katika Sekta ya Afya

		Shabaha	
Na.	**Kiashiria**	**2020/21**	**2025/26**
1.1	Idadi ya vifo vya watoto, kwa kila vizazi hai 1000	36	30
1.2	Idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano, kwa kila vizazi hai 1000	50	40
1.3	Uzazi uliohudumiwa na wakunga waliohitimu (asilimia)	80	85
1.4	Idadi ya vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua kwa kila akina mama 100,000	220	180
1.5	Umri wa kuishi (miaka)	66	68
1.6	Kuenea kwa UKIMWI kitaifa (asilimia)	4.7	3.1
1.7	Matumizi ya Serikali katika afya (% ya matumizi yote ya Serikali)	10	12.2

5.4.21 Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira

Huduma ya maji na usafi wa mazingira ni miongoni mwa mahitaji muhimu yanayochochea maendeleo ya watu. Sekta hii inahusisha upatikanaji na usambazaji wa maji pamoja na utunzaji wa vyanzo vya maji na mazingira. Mpango huu utatoa

kipaumbele katika upatinaji na usamazaji wa maji safi na salama vijijini na mijini, na utunzaji wa vyanzo vya maji na mazingira.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kuimarisha miundombinu ya upatikanaji na usambazaji wa maji safi na salama nchini;

(ii) Kuimarisha na kuwezesha uanzishwaji wa Jumuiya za Watoa Huduma za Maji katika Jamii;

(iii) Kuhimiza uwekezaji na matumizi ya teknolojia endelevu katika kutibu na kuchakata maji-taka;

(iv) Kujenga mabwawa ya kimkakati ya kuhifadhi maji;

(v) Kuhamasisha na kuwezesha usimamizi, uendelezaji na matumizi endelevu ya vyanzo vya maji mipakani;

(vi) Kuimarisha programu za uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji;

(vii) Kuimarisha mifumo ya tafiti, ukusanyaji, utunzaji, uchakataji na usambazaji wa takwimu za maji; na

(viii) Kuimarisha programu za ufuatiliaji na tathmini ya maji na ubora wa majitaka.

Jedwali Na. 30 Viashiria vya Usambazaji wa Maji na Huduma za Usafi wa Mazingira

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1.1	Asilimia ya idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba au maji yalivyolindwa kama chanzo kikuu	70	85
1.2	Uwiano wa kaya za vijijini zenye miundombinu iliyoboreshwa ya usafi wa mazingira	36	75
1.3	Asilimia ya watu katika makao makuu ya mikoa wanaopata maji ya bomba au maji yaliyolindwa	84	95
1.4	Asilimia ya kaya katika makao makuu ya mikoa iliyounganishwa kwenye mfumo rasmi wa maji-taka	13	30
1.5	Asilimia ya upotevu wa maji (NRW) katika makao makuu ya mikoa	30	20
1.6	Asilimia ya watu katika makao makuu ya wilaya na miji midogo wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji yaliyolindwa kama chanzo kikuu	70	85
1.7	Asilimia ya watu katika jiji la Dar es Salaam wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji salama kama chanzo chao kikuu	85	95
1.8	Asilimia ya kaya katika jiji la Dar es Salaam waliounganishwa kwenye mfumo rasmi wa maji-taka	13	30
1.9	Kiwango cha upotevu wa maji (NRW) katika jiji la Dar es Salaam	35	20
1.10	Idadi ya vyanzo vya maji vilivyotengwa na kutangazwa kwa ajili ya ulinzi na uhifadhi	18	200

5.4.22 Mipango Miji, Maendeleo ya Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mwelekeo wa kimkakati wa Mpango huu ni kuendeleza upimaji wa maeneo ya makazi, biashara, uwekezaji na huduma za jamii. Shughuli hizo huendana na Mipango Kabambe ya Miji, Sera na Sheria. Mipango Miji, Maendeleo ya Nyumba na Maendeleo ya Makazi yanahusisha makazi bora, miundombinu wezeshi na upatikanaji wa huduma muhimu za jamii kulingana na mahitaji ya wananchi katika eneo husika.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kuhamasisha uwekezaji katika upangaji, upimaji na utoaji wa hati miliki za ardhi nchini;

(ii) Kuimarisha mifumo ya uandaaji wa mipango kabambe ya matumizi ya ardhi, kuendeleza miji, maeneo tengefu, visiwa na ukanda wa pwani;

(iii) Kuimarisha uwekezaji katika ujenzi wa nyumba za gharama nafuu;

(iv) Kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Ardhi;

(v) Kuwianisha mifumo ya usimamizi wa ardhi na Mpango kisekta katika matumizi ya ardhi; na

(vi) Kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika upimaji wa ardhi.

Jedwali Na. 31 Viashiria na Shabaha ya Uendelezaji Miji, Nyumba na Makazi Endelevu ya Watu

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1.1	% ya ardhi iliyopimwa	25	37
1.2	Idadi ya miliki zilizorasimishwa katika makazi yasiyorasmi	1,496,357	2,496,357
1.3	Idadi ya liseni za makazi zilizotolewa katika makazi yasiyorasmi	1,738	20,000
1.4	% ya ardhi yenye makazi yasiyo rasmi	70	25
1.5	Eneo la ardhi (eka) lililotengwa na kulindwa kwa matumizi ya umma	858,665	1,452,415
1.6	Idadi ya mabaraza ya ardhi yanayofanya kazi (district land housing tribunals)	57	139
1.7	Uwiano wa vijiji yenye mipango ya matumizi bora ya ardhi	19.3	52.7
1.8	Urefu (km) wa Ukanda Maalum wa Kichumi katika Bahari ya India	0	370
1.9	Idadi ya ramani za msingi zilizohuishwa kwa eneo (updated base maps)	1	26
1.10	Idadi ya viwanja vilivyotolewa	1,551,716	4,051,716
1.11	Idadi ya mashamba yaliyotolewa		
1.12	Idadi ya miji yenye mipango kabambe ya upimaji iliyohuishwa	24	54

5.4.23 Chakula na Lishe

Lishe bora ni muhimu katika kujenga mwili, akili na fikra ya mwanadamu. Ubora wa lishe unahusisha mlo unaojumuisha makundi yote ya chakula ambayo ni: protini; wanga; mafuta; matunda na vitamini; pamoja na maji. Aidha, upatikanaji wa chakula na lishe ni msingi wa afya bora na maendeleo ya watu. Kwa msingi huo, Mpango huu utahimiza jamii kuwekeza katika uzalishaji wa chakula na lishe bora ili kupunguza baadhi ya matatizo ya kiafya.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kuimarisha usimamizi wa huduma za kupambana na utapiamlo;
(ii) Kuimarisha programu za mtindo wa maisha na lishe bora;
(iii) Kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji na utumiaji wa virutubisho na viini lishe katika chakula;
(iv) Kuhamasisha ulaji wa vyakula vya asilia; na
(v) Kuendelea kuwajengea uwezo watoa huduma za lishe.

Jedwali Na. 32 Viashiria na Shabaha ya Usalama wa Chakula na Lishe

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1.1	Kuenea kwa udumavu kwa watoto wenye umri kati ya miezi 0 – 59	31.8	24
1.2	Kuenea kwa upungufu wa uzito (uwiano kati ya uzito na urefu) kwa watoto wenye umri kati ya miezi 0-59	3.5	< 5
1.3	Kuenea kwa uzito mdogo wakati wa kuzaliwa (LBW)	6.3	< 3
1.4	Uwiano wa wanawake wenye umri kati ya miaka 15-49, wenye upungufu wa damu (anaemic)	44	22
1.5	Kuenea kwa utapiamlo uliokithiri ulimwenguni kwa wattoto wenye umri kati ya miezi 0-59	3.5	< 5
1.6	Wastani wa wanawake wenye umri kati ya miaka 15-49 wenye madini-joto kwenye mkojo, 100-299 µg/L;	100- 299 µg/L	100- 299 µg/L
1.7	Kuenea kwa uzito uliokithiri kwa watoto wenye umri wa kati ya miezi 0-59	2.8	< 5
1.8	Uzito uliokithiri kwa watu wazima wenye umri wa kati ya miaka 15-49	30	< 29
1.9	Uwiano wa kaya zinazopata chumvi yenye madini-joto ya kutosha	62	80
1.20	Kiwango cha kunyonyesha kipekee (Rate of Exclusive Breast Feeding - EBF)	59	65
1.21	Kuenea kwa upungufa wa vitamin A kwa watoto wenye umri kati ya miezi 5-59 (serum retinol level < 20 µg/dl)	-	< 20

5.4.24 Hifadhi ya Jamii

Dhana ya hifadhi ya jamii inajumuisha uwezeshaji wananchi kiuchumi, ushirikishwaji wananchi katika shughuli za uzalishaji mali na kuboresha mazingira ya watu wenye mahitaji maalumu ili kupunguza umaskini wa kipato na utegemezi. Aidha, hatua za kuwawezesha wananchi kiuchumi zinalenga kuwajengea uwezo wa kupambana na mazingira na kujitegemea.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kuimarisha huduma mbadala za matunzo, malezi na uasilishaji watoto;
(ii) Kuimarisha huduma za maendeleo na ulinzi wa mtoto;
(iii) Kuimarisha huduma kwa watu yenye mahitaji maalumu;
(iv) Kuimarisha Mabaraza ya Wazee;
(v) Kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma za hifadhi ya jamii;
(vi) Kuhamasisha ushirikishwaji wa watu wenye mahitaji maalumu kwenye shughuli za kiuchumi;
(vii) Kuhamasisha tabia ya kuweka akiba na kuwekeza katika shughuli za uzalishaji; na
(viii) Kuimarisha usimamizi wa mifuko ya uwekezaji wa wananchi kiuchumi.

Jedwali Na. 33 Viashiria na Shabaha kwa Hifadhi ya Jamii

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1.1	Ongezeko la eneo la hifadhi ya jamii (%)	20	30
1.2	Kuenea kwa Mpango wa Bima ya Afya (%)	50	80
1.3	Kuenea kwa Hifadhi ya Jamii (%)	7.3	13.1
1.4	Ajira za vijana walio katika mazingira magumu (%)	56.3	38.3
1.5	Kiwango cha watoto wenye ulemavu wanaosoma elimu ya msingi (%)	80	100
1.6	Watoto wenye umri kati ya miaka 5-17 walio katika ajira za watoto (%)	24.9	21
1.7	Idadi ya watoto wanaolelewa baada ya mapatano	12,068	50,000
1.8	Idadi ya vijana waliopata mafunzo ya afya na ustawi	0	2,000,000
1.9	Idadi ya vituo vya malezi ya watoto mchana vilivyosajiriwa	1,543	7,500
1.10	Idadi ya wazee wasiojiweza wenye kadi za bima ya afya zinazowawezesha kutibiwa bila ya malipo	166,866	500,000
2	**Ushirikishwaji wenye Tija**		
2.1	Kaya zilizonufaika ambazo zinashiriki katika vikundi vya amana (%)	40	50
2.2	Idadi ya wanufaika wanaopata taarifa za huduma za kuinua maisha	628,037	1,119,676
2.3	Idadi ya kaya zinazostahili kunufaika na misaada ya kuinua maisha, pamoja na msaada wa mafunzo ya msingi na ujuzi	75,000	200,000

2.4	Shughuli za Kuzalisha Kipato (IGAs) zenye mipango-kazi iliyoandaliwa ndani ya miezi sita ya kupata msaada wa kuinua maisha (%)	70	90
2.5	Kaya zenye watu waliopata mafunzo, zilizonufaika na misaada ambazo ujuzi umeboreshwa kufuatia mafunzo yaliyotolewa na Programu ya PSSN (%)	60	70
3.	**Kazi za Umma**		
3.1	Idadi ya kaya zilizonufaika, ambazo zinapata misaada kupitia kazi za umma	255,756	1,250,000
3.2	Miradi midogo ya PWP/jumla ya rasilimali za jamii zilizotokana na Programu ya PSSN (idadi)	16,000	27,000
3.3	Miradi midogo ya PW yenye mipango ya matengenezo na hatua endelevu *(%)*	60	70
4	**Uhawilishaji Fedha**		
4.1	Idadi ya kaya zilizonufaika zinazopata misaada ya pesa taslimu (yenye masharti na isiyo na masharti)	1,167,243	1,219,347
4.2	Uwiano wa watoto katika kaya zilizonufaika wenye umri kati ya miezi 0-24 wanaopata huduma za afya mara kwa mara (%)	94	95
4.3	Uwiano wa watoto katika kaya zilizonufaika wenye umri kati ya miaka 0-18 waliodahiliwa shule za msingi, wenye mahudhurio ya zaidi ya asilimia 80 (%)	94	95
4.4	Uwiano wa watoto katika kaya zilizonufaika wanaostahili kuwa shule za sekondari (%)	7	8
4.5	Uwiano wa kaya zilizopata misaada ya wenye ulemavu *(%)*	4	6

5.4.25 Mahusiano na Nchi za Nje

Serikali inatekeleza Sera ya Nje kulingana na mahitaji na vipaumbele vya nchi ili kudumisha amani, utulivu, ustawi wa jamii na diplomasia ya kiuchumi na kisiasa. Mashirikiano ya kikanda na kimataifa ni fursa ya kutatua migogoro ya kiuchumi, kisiasa na kuvutia uwekezaji. Hivyo, katika utekelezaji wa Mpango huu, Tanzania itaendelea kuimarisha Sera ya Nje kwa kuzingatia mikataba ya kikanda na kimataifa iliyoridhia.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kuandaa na kutekelezea Mpango Mkakati wa diplomasia ya kisiasa na kiuchumi;

(ii) Kutanua na kuimarisha ushirikiano na ushiriki wa Tanzania katika shughuli za kikanda na kimataifa;

(iii) Kujenga na boresha miundombinu ya ofisi za ubalozi za Tanzania nje ya nchi.

Jedwali Na. 34 Viashiria na Shabaha Katika Mahusiano na Nchi za Nje na Uchumi wa Kidiplomasia

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1	**Utekelezaji wa kimkakati wa diplomasia ya kisiasa**		
1.1	Idadi ya mikutano kati ya Tanzania na nchi moja moja, ya kikanda na kimataifa iliyoshiriki	50	250
1.2	Idadi ya wa Tanzania walioshiriki katika ulinzi wa amani nchi za nje	2,303	3,500
1.3	Idadi ya ofisi mpya za ubalozi zilizofunguliwa	1	10
1.4	Idadi ya ofisi ndogo mpya za ubalozi zilizofunguliwa	1	6
1.5	Idadi ya mikutano ya Tume za Kudumu za Pamoja (Joint Permanent Commissions) iliyofanyika	5	30
1.6	Idadi ya Hati za Makubaliano ya Pamoja (MoUs) zilizosainiwa kati ya Tanzania na nchi nyingine	15	80
1.7	Idadi ya Mikutano ya Pamoja na nchi jirani iliyofanyika	5	40
1.8	Idadi ya majukwaa ya Kikanda na Kimataifa yanayotumia lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi	5	6
1.9	Idadi ya taasisi zinazofundisha Kiswahili maeneo ya Kikanda na Kimataifa	5	10
2.	**Utekelezaji wa kimkakati wa diplomasia ya kiuchumi**		
2.1	Idadi ya wa Tanzania walioshiriki katika maonesho na majukwaa ya biashara (trade forums)	240	1,200
2.2	Idadi ya maonesho na majukwaa ya biashara ambayo Tanzania ilishiriki	20	100
2.3	Idadi ya wawekezaji wa nje	86	430
2.4	Idadi ya watalii wa nje	1,600,000	8,000,000
2.5	Idadi ya wa Tanzania waliosomeshwa nje kwa udhamini wa nchi za nje	7,600	10,000
3	**Kupanua nafasi ya Tanzani katika uwanda wa kimataifa**		
3.1	Idadi ya ofisi na nyumba za kuishi zilizokarabatiwa	3	11
3.2	Idadi ya viwanja vilivyoendelezwa ambavyo vinavyomilikiwa na serikali nchi za nje katika maeneo muhimu ya kibiashara	1	11

5.4.26 Uongozi Bora na Utawala wa Sheria

Uongozi bora ni msingi wa mwelekeo wa maendeleo ya Taifa. Aidha, utawala wa sheria unahusisha uzingatiaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo katika kufanya maamuzi. Hivyo, uongozi bora na utawala wa sheria ni sehemu ya nguzo kuu za Mpango katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa 2025.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kuhamasisha ufanisi katika mifumo ya utoaji haki;
(ii) Kuimarisha misingi ya kidemokrasia;

(iii) Kudumisha amani, usalama na utulivu wa kisiasa;
(iv) Kuimarisha usimamizi wa shughuli za kiuchumi; na
(v) Kuimarisha ushirikishwaji wa jamii katika shughuli za maendeleo.

5.7.1 Ujenzi wa Mji Mkuu Mpya wa Serikali – Dodoma

Miongoni mwa sababu za Serikali kuhamishia shughuli zake Dodoma ni kusogeza huduma karibu na wananchi. Mpango wa kuhamia Dodoma ulihusisha ujenzi na uimarishaji wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji, elimu, afya, maji na ofisi za Serikali ilikukidhi mahitaji ya ongezeko la watu.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Ujenzi wa majengo ya ofisi za Serikali;
(ii) Kuimarisha miundombinu ya michezo, burudani na sanaa;
(iii) Kujenga na kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji;
(iv) Kuendelea na jitihada za kuhifadhi mazingira na kuifanya Dodoma kuwa jiji la kijani;
(v) Kuboresha miundombinu ya elimu, ufundi na ufundistadi; na
(vi) Kuendelea kuimarisha miundombinu ya afya.

5.7.2 Mifumo ya Utoaji Haki

Mifumo ya utoaji na upatikanaji wa haki ni muhimu katika kuimarisha usawa na ustawi wa jamii. Utoaji na upatikanaji wa haki unawezekana ikiwa kuna mifumo imara ya kitaasisi. Mifumo hiyo inajumuisha watumishi wenye weledi, vitendea kazi, miundombinu wezeshi na miongozo rafiki katika utoaji haki. Kwa msingi huo, mifumo ya utoaji haki ni moja ya nguzo za utawala bora.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kuboresha mifumo na miundombinu ya mahakama;
(ii) Kuhamasisha ya TEHAMA katika utoaji na upatikanaji haki;
(iii) Kuimarisha mifumo ya utunzaji wa taarifa na kumbukumbu za mahakama;
(iv) Kuimarisha taratibu na miongozo ya utoaji wa msaada wa kisheria nchini; na
(v) Kuimarisha za huduma za usajili wa uzazi na vifo.

Jedwali Na. 35 Viashiria na Shabaha za Mfumo Fanisi wa Utoaji Haki.

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1	**Huduma ya Utoaji Haki**		
1.1	**Upatikanaji wa Huduma za Utoaji Haki**		
1.1.1	Asilimia ya raia wanaoishi katika mikoa yenye Mahakama Kuu inayofanya kazi	69	100
1.1.2	Asilimia ya kesi zilizohudumiwa na watoa msaada wa huduma za kisheria	0.13	2.0
1.1.3	Idadi ya IJCs zilizojengwa na zinafanya kazi katika maeneo yaliyochaguliwa.	10	28
1.1.4	Idadi ya majengo ya mahakama ya wilaya yaliyojengwa	64	139
1.1.5	Idadi ya majengo ya mahakama ya mwanzo yaliyojengwa	649	791
1.1.6	Idadi ya ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali zilizojengwa mikoani	0	10
1.1.7	Idadi ya ofisi za NPS zilizojengwa mikoani	1	7
1.1.8	Idadi ya ofisi za NPS zilizojengwa wilayani	1	11
1.1.9	Idadi ya ofisi za Wakili Mkuu wa Serikali zilizojengwa mikoani	0	5
1.1.10	Idadi ya wilaya zenye watoa msaada wa huduma za kisheria waliosajiliwa	52	138
1.1.11	Idadi ya taasisi zilizounganishwa na mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za utoaji haki	2	8
1.1.12	% usajili wa uzazi wa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano na kupewa cheti cha kuzaliwa	55	100
1.1.13	Kupitia na kutekeleza mfumo wa ufilisi	0	1
1.2	**Ufanisi wa Huduma ya Utoaji Haki**		
1.2.1	Idadi ya wastani ya siku, tangu kufunguliwa kwa kesi na kutolewa hukumu	390	350
1.2.2	Asilimia ya kuridhishwa na huduma za mahakama	78	80
1.2.3	Idadi ya wastani ya siku, tangu kufunguliwa kwa kesi na kutolewa hukumu katika Mahakama ya Biashara	480	350
1.2.4	Asilimia ya mlundikano wa kesi, kwa jumla ya kesi zote zinazosubiri kushughulikiwa	5	2
1.2.5	Idadi ya Sheria na Taratibu zilizofanyiwa mapitio	410	1,410
1.2.6	Idadi ya Sheria na Taratibu zilizotafsiriwa kwa kiswahili	50	250
1.2.7	Muda wa wastani wa kujibu malamiko juu ya ukiukaji wa haki za binadamu kitaifa na kimataifa	Mwaka 1	Miezi 6
1.2.8	Muda wa wastani katika uidhinishaji wa mikataba ya uwekezaji	21	14
1.3	**Uwazi katika utoaji haki**		
1.3.1	Idadi ya mikataba ya maliasili na rasilimali iliyoidhinishwa na Bunge kwa utekeleaji	0	10
1.3.2	% ya maamuzi ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa iliyochapishwa kwenye mtandao wa TEHAMA	5	25

5.7.3 Amani, Utulivu na Usalama

Maendeleo na ustawi wa Taifa unategemea amani, utulivu na usalama. Adhima ya amani, ututlivu na usalama itafikiwa kwa kuwa na mifumo imara na thabiti ya vyombo vya ulinzi na usalama. Hivyo, mafanikio ya utekelezaji wa Mpango huu yanategemea uimara wa taasisi za ulinzi na usalama.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kuendelea kudumisha usalama, utulivu na amani;
(ii) Kuimarisha usimamizi wa taratibu za utambuzi na usajili wa raia;
(iii) Kuimarisha mifumo ya ushirikiano; na
(iv) Kufungamanisha mifumo ya utunzaji taarifa.

Jedwali Na. 36 Viashiria na Shabaha Katika Uimarishaji wa Usalama wa Umma, Sheria na Taratibu

Na.	Kiashiria	Shabaha	
		2020/21	2025/26
1.1	(%) ya maboresho katika mifumo ya ulinzi wa jamii	60	95
1.2	Kiwango cha matukio ya hatari yaliyotambuliwa na kuripotiwa na jamii (%)	75	98
1.3	Kiwango cha ushiriki wa vikosi vya ulinzi na usalama katika shughuli za uchumi (%)	5	10
1.4	Kiwango cha kupungua kwa uhalifu nchini (%)	5.20	35
1.5	Kiwango cha kupungua kwa ajali za barabarani (%)	30.50	35
1.6	Kiwango cha ongezeko la ufanisi katika upelelezi wa kesi za jinai (%)	45.10	50
1.7	Idadi ya askari waliohitimu	15,234	77,891
1.8	Kiwango cha upatikanaji wa zana na vifaa vya kufanyia kazi	1,776	10,140
1.9	Idadi ya askari waliopatiwa makazi bora	11,824	20,688
2.0	Kiwango cha ushirikiano na nchi nyingine katika masuala ya usalama (%)	52	70
2.1	Kiwango cha kupungua kwa matishio ya usalama na uhalifu wa mipakani (%)	8.70%	35%
2.2	Idadi ya wahalifu/wafungwa waliopata mafunzo ya uzalishaji na shughuli za kujiajiri	12,000	50,000
2.3	Kiwango cha thamani ya uzalishaji katika magereza na vyuo vya mafunzo (Tshs milioni)	2,343.57	34,000.00
2.4	Idadi ya matukio ya uokozi yaliyofanyika nchini	2,768	3,600
2.5	Idadi ya simu za matukio ya moto zilizopokelewa	8,511	9,000
2.6	Ongezeko la idadi ya wanufaika wa huduma mbalimbali za uhamiaji	968,624	17,204,620
2.7	Idadi ya wakimbizi waliotambuliwa na kusajiliwa	207,644	150,000
2.8	Idadi ya watu wenye ujuzi waliosajiliwa na kupewa vitambulisho	22,194,288	34,080,610
2.9	Idadi ya taasisi za umma na binafsi zilizounganishwa na mfumo wa NIDA	40	200

5.8 Uchumi wa Rasilimali za Majini

Uchumi wa rasilimali za majini unahamasisha shughuli zinazofanyika katika bahari, mito na maziwa. Shughuli mahususi zinazotekelezwa katika rasilimali za majini ni uvuvi, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi, utalii, ufugaji wa samaki, kilimo, usafiri na usafirishaji, uvunaji wa madini ya chumvi na nishati jadidifu. Aidha, mifumo imara ya ulinzi na usalama ni muhimu katika kuvutia uwekezaji wa rasilimali za majini. Hivyo, katika utekelezaji wa Mpango huu, Serikali itaweka mazingira wezeshi ya uwekezaji ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kwa lengo la kuongeza mchango wa sekta hii kwenye uchumi.

Hatua muhimu zinahusisha:

(i) Kuendelea kuwezesha tafiti ili kubaini fursa za rasilimali za majini;

(ii) Kuhamasisha uwekezaji na matumizi ya sayansi na teknolojia katika shughuli za kiuchumi za rasilimali za majini;

(iii) Kuimarisha na kufungamanisha miundombinu ya utafiti, uwekezaji, uzalishaji utunzaji, utalii na usafirishaji wa bidhaa na huduma za majini;

(iv) Kuhamasisha ushirikishwaji wa wananchi katika fursa za kiuchumi zinazotokana na rasilimali za majini;

(v) Kuimarisha mifumo ya ulinzi na usalama wa shughuli na huduma za majini; na

(vi) Kuimarisha ushirikiano na taasisi za kikanda na kimataifa katika usimamzi wa rasilimali za majini.

Uchumi wa Rasilimali za Majini

Uchumi wa rasilimali za majini unajumuisha shughuli za uvuvi, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi, utalii wa fukwe, ufugaji wa samaki, kilimo, usafiri na usafirishaji, uvunaji wa madini ya chumvi na nishati jadidifu. Shughuli hizi ni fursa kwa uwekezaji na uwezeshaji wananchi kiuchumi. Pamoja na fursa zilizopo tathmini inaonesha kuwa uvuvi na kilimo cha baharini vinachangia asilimia 2.2 kwenye Pato la Taifa, asilimia 3.0 kwenye mapato ya fedha za kigeni na inatoa ajira za kudumu zaidi ya 200,000 na ajira zisizo za kudumu zipatazo milioni 4.2. Aidha, kukosekana kwa takwimu za shughuli nyingine za uchumi wa rasilimali za majini ni ishara kuwa kuna uwekezaji mdogo ikilinganishwa na fursa zilizopo.

Tanzania ina eneo lenye kilometa za mraba 62,000 za maji baridi, zikijumuisha maziwa makuu manne ambayo ni Ziwa Victoria, Nyasa, Tanganyika na Rukwa. Aidha, eneo la maji ya bahari linajumla ya kilometa za mraba 64,500. Katika maeneo fursa za uwekezaji zinazopatikana ni za uvuvi wa samaki, ufugaji wa samaki, madini ya chumvi, utafutaji wa gesi na mafuta, kilimo cha mwani, utalii wa fukwe, usafiri na usafirshaji.

Aidha, Serikali imeimarisha sekta hizi kwa kuweka mifumo ya kitaasisi, sera, sheria, taratibu na miongozo. Ijapokuwa juhudi za Serikali zimefanyika kwa kuboresha miundombinu hususan bandari na meli kwenye maziwa makuu bado mchango wa sekta hii ni mdogo kwenye Pato la Taifa na ajira. Kwa msingi huo, Mpango unahamasisha uwekezaji katika uchumi wa rasilimali za majini.

5.9 Miradi ya Kielelezo Katika Mpango

Miradi ya kielelezo ni miradi yenye matokeo mahususi na ya haraka kwenye maeneo mengi ya kiuchumi na kijamii. Kutokana na umuhimu wa miradi ya kielelezo katika uchumi, utekelezaji utahusisha sekta binafsi na Serikali. Hivyo, utekelezaji wa miradi hiyo unatarajiwa kuchochea shughuli za kiuchumi, kuongeza uzalishaji wa bidhaa, ushindani kikanda na kimataifa, mauzo nje, ajira na kuboresha ustawi wa jamii. Miradi ya kielelezo ni kama ilivyoainishwa kwenye Boksi Na. 9

Boksi Na. 9 Miradi ya Kielelezo kwenye Mpango

1.	**Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Standard Gauge (SGR):** Utekelezaji wa mradi unahusisha ukamilishaji wa vipande vya Dar es Salaam – Morogoro (km 300) na Morogoro – Makotopora (km 422). Aidha, mradi huu, utahusisha ujenzi wa vipande vingine ambavyo ni Makutupora – Tabora (km 294); Tabora –Isaka (km 133); Isaka – Mwanza (km 249); (Isaka – Rusumo km 371); Tabora – Kigoma (km 411); Kaliua – Mpanda – Karema (km 321); na Keza – Ruvubu (km 36). Kukamilika kwa ujenzi wa reli hii utaiwezesha Tanzania kuunganisha mtandao wa usafirishaji na nchi jirani.
2.	**Ujenzi wa Reli ya Kusini:** Mradi huu unahusisha ujenzi wa reli kwa kiwango cha *standard gauge* kwa kipande cha Mtwara – Mbambabay na matawi ya Liganga na Mchuchuma. Aidha, reli hii itaunganishwa na reli ya TAZARA.
3.	**Ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji Julius Nyerere (JNHPP) – 2,115 MW:** Shughuli zinazotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa bwawa, miundombinu ya usafirishaji wa umeme na vituo vya kupozea umeme. Uwekezaji katika mradi huu utaongeza kiwango cha nishati ya umeme kwenye gridi ya Taifa na kuchochea fursa za kiuchumi.
4.	**Kuendelea Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania –ATCL:** Serikali itaendelea kuimarisha uendeshaji wa Shirika la Ndege Tanzania na kununua ndege mpya nane (8), kutoa mafunzo kwa marubani na wahandisi na kuboresha miundombinu ya karakana. Uboreshaji wa huduma za Shirika la Ndege unatarajiwa kuchochea uwekezaji katika sekta ya utalii na usafirishaji.
5.	**Ujenzi wa Bomba la Mafuta -East African Crude Oil Pipeline (EACOP):** Mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba lenye urefu wa km 1,443 kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) ambapo kati ya urefu huo, km 1,115 za bomba hilo zitapita Tanzania na kusafirisha mafuta ghafi, mapipa 216,000 kwa siku. Vile vile, mradi utajumuisha ujenzi wa matenki ya kuhifadhi mafuta, vituo vya kupasha joto mafuta na nyenzo za kupakia mafuta ya kuuzwa nje.
6.	**Mradi wa Chuma wa Mchuchuma na Liganga:** Mradi huu ni pacha na unalenga Kuzalisha tani milioni tatu (3) za makaa ya mawe kwa mwaka, chuma (tani milioni 2.9) kwa mwaka, *Vanadium na Titanium* Pamoja na tani milioni 1.0 za chuma cha pua kwa mwaka. Makaa ya mawe kutoka Mchuchuma yatazalisha umeme wa

	kiasi cha MW 600; ambapo MW 300 zitatumika katika mradi wa Chuma - Liganga na MW 300 zitaingizwa katika gridi ya Taifa. Mradi unatarajiwa kuchangia katika agenda ya mageuzi ya viwanda hususan katika maeneo ya saruji, chuma cha pua na mbolea. Miradi hii inatarajiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa Ubia.
7.	**Mradi wa Kufua Umeme wa Ruhudji (Ruhudji Hydropower – 358 MW):** Serikali itatekeleza mradi wa Kufua umeme wa MW 358 mkoani Njombe na ujenzi wa njia ya usafirishaji wa umeme wa urefu wa km 170. Mradi huu utaimarisha upatikanaji na kupunguza gharama za umeme.
8.	**Mradi wa Kufua Umeme wa Rumakali –MW 222:** Mradi unahusisha ujenzi wa kituo cha Kufua umeme wa MW 222 katika mkoa wa Njombe na njia ya usafirishaji umeme yenye urefu wa km 150. Mradi utaimarisha upatikanaji na kupunguza gharama ya umeme na ziada kuuzwa nchi jirani za Zambia na Malawi.
9.	**Ujenzi wa mradi wa Gesi (LNG) – Lindi:** Serikali itatekeleza mradi huu kwa ushirikiano na kampuni za binafsi za mafuta na gesi. Mradi huu utajengwa nchi kavu katika Kijiji cha Likong'o mkoani Lindi. Mradi utakuwa na uwezo wa kuzalisha tani milioni 5 za gesi kwa mwaka. Aidha, mradi utachangia katika ukuaji wa uchumi, fursa za ajira na huduma za ugavi na kibiashara.
10.	**Mradi wa Magadi Soda wa Engaruka:** Mradi huu utatekelezwa katika Bonde la Engaruka wilayani Monduli. Utafutaji wa kijiolojia unaohusisha uchimbaji umegundua uwepo wa mita za ujazo bilioni 4.68 za magadi ambayo yameambatana na madini ya chumvi yanayofikia mita ujazo bilioni 9.36. Pamoja na kuwepo kwa magadi soda, vile vile kuna madini mengine yanayopatikana ikiwemo *Calcium Sulphate, Sodium Chloride and Potassium Chloride.* Utekelezaji wa mradi huu utawezesha ukuaji wa viwanda na uzalishaji wa fursa za ajira.
11.	**Ujenzi wa Kiwanda cha Sukari – Mkulazi:** Kiwanda kinatarajiwa kuzalisha tani 250,000 za sukari kwa mwaka na mradi unatarajiwa Kuzalisha fursa za ajira 100,000. Mradi huu unaendelea kutekelezwa kwa utaratibu wa *joint venture.*
12.	**Ujenzi wa Madaraja Makubwa na Madaraja ya Juu; Kigongo – Busisi, Tanzanite na KAMATA Flyover:** Mradi unalenga ujenzi wa madaraja ya kimkakati yakiwemo Kigongo -Busisi (Mwanza) km 3.2 na njia za kuingia na kutoka zenye urefu wa km 1.66 pamoja na barabara ya njia mbili kutoka Jiji la Mwanza hadi Busisi. Mradi huu utachochea shughuli za kiuchumi na kurahishisha usafiri na usafirishaji kwenda nchi jirani. Madaraja mengine yanayotarajiwa kujengwa ni pamoja na Tanzanite (Dar es Salaam), makutano ya barabara kuu za UHASIBU, Chang'ombe, Jangwani, KAMATA, Morocco, Mwenge, Magomeni, Tabata na Gerezani. Kukamilika kwa miradi hiyo itapunguza msongamano wa magari na hivyo kuwezesha shughuli za kiuchumi kufanyika kwa urahisi.
13.	**Ununuzi wa Meli na Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi:** Lengo la kutekelezwa kwa mradi huu ni kuwezesha uwekezaji katika rasilimali za majini hususan uvuvi na hivyo kuuza katika soko la ndani na la kimataifa. Aidha, kuongeza ufanisi katika sekta ya uvuvi Serikali inatarajia kujenga bandari ya Uvuvi Mbegani – Bagamoyo.
14.	**Mradi wa Utafutaji wa Mafuta na Gesi katika Kitalu cha Eyasi Wembere:** Mradi huu ni wa kimkakati wenye lengo la kutafuta mafuta na gesi asilia katika bonde la Eyasi Wembele. Mradi huu utatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi.
15.	**Mradi wa Utafutaji wa Mafuta na Gesi wa Mnazi Bay:** Mradi huu ni wa kimkakati wenye lengo la kutafuta mafuta na gesi asilia katika eneo la Mnazi bay. Mradi huu utatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi.

16.	**Kanda Maalumu za Uchumi na Maeneo Maalum ya Uwekekezaji:** Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu katika kanda maalumu za uchumi na maeneo maalumu ya uwekezaji. Vile vile, itaanzisha maeneo mengine mapya katika mikoa ya Singida (Manyoni), Pwani, Kigoma, Tanga, Manyara, Mara, na Ruvuma. Aidha, sekta binafsi itahamasishwa kuwekeza katika maeneo hayo.
17.	**Programu ya kuendeleza ujuzi adimu :** Programu hii itatekelezwa kwa kuongeza rasilimali fedha katika tafiti, ubunifu, uhaulishaji wa teknolojia na mafunzo kwa vitendo.

5.10 Miradi ya Kimkakati

Miradi ya kimkakati itaibuliwa na kutekelezwa na Wizara husika, kupitia mipango ya maendeleo ya kila mwaka kulingana na vipaumbele vya kisekta. Uibuaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kisekta, utazingatia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, vipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati akizindua Bunge la 12, Ilani ya Chama Tawala na Agenda na Mipango ya Maendeleo ya Kikanda na Kimataifa. Aidha, miradi ya sekta za kiuchumi na uzalishaji, hususan ujenzi wa barabara, madaraja, viwanja vya ndege, nishati, reli, bandari pamoja na kilimo, uvuvi, mifugo na viwanda itapewa kipaumbele kuchochea uchumi ushindani na maendeleo na watu.

5.11 Matokeo Tarajiwa

Utekelezaji wa Mpango unatarajiwa kuleta matokeo mahususi yakijumuisha: kuchochea ukuaji wa uchumi, kuongezeka kwa Pato la Taifa, kuboreshwa kwa mazingira ya kufanya biashara, kuongezeka kwa mapato ya Serikali na mauzo nje ya nchi. Aidha, viashiria vya matokeo hayo vimegawanyika katika uchumi na ustawi wa jamii kama ilivyoanishwa kwenye Jedwali Na. 38.

Jedwali Na 37: Matokeo Yanayotarajiwa

A. Uchumi wa Ushindani	
(i).	Kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa mwaka wenye wastani wa asilimia 8, ifikiapo mwaka 2025/26;
(ii).	Pato la Jumla la Taifa kwa mtu mmoja (GDP per Capita) kuongezeka kutoka dola za Marekani 1,080 kwa mwaka 2019/20 hadi dola za Marekani 3,000 ifikapo mwaka 2025/26, kwa bei za sasa;
(iii).	Kuongezeka kwa uwekezaji wa moja kwa moja toka nje (FDI) kutoka dola za Marekani milioni 1,173.5 mwaka 2019/20 hadi zaidi ya dola za Marekani milioni 7,980.7 (sawa Sh. trilioni 19.583) mwaka 2025/26;
(iv).	Kuongezeka kwa mapato ya kodi kutoka asilimia 13.5 ya Pato la Taifa mwaka 2019/20, hadi asilimia 14.4 ifikapo mwaka 2025/26;
(v).	Kuongezeka kwa uwezo wa kufua umeme kutoka MW 1,601.3 mwaka 2019 hadi MW 4,915 ifikapo mwaka 2025;
(vi).	Kuongezeka kwa kaya zilizounganishwa na umeme kutoka asilimia 39.9 mwaka 2019/20 hadi asilimia 60 mwaka 2026;

(vii).	Kuongezeka kwa bidhaa zinazouzwa nje kutoka asilimia 17.1 mwaka 2019/20 hadi asilimia 19 ifikapo mwaka 2025/26 ya bidhaa zinazozalishwa viwandani;
(viii).	Kuongezeka kwa utoshelevu wa chakula kutoka asilimia 121 mwaka 2019 hadi asilimia 140 ifikapo mwaka 2025;
(ix).	Kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka 1,500,000 mwaka 2019 hadi 5,000,000 ifikapo mwaka 2025;
(x).	Kuongezeka kwa mapato ya utalii kutoka dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2019 hadi dola za Marekani bilioni 4.2 mwaka 2025.
B. Ustawi wa Jamii	
(i).	Kupungua kwa kiwango cha umaskini wa mahitaji ya muhimu kutoka asilimia 26.4 (kitaifa), asilimia 31.3 (vijijini) na asilimia 15.8 (mijini) mwaka 2019/20, hadi kufikia asilimia 22 (kitaifa), asilimia 28.4 (vijijini) na asilimia 13.2 (mijini) mwaka 2025/26,
(ii).	Fahirisi ya Maendeleo ya Watu (Human Development Index) kuboreka kutoka asilimia 0.57 mwaka 2019/20, hadi asilimia 0.60 mwaka 2025/26;
(iii).	Kuongezeka kwa idadi ya wahitimu wa elimu ya juu kutoka 61,000 mwaka 2019/20 hadi wahitimu 98,000 mwaka 2025/26,
(iv).	Kuongezeka kwa idadi ya wahitimu wa vyuo vya maendeleo ya jamii, vyuo vya mafundi mchundo na wasanifu kutoka 86,547 mwaka 2019 hadi 222,000 mwaka 2025/26;
(v).	Kupungua kwa vifo ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kutoka vifo 50.8 kwa kila watoto 1,000 waonazaliwa hai kwa mwaka 2019/20, hadi vifo 40 mwaka 2025/26;
(vi).	Kupungua kwa vifo vya uzazi 321 kwa kila wazazi 100,000 wanaojifungua hai mwaka 2019/20, hadi vifo 220 mwaka 2025/26;

SURA YA SITA

UGHARAMIAJI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO

6.1 Maelezo ya Jumla

Sura hii inawasilisha makadirio ya rasilimali fedha kwa ajili ya kugharimia utekelezaji wa Mpango kutoka vyanzo mbalimbali pamoja na hatua na mikakati ya kuboresha ukusanyaji wake. Aidha, sura hii inaelezea kwa kina jinsi ambavyo ugharamiaji kutoka sekta ya umma na binafsi itakavyokuwa. Vilevile, Sura inaainisha uratibu za kitaasisi, kisera na kisheria juu ya ugharamiaji wa Mpango, pamoja na majukumu ya wadau mbalimbali katika kugharimia Mpango na kufikia malengo husika.

6.2 Rasilimali Fedha za Kugharamia Mpango

Mojawapo ya kigezo muhimu katika kufanikisha utekelezaji endelevu wa Mpango ni kuwepo kwa upatikanaji wa uhakika na unaotabirika wa rasilimali fedha. Hivyo, uwezo wa kukusanya rasilimali kutoka vyanzo vya umma na sekta binafsi ni muhimu katika utekelezaji wa Mpango. Vyanzo mbalimbali vya ugharamiaji vimechaguliwa kimakakati kulingana na eneo la ugharamiaji, aina na ukubwa wa mradi na programu, uwezekano kiuchumi na kijamii, vihatarishi na matokeo makubwa katika sekta mbalimbali za uchumi. Sekta ya umma itajielekeza katika maeneo yasiyovutia uwekezaji wa sekta binafsi. Mashirika ya umma yatahimizwa kuwekeza katika maeneo ya kimkakati kulingana na majukumu yao na hivyo kuweza kulipa gawio kwa Serikali. Serikali inaweka msisitizo wa kipekee kwa sekta binafsi kushiriki kwenye maeneo yanayovutia uwekezaji wa sekta hiyo. Aidha, Serikali itaelekeza rasilimali nyingi kwenye miradi mikubwa yenye matokeo ya muda mrefu, hususani, ile isiyovutia sekta binafsi kuwekeza.

Rasilimali fedha za kugharamia Mpango zinakadiriwa kuwa shilingi trilioni 114.8, ikijumuisha vyanzo vya sekta ya umma na binafsi. Hili ni ongezeko la asilimia 6.7 ikilinganishwa na rasilimali fedha kwa Mpango wa Pili ambayo ilikuwa shilingi trilioni 107.7. Mpango wa Tatu utagharamiwa kupitia Bajeti ya Maendeleo ya Serikali ambayo ni shilingi trilioni 74.2 kwa kipindi chote cha miaka mitano. Hili ni ongezeko la asilimia 25.8 kutoka Bajeti ya Serikali ya Mpango wa Pili ambayo ilikuwa shilingi trilioni 59. Mapato ya ndani ni shilingi trilioni 62.02 wakati misaada na mikopo yenye masharti nafuu ni shilingi trilioni 12.2. Vyanzo vya sekta binafsi vinakadiriwa kuchangia shilingi trilioni 40.6 ikijumuisha shilingi trilioni 21.03 kutoka vyanzo vya ndani na shilingi trilioni 19.6 kutoka vyanzo vya nje. Rasilimali za sekta ya umma za kugharamia Mpango zinajumuisha mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, misaada, na mikopo kutoka nje na ndani ya nchi. Mchango wa sekta binafsi

katika kugharamia Mpango utapitia miradi ya pamoja ya sekta binafsi (Joint ventures) na miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (Public - Private Partnership -PPP).

Mpango umezingatia matokeo chanya hususan ya Tanzania kuingia katika kundi la nchi zenye uchumi wa kipato cha kati. Ingawa Serikali itaendelea kupata misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka nchi wafadhili na mashirika ya kimataifa, upatikanaji wa fedha kutoka vyanzo hivi unatarajiwa kupungua. Hivyo, kukopa kutoka masoko ya mitaji ya kimataifa itabaki kuwa fursa itakayofikiriwa kugharamia utekelezaji wa Mpango. Mapendekezo ya vyanzo vya nje vya fedha yamezingatia mitikisiko ya kiuchumi, mathalan athari za janga la homa kali ya mapafu ambalo limezikumba nchi washirika wa maendeleo na kuwepo uwezekano wa kupungua kwa misaada yao. **Jedwali Na. 38 na 39** linachanganua vyanzo vya ugharamiaji Mpango.

Jedwali Na. 38 Rasilimali Fedha za Kugharamia Mpango (Shilingi Milioni)

	2021/22	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26	JUMLA
Mapato ya Ndani	**26,032,576**	**28,214,919**	**30,852,142**	**33,503,374**	**36,059,574**	**154,662,586**
Mapato ya Kodi	22,097,676	24,104,998	26,269,832	28,574,140	30,658,286	**131,704,932**
Yasiyo ya Kodi	3,071,042	3,192,899	3,606,752	3,885,388	4,299,588	**18,055,669**
Mapato ya Ndani Halmashauri	863,858	917,022	975,558	1,043,847	1,101,700	**4,901,985**
Misaada	**1,127,188**	**959,108**	**865,416**	**745,557**	**520,261**	**4,217,530**
Ugharamiaji	**2,933,636**	**2,880,930**	**2,345,708**	**2,136,303**	**2,051,673**	**12,348,250**
Nje (*Net*)	1,094,839	1,097,745	429,783	58,989	-178,308	**2,503,048**
Mikopo Nafuu	1,757,802	1,706,574	1,663,106	1,627,871	1,596,144	**8,351,497**
Mikopo ya Kibiashara	2,352,107	2,421,900	1,840,650	1,745,450	1,646,775	**10,006,882**
Malipo ya Deni	-3,015,070	-3,030,729	-3,073,973	-3,314,332	-3,421,227	**-15,855,330**
Ndani (*Net*)	1,838,796	1,783,185	1,915,925	2,077,315	2,229,981	9,845,201
NDF	1,838,796	1,783,185	1,915,925	2,077,315	2,229,981	9,845,201
Kusogeza mbele malipo ya mtaji (*Rollover*)	3,150,337	3,050,728	3,070,117	3,264,332	3,321,227	15,856,741
Jumla: Bajeti ya Serikali	**36,258,806**	**38,136,414**	**40,207,356**	**42,963,899**	**45,373,962**	**202,940,437**
Jumla Rasilimali Zote Mpango wa III	**13,255,855**	**14,023,994**	**14,936,994**	**15,815,289**	**16,214,611**	**74,246,744**
Nje	10,370,865	11,408,312	12,459,472	13,564,196	14,220,541	**62,023,386**
Ndani	2,884,990	2,615,682	2,477,522	2,251,093	1,994,071	**12,223,358**
Jumla Rasilimali Sekta Binafsi	**4,132,000**	**4,546,000**	**9,076,000**	**12,297,000**	**10,560,000**	**40,611,000**
Miradi ya PPP	1,355,000	719000	5,165,000	7,902,000	5,887,000	**21,028,000**

Miradi ya Ubia (JV)	2,777,000	3,827,000	3,911,000	4,395,000	4,673,000	**19,583,000**
Jumla: Rasilimali zote Mpango wa III	**17,387,855**	**18,569,994**	**24,012,994**	**28,112,289**	**26,774,611**	**114,857,744**

Jedwali Na. 39 Uwiano kwa Pato la Taifa

	2021/22	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26
Pato la Taifa (bei ya Soko) – Milioni	**163,879,616**	**174,534,634**	**185,936,799**	**198,952,375**	**212,879,041**
Kodi: Uwiano/Pato la Taifa	13.5%	13.8%	14.1%	14.4%	14.4%
Isiyo ya Kodi: Uwiano/Pato la Taifa	1.9%	1.8%	1.9%	2.0%	2.0%
Fedha za Halmashauri	0.5%	0.5%	0.5%	0.5%	0.5%
Mapato ya ndani/Pato la Taifa	15.9%	16.2%	16.6%	16.8%	16.9%
NDF /Pato la Taifa	1.1%	1.0%	1.0%	1.0%	1.0%
Sekta ya Umma Mpango wa III /Jumla ya Bajeti	36.6%	36.8%	37.1%	36.8%	35.7%

6.3 Vyanzo vya Ugharamiaji vya Mpango

Kwa mapana, vyanzo vya ugharamiaji Mpango vinajumuisha sekta ya umma (Serikali na taasisi za umma) na sekta binafsi.

6.3.1 Vyanzo vya Mapato ya Sekta ya Umma

Vyanzo vya umma vinajumuisha mapato ya ndani (kodi, mapato yasiyo ya kodi na vyanzo bunifu), misaada, na mikopo kutoka ndani na nje ya nchi.

6.3.1.1 Vyanzo vya Ndani

Mapato ya ndani yanatarajiwa kuchangia sehemu kubwa ya fedha katika bajeti ya Serikali na mchango wake ukitarajiwa kuendelea kuongezeka kutoka asilimia 71.8 mwaka 2021/22 hadi asilimia 79.3 mwaka 2025/26. Uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa unatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 15.9 mwaka 2021/22 hadi asilimia 16.9 mwaka 2025/26 (Jedwali 39). Vyanzo asilia vya mapato vitabaki kuwa vya kodi na yasiyo ya kodi zikijumuisha mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Rasilimali za Ugharamiaji Zitokanazo na Kodi: Kodi itokanayo na uagizaji wa bidhaa kutoka nje, mapato ya ndani na kodi ya mlaji (ambazo kwa sasa zinachangia hadi asilimia 65 ya mapato) itaendelea kuwa chanzo kikubwa na muhimu cha mapato ya kodi. Kiwango cha kodi kwenye bidhaa za ndani (hususani kodi ya ongezeko la thamani) na mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajiwa kuongezeka. Ongezeko la mapato ya kodi litatokana na ukuaji jumla wa uchumi na hatua za kuimarisha utendaji, ambapo uwiano kwa Pato la Taifa unatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 13.5 mwaka 2021/22 hadi asilimia 14.4 ifikapo mwaka 2025/26.

Mapato yasiyo ya Kodi: Hili ni eneo lingine ambalo Serikali itaendelea kukusanya mapato yake. Wakati wa utekelezaji wa Mpango, ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi unatarajiwa kuongezeka kutoka shilingi trilioni 3.1 mwaka 2021/22 hadi shilingi trilioni 4.3 mwaka 2025/26. Serikali itaimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kutoka vyanzo vyote husika zikiwemo Wakala za Serikali na mali za umma. Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yanatarajiwa kuongezeka kutoka shilingi trilioni 0.86 mwaka 2021/22 hadi shilingi trilioni 1.102 mwaka 2025/26.

Vyanzo visivyo asilia na bunifu vinajitokeza kuwa fursa vya kuungana na vyanzo asilia katika ukusanyaji wa mapato ya kugharamia miradi ya maendeleo. Vyanzo hivi vinajumuisha hatifungani za Halmashauri, hatifungani za diaspora, bima na ugharamiaji hatarishi (risk financing) na hatifungani za kiislam (Sukuk). Hata hivyo, ili Tanzania iweze kutumia fursa hizi, Serikali itaweka mazingira wezeshi ikiwemo sera, sheria na mifumo. Tafiti mbalimbali zinafanyika juu ya ubunifu wa masuala ya kifedha ikijumuisha mfumo wa kitaifa wa ugharamiaji maendeleo (Integrated National Financing Framework - INFF) ambao utaondoa baadhi ya vikwazo katika vyanzo bunifu vya ugharamiaji miradi ya maendeleo. Vilevile, ubunifu utatumika kugharamia miradi inayoshindikana kutekelezwa kwa kutumia bajeti ya Serikali au vyanzo vya kibiashara ambavyo ni vya gharama kubwa. Mfano ni miradi ya Liganga na Mchuchuma ambayo utaratibu wa hatifungani za bidhaa unaweza kutumika kwa vile imefanikiwa katika baadhi ya nchi. Mapato yatokanayo na miradi yanaweza kutumika kulipia deni husika. Ili kufanikisha utekelezaji wa miradi kama hii, utaratibu wa kampuni maalum (Special Purpose Vehicle) unaweza kuanzishwa katika kusimamia miradi.

6.3.1.2 Mikopo ya Ndani

Ukopaji kutoka vyanzo vya ndani utaongozwa na Mkakati wa Muda wa Kati wa Usimamizi Madeni (MTDS) ambao unaonesha kwamba dhamana zote za Serikali (Government securities) zitatumika, upendeleo ukiwa hatifungani za muda mrefu (long-term bonds). Kwa sasa, hatifungani za Serikali zinazotumika ni za miaka miwili (2), miaka mitano (5), miaka saba (7), miaka 10, miaka 15 na miaka 20. Vilevile, maandalizi ya kuanzisha Hatifungani ya miaka 25 yapo katika hatua za mwisho. Ni muhimu kutambua kwamba kiwango cha ugharamiaji wa ndani wa chini ya asilimia 1.0 ya Pato la Taifa kitaendelea kuzingatiwa ili kutoa nafasi kwa sekta binafsi kukopa kwenye taasisi za fedha.

6.3.1.3 Vyanzo vya Nje

Misaada na mikopo yenye masharti nafuu: Vyanzo vikuu vya kimataifa vya ugharamiaji vitajumuisha misaada na mikopo yenye masharti nafuu. Inatarajiwa kuwa misaada itaendelea kupungua kama ilivyoonekana wakati wa kutekeleza Mpango wa Pili. Pamoja na mambo mengine, misaada inaathiriwa na kuendelea kupungua kwa mapato ya kodi katika nchi wafadhili; athari za homa kali ya

mapafu; kupungua kwa mwitikio kwa baadhi ya wafadhili; kuendelea kuwepo mashaka juu ya ubora wa miradi na programu zinazofadhiliwa na nchi wahisani katika baadhi ya nchi zinazoendelea; na suala la Tanzania kuingia kwenye kundi la nchi zenye uchumi wa kipato cha kati.

Hivi karibuni homa kali ya mapafu imeathiri wadau wengi wa maendeleo na kuna uwezekano wa kupunguza misaada ili waweze kushughulika na changamoto zinazowakabili kiuchumi na kibajeti. Aidha, kutokana na Tanzania kuingia kwenye kundi la nchi za uchumi wa kipato cha kati cha chini, hali ya ufadhili inatarajiwa kubadilika. Inategemewa kuwa misaada itapungua na michango katika jumuiya za kikanda hususan Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Afrika itaongezeka. Hii inamaanisha kuwa Tanzania italazimika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Kwa kipindi cha miaka mitano ijayo misaada inatarajiwa kufikia shilingi trilioni 4.2. Misaada itapungua kutoka shilingi trilioni 1.127 mwaka 2021/22 hadi shilingi trilioni 0.520 mwaka 2025/26. Mchango wa misaada katika Pato la Taifa utapungua kutoka asilimia 0.7 mwaka 2021/22 hadi asilimia 0.2 mwaka 2025/26. Serikali inatarajiwa kupata rasilimali kupitia mikopo yenye masharti nafuu ya kibajeti, miradi pamoja na mfuko wa pamoja (*Basket funding).* Mikopo ya masharti nafuu itapungua kutoka shilingi trilioni 1.76 mwaka 2021/22 hadi shilingi trilioni 1.60 mwaka 2025/26. Hata hivyo, mikopo ya kibajeti haitarajiwi kuchangia kiasi kikubwa kufuatia kuendelea kupungua kwa mwitikio wa wadau wengi wa maendeleo katika eneo hili. Vilevile, mikopo ya masharti ya kibiashara inatarajiwa kupungua kutoka shilingi trilioni 2.35 mwaka 2021/22 hadi shilingi trilioni 1.65 mwaka 2025/26. Ni muhimu kuhakikisha kuwa vyanzo hivi vinatumika kikamilifu.

Jitihada za kujenga imani, kuendeleza mifumo iliyopo na kutafuta fursa mpya pamoja na kuboresha hatua za uratibu zitaimarishwa. Tanzania itatumia fursa ya kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati kujenga uwezo wa utayarishaji wa miradi inayokopesheka pamoja na kuimarisha mbinu za majadiliano. Hatua hizi zitapanua wigo wa miradi inayokopesheka na hivyo kuwa na ukopaji wenye tija. Misaada ya kiufundi na mahusiano ya nchi na nchi iitakuwa muhimu katika kupata ujuzi na teknolojia ili kuimarisha usimamizi wa upatikanaji wa rasilimali kutoka nje.

Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (CCF): Ingawa fursa za mfuko huu hazikutumiwa wakati wa Mpango wa wa Pili, CCF itakuwa chanzo muhimu cha mapato ya utekelezaji wa Mpango huu. Kiasi cha dola za Marekani milioni 304 (sawa na takribani shilingi milioni 705,280) kilichokisiwa kutumika wakati wa Mpango wa Pili kitatafutwa na kutumika. Kutokana na uzoefu uliopatikana wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Pili ambapo upatikanaji fedha kutoka Mfuko wa

Mabadiliko ya Tabianchi haukufanikiwa kutokana na uwezo mdogo wa kutayarisha miradi inayouzika, juhudi za kujenga uwezo husika zitaimarishwa kuanzia mwanzo wa utekelezaji wa Mpango. Mpango kazi wa kuhakikisha kuwa uwezo unaohitajika unapatikana katika kipindi cha miaka miwili ya mwanzo wa utekelezaji wa Mpango utatayarishwa na kutekelezwa. Hatua za kuchukuliwa zinajumuisha uwezo wa kuainisha na kutayarisha miradi sahihi, kujenga mbinu za majadiliano (kwa mikopo ya pamoja, mikopo ya masharti ya kati na mikopo ya uagizaji bidhaa) na kuendelea na mchakatao wa kuidhinisha Wizara ya Fedha na Mipango ilie iweze kupata fedha moja kwa moja kutoka Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi.

6.3.2 Vyanzo vya Mapato ya Sekta Binafsi

Kama ilivyo kwa sekta ya umma, vyanzo vya kugharamia mchango wa sekta binafsi vimegawanyika katika mafungu mawili makubwa, yaani vyanzo vya ndani na nje.

6.3.2.1 Vyanzo vya Ndani vya Sekta Binafsi

Sekta binafsi inatarajiwa kushiriki katika Mpango kupitia miradi ya pamoja (JV) na ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) pamoja na uwekezaji wake kwa ujumla katika uchumi. Mchango wa moja kwa moja wa Sekta binafsi katika Mpango kupitia miradi ya Pamoja (JV) na Ubia (PPP) unakadiriwa kuwa shilingi trilioni 21.03. Mchango wa sekta binafsi usiokuwa wa moja kwa moja unakisiwa kufikia shilingi trilioni 250.85 katika sekta za kilimo, madini, viwanda na uzalishaji, ujenzi, biashara, huduma za hoteli, usafiri na mawasiliano, huduma za kifedha, elimu na huduma za afya. Rasilimali za sekta binafsi katika Mpango (na uwekezaji mwingine) zinatarajiwa kutokana na huduma za mikopo, soko la hisa, hatifungani za makampuni, makampuni ya bima, mitaji ya kampuni na itokanayo na faida za uwekezaji kwenye biashara.

Utaratibu wa miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) siyo mpya kwa Tanzania. Kabla ya kupitishwa kwa sera ya PPP mwaka 2009, miradi yenye thamani ya dola za Marekani milioni 1,000 ilikuwa ikitekelezwa katika sekta za usafiri, TEHAMA na nishati. Mfumo wa usimamizi wa PPP umeendelea kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kupitishwa kwa Sera ya PPP mwaka 2009, marekebisho ya Sheria mwaka 2014 na mwaka 2018 - yote yakilenga kurahisha mfumo wa utekelezaji wake. Kanuni za PPP zilitolewa mwezi Januari 2020 baada ya kurekebishwa kwa sheria ya PPP mwaka 2018. Kwa lengo la kuendelea kuvutia sekta binafsi katika PPP, juhudi zitafanywa kuhakikisha kuwa malengo yake yanakubalika katika ngazi zote ili kuepuka kurejea kwenye taratibu za ununuzi wa kawaida kuhusu miradi ya PPP (ili kuzingatia thamani ya fedha). Uchanganuzi wa miradi na kupitishwa kwake kutaharakishwa katika ngazi za Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na kujadili miradi ya PPP wakati wa kutayarisha

bajeti zao. Serikali itashirikiana na sekta binafsi kupitia utaratibu wa PPP katika kutenga rasilimali za kuboresha miundombinu wezeshi katika maeneo maalum ya uwekezaji (EPZs).

Makadirio ya uwekezaji wa sekta binafsi kupitia PPP na JV pamoja na uwekezaji wake katika sekta mbalimbali umezingatia misingi zifuatazo:

(a) Fursa chanya za sekta binafsi kutokana na mageuzi katika sekta binafsi (Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara) na sekta ya fedha na (Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha). Mageuzi haya yanatarajiwa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na hatimaye kuharakisha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa ajili ya uwekezaji wa sekta binafsi;

(b) Mazingira bora ya usimamizi wa sekta binafsi kushiriki kupitia utaratibu za PPP;

(c) Sera mpya ya kukuza uwekezaji inayoandaliwa; na

(d) Mazingira ya miundombinu yaliyoboreshwa ya uwekezaji na biashara (nishati, usafirishaji na mawasiliano).

Duniani kote, ongezeko la vyanzo bunifu vya mapato ya sekta binafsi linaweza kugharamia miradi ya maendeleo inayotumia rasilimali za umma katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Mifano ni kama hatifungani za kijamii (social impact bonds) na hatifungani za maendeleo (Development Impact bond) na utaratibu wa kugharamia kwa makundi (crowd funding), mbinu ambazo zinatumika mara nyingi katika nchi zilizoendelea. Serikali itaendelea kupata uzoefu kutoka nchi nyingine juu ya vyanzo bunifu, kanuni zake, vihatarishi vya kifedha vitakavyojitokeza pamoja na ufumbuzi unaohitajika. Sekta binafsi pia itahusishwa kupitia Serikali kuuza hisa zake katika soko la mitaji na hatimaye kuoredheswa kwenye Soko la Hisa la Dar-es-salaam. Fedha zinazopatikana zitatumika kupanua wigo wa rasilimali za kugharamia Mpango.

6.3.2.2 Vyanzo vya Nje vya Sekta Binafsi

Vyanzo vikubwa vya fedha vya sekta binafsi kutoka nje vitatokana na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI), ijapokuwa chanzo hiki kimeendelea kupungua katika miaka ya karibuni. Kiasi cha dola za Marekani milioni 7,980.7 sawa na shilingi trilioni 19.583 kinatarajiwa kuwekezwa katika sekta mbalimbali za uchumi kwa miaka mitano ijayo kupitia FDI. Inakisiwa kuwa wakati wa utekelezaji wa Mpango, mapato ya FDI yataongezeka kwa wastani wa asilimia 13 kwa mwaka kutoka dola za Marekani milioni 1,173.5 mwaka 2021/22 hadi dola za Marekani milioni 1,871.1 mwaka 2025/26. Uwekezaji mkubwa unatarajiwa katika mafuta na gesi, uchimbaji wa madini na mawe, chakula na mahoteli, uzalishaji, fedha na huduma za bima. Hii itatokana na kuboreshwa hali ya uwekezaji nchini hususan

kujenga mazingira mazuri ya uchumi jumla. Vyanzo vingine vitajumuisha fedha za uwekezaji kwa faida (*portfolio investment*) pamoja na uhamishaji binafsi wa fedha kimataifa.

Ili kupata uwekezaji endelevu wa moja kwa moja wa ndani (DDI) na uwekezaji wa moja kwa moja toka nje (FDI), Serikali itaendelea kujenga mazingira mazuri ya biashara na kukuza fursa za uwekezaji. Serikali inatambua mchango wa sekta binafsi kama mhimili wa kukuza uchumi na itaendelea kuikuza kwa lengo la kuboresha uwekezaji wake nchini. Serikali itaendelea kukuza uwekezaji kwa kutoa vivutio shindani kwa wawekezaji wa nje na ndani. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango, maboresho zaidi yatafanyika katika uendeshaji wa kituo cha pamoja cha uwekezaji sanjari na uratibu madhubuti kati ya kituo cha uwekezaji - TIC na Wizara zinazohusika katika kuwezesha wawekezaji. Msukumo wa pekee utawekwa katika kurahisisha na kuweka wazi taratibu na kasi ya kufanya maamuzi. Tanzania imeshakubaliana na baadhi ya nchi kutekeleza mikataba ya Kukuza na Kulinda Rasilimali (BITs) pamoja na mikataba ya Biashara (BTAs) kwa lengo la kukuza na kulinda uwekezaji na biashara. Vile vile, Tanzania ni mwanachama wa Taasisi ya Kusimamia Uwekezaji Duniani (MIGA) ili kulinda uwekezaji dhidi ya athari zisizotokana na biashara.

6.4 Mageuzi ya Mifumo, Taasisi, Sera na Sheria

6.4.1 Mapato ya Ndani

Ili kuimarisha uhimilivu wa mapato, Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri na tulivu ya uchumi jumla ili kuchangia kukua kwa uchumi, kuongeza makusanyo kwa kupanua wigo wa kodi, kuongeza wigo wa walipa kodi na kuimarisha mfumo wa usimamizi wa kodi. Hatua mahususi zitakazochukuliwa ni pamoja na:

(a) Kuimarisha ukusanyaji wa kodi mbalimbali kama ushuru wa uagizaji wa bidhaa, ushuru wa bidhaa, Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na kodi nyinginezo kwa kutumia mifumo ya teknolojia ili kuepusha vitendo vya rushwa vinavyotokana na mlipa kodi kukutana na mtoza kodi;

(b) Kuijengea Mamlaka ya Mapato Tanzania - TRA uwezo wa kufuatilia vitendo vya udanganyifu katika ulipaji kodi;

(c) Kuimarisha ukusanyaji wa tozo katika bandari ya Dar-es-Salaam, vituo vyote vya mipakani na bandari kavu zote nchini ili kuzuia ukwepaji wa ulipaji kodi. Hatua hizi zitahitaji kuimarisha uwezo wa vyombo vya ukusanyaji kodi na kuanzisha mifumo ya ufuatiliaji wa magari ya mizigo na kuharakisha hatua za ukusanyaji kodi;

(d) Kupanua wigo wa walipa kodi kwa kulenga sekta isiyo rasmi na kuitoza kodi. Mikakati itahusisha kutafuta namna bora ya kuunganisha mifumo ya utambuzi wa mlipa kodi (TIN) na utambuzi wa utaifa (NID) na kutambua

ukubwa wa uchumi usio rasmi na kuhakikisha upatikanaji wa taarifa kupitia malipo ya kodi za zuio;

(e) Kuongeza maeneo ya wigo wa kodi kijiografia na kutambua mchango wa sekta husika ikiwemo kuimarisha makusanyo ya kodi ya ardhi inayomilikiwa;

(f) Kuweka mfumo wa kutoza kodi miamala ya simu za mkononi ili kukusanya mapato ya malipo ya kielektoniki;

(g) Kuimarisha ukaguzi wa madini ikijumuisha utambuzi wa kiasi, ujazo wa madini yaliyomo (*content)* na miamala ya kampuni za madini, kuimarisha makusanyo ya kodi na mrabaha kutoka kwenye rasilimali za madini na kuimarisha uwezo wa Tume ya Madini Tanzania (TMC) na Taasisi ya Uwazi ya Viwanda vya Uchimbaji madini Tanzania (TEITI);

(h) Kuhakikisha hakuna nafasi ya rushwa katika masuala ya ukusanyaji mapato kwenye Wizara, Idara na Wakala wa Serikali pamoja na Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(i) Kupitia upya misamaha ya kodi na punguzo la kiwango cha kulipa kodi, na kurekebisha inapobidi, kama njia ya kuwapa motisha kwa wawekezaji;

(j) Kutengeneza mifumo ya ndani ya kieletroniki ya kukadiria kodi na kuepusha mlipa kodi kukutana na mtoza kodi kwa ajili ya kupunguza vitendo vya kibinadamu, kuongeza ufanisi na imani kwa walipa kodi;

(k) Kuimarisha mitaji ya Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ili kukuza ufanisi;

(l) Kuyawezesha mashirika ya umma kuwekeza kwenye maeneo ya kimkakati ili yaweze kulipa michango na gawio kwa Serikali; na

(m) Kuanzisha kampuni maalum (SPV) au kamati maalum ya kusimamia uwekezaji wa ubia ambao Serikali ina maslahi, badala ya Serikali kusimamia moja kwa moja.

6.4.2 Ufadhili wa Ndani wa Sekta Binafsi

Serikali imepiga hatua katika kuendeleza mfumo wa soko la fedha nchini, ikiwa ni pamoja na idadi ya taasisi za kifedha za kugharamia maendeleo lakini maendeleo ya masoko ya fedha bado hayaridhishi. Hatua za kimkakati ya kukabiliana na changamoto za masoko ya fedhazimeainishwa katika Mpango na mikakati wa kifedha na Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha (2020/21 – 2029/30). Masuala ya kuzingatia ni kuendeleza upatikanaji wa huduma za fedha za gharamanafuu, jumuishi na rasmi kwa kupanua huduma za kidigitali; kuimarisha ulinzi wa mlaji pamoja na huduma za kibenki; mitaji na masoko ya bima (ikijumuisha sekta binafsi kuingia katika masoko ya ubia); pamoja na vyama vya ushirika vya akiba na mikopo.

Ili kukuza ubia wa sekta binafsi na uvutiaji wa mitaji, maeneo manne yatapewa kipaumbele. Kwanza, kupitia kiwango kilichowekwa na Tume ya Haki na Ushindani (FCC) cha dola za Marekani milioni 1.5 ili kuungana na kununua kampuni (merger and Acquisition) ambacho ni kikubwa ikilinganishwa na viwango vya nchi jirani. Pili, kuainisha punguzo la kodi kwa mitaji ya kuingia ubia na kujitoa kupitia Soko la Hisa la Dar es salaam (DSE). Tatu, Mamlaka ya takwimu kuhamasisha umma na wawekezaji wa sekta binafsi kutoa taarifa zinazohitajika kuwezesha kufanya maamuzi sahihi ya uwekezaji. Nne, Mamlaka zinazohusika na kuendeleza mitaji kutayarisha programu za kuelimisha sekta isiyo rasmi kuimarisha mifumo ya usimamizi na kuongeza uwazi ili kuvutia ubia na mitaji.

6.4.3 Ugharamiaji Kutoka Nje

Licha ya vyanzo vya mapato kutoka nje kuendelea kupungua, uwezo wa kitaasisi wa kuchambua na kujadiliana kuhusu upatikanaji wa misaada na mikopo utaimarishwa kwa faida ya Taifa. Wizara inayohusika na mambo ya nje itaimarisha majukumu ya diplomasia ya uchumi ili kuchochea upatikanaji wa misaada na mikopo yenye masharti nafuu.

Ili kujenga imani na wawekezaji wa kimataifa, upimaji na uwekaji madaraja *(rating)* utafanyika kuwezesha sekta binafsi kuaminika kukopa kutoka katika masoko ya mitaji ya kimataifa. Kuna manufaa mengi yanayotokana na kupimwa, ikiwemo kuwezesha Serikali na sekta binafsi kuaminiwa kimataifa na hivyo kuwezesha kujadiliana ili kupata mikopo yenye unafuu. Manufaa mengine ni pamoja na kuongezeka kuaminiwa kimataifa, kuongeza uwezo wa kukopa kwa riba nafuu, kuongezeka kwa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje na kuwezesha sekta binafsi kuwekeza nje ya nchi. Hivi sasa Tanzania imewekwa kwenye daraja la sita ya nchi zenye viashiria hatarishi, ikimaanisha kuwa inalazimika kulipa riba na ada ya bima kubwa ukilinganisha na nchi za daraja la chini. Nchi ikipimwa, inaweza kuboresha viashiria hatarishi na hivyo kutozwa riba na ada ndogo ya bima pale taasisi zake zinapokopa.

Kwa lengo la kuvutia na kupata uwekezaji wa moja kwa moja toka nje, kukuza uzalishaji na kuongeza uwezo wa kuzalisha katika Mpango, yafuatayo yatatekelezwa:

(i) Kuandaa mkakati wa kuhamasisha uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje unaoendana na maboresho yanayofanyika pamoja na kuweka vipaumbele vya sera ya uwekezaji katika ngazi ya uchumi kitaifa na kisekta;

(ii) Kuboresha jitihada zinazolenga kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ikijumuisha kuanzisha namna bora ya upokeaji wa wawekezaji, kupunguza urasimu wa taratibu za kuvutia uwekezaji na kujenga uwezo wa kuhamasisha uwekezaji;

(iii) Kuboresha vivutio vya wawekezaji ikiwemo kupitia upya vivutio vilivyopo kuvifanya viwe bora na rafiki kwa wawekezaji;
(iv) Kuimarisha imani kwa wawekezaji hususan kuweka kanuni bora za kutatua malalamiko yatokanayo na uwekezaji;
(v) Kuhamasisha hatua zinazolenga kukuza mashirikiano yenye matokeo chanya yatokanayo na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje katika uchumi;
(vi) Kuboresha mtaji watu utakaotumiwa na wawekezaji kufikia matarajio ya uwekezaji;
(vii) Kuweka mazingira bora ya kufanya kazi ili kuwajengea imani na kujiamini kwa wawekezaji;
(viii) Kujenga miundombinu wezeshi ya maeneo ya kutengeneza Bidhaa za Kuuzwa Nje (EPZs) na Maeneo Maalum ya Kutengeneza Bidhaa (SEZ) ili kuvutia wawekezaji; na
(ix) Kuimarisha upatikanaji wa malighafi za ndani.

6.4.4 Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi

Rasilimali za Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi ni fursa muhimu iwapo zitatumika ipasavyo. Hivyo, ni muhimu kujenga uwezo wa kitaasisi ili kuweza kuzipata. Uwezo unaohitajika kujengwa ni katika maeneo yanayohusika na uandaaji wa nyaraka husika na mifumo, upatikanaji wa Taasisi zilizoidhinishwa kukidhi vigezo vinavyohitajika kwa utekelezaji, ujenzi wa mifumo ya uratibu na ufuatiliaji hususani rasilimali zinazotokana na asasi zisizo za kiserikali. Kama ilivyopendekezwa kwenye Mpango wa Pili, uanzishaji na usimamizi wa mfumo wa Kitaifa wa kufadhili mabadiliko ya Tabianchi ni muhimu kwa ajili ya kuunganisha juhudi za kutafuta rasilimali stahiki.

6.5 Vihatarishi vya Ugharamiaji wa Mpango na Njia za Kukabiliana Navyo

Vihatarishi katika ugharamiaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo vinaendana na masuala ya kiuchumi, kisiasa, kimazingira na kijamii. Vile vile vinaweza kuwa ni vya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Baadhi ya vihatarishi hivyo ni kama ifuatavyo:

(i) **Ufinyu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa maeneo yaliyopendekezwa.** Mpango umependekeza vyanzo mbalimbali vya ugharamiaji na iwapo rasilimali fedha za kutosha hazitaweza kupatikana kutoka katika vyanzo hivyo kama ilivyopangwa kunaweza kuathiri utekelezaji wa Mpango. Baadhi ya vyanzo vilivyopendekezwa na Mpango wa Pili wa Maendeleo vilifikia malengo na vingine vilikuwa chini ya lengo na baadhi ya sababu za kutokufikia malengo hayo zilikuwa nje ya uwezo wa Serikali. Katika kukabiliana na hali hiyo, umeandaliwa Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Tatu ambao una vipaumbele na kulenga vyanzo vyenye kuleta matokeo makubwa kiuchumi. Aidha, Mkakati wa Ugharamiaji

umeoanisha baadhi ya maeneo ya utekelezaji na vyanzo vya fedha ikiwemo mikopo yenye riba nafuu na mikopo ya kibiashara;

(ii) **Kupotea kwa mapato ya Serikali kupitia biashara mtandao**: Ukuaji wa uchumi wa kidigitali umeleta mageuzi makubwa katika taratibu za kufanya biashara kupitia mitandao kwa kuanzisha moduli mpya za kibiashara ikiwemo biashara mtandao na matangazo ya mtandaoni. Mageuzi hayo yameleta changamoto kubwa katika nyanja za kodi. Katika kukabiliana na changamoto hii, Serikali inaandaa Mkakati wa kuwezesha utozaji kodi katika uchumi wa kidigitali ikijumuisha kufanya mapitio ya mifumo ya kisheria iliyopo ili kutatua changamoto za biashara mtandao, kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 2014 ili kujumuisha tafsiri ya bidhaa mtandao na uwekezaji katika TEHAMA;

(iii) **Misukosuko inayoathiri uchumi au vyanzo vya mapato**: Hii inajumuisha majanga asilia na majanga ya mlipuko ambayo yanaweza kupelekea kubadilika kwa matumizi ya rasilimali fedha kwenda katika maeneo yaliyoathirika badala ya kutumika katika maeneo yaliyopendekezwa katika Mpango. Hali hii itaathiri ukuaji wa uchumi na kupelekea kutofikiwa kwa kiwango cha ukuaji kilichotarajiwa hivyo kuathiri mapato, kama vile mapato ya kodi yatokanayo na kipato. Mitikisiko duniani pia inaweza kutokea kama vile mitikisiko ya fedha duniani, majanga ya asili, na magonjwa ya mlipuko. Hali hiyo inaweza kusababisha rasilimali fedha zilizokusudiwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kuelekezwa katika kukabiliana na mitikisiko hiyo. Kutokana na uzoefu wa hivi karibuni hususan mitikisiko katika baadhi ya nchi za Ulaya na mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu, ufadhili unaotarajiwa (misaada, mikopo nafuu na uwekezaji wa moja kwa moja) unaweza kupungua na hivyo kuathiri utekelezaji wa Mpango. Hivyo, ni muhimu kuchukua hatua mbadala; kuboresha mifumo ya kuzuia na kukabiliana na majanga; kuimarisha ugharamiaji wa vihatarishi vitokanavyo na majanga; kutumia bima na nyenzo za kugharamia vihatarishi; kurekebisha mipango ili iendane na upatikanaji wa fedha; na kuimarisha mifumo ya majadiliano na Washirika wa Maendeleo; na

(iv) **Mikopo ya kibiashara**: kupungua kwa mwenendo wa mikopo yenye msharti nafuu na misaada inaashiria kuwa Serikali itategemea zaidi mikopo ya kibiashara kugharamia miradi ya kipaumbele. Kuongezeka kwa mikopo ya kibiashara itasababisha vihatarishi katika uhimilivu wa Deni la taifa kutokana na gharama kubwa ya kuhudumia deni kutokana na mikopo hiyo. Serikali itaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo vyenye masharti nafuu na kuimarisha hatua za ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kugharamia miradi yenye matokeo makubwa.

6.6 Mchango wa Wadau Katika Kugharamia Mpango

Ushirikiano wa kufanya kazi pamoja kati ya wadau mbalimbali ni muhimu katika kuhakikisha kuwa Mpango huu unatekelezwa kikamilifu. Wadau muhimu watajumuisha Serikali, sekta binafsi, asasi zisizo za kiserikali na Washirika wa Maendeleo.

6.6.1 Serikali

Serikali itakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

(i) Kuweka vipaumbele, mpangilio na kuharakisha mageuzi ya kutatua changamoto za ufinyu wa soko la fedha.Maeneo hayo matatu yana uwezo wa kuleta ufanisi mkubwa wa mageuzi kuliko kutumia mlolongo wa hatua zisizokuwa na uwezo wa kutekeleza mageuzi kikamilifu;

(ii) Kuimarisha mashirikiano katika mageuzi ya sekta ya fedha na mageuzi mengine ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara na kuharakisha maendeleo ya sekta binafsi. Mfano mmoja wapo ni mageuzi katika sekta ya elimu au maboresho ya mitaala ambayo yanahitaji kuongezewa mahitaji mahususi ya ujuzi na sifa zinazihitajika katika sekta ya fedha. Kwa ufupi ni kuwa kuna haja ya kuunganisha mageuzi ya sekta ya fedha yaendane na mageuzi mengine yanayofanyika katika sekta binafsi na sekta ya umma;

(iii) Kuweka vivutio vitakavyosaidia kuongeza wigo wa matumizi ya masoko ya mitaji kupata mtaji wa uwekezaji wa muda mrefu;

(iv) Kuimarisha utendaji ikiwemo kusimamia matokeo ya utekelezaji na kuhakikisha uwajibikaji na kufanya maamuzi yenye kuzingatia uwepo wa taarifa sahihi zinazotokana na tathmini ya athari;

(v) Kuimarisha uratibu wa taasisi zisizo za kiserikali ili ziweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu kwa kuzingatia kanuni za uwajibikaji na uwazi pamoja na vipaumbele vya taifa;

(vi) Kubainisha mahitaji halisi ya rasilimali watu na sifa stahiki katika sekta ya umma na taasisi zisizo za kiserikali ili kuwezesha upangaji mzuri wa rasilimali watu utakaoleta tija zaidi;

(vii) Kuweka mazingira wezeshi na uratibu wa watanzania walioko nje ya nchi kutangaza kikamilifu vivutio vya uwekezaji vilivyopo nchini na pia kushiriki katika kuwekeza nchini;

(viii) Kufanikisha mchakato wa kupata idhini ya kutumia fursa ya fedha zitokanazo na mabadiliko ya hali ya hewa ikiwemo *Adaptation Fund* na *Green Climate Fund.* Kwa kuwa fursa hii ni pana ni muhimu taasisi nyingi za umma na binafsi zikaomba na kushiriki katika mchakato wa uidhinishwaji;

(ix) Kupitia balozi zetu zilizopo nje Wizara inayohusika na mambo ya nje itashiriki kikamilifu kuiunganisha Tanzania na wawekezaji mbalimbali nje ya nchi, kuwezesha majadiliano na makubaliano kuhusiana na misaada, mikopo na uwekezaji wa moja kwa moja. Wizara pia itakuwa na wajibu wa

kuimarisha diplomasia ya uchumi kwa kuunganisha wawekezaji na wafanyabiashara wa kimataifa na hivyo itahitaji kufanya kazi kwa karibu na Wizara za uzalishaji za kisekta ili kuimarisha uwekezaji na kupanua wigo wa masoko ya bidhaa na huduma; na

(x) Kuimarisha uwezo wa MDAs na LGAs kuandaa miradi inayokopesheka kutoka taasisi mbalimbali za fedha na kwa wawekezaji.

6.6.2 Sekta Binafsi

Jukumu la sekta binafsi katika kugharamia Mpango ni kama ifuatavyo:

(i). kutumia vyanzo binafsi vilivyopo na kuwekeza kupitia njia za ubia (JV) na baina ya sekta binafsi na ya umma (PPP);

(ii). Kuendelea kutumia rasilimali binafsi (mikopo na masoko ya mitaji) kuwekeza katika shughuli mbalimbali za uzalishaji ambazo ni za kibiashara tu na hazihitaji rasilimali za umma;

(iii). Kuendeleza ubunifu, ujuzi, rasilimali, fikra na ushirikiano miongoni mwa wadau wa sekta binafsi siyo tu kwa ajili ya kugharamia uwekezaji bali pia kuinua sekta ya fedha;

(iv). Kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya kisera kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kutambua udhaifu kwenye sekta ya fedha kama sehemu ya juhudi za Serikali kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji;

(v). Kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa viwanda vidogo (SMEs) kupitia hatua za kujenga uwezo kama vile mafunzo ya ufundi na usimamizi pamoja na upatikanaji wa huduma za kifedha; na

(vi). Kutoa taarifa muhimu na takwimu zinazohitajika kwa ajili ya kupanga na kutoa maamuzi katika ngazi zote.

6.6.3 Wadau wa Maendeleo

Wadau wa Maendeleo watakuwa na majukumu yafuatayo:

(i) Kufanya majaribio ya modeli mpya na bunifu zinazohusu misaada inayotolewa ili kujenga uzoefu na uelewa wa pamoja na namna bora ya kutumia fedha za misaada;

(ii) Kuunga mkono mageuzi kwa lengo la kuingia katika masoko ya fedha kwa kutumia misaada ya kiufundi na uzoefu. Aidha, watasaidia kutumia ubunifu kubainisha mbinu mahsusi za kutanzua changamoto zinazoweza kujitokeza;

(iii) Kukuza na kuwezesha majadiliano kati ya Serikali, sekta binafsi na asasi za kiraia.

6.6.4 Asasi Zisizo za Kiserikali

Hawa watakuwa na majukumu yafuatayo:

(i) Kuunga mkono mchakato wa utayarishaji sera kupitia uwekezaji katika tafiti, kufanya uchambuzi na kutoa mapendekezo ya kutatua vikwazo katika kuendeleza sekta ya fedha;
(ii) Kuwekeza na kushiriki katika majadiliano ya sera zinazohusu sekta ya maendeleo ya fedha katika ngazi zote;
(iii) Kuwekeza katika programu za maendeleo ambazo zinaleta ubunifu na kutoa huduma za fedha kwa jamii ambazo hazijafikiwa na huduma hizo;
(iv) Kubadilishana uzoefu na kujifunza kutoka nchi zingine kuhusu maendeleo ya sekta ya fedha pamoja na uwekezaji ambapo sekta binafsi na sekta ya umma zitashirikiana; na
(v) Kujihusisha na kutafuta rasilimali za kuwekeza katika sekta za kijamii na kiuchumi zitakazosaidia juhudi za uwekezaji wa sekta ya umma za kuwekeza katika sekta hizo.

6.6.5 Watoa Huduma za Kifedha

Watoa huduma za kifedha watahimizwa kuendeleza bidhaa na huduma zinazohitajika na jamii yenye kipato cha chini ikiwemo kuwezesha upatikanaji na utumiaji wa fedha za miradi ya maendeleo. Serikali itatekeleza hatua za mageuzi ikijumuishazilizoainishwa katika Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha 2020/21-2029/30 ili kuimarisha upatikanaji wa fedha za maendeleo.

6.6.6 Taasisi za Elimu na Utafiti

Taasisi za elimu na utafiti zitaendeleza uwezo wa wadau mbalimbali pamoja na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu namna bora ya kutayarisha miradi inayouzika na kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali. Kujenga uwezo kutafanyika kupitia programu maalum, mafunzo ya muda mfupi na programu za muda mrefu. Vile vile, taasisi hizi zitakuwa na jukumu la kufanya tafiti kuhusu utafutaji rasilimali na uendeshaji wa huduma za kifedha.

SURA YA SABA

UTEKELEZAJI WA MPANGO

7.1 Utangulizi

Utekelezaji wa Mpango utahusisha uandaaji wa sera, miongozo na mikakati kulingana na mgawanyo wa majukumu. Aidha, Serikali na wadau wengine itaendelea kuibua na kutekeleza miradi na programu za maendeleo ili kufikia malengo ya Mpango. Miradi na programu zitakazo ibuliwa na kutekelezwa zitaendana na vipaumbele vya kisekta. Vile vile, Mpango wa Miaka Mitano utatekelezwa kupitia Mipango ya Mwaka Moja Moja.

7.2 Mfumo wa Utekelezaji wa Mpango

Mfumo wa utekelezaji wa Mpango huu utahusisha taratibu za kiutendaji za Serikali. Taratibu hizo zinajumuisha maandalizi ya mpango kazi wa utekelezaji wa miradi na programu za sekta, mtiririko wa mahitaji ya rasilimali fedha na mpango wa ufuatiliaji na tathmini. Aidha, miongozo mbalimbali ikijumuisha Mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali itazingatiwa ili kuboresha ufanisi wa utekelezaji. Kwa kuzingatia nguzo ya utawala bora, utekelezaji wa Mpango utazingatia Sheria ya Bajeti Sura 439 na Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410.

7.3 Mikakati ya Utekelezaji wa Mpango

Maandalizi ya Mpango huu yalifanyika sanjari na maandalizi ya Mkakati wa Ugharamiaji, Utekelezaji na Ufuatiliaji na Tathmini. Mikakati hiyo, imeainisha maeneo ya msingi katika utekelezaji wa Mpango ambayo ni:

(a) **Kuwianisha Mipango ya Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali na Mpango:** Wizara za kisekta, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitawianisha mipango ya kisekta na Mpango. Lengo la kuwianisha mipango ya kisekta na Mpango huu ni kufikia shabaha za Mpango na Dira ya Taifa ya mwaka 2025.

(b) **Kuimarisha Mifumo ya Upatikanaji wa Takwimu:** Ili kurahisisha zoezi la ufuatiliaji na tathmini Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi itaimarisha mifumo na mikakati ya ukusanya, uchakataji, utunzaji na usambazaji wa takwimu. Takwimu hizo zitahusisha viashiria vya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango.

(c) **Kuimarisha Usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango:** Ili kuboresha ufanisi wa utekelezaji wa Mpango, ni muhimu taasisi zote kutimiza wajibu na majukumu yao. Aidha, Serikali itajielekeza katika uratibu wa mashirkiano miongoni mwa wadau wa Mpango ili kufikia malengo tarajiwa.

(d) **Uibuaji na Uandaaji wa Miradi ya Maendeleo:** katika utekelezaji wa Mpango huu, wadau wanaelekezwa kuzingatia Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo – NPMIS katika uibuaji na uandaaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, Serikali itandaa mkakati kuziwezesha sekta kuandaa nyaraka za miradi ili kuwianisha malengo ya Serikali na wadau wa maendeleo.

(e) **Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa**: kila mdau, hususan Wizara za Kisekta atandaa mkakati wa ufuatiliaji na tathmini kuendana na Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango. Lengo la zoezi hili ni kurahisisha shughuli ya ufuatiliaji na tathmini na punguza gharama usimamizi wa utekelezaji wa Mpango.

(f) **Uwezeshaji wa Uwekezaji na Biashara:** Serikali itaimarisha mfumo wa mashauriano na sekta binafsi ili kubaini maeneo yatakayo imarisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango. Aidha, Serikali na wadau itaendelea kufanya tathmini na tafiti kuhusu mahitaji na urasimishaji wa sekta isiyo rasmi ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika utekelezaji wa Mpango na uchumi.

(g) **Ushirikishwaji wa Wananchi katika Utekelezaji wa Mpango:** Katika utekelezaji wa Mpango huu, Serikali inawahimiza wananchi kushiriki, kuibua na kutekeleza shughuli za kiuchumi kuendana na vipaumbele vya Mpango. Hatua hii itawezesha wananchi kushiriki katika utekelezaji wa Mipango ya Kitaifa na kuchochea hamasa ya kuibua shughuli za kiuchumi katika maeneo yao ili kutatua changamoto ya umaskini wa kipato. Aidha, Serikali itaweka utaratibu wa kuelimisha umma kuhusu fursa zinazotokana na Mpango kupitia vyombo vya habari, majarida na makongamao.

7.4 Muundo wa Utekelezaji wa Mpango

Utekelezaji wa Mpango utahusisha Wizara za Kisekta, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretariati za Mikoa na Mamalaka za Serikali za Mitaa pamoja na Sekta Binafsi. Wadau hawa watahusika na utekelezaji wa Mpango kupitia mipango mikakati ya kisekta. Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango itakuwa na jukumu la kuratibu utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya Mpango.

Kielelezo Na. 4 Utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano



7.5 Muundo wa Uratibu wa Utekelezaji wa Mpango na Mgawanyo wa Majukumu

7.5.1 Serikali

Uratibu wa utekelezaji wa Mpango utafanyika katika ngazi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa - TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango. TAMISEMI, itaratibu utekelezaji wa Mpango katika Sekretariati za Mikoa na Mamalaka za Serikali za Mitaa. TAMISEMI itawajibika kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuandaa na kuwasilisha taarifa Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, katika ngazi ya Serikali Kuu Wizara ya Fedha na Mipango itapokea na kufanya mapitio ya taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka Wizara za Kisekta na kuandaa taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa Mpango.

7.5.2 Sekta Binafsi na Asasi Za Kiraia:

Uratibu wa utekelezaji wa Mpango kwa sekta binafsi na asasi za kiraia utatekelezwa kupitia majukwaa ya jumuiya mbalimbali za kibiashara, uwekezaji na huduma za kijamii. Aidha, Baraza la Taifa la Biashara – TNBC litawajibika kupokea maoni na mapendekezo kutoka sekta binafsi na kuwasilisha kwenye vikao vya mashauriano na Serikali. Vile vile, Serikali itapokea maoni kuhusu utekelezaji wa Mpango kutoka asasi za kiraia na washirika wa maendeleo.

7.6 Viatarishi vya Utekelezaji wa Mpango

Viatarishi vya utekelezaji wa Mpango vinajumuisha viatarishi asilia na ambavyo sio asilia kama ifuatavyo:

(a) **Mitikisiko ya Kiuchumi:** Shughuli za kiuchumi na kijamii nchini zimefungamanishwa na maendeleo ya dunia. Kwa msingi huo, mabadiliko ya shughuli hizo yanaweza yakaathiri utekelezaji wa Mpango. Hivyo, Serikali itaandaa mikakati ya kisera kwa lengo la kukabiliana na mabadiliko ya kiuchumi yanayoweza kutokea duniani na kuathiri utekelezaji wa Mpango.

(b) **Mabadiliko ya Kisiasa:** utekelezaji wa Mpango unaweza ukaathiriwa na mabadiliko ya kisiasa ya ndani na ya nje. Ili kukabiliana na athari za mabadiliko hayo, Serikali itasimamia misingi ya utawala bora. Aidha, Serikali itaimarisha diplomasia ya kiuchumi na kisiasa ili kupunguza athari za mabadiliko ya kisiasa ya nje.

(c) **Majanga ya Asili:** majanga ya asili yanayoweza kuathiri utekelezaji wa Mpango ni pamoja na: mabadiliko ya tabia ya nchi, tetemeko la ardhi, mafuriko, ukame na mlipuko wa magonjwa. Ili kukabilinana na athari za viatarishi hivi, Serikali itaimarisha mifumo ya kitaasisi ya kubaini na kudhibiti kiwango cha madhara kinachoweza kujitokeza kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Mpango.

SURA YA NANE
UFUATILIAJI NA TATHMINI

8.1 Utangulizi

Mpango huu unatekelezwa na wadau mbalimbali zikiwemo Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta binafsi, na Asasi za Kiraia. Hivyo, ni muhimu kuwa na Mfumo Madhubuti wa Ufuatiliaji na Tathmnini wa Utekeleza wa Mpango.

8.2 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango

Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango unajumuisha miundo ya kitaasisi na miongozo ya kiutendaji. Nyenzo hizio zitatumika kubaini kiwango na ubora wa utekelezaji wa Mpango. Hivyo, ni muhimu kujenga msingi wa kutathmini mwenendo na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shughuli za kiuchumi. Aidha, mfumo huo utahusisha udhibiti, ukaguzi, mapitio, kuandaa taarifa za mwenendo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na maoni na mapendekezo ya kuboresha na kuimarisha utekelezaji wa Mpango. Vile vile, Serikali itaweka utaratibu wa kubadilishana uzoefu kwa miradi iliyotekelezwa kwa ustadi.

Kielelezo Na. 5 Dhana ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango



8.3 Malengo ya Ufuatiliaji na Tathmini

Taratibu na mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya Mpango inalenga:

(i). Kuonesha mwenendo wa matokeo ya utekelezaji wa Mpango kwa kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu;

(ii). Kuratibu na kuwezesha Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sekta binafsi, na wadau wengine kufuatilia utekelezaji wa vipaumbele vya Mpango;

(iii). Kupima ufanisi wa mfumo wa utekelezaji na usimamizi wa Mpango;

(iv). Kubaini maeneo yenye tija na changamoto katika utekelezaji wa Mpango; na

(v). Kutoa maoni na mapendekezo ya kuboresha utekelezaji wa Mpango.

8.5 Matarajio ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango, matarajio ya ufuatiliaji na tathmini ni:

(i) Utekelezaji wa mipango ya kisekta kuwiana na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Ni matarajio kuwa mipango ya kisekta itaakisi vipaumbele vya Mpango ambavyo ni: kuchochea uchumi shirikishi na shindani; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza uwekezaji na biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu;

(ii) Ugawaji na utowaji wa rasilimali fedha kwendana na vipaumbele vya Mpango. Katika zoezi la ufuatiliaji na tathmini, Serikali itapata fursa ya kubaini kama ugawaji na utowaji rasilimali fedha unazingatia vipaumbele vya Mpango na bajeti iliyoidhinishwa;

(iii) Uwajibikaji katika matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo. Taarifa za ufuatiliaji na tathmini zitaiwezesha Serikali kubaini kiwango cha uwazi, ushirikishwaji na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma;

(iv) Matokeo ya utekelezaji wa Mpango kwenye ustawi wa maisha ya wananchi. Moja ya vipaumbele vya Mpango ni kuboresha maendeleo ya watu. Kwa msingi huo, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango unatarajiwa kubaini matokeo endelevu ya maendeleo ya watu yaliyotokana na utekelezaji.

Aidha, ufuatiliaji na tathmini ya Mpango, itatekelezwa katika shughuli za kawaida za Serikali za kila mwaka. Vile vile, ufuatiliaji na tathmini ya Mpango utafanyika katika kipindi cha muda wa kati wa mapitio na kipindi cha mwisho cha utekelezaji wa Mpango. Zoezi hili linalenga kupima mafanikio na changamoto ya utekelezaji wa Mpango. Hivyo, kuweka msingi wa maandalizi ya Mpango unaofuata kwa

miaka mitano.